**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NANE**

**Kikao cha Thelathini na Nne – Tarehe 30 Julai, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa 3.00 Asubuhi)*

**DUA**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Benki ya Rasilimali Tanzania *(TIB)* kwa Mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2006 *(The Annual Report and Accounts of the Tanzania Investment Bank Limited for the year ended 31st December, 2006).*

**SPIKA:** Vipi husemi chochote?

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia Kanuni ya 32 Kanuni Ndogo ya (1).

**SPIKA:** Umesimama kwa ajili ya suala la utaratibu?

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Hapana, kuhusu Hati iliyowasilishwa Mezani.

**SPIKA:** Kuhusu Hati, endelea!!

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Kwa mujibu kifungu cha 32 kifungu kidogo cha kwanza. Kwa ajili ya umuhimu wa Benki hapa nchini hasa hii *TIB* au benki ya Maendeleo hii, kuna haja kwa Bunge kupewa nafasi ya kulijadili hili hasa kuangalia namna ambavyo tungeweza kusaidia kilimo kwa kuweka mikopo ambayo inazingatia umuhimu wa kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Imeungwa mkono. Ahsante sana. Basi katika wakati muafaka itapangiwa nafasi ili iweze kujadiliwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba kwa mwaka wa fedha 2007/2008.

**SPIKA:** Ahsante sana. Bado nasisitiza kuhusu utata wa hili jina la Wizara, kwa kweli haipendezi hata kidogo.

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA– (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):** Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba kwa mwaka wa fedha uliopita, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2007/2008. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tufuate jina lililoko katika *Government Notice*. Ni Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, sisi ndiyo tunavyoifahamu hivyo.

**MHE. FATMA MUSSA MAGHIMBI – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI:** Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba kwa mwaka wa fedha uliopita, pamoja na maoni ya kambi ya upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2007/2008. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa kuitamka Wizara kama ilivyoandikwa katika *Order Papaer*. *(Makofi)*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 311

### Madaktari wanaofanya kazi nje ya nchi

**MHE. FATMA MUSSA MAGHIMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa kusomesha madaktari ni gharama kubwa sana na hivyo daktari aliyesomeshwa na kwenda kufanya kazi nchi nyingine anasababisha pengo kubwa sana:-

(a) Je, Serikali imewahi kufanya utafiti na kujua ni madaktari wangapi waliokimbia Tanzania kwenda nchi za nje kutafuta maslahi zaidi?

(b) Je, Serikali imeshachukua hatua gani za kuwafanya madaktari hao warudi nyumbani?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Maghimbi, Mbunge wa Chakechake, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa kusomesha madaktari ni gharama kubwa na kitendo cha madaktari wanasomeshwa kwenda kufanya kazi nchi nyingine kinasababisha pengo kubwa hasa ikizingatiwa tatizo kubwa la wataalam hao linaloikabili nchi yetu.

(a) Mheshimiwa Spika, kama nilivyolieleza Bunge lako Tukufu wakati nikijibu swali Na. 24 la Mheshimiwa Kidawa Salehe, katika Mkutano wa Sita; utafiti uliofanywa na Chama cha Madaktari Tanganyika *(Medical Association of Tanganyika)* mwaka 2006 unaonyesha kuwa kuna jumla ya watumishi wa Afya 342 ambao wanafanya kazi nje ya nchi, kati ya hao 111 ni madaktari. Aidha, utafiti huo unaonyesha kuwa asilimia kubwa ya watumishi hao wanafanya kazi katika nchi za Boswana, Lesotho, Namibia, Malawi, Afrika ya Kusini, Swaziland, Zambia na Zimbabwe.

(b) Sababu kubwa inayofanya wataalam wetu wengi wakiwemo madaktari kwenda kufanya kazi nje ya nchi ni kutafuta maslahi bora zaidi. Kwa kulitambua hilo Serikali yetu imekuwa ikijitahidi kuboresha maslahi ya watumishi wakiwemo madaktari mwaka hadi mwaka. Kwa mfano mwezi Januari mwaka 2006 ngazi ya mshahara wa kuanzia kwa madaktari ilipandishwa karibu mara mbili.

Aidha, kufuatia nyongeza ya mishahara ya watumishi wote wa umma ya mwezi Julai 2006 mishahara ya madaktari pia iliongezwa. Vile vile, kuanzia mwaka huu 2007 mishahara ya watumishi wa umma wakiwemo madaktari imeongezwa. Ni matumaini yangu kuwa juhudi hizi zinazoendelea kufanywa na Serikali yetu katika kuboresha maslahi ya watumishi zitasaidia kwa kiwango kikubwa kuwashawishi wataalam wetu, wakiwemo madaktari, waliokuwa na nia ya kwenda kufanya kazi nje ya nchi kubaki hapa nchini na walio nje ya nchi kurejea nchini.

**MHE. FATMA MUSSA MAGHIMBI:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa wanachofuata nje madaktari ni maslahi ni maslahi ya juu zaidi na kwa kuwa mishahara ya hapa ni midogo.

Lakini kila linapoulizwa swali juu ya mishahara ya madaktari huwa Naibu Waziri, au Waziri haitaji mishahara yao, huwa anasema tu inaongezwa.

Je, Mheshimiwa Waziri haoni kuwa kuna haja sasa wananchi wakajua kiasi gani madaktari wanapata ili wao nao waone huruma na kuwatafutia maslahi zaidi? Ahsante sana.

**WAZIRI WA NCHI, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kama nilivyokuwa nikisema kwamba mshahara wa mtumishi ni siri yake na mwajiri wake. Pia vyama vya wafanyakazi tulikubaliana kwamba hawapendi mishahara yao ikasemwa hadhari. Kwa hiyo, bado tutaendelea kuheshimu kwamba mshahara wa mtumishi ni siri yake na mwajiri wake na pia tutaendelea kuheshimu matakwa ya vyama vya wafanyakazi. *(Makofi)*

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Utumishi sasa hivi. Nina swali dogo tu la kuuliza. Kimsingi madaktari wanapoondoka katika nchi yetu kwenda kufanya kazi sehemu nyingine, wanaondoka katika namna mbili, wengine wanajiondokea tu lakini wengine huwa wanachukua livu ya muda mrefu ili wakapate kufanya kazi.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuwatumia Mabalozi wetu walioko katika kanda hizo ili kuwaelimisha hawa madaktari kuwa kama wakirudi nyumbani wale walioondoka pengine wana hofu kwamba labda wakirudi watakosa kazi ili wakaelewa kitakachowakabili wakirudi nyumbani ili waweze kurudi kuwasaidia wananchi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama anavyosema madaktari wanaokwenda, wanakwenda aidha kwa kuondoka au kwa kujulikana. Lakini napenda kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba wananchi kama nilivyojibu maswali mengine ni kwamba lazima wananchi tuwe na uzalendo na nchi yetu.

Lakini kama atakuwa anasikiliza habari, anaangalia televisheni, viongozi wetu wa ngazi za juu mara nyingi wakienda kama Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na viongozi wengine wa juu wakienda wanakaa wanakutana na wananchi katika nchi husika wanakaa na Watanzania walioko kule na kuwaambia warudi nyumbani ili waweze kuwekeza na kufanya kazi Tanzania.

Kwa hiyo, nafikiri sisi kama viongozi wote tukiwasaidia viongozi wakubwa basi tuwe tunaangalia. Lakini napenda kuwahakikishia kwamba na wale wafanyakazi walioko hata nje ya nchi wanatusikia na wanatuona, kwa sababu wanatumia *internet* wajue kwamba Tanzania sasa hivi hali yetu ni mzuri, madaktari wanapata huduma nzuri, kwa hiyo warudi na kwa uzalendo wao kuja kujenga nchi yao. *(Makofi)*

Na. 312

**Hadhi ya Hospitali ya Mtinko**

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH (K.n.y. MHE. LAZARO S. NYALANDU)** aliuliza:-

Kwa kuwa hospitali ya Mtinko iliyoko katika jimbo la Singida Kaskazini imesajiliwa rasmi; na kwa kuwa zaidi ya wananchi 70,000 wa Tarafa ya Mtinko, Ilongero na maeneo yanayozunguka wanategemea huduma ya hospitali hiyo:-

(a) Je, Serikali iko tayari kupokea ombi la hospitali hiyo na wananchi wa Singida Kaskazini kuifanya hospitali hiyo kuwa hospitali teule ya Wilaya?

(b) Kwa kuwa ujenzi wa kiwanja kidogo cha ndege *(Air strip)* unaotarajiwa kujengwa utasaidia kuongezeka kwa huduma za kitaalam hasa kutoka kwa *Flying Doctors.* Je, Serikali itakubali kuongeza idadi ya madaktari bingwa hasa wa upasuaji, macho, akina mama na watoto?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lazaro Samwel Nyalandu, Mbunge wa Singida Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kabla ya maboresho ya huduma za afya 1996 *(Health Sector Reform)* Wizara ilikuwa na mamlaka ya kuingia mkataba na hospitali za mashirika ya dini ili kutoa huduma kama hospitali teule za Wilaya *(Designated District Hospitals).*

Baada ya maboresho ya huduma za afya na kurudisha madaraka kwa wananchi na Halmashauri zao, sasa Halmashauri hizo ndizo zenye mamlaka ya kukubaliana na kuingia mkataba na Shirika linalotoa huduma kuendesha hospitali kama hospitali teule ya Wilaya. Namshauri Mheshimiwa Mbunge awasiliane na Halmashauri yake ili kuona uwezekano wa kufanya hospitali ya Mtinko kuwa hospitali teule ya Wilaya.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ikama ya watumishi katika vituo vya kutolea huduma za afya, hospitali ya Wilaya inatakiwa kuwa na madaktari wa kawaida watatu *(General Practitioners)* pamoja na wataalam wengine. Madaktari bingwa hupangwa kufanya kazi kwenye hospitali za mikoa na rufaa. Utaratibu huo unazingatia ukweli kwamba bado kiwango chetu cha kuzalisha wataalam wa kutosha ni kidogo. Hata hivyo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkoa Singida, tutaendelea kushughulikia upatikanaji wa madaktari bingwa wa upasuaji, macho na magonjwa mengine katika hospitali ya mkoa wa Singida ili wagonjwa wa Mtinko na Singida kwa ujumla watakaohitaji huduma za madaktari bingwa waweze kuzipatia hapo hapo Singida.

Nilikwisha litaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara tayari imekwishampeleka Singida daktari bingwa mmoja wa magonjwa ya kina mama na watoto wakati nikijibu swali Na. 184 la Mheshimiwa Diana Chilolo tarehe 10 Julai, 2007. *(Makofi)*

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameeleza vizuri hasa alipojibu hili jibu (b) lakini nataka niulizie kuhusiana na tatizo lililopo Singida Vijijini linafanana kabisa na lililopo Iramba. Kwa kuwa Wilaya ya Iramba ina watu takribani 400,000 na kulingana na idadi ya watu hao tumekuwa na vituo vya afya ambavyo vinahudumia wilaya ambao watu wako sehemu mbalimbali. Sasa ninauliza je, ili kuweza kuondoa lile tatizo ambalo tumekuwa tukitegemea hospitali moja ya Wilaya ambayo ipo Kiomboi Wizara ipo tayari kutujengea uwezo kwa kutupatia madaktari katika vituo vya afya vya Kinyangiri, Ndago, Namgongo ili kupunguza tatizo lile wakati wagonjwa wanapotaka kwenda hospitali ya Wilaya na usumbufu kuondoka? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyosema kwamba Iramba tatizo lake limefanana sana na tatizo la Singida Vijijini na watu wake ni wengi. Naomba nimfahamishe Mheshimiwa Killimbah kwamba idadi ya watumishi ambao sisi Wizara tunapeleka huwa inatoka kule kwenye Halmashauri husika na tunapata vibali ikishatoka Utumishi sisi ndiyo tunawapelekea. Nashauri kwamba wanapokuwa wanapelekewa watumishi kule Iramba au Singida, basi Halmashauri husika ziweze kuangalia sehemu ambazo zina upungufu ili ziweze kuwapeleka badala ya kuwalundika wengi katika makao makuu ya Wilaya. Lakini vile vile kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kuwa uhaba wa watumishi ambao ni kwa nchi nzima tunajitahidi ili tukipata tuweze kuwaongezea watumishi ili waweze kutoa huduma bora.

Na. 313

**Kero za Wakulima wa Korosho msimu wa 2006**

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR (K.n.y. MHE. HASSAN C. KIGWALILO)** aliuliza:-

Kwa kuwa wakulima wa korosho wakiwemo wa Wilaya ya Liwale, msimu wa 2006 walipata vikwazo mbalimbali kutoka kwa kampuni zinazonunua zao hilo, mfano kushuka kwa bei iliyokubaliwa na Serikali ya shilingi 600/= kwa kilo ya korosho gredi I na shilingi 480/= kwa kilo moja ya korosho gredi II:-

(a) Je, Serikali inafahamu kuwa baadhi ya wakulima wa korosho walilazimishwa kuuza korosho zao kwa bei ya chini hadi shilingi 200/= kwa kilo kwa hofu ya kukosa wanunuzi kwa bei ya Serikali, na Serikali inatoa tamko gani kwa kampuni hizo na inawashauri nini wakulima wa korosho?

(b) Je, ni tani ngapi za korosho zimenunuliwa mwaka 2006 na zina thamani gani na je, korosho zote za mwaka 2006 zilinunuliwa?

(c) Je, kuna kampuni yoyote iliyofuata masharti ya Serikali juu ya ununuzi wa zao hilo kwa kipindi chote cha msimu wa mauzo ya zao hilo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA)**alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, Mbunge wa Liwale, lenye sehemu (a) (b) na (c) napenda kutoa maelezo mafupi tu ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006 kama ilivyokuwa kwa miaka kadhaa huko nyuma, pamekuwepo na tatizo kubwa katika ununuzi wa zao la korosho. Mapema mwaka 2006, wanunuzi wa korosho na wawakilishi wa wakulima, katika mikutano kadhaa, walikubaliana kuweka bei dira ya shilingi 600 kwa korosho ya daraja la kwanza na shilingi 480 kwa korosho daraja la pili. Licha ya makubaliano hayo ulipokaribia msimu wa korosho mwezi Oktoba, wanunuzi waligeuka na kugoma kununua korosho kwa bei ya dira. Hatua hiyo ya wanunuzi ilisababisha usumbufu mkubwa kwa wakulima na hivyo kusababisha wakulima kuuza korosho zao kwa bei ya chini kwa kutumia kipimo kinachojulikana kwa jina la (kangoba). Kutokana na hali hii, Serikali licha ya kuwa haihusiki kupanga bei, ililazimika kuingilia kati kwa nia ya kulinda maslahi ya wakulima na maendeleo ya zao la korosho.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inafahamu kuwa, kutokana na usumbufu uliotokana na migomo ya wanunuzi baadhi ya wakulima waliuza korosho zao kwa bei ya chini katika masoko yasiyo rasmi. Hata hivyo, baada ya Serikali kuingilia kati, sehemu kubwa ya korosho iliuzwa katika vituo rasmi na kwa bei ya makubaliano baina ya wadau wa zao la korosho ambayo ilikuwa shilingi 600 na shilingi 480 kwa daraja la kwanza na la pili sawia.

Mheshimiwa Spika, ili kuondokana na tatizo hili Serikali imechukua hatua ya kuimarisha vyama vya ushirika vya msingi, ili vishiriki katika ununuzi wa korosho ili viongoze ushindani na hivyo kuwaongezea wakulima kipato chao. Wakulima wanashauriwa sasa kuuza korosho zao kwa vyama vya ushirika ili kujiepusha na balaa lililowakumba mwaka jana.

(b) Katika msimu wa 2006/2007, Serikali ilikadiria ununuzi wa korosho ungekuwa tani 110,000. Tangu ununuzi wa korosho ulipoanza tarehe 2 Oktoba, 2006 hadi tarehe 31 Mei, 2007 jumla ya tani 92,573 za korosho zenye thamani ya shilingi bilioni 59.2 zilikuwa zimenunuliwa. Kiwango hicho cha ununuzi ni sawa na asilimia ya 82.2 ya lengo la ununuzi, na bado msimu wa ununuzi wa korosho za msimu wa 2006/2007 unaendelea hadi Oktoba, 2007.

(c) Katika msimu wa 2006/2007, jumla ya makampuni 27 yalipewa leseni za ununuzi wa korosho. Kati ya hayo, makampuni saba yalifutiwa leseni zao na Serikali waliposhindwa kutimiza baadhi ya masharti tuliyokubaliana nao katika ununuzi wa korosho. Makampuni mengine, yanaendelea na ununuzi kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zinazosimamia biashara ya mazao nchini pamoja na bei walizoafikiana wakulima na wafanyabiashara. Kwa kuwa msimu wa mauzo ya korosho unaendelea Serikali inaendelea kusimamia utendaji wa kampuni hizo ili kuhakikisha zinaendelea kufuata masharti tuliyokubaliana kwa kipindi chote kilichobaki cha msimu wa mauzo.

**SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Mudhihir. Alaa, lakini Mheshimiwa ulichelewa wewe, haya kwa kuwa ni swali lako Mheshimiwa Kigwalilo.*(Kicheko)*

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza baada ya majibu mazuri. La kwanza je, makampuni mangapi ambayo yameteuliwa kwa kipindi hiki kusambaza pembejeo za zao hilo la korosho nchini kote?

Pili, kutokana na zao hilo la korosho ningetaka kujua ruzuku sasa hivi Maendeleo yake yakoje kwa zao hilo nchini kote? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA):** Mheshimiwa Spika, makampuni ambayo yameruhusiwa kusambaza pembejeo hizi nitamkabidhi orodha, lakini ningependa kumtajia baadhi ya makampuni ambayo tayari yamekwisha anza kufanya kazi hiyo ya kusambaza. Kampuni ya *Mukpa Tanzania Limited,* tayari imeshaanza kufanya kazi na imeshalipwa na fedha. Kampuni ya *By Trade, Abbas Limited* hizo zimekwishaanza kazi.

Sasa ziko zingine tayari zinaendelea na utaratibu wa kuomba kufanya kazi hiyo. Sasa ninachoomba tu ni kwamba nitamkabidhi orodha ya makampuni mengine ambayo yamejiorodhesha au yameomba kufanya kazi hiyo ili aweze kuyajua.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ruzuku sijui Mheshimiwa Mbunge anataka kuuliza utaratibu gani mwingine wa ruzuku labda sijamwelewa. Lakini ninavyomwelewa mimi na yeye mwenyewe anajua kwamba Serikali inatoa ruzuku kwa zao la korosho. Inatoa zuruku kwa ajili ya madawa ya korosho hususan madawa ya *sulpher* na madawa mengine. Ndiyo maana tumekuwa tukisema kwamba madawa yale ambayo hatuyahitaji sana kama *sulpher* utakuta tumeweka utaratibu wa ruzuku hiyo iwe inapunguziwa kusudi tuya-*discourage* yasiweze kutumika kwa sababu yanaharibu.

Lakini kwa sasa hivi wakulima wanayapenda sana basi inabidi tuweke tu utaratibu huu kwamba ile ruzuku yake tutakuwa tunaipunguza kila mwaka, wakati wakulima wanakubali yale madawa mengine yanayoingia nchini.

Sasa kuhusu hiyo ruzuku nyingine sijui utaratibu anaoutaka lakini utaratibu wa ruzuku ndiyo huo huo ambao tumeuelezea wakati wote na Mheshimiwa Mbunge pia

anajua kwamba kila mwaka kuanzia mwaka juzi Serikali inatoa shilingi bilioni 1 kwa ajili ya ruzuku hiyo ya korosho. Sasa mimi nafikiri sina maelezo zaidi ya hapa. Labda kama angesisitiza, angeweza kunifafanulia anataka ruzuku ipi.

**SPIKA:** Mengine hayo mtaonana huko nje ya Ukumbi. Nilimwona Mheshimiwa Mudhihir kwa sababu ndiye aliyeuliza, basi liwe la mwisho. Korosho tunaweza kuendelea hata mpaka saa 7 mchana. Lakini tuishie hapo. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kuniona. Nina swali moja tu dogo. Kwa kuwa sasa hivi imebakia miezi miwili tu kabla ya msimu wa korosho kuanza. Haya maandalizi ya kuimarisha ushirika aliozungumza Mheshimiwa Naibu Waziri katika kununua korosho, hivi sasa yamefikia wapi, hatua gani? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA):** Mheshimiwa Spika, Serikali imepeleka wataalam wa ushirika wengi tu kule katika Kanda ile inayolima korosho na kazi wanayoifanya hivi sasa ni kuhakikisha kwamba vyama hivi vya msingi vinasajiliwa. Kwa hiyo, shughuli zinaendelea kuvisajili vyama hivyo vya ushirika na vitaanza kufanya kazi katika msimu huu.

Na. 314

**Kutowapa wawekezaji kuchimba Tanzanite**

**MHE. DORAH H. MUSHI** aliuliza:-

Kwa kuwa nchi nyingi duniani zinazochimba madini ya vito kama *Tanzanite* hawatoi nafasi kwa wawekezaji wageni:-

Je, Serikali haioni kuwa wakati umefika kwa nchi yetu kuacha kabisa kutoa maeneo kama haya kwa wawekezaji wageni?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dorah Herial Mushi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa madini ya vito ambayo hujumuisha madini ya *Tanzanite* Sera ya Madini ya mwaka 1997, iliweka dira ya kuendeleza madini ya vito na kuifanya Tanzania kuwa kituo cha maonyesho kwa madini ya vito Barani Afrika. Mwaka 1998, Serikali ilitunga Sheria ya Madini inayosimamia sekta ya madini ambayo inaruhusu madini ya vito kuchimbwa na Watanzania tu au iwapo

wawekezaji wa kigeni watashiriki, Watanzania wamiliki hisa zisizopungua asilimia 25 katika kampuni hizo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004, Wizara iliunda Kamati ya Kudurusu Sera ya Madini iliyotazama maeneo muhimu yanayohitaji marekebisho katika Sera na Sheria za Madini. Katika kufanya kazi yake Kamati hii ilikusanya maoni ya wadau mbalimbali nchini, wakiwemo wananchi na wachimbaji wa *Tanzanite* wa Mererani. Mchakato wa kudurusu Sera ya Madini kwa kuzingatia mapendekezo ya Kamati iliyoundwa mwaka 2004 upo katika hatua za mwisho.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mapendekezo ya Kamati iliyoundwa mwaka 2004, katika mwaka 2007/2008 Serikali itakamilisha mchakato wa kudurusu Sera ya Madini ya mwaka 1997.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa ruhusa ya kuuliza swali la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ningependa kuuliza swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa, madini haya ya *Tanzanite* miaka ya nyuma, miaka ya 80 yalikuwa yakichimbwa na kampuni ya wazawa ya *Tanganyika James Stone Industries* kwa ubia na kampuni ya *Grafight Ltd* na baada ya hapo natumaini kampuni ya *James Stone* ilijiondoa ikabaki ile ya *Graphtone Ltd,* lakini baada ya hapo pia *graphtone* waliwapa *sumunce* baadaye *sumunce* wakawapa *African James* na baada ya hapo wakawapa tena *Tanzanite One.* Je, ni kampuni gani ya kizawa ambayo ilikuwa inashirikiana na haya makampuni au walikuwa wanabadilisha kwa kupeana vijiti kama mchezo wa kupeana vijiti?

**NAIBU WAZIRI NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, labda nitoe ufafanuzi kuhusu umiliki wa leseni ambazo zimetolewa na Serikali Mererani. Kihistoria inaonekana kumekuwa na wamiliki kadhaa katika maeneo hayo, na kwa sasa na hasa baada ya kubadilishwa sera ya madini mwaka 1997 na sheria yake kuundwa mwaka 1998 iliyoanza kufanya kazi mwaka 1999. Umiliki wa vitalu vya madini ya *Tanzanite* katika eneo la Mererani uko kama ifuatavyo:-

Kuna vitalu kimsingi vinne ambavyo viko pale vimeshaainishwa kitalu (a) kinamilikiwa na Kampuni ya *Kilimanjaro Minings*, kitalu (b) kinamilikiwa na *Building Activities* na Kitalu (c) kinamilikiwa na *Tanzanite one* ambayo umiliki wake umekuwa ukihama kutoka kwa mwekezaji mmoja kwenda mwingine kulingana na uwezekano wa kisheria ambao umekuwepo hapa na hasa na utashi wa miliki ambao wanakuwepo kwa wakati na kitalu (d) ambacho wamiliki wake ni *Arusha Regional Mining Registration* ambao kimsingi ilikuwa ni umoja wa wachimbaji madini ya *Tanzanite* katika mkoa wa Arusha kabla mkoa wa Arusha haujagawanywa.

Mheshimiwa Spika, sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge ni kwamba kwa sasa hivi vipo vitalu ambavyo vinamilikiwa na wazawa, na hawa *Tanzanite One* ambao leo tunasema wanamiliki kitalu (c) wamemiliki kitalu hicho kisheria kwa sababu wamiliki waliokuwepo waliokuwepo awali ambao ni pamoja na *Tanzanite* kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge lilikuwa ni jambo la kisheria na hili jambo ni jambo la

kawaida katika biashara mtu, anaweza kuwa na kampuni akafanya biashara fulani ikafikia mahali akajisikia kuuza kwa sababu mbalimbali unaomiliki ule mradi unazingatia sheria itakuwa haina tatizo.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kilichotokea kilizingatia utashi wa sheria, sera na kanuni zetu za nchi.(*Makofi*)

**MHE. ANNA K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza katika swali hili ambalo ni swali muhimu sana. Kwa kuwa katika kipindi hiki cha *Globalization* duniani mataifa makubwa yawe yanaringia kwamba yana uwezo upande wa *modern technology.* Na kwa kuwa sisi ambao hatuna uwezo huo tunachopaswa kuringia ni *natural rsource* tulizonazo, na kwa kuwa upande wa *Tanzanite* ni Tanzania peke tu ndiyo ambao wana *product* hii.

Je, Serikali haioni kwamba ni vyema tukajitahidi tukahakikisha kwamba *the only supplier and the only producer* wa zao hili kwa sababu tusipoingia kwenye ku-*nopolize* hii *product* itafikia mahali *suppliers* wengine ndio watapata faida kuliko sisi ambao Mwenyezi Mungu ametujalia kupata vito hivi.

**SPIKA**: Nadhani umepata ushauri tu, kwa hiyo ni vizuri kuuzingatia ushauri mzito kama huo. (*Makofi*)

Na. 315

**Ujenzi wa Mabweni kwa Mpango wa MMES**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa Shule nyingi za Sekondari za kutwa ziko Makao Makuu ya Kata na hazina mabweni na kwa kuwa wanafunzi wengi wa kike wanapopanga nyumba mitaani hutumia uhuru wao vibaya na kusababisha kupata vishawishi vya wanaume na hivyo kusababisha mimba na kwa sababu hiyo kushindwa kumaliza masomo yao:-

Je, ni lini Serikali italitatua tatizo hilo kwa kujenga mabweni kupitia mpango wa MMES?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kimsingi Shule za Sekondari za Kata ni za kutwa. Pale ambapo wakazi wa Kata wametawanyika mno kiasi cha wengine kuwa mbali na ilipo shule, Wizara inawahamasisha wananchi kujenga hosteli. Serikali itaendelea kuunga mkono ujenzi wa hosteli kadri ya upatikanaji wa fedha.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, kwa kuwa wananchi wa mkoa wa Singida wa Kata zote wako tayari kwa asilimia 100 kujenga hosteli kama walivyofanya kujenga madarasa ya shule za sekondari. Je, Serikali iko tayari kumalizia ujenzi huo endapo kata hizi zote zitakamilisha ujenzi wa maboma?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Diana kwa namna ya kipekee anavyofuatalia Maendeleo ya elimu tunamshukuru sana.

Pili ni adhima ya Serikali ya kusaidia nguvu za wananchi pale fedha zitakapowezekana. Mwaka huu tumeanza utaratibu wa kutelemsha madaraka kwa wananchi *D by D.* Hivyo kila Halmashauri inayo uwezo wa kuweka kipaumbele chake ili kuweza kutatua kero za wananchi. Maboma watakayokuwa wameanza kujenga endapo Halmashauri yao itakuwa na uwezo basi wataelekeza kipaumbele hapo.

Hata hivyo, kama tulivyojibu maswali kadhaa pale ambapo wananchi wataonyesha nia Serikali itasaidia kutegemea na fedha zitakavyopatikana.

Na. 316

**Kujali Walimu**

**MHE. SIJAPATA NKAYAMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, walimu wachache katika shule za msingi na sekondari; na kwa kuwa, walimu hao wamekuwa wakifanya kazi bila kupumzika, vipindi vimekuwa vingi kwa kila mwalimu:-

(a) Je, Serikali itawajali lini walimu hao kwa kuwalipa posho ya kazi ya ziada?

(b) Je, ni lini Serikali itawapa walimu kipaumbele kwa kuwalipa posho ya taaluma kama ilivyokuwa miaka ya nyuma?

(c) Je, ni lini Serikali itafikiria kuwakopesha walimu pikipiki ili kuepuka usumbufu wanaoupata kwa kutembea kwa miguu kufuatilia mishahara yao?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sijapata Fadhili Nkayamba, Mbunge wa Viti Maalumu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, na Serikali inatambua majukumu na kazi kubwa wanayoifanya walimu. Serikali kwa sasa inautazama mfumo mzima wa ajira na namna bora ya kuwahudumia walimu, ikiwa ni pamoja na kuangalia maslahi yao kwa kuzingatia mapendekezo ya Tume ya Rais ya Maslahi ya Wafanyakazi. Maslahi ya walimu yataendela kuboreshwa kulingana na uwezo wa Serikali.

(b) Mheshimiwa Spika, katika miaka ya nyuma Serikali ilikuwa inatoa posho ya taaluma kwa walimu. Kwa hivi sasa posho hiyo imejumuishwa kwenye mishahara ya walimu ili iweze kuboresha pensheni wakati walimu watakapokuwa wamestaafu.

(c) Mheshimiwa Spika, kuhusu walimu kukopeshwa vyombo vya usafiri ikiwa ni pamoja na pikipiki hili ni jambo nzuri. Wizara yangu badala ya kukopesha fedha, inawadhamini walimu wanaoomba mikopo kutoka Taasisi za Fedha kama vile *NMB,* na Benki ya Posta. Aidha, walimu wanaweza kukopa kupitia *SACCOS* zao.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa walimu ndiyo chombo kikubwa katika Serikali, na bila walimu hakuna kitakachotendeka. Kwa kuwa walimu wamekuwa wakipata mshahara ambao sasa hivi maisha yao yamekuwa ni ya ghali sana. Je, Serikali haiwezi kufanya mpango wa kuweza kuwajengea nyumba kwa kuwakopesha ili watakapostaafu waweze kufikia kwenye nyumba nzuri?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli umuhimu wa walimu unatambulika na Watanzania wote, lakini kama nilivyosema kwenye swali la msingi ni kwamba maslahi yao yanazingatiwa katika mishahara yao.

Suala hili la kuwakopesha fedha ili waweze kujenga nyumba zao binafsi za kuishi kipo chombo cha Serikali ambacho hivi sasa kinaundwa ambacho wafanyakazi wakulima na wafanyabiashara watakwenda kukopa ili waweze kujenga nyumba zao. Na walimu watashauriwa kwenda katika vyombo hivyo ili kuweza kujipatia fedha za mkopo, lakini kwa sasa mabenki yaliyopo pamoja na *SACCOS* ambazo zimeshamiri sana katika chama cha walimu tunaomba walimu waweze kuzitumia fedha hizo vizuri wanapokwenda kuzikopa ili waweze kujengea nyumba zao wakijiandaa kwa kustaafu. Lakini wapo, tunajua wanaokopa wengi hawazitumii vizuri, lakini tunawashauri wanaokopa fedha wazikope hizo fedha waende wakafanye yale waliyoyapanga ikiwa ni pamoja na kujenga nyumba zitakazowastiri pale watakapostaafu.

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza, kwa kuwa, walimu wamekuwa na kipato kidogo ambacho hakitoshi kutokana na mazingira yao. Je, Serikali haioni kwamba sasa umefika muda muafaka wa kuruhusu walimu hao wafundishe *tuition* ili waweze kujipatia kipato chao?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA):** Mheshimiwa Spika, walimu wanapofanya kazi wana muda mdogo sana ambao wanaweza kuutumia kwa mambo mengine, kwa sababu ukiangalia ratiba ya mwalimu akitoa kazi darasani na watoto wakafanya mazoezi yale wakampelekea madaftari kwa ajili ya kusahihisha atakuwa na muda mwingi sana atakaoutumia pale nyumbani kwa ajili ya kusahihisha. Sasa kama atafanya kazi ya *tuition* yawezekana akaanza kuzembea kazi ile ambazo ameajiriwa kuzifanya, nia ya Serikali ni kumtaka mwalimu afanye kazi hiyo aliyopangiwa aifanye vizuri.

Tukimruhusu aanze kufanya kazi ya *tuition* itazorotesha utendaji wake wa kazi, lakini kufanya kazi nyingine za ziada kama kufuga kuku au kufuga ng'ombe hiyo inaruhusiwa anaweza kufanya kazi, lakini tumekataza mara nyingi kwamba walimu wanapojitumbukiza katika kazi hizi za ziada za kufundisha *tuition* wanazorotesha Maendeleo ya elimu katika shule zao kwa sababu hawazingatii darasani kwa sababu anajua atafanya kazi ya ziada. Hivyo tunawashauri walimu wafanye kazi zingine za kiuchumi za kuwasaidia kupata kipato zaidi, lakini suala la *tuition* lifanyike kwa uangalifu sana kwa sababu linaweza likaongezea tatizo la kuzorotesha elimu katika nchi yetu. *(Makofi)*

Na. 317

**Uingizaji wa Nguo Kuu Kuu Nchini**

**MHE. WILLIAM HEZEKIA SHELLUKINDO** aliuliza:-

Kwa kuwa, nguo kuu kuu huingizwa nchini, licha ya kwamba Serikali ilipiga marufuku kuingiza nguo za ndani kuu kuu:-

(a) Je, Nguo za ndani zinazouzwa mitaani nchini kote ni kuu kuu au mpya?

(b) Je, ni chombo gani kilichopewa jukumu la kudhibiti uingizaji nchini nguo hizo kuu kuu?

(c) Je, ni wafanyabiashara wangapi wa nguo kuu kuu wamechukuliwa hatua za kisheria kwa kukiuka tangazo lililotolewa?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa William Hezekia Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nguo za ndani zinazouzwa mitaani nchini baadhi ni mpya na nyingine ni kuu kuu ambazo zinaingizwa nchini na wafanyabiashara wasio waaminifu.

(b) Mheshimiwa Spika, chombo kilichopewa jukumu la kudhibiti uingizaji wa nguo kuu kuu ni shirika la Viwango Tanzania (*TBS*) lenye wajibu wa kusimamia utekelezaji wa viwango vya kitaifa ambapo kiwango cha nguo zilizotumika ni TZS 758:2003 *Code of Practice for Inspection* and *Acceptance Criteria for Used Textile Products* (Mitumba) Aidha, Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* imekuwa ikitoa ushirikiano wa kupambana na wafanyabiashara wa aina hiyo na pindi wanapobainika *TBS* hupewa taarifa kwa ajili ya kufanya ukaguzi.

(c) Mheshimiwa Spika, tangu *TBS* ianze utekelezaji wa kiwango cha nguo zilizotumika (mitumba) jumla ya wafanyabiashara 12 walioingiza makontena 16 walizuiliwa kuingiza katika soko la Tanzania baada ya kubainika kuwepo kwa baadhi ya nguo kuu kuu za ndani katika makontena yao. Baada ya ukaguzi nguo zote kuu kuu za ndani zilizobainika ziliteketezwa kwa moto na waingizaji husika kwa gharama zao chini ya uangalizi wa maofisa wa *TBS*. Katika kukabiliana na tatizo hilo la uuzaji wa nguo kuu kuu za ndani *TBS* inaendelea kudhibiti uagizaji wa nguo hizo, pamoja na kuelimisha umma kuhusu athari zinazotokana na matumizi ya nguo kuu kuu za ndani.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa katazo lililotolewa na Serikali ni hasa madhumuni yake ilikuwa ni kulinda afya za wananchi. Je, Waziri atakubaliana na mimi kwamba kwa kweli kuna haja sasa hivi ya kutoa elimu ya kutosha na kuwaeleza wananchi hasa mavazi haya ya ndani yanaweza kutuletea madhara gani?

**SPIKA:** Kabla Mheshimiwa Naibu Waziri hajajibu, ninavyomfahamu Mheshimiwa Shellukindo, sidhani kama ni mteja wa hizi nguo kuu kuu za ndani lakini... (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, mimi nakubaliana naye kabisa kwamba suala la kuelimisha umma juu ya athari zinazoweza kuwakabili wanapotumia nguo hizi za ndani kuna umuhimu, ina umuhimu sana. Ndiyo hata katika jibu langu hapa nimesema kwamba moja ya jitihada tunazozifanya ni kuelimisha umma juu ya athari hizo. Kwa hiyo tutashirikiana na wenzetu wa Wizara ya Afya na taasisi nyingine kwa ujumla ambazo zinaweza zikatoa maelezo muafaka juu ya athari mahususi zinazoweza zikapata wanunuaji wa nguo hizi za ndani ili tatizo hili liweze kutatuliwa.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Serikali ya awamu ya tatu kupitia Wizara ya Mambo ya

Ndani wakati huo ilipiga marufuku kabisa nguo kuu kuu za ndani kuuzwa, na kwamba yeyote atakayeonekana anauza mitaani ashikwe na kufikishwa mahakamani.

Lakini agizo hilo bado linakiukwa, nguo hizo zinauzwa mitaani, na wahusika wetu wa vyombo vya usalama wanaangalia na wao wenyewe kununua. Je, kwanini basi sheria hizi au maagizo haya ya viongozi mara nyingi yanapotolewa huwa yanakiukwa hata pamoja na watendaji, ni kwa nini hasa ni dharau au wanaona tu mambo yatakwisha?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, mimi nilipokuwa najibu swali hapa nilisema kwamba nguo hizi za ndani zinaingizwa na wafanyabiashara wasio waaminifu. Kwa hiyo, kwa kweli sheria ipo, sasa sheria zote zilizopo zinavunjwa na baadhi ya watu ambao sio waaminifu.

Kwa hiyo, nataka tu kusisitiza kwamba upigaji marufuku bado uko pale pale kwa hiyo tushirikiane pamoja na Mheshimiwa Mbunge mwenyewe endapo atabaini kwamba kuna watu wanaendelea kununua nguo hizo za ndani pamoja na hapo watendaji atoe taarifa kwa vyombo husika ili waweze kuchukuliwa hatua.

Na. 318

**Ofisi ya Shirika la Posta Tanzania**

**MHE. SAID JUMA NKUMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa shirika la Posta Tanzania halijajenga Ofisi yake ya kufanyia shughuli zake kwani bado imepanga chumba kidogo ambacho kinalifanya shirika liendeshe shughuli zake kama duka la mtaani:-

(a) Je, ni lini shirika litajenga ofisi yake ya kufanyia shughuli zake?

(b) Je, kuna makubaliano gani na *TTCL* ya kufanikisha huduma nyingine kama *Fax, EMS* n.k. ambavyo vikikamilika huduma hizo hupatikana kwa urahisi na kwa muda mfupi?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba shirika la Posta Tanzania halina jengo la kuendeshea huduma zake katika mji wa Sikonge na hivyo kulazimika kuendeshea shughuli zake katika jengo la kukodi. Hata hivyo, Shirika la Posta limeshawasiliana na Mamlaka husika na kuahidiwa kupatiwa kiwanja katika mji wa Sikonge ili kujenga jengo la Posta. Aidha,

michoro ya jengo hilo imeshakamilishwa na hivyo kiwanja kikishapatikana ujenzi utafanyika kutegemeana na hali ya fedha ndani ya Shirika.

Mheshimiwa Spika, huduma ya *EMS* na *money fax* ilikuwa haipatikani katika Posta ya Sikonge kwa vile Kampuni ya Simu Tanzania ilikuwa haijaweza kulipatia Shirika la Posta Tanzania *line* ya simu kwa madhumuni hayo.

Napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, Kampuni ya Simu Tanzania imeshaweka mtambo ambao umeliwezesha Shirika la Posta kupata *line* hiyo ya simu kuanzia tarehe 20 Juni, 2007. Hivi sasa huduma ya *EMS* na *Money fax* inatolewa na Shirika la posta mjini hapo. *(Makofi)*

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kutekeleza yale ambayo alikuwa ameahidi siku za nyuma. Nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Shirika la posta, huko nyuma lilifanya kazi nzuri sana na kwa sasa hivi Shirika hili maeneo mengi linaonekana kwamba limekufa kufa. Je, Serikali inampango gani wa kuhakikisha kwamba shirika hili sasa linapata ofisi kila mahali hasa makao makuu ya Wilaya na maeneo mengine kupatiwa vifaa ambavyo havipo ili kuhakikisha kwamba shirika hili linarejea katika hali yake ya zamani?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, napenda nimhakikishiea Mheshimiwa Nkumba kwamba nia ya Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu ni kulifufua Shirika la Posta ili liweze kuhudumia wananchi katika huduma zote za posta.

Mheshimiowa Spika, napenda nimhakikishia Mheshimiwa Nkumba na Wabunge wote kwamba Serikali imo njiani kutekeleza wajibu huo kwa kuona kwamba tunaweza kulifutia madeni yake na kuwezekana kuliongezea mtaji na hivi sasa ninavyosema wao wenyewe Shirika la Posta wameanza kujifufua kwa sababu wameanza kuanza kutoa huduma za kompyuta katika maeneo yote ili waweze kutoa huduma za *internet* na shughuli zingine. Katika suala la *money fax* kuna posta kama 74 nchini ambazo zinatoa huduma hizi na shughuli hii bado inaendelea. Ni nia ya Serikali kuona Serikali posta nayo inachangia uchumi wa nchi hii.

Na. 319

**Utaratibu wa Kukusanya Kodi**

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR** aliuliza:-

Kwa kuwa katika kipindi cha miezi 6- 7 hivi sasa, Serikali imeanzisha utaratibu wa kutoza kodi kwa magari yanayoingia na kutoka Uwanja wa Ndege wa Mwalimu Julius Nyerere, Dar es Salaam:-

(a) Je, hadi sasa Serikali imekusanya kiasi gani cha fedha?

(b) Je, makisio ya makusanyo kwa mwaka ni kiasi gani na nini lengo la matumizi ya fedha hizo?

(c) Je, utaratibu kama huo unafanywa wapi katika viwanja vyetu hapa Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI)** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mbunge wa Dimani, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Utaratibu wa kutoza ada ya maegesho ya magari katika viwanja vya ndege ni wa kawaida duniani na ni moja ya vyanzo vya mapato katika viwanja vya ndege kinachotozwa ni ada ya maegesho (*parking fee)* na siyo ada ya kuingia kiwanjani (*entry fee*). Katika kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere utaratibu wa kutoza ada ya kuegesha magari ulianza mwezi Januari 2006, baada ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania Tanzania kuingia mkataba na kampuni binafsi wa kuweka mitambo ambayo inawezesha ukusanyaji wa ada ya maegesho kufanywa kwa ufanisi na bila usumbufu.

Ada hii inahusu magari yote yanayoingia na kukaa ndani ya eneo la kiwanja kwa zaidi ya dakika kumi. Magari yanayoingia kiwanjani kwa lengo la kushusha au kuchukua abiria bila kukaa kwenye kiwanja hayahusiki na kulipa ada hii.

Mheshimiwa Spika, tangu utaratibu wa kukusanya ada ya maegesho katika kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Juliusa Nyerere uanzishwe, mamlaka ya Viwanja vya ndege Tanzania, imekusanya kiasi cha shilingi 19,940,000. Mamlaka ya Viwanja vya ndege Tanzania, imejiwekea lengo la kukusanya kiasi cha shilingi milioni 75,000,000 kwa mwaka kutokana na ada ya maegesho katika Kiwanja cha Julius Nyerere. Kimsingi fedha hizo ni moja ya vyanzo vya mapato vya mamlaka na hutumika katika kuendesha shughuli za mamlaka ikiwemo matengenezo ya viwanja vinavyomilikiwa au kuendeshwa na mamlaka.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kukusanya ada za maegesho kwenye viwanja vya ndege kwa sasa unafanywa katika viwanjwa vya ndege vya kimataifa vya Julius Nyerere na Kilimanjaro.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza baada ya majibu mwanana ya Mheshimiwa Naibu Waziri kutokana na swali langu la msingi.

Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza akalimbia Bunge letu Tukufu pamoja na wananchi kwamba Je, ni kampuni gani za wananchi zilizopewa jukumu la kufanya kazi hii katika viwanja vya Mwalimu Nyerere na kule Kilimanjaro na zinaitwaje.

Lakini pili Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba unafika wakati mashine za uwanjani hapo huwa hazifanyi kazi na kusababisha suala zima la upotevu wa fedha katika kiwanja hicho, wakati ule wafanyakazi walipopokea pesa mkononi.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, kampuni zinazotoa huduma hii kwa *Dar es Salaam Julius Nyerere Internationa Airport* ni *Degency System Tanzania Ltd,* na kwa Kilimanjaro ni *Cadico.* Napenda nimwambie Mheshimiwa Mbunge ni kweli yamekuwepo na matatizo ya hapa na pale ya zile mashine na si hilo tu. Kulikuwa na machache ya kwamba hata huyu mtu mwenyewe alikuwa hakusanyi ipasavyo.

Kwa hivyo hivi sasa shauri hili liko mahakani na tunategemea tarehe 24 mwezi huu tutaitwa tena na mamlaka kujadili zaidi kwa sababu utendaji wake kidogo ulikuwa ni dhaifu.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umefika umewadia, umekwisha na pia maswali yenyewe yameisha ninayo matangazo. Kwanza Waheshimiwa Wabunge nafurahi kuwafahamisha kuwa mwenzetu Mheshimiwa Mporogomyi amerejea Bungeni baada ya matibabu kule India na ameniandikia kwamba amerejea salama, yule pale. Naomba kama kawaida nimpe dakika moja tu awasalimie.

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa jinsi alivyonisaidia toka niugue mpaka leo hii ninaporejea Bungeni hapa, lakini pia napenda kuishukuru Ofisi ya Bunge na kuwashukuru nyie wenzangu ambao wengi wenu mlinifariji sana nilipokuwa naumwa, nimepata matibabu mazuri sana kule India nilifanyiwa *operation* ya *cervical spin* kwa mara ya kwanza na safari ya pili nikafanyiwa *operation* ya *lumber spin* kwa sababu nilikuwa na *sleep disks* mbili juu na chini lakini naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu sana nashindwa hata kuzungumza kwa sababu ya furaha niliyonayo maana sikujua tena kama nitafika hapa.

Lakini Mwenyezi Mungu amenisaidia nimefika hapa tena na mimi ninawahakikishieni kwamba mimi ni mzima sasa nguvu ninazo nitashirikiana nanyi na ninao uwezo wa kufanya kazi ya aina yoyote ile ambayo ninaweza kupewa, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi ingawa nilipokuomba utusalimie sikutazamia kwamba utaenda mbali kiasi hicho. Leo tuna baraka kubwa ya wageni Waheshimiwa wageni wetu utaratibu wetu ni kwamba nikitaja mgeni husika huwa tunamwomba asimame ili Wabunge waweze kumtambua.

Tunao Waheshimiwa Majaji wakiongozwa na Jaji Mfawidhi Mheshimiwa Joseph Masanje wa hapa Dodoma ambaye nitamwomba Mheshimiwa Jaji Mfawidhi Dodoma asimame, Mheshimiwa Jaji Lila na Mheshimiwa Jaji Kwalika, Waheshimiwa Majaji karibuni sana na ninaelewa pamoja nanyi wapo Mahakimu kadhaa, ningeomba Waheshimiwa Mahakimu msimame pale tafadhali, kama mnavyojua leo ni Wizara ya

Sheria na Mambo ya Katibu kwa hiyo wamekuja Waheshimiwa kutoka Mahakama kuweza kuwa na sisi hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mary Nagu Waziri wa Wizara hiyoameniomba niwatangaze wageni wake hawa na wa kwanza ni Prof. Nagu, Mhadhiri Mhandamizi kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe ambaye haikuelezwa hapa uhusiano nadhani ndio mume wake, karibu sana Mheshimiwa Nagu mama anafanya kazi vizuri sana hapa Bungeni tunatumaini utaendelea kumlea vizuri na watoto wao ni Neema Nagu na Margwe Nagu, ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

Pamoja nao wapo Mwenyekiti Mstaafu wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang Mheshimiwa Joseph Mark pia wapo waliomsindikiza nao ni Kessy Agress, Issa Kamunga mtaniwia radhi haya majini ya Hanang yanahitaji mtu labda ukakae kidogo huko huko uyaelewe vizuri, Mama Vanesa na Joseph Nada, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wa Wizara wa ambao ni wa Mheshimiwa Waziri ni Waheshimiwa kutoka Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora wakiongozwa na Mwenyekiti mwenyewe Mheshimiwa Jaji Robert Kisanga, naye ameambatana na Makamishna, Kwanza Balozi Mohamed Ramia Abdiwawa, ambaye nadhani ndio Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Catherine Kivanda Kamishna, Mheshimiwa Steven Zakaria Mwaduma Kamishna, Mheshimiwa Jecha Salum Jecha, Kamishna na Mheshimiwa Sophia Masoud Khamis Kamishna, karibuni sana Makamishna na Mwenyekiti. Pia wapo Tume ya Kurekebisha Sheria wakiongozwa na Mwenyekiti wao Mheshimiwa Prof. Ibrahim Juma, Mheshimiwa Edward Mwisumo Jaji mstaafu. Niongezee pia ni Mbunge mstaafu na Naibu Waziri Mstaafu. Tunafurahi sana kukuona Jaji Edward Mwisumo na ukiendelea kuhudumia umma wa Tanzania. Mheshimiwa William Mdundo Kamishna, Mheshimiwa William Maina, Jaji mstaafu na niongezee kuwa ni Katibu wa Bunge Mstaafu. Aliwahi kuwa Katibu wa Bunge hili Tukufu. Karibu sana Jaji Maina *is a pleasure to see you here today*. (*Makofi*)

Pia Mheshimiwa Agusta Bubeshi ambaye ni Jaji mstaafu ambaye ni Kamishna. Wapo wageni wengine mashuhuri kama ifuatavyo kwanza binafsi nafurahi sana kumwomba hapa Mheshimiwa Asha Bakari Makame, Mheshimiwa Asha Bakari Karibu sana hapa Bungeni kwa niaba ya Wabunge nakupongeza sana kwa kuchaguliwa kwenye uchaguzi juzi kuwa Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania na ninatumaini unaendelea kupona majeraha yanayotokana na misuguano ya shughuli za kampeni basi Mungu akujalie ili usaidiane kuongoza Jumuiya hiyo vizuri, ahsante na karibu sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa tuna bahati kweli leo tunao wageni kutoka nje nao ni Wabunge kutoka nchi rafiki na Ndugu ya Ethiopia hawa Wabunge wapo nane. *We are very happy to welcome you Honourable Members of Parliament from friendly country of Ethiopia, it is a pleasure to have you with us. We know that we learn from each other and because our eventual aim is total unit of Africa, is indeed a pleasure for us to be here with you. Feel at home and please welcome.* (*Makofi*)

Wapo pia sasa Madiwani wa Halmashauri ya Mpanda ni wageni wa Wabunge wote wa Wilaya ya Mpanda hii ni pamoja na Mheshimiwa Pinda ambaye hivi sasa naona anamazungumzo mazito na Mzee Ngombale Mwiru, lakini ndio mambo ya TAMISEMI anachota uzoefu wa Mzee pale. Waheshimiwa kutoka Mpanda karibuni sana majirani zangu si mnajua na mimi natoka Urambo pale kwa hiyo tunafurahi sana kuwakaribisha hapa na tunawatakia shughuli njema na safari njema mtakaporejea, karibuni sana. (*Makofi*)

Madiwani na Makatibu Kata wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya ni wageni wa Mheshimiwa Benson Mpesya, karibuni sana Waheshimiwa Madiwani wa Jiji la Mbeya tunafurahi sana kuwakaribisha hapa na mtusalimie huko Mbeya mtakaporejea. Mheshimiwa Maida Abdallah anao wageni wake ambao ni kama ifuatavyo Mheshimiwa Masoud Abdallah mdogo wake na ndugu Anuari Said Mwanawe, karibu sana babu nadhani kwa leo ndio mgeni mdogo sana kwa umri kuliko wote. Tunao pia wanafunzi 41 kutoka Shule ya Msingi Kizota, Dodoma pamoja na walimu wao, ahsante sana vijana na walimu tunafurahi sana mnapowaleta vijana kujionea wenyewe badala ya kusoma kwenye vitabu jinsi ambavyo Bunge linavyofanya kazi yake, karibuni sana. (*Makofi*)

Kuhusu vikao, Mheshimiwa Mussa Azan Zungu Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje ameniomba niwatangazie Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje kuwa kutakuwa na Kikao cha Kamati leo hii tarehe 30 Julai, 2007 saa tano na nusu asubuhi chumba namba 133, Mheshimiwa Job Ndugai Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Asili na Mazingira ameniomba niwatangazie wajumbe wa Kamati ya Maliasilia na Mazingira kwamba leo saa saba mchana katika ukumbi namba 219, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi ameniomba niwatangazie Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati ya Fedha na Uchumi kuwa leo tarehe 30 kutakuwa na kikao saa tano asubuhi ukumbi namba 231.

Waheshimiwa Wabunge, nina udhuru ambao utanilazimisha nitoke nikitumaini kwamba jioni saa 11 tunaweza kuwa pamoja, kwa sasa hivi ningemwomba Mwenyekiti Job Ndugai aje kwenye kiti ili kuendeleza shughuli ambazo zinafuatia. (*Makofi*)

*Hapa Mwenyekiti (Mheshimiwa Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti.*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2007/2008
### Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia Taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni leo na kusoma na Mheshimiwa Ngalinoma Mbunge wa Kalenga kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa George Malima Lubeleje Mbunge, naomba kutoa hoja kwamba

sasa Bunge lako Tukufu likubali kujadili na hatimaye kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria, kwa mwaka wa fedha 2007/2008.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa dakika moja nikukatize kidogo, kuna tangazo muhimu hapa kutoka kwa *Chief Whip* nimeona nilitoe sasa hivi kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wengine wanaenda kwenye kamati, Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa leo saa tisa mchana katika Ukumbi wa Kilimani ili kusikiliza hotuba ya Mheshimiwa Rais ya mwisho wa mwezi naomba kuwasilisha taarifa hii, kwa hiyo narekebisha ni kesho. Mheshimiwa Waziri anomba uendelee.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa uongozi wake mahiri ambao umeipeleka nchi mbele kwa kasi kama alivyoahidi katika kauli mbiu ya Ilani ya Uchaguzi ya Ari mpya, Nguvu mpya na Kasi mpya. Pili, napenda pia kuishukuru kwa dhati Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kwa michango na ushauri ambao imekuwa ikitoa kwa Wizara yangu. Mara kwa mara Kamati imekuwa mstari wa mbele katika kutembelea maeneo mbalimbali ya Wizara na kutoa ushauri mzuri ambao umeisaidia Wizara yangu kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Hivyo naishukuru sana Kamati kwa mchango wake wa maelekezo iliyotoa wakati wa kupitisha bajeti ya Wizara yangu ilipokaa tarehe 31 Mei, 2007. Michango na ushauri wao umekuwa na manufaa kwangu katika kuongoza Wizara hii na pia umesaidia sana kuiboresha hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Hanang kwa ushirikiano wao wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Kutokana na majukumu yangu, wapiga kura hao wamekuwa hawanioni mara kwa mara kama ambavyo wangependa kuniona nikishirikiana nao katika shughuli za maendeleo, lakini wamekuwa wanatekeleza Ilani bila kunisubiri.

Naomba waendelee na moyo huu wa uvumilivu na pia naahidi nipatapo nafasi, nitajitahidi kuziba pengo hilo kwa namna nyingine na kufika mara nyingi zaidi Jimboni kushirikiana nao katika kuleta maendeleo ya Jimbo letu, ili kila mmoja wetu awe na maisha bora. Vile vile, naomba nitumie fursa hii kumshukuru kwa dhati sana mume wangu Prof. Joseph Nagu na familia yetu kwa kunitia moyo na kwa uvumilivu wao waliouonesha kwa kukubali kutokuwa nao karibu mara kwa mara kutokana na kutekeleza majukumu yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa hotuba yake ambayo imeelekeza mwenendo wa utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa mwaka 2007/2008. Napenda kukupongeza wewe mwenyewe Mheshimiwa Mwenyekiti, Spika na Naibu Spika na Mwenyekiti Mheshimiwa Jenista Mhagama, kwa uongozi wenu mahiri wa vikao vya Bunge. Katika mwaka huu shughuli za Bunge zimeenda kwa viwango vya juu na spidi kama mlivyoahidi pale mwanzo bunge lilipozinduliwa. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Dr. Juma Khalifa Ngasongwa, Mbunge Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na

Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, Mbunge Waziri wa Fedha kwa hotuba zao zilizobainisha misingi na mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Taifa na Bajeti kwa mwaka 2007/2008. Hali kadhalika, nawapongeza Mawaziri wenzangu walionitangulia kwa hotuba zao nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dr. Asha – Rose Migiro kwa kuteuliwa kwake kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Wananchi wa Tanzania wana imani kubwa na uwezo wake kiutendaji na hivyo hawana shaka kuwa atatekeleza kazi zake kwa ufanisi mkubwa. Ninamtakia afya njema na mafanikio makubwa katika wadhifa huo mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie pia fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya walioteuliwa au kuchaguliwa kuwa Wabunge wa Bunge lako hili Tukufu. Wabunge hao ni, Mheshimiwa Yusuf Rajab Makamba Mbunge wa Kuteuliwa (CCM), Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura Mbunge wa Jimbo la Tunduru (CCM) na Mheshimiwa Bibi Florence Essa Kyendesya Mbunge wa Viti Maalum Wanawake (CCM).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi kilichopita kumetokea ajali na majanga mbali mbali yaliyosababisha kupotea kwa maisha na mali za watu pamoja na kuliletea Taifa hasara kubwa. Napenda kuchukua fursa hii kupitia Bunge lako tukufu kutoa pole na salamu zangu za rambirambi kwa familia ya Hayati Mheshimiwa Juma Jamaldini Akukweti Mbunge aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, shughuli za Bunge, na Mbunge wa Jimbo la Tunduru. Natoa pia pole kwa ndugu na jamaa wa familia zote zilizopatwa na misiba katika ajali hiyo ya ndege. Napenda pia kuipa pole familia ya Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia, Mbunge aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum (CCM) aliyefariki ghafla kwa maradhi. Ningependa pia kutoa pole kwa wafiwa wote waliopoteza ndugu zao katika ajali nyingi za barabarani na majini na majanga mbalimbali yaliyotokea yakiwemo ya ugonjwa wa homa ya bonde la ufa na ukame. Mungu azilaze pema peponi roho za marehemu, Amin.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuzungumzia kuhusu hoja iliyojitokeza kuhusiana na jina la Wizara yangu, tangazo la Serikali lina jina la kiingereza la Wizara ambalo ni *Ministry of Justice and Constitutional Affairs,* tafsiri ya mamlaka yenye uwezo wa kuamua majina Wizara ni Wizara ya Katiba na Sheria. Kwa kuwa Katiba ndio sheria mama imeonekana inafaa itanguliwe kutajwa halafu ndio ifuatwe na neno Sheria ambayo ni ndogo kwake, hivyo ndio tafsiri ya mwenye mamlaka ya kuzipa majina Wizara na ninaomba kutoka sasa Wizara hii ijulikane kama Wizara ya Katiba na Sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Majukumu ya Wizara, majukumu ya msingi ya Wizara yangu ni kuhakikisha nchi yetu inazingatia Utawala wa Kisheria kwa kusimamia utoaji haki, Hifadhi ya Katiba, Kutoa ushauri wa kisheria kwa Serikali na Taasisi zake, Kusimamia hifadhi ya haki za Binadamu na kuhakikisha sheria zetu zinaenda na wakati. Ni jukumu la Wizara yangu kuona kuwa nchi yetu ina utawala wa sheria. Utawala wa sheria unahitaji wale wanaosimamia sheria, ambao ni Serikali na vyombo vyake vya dola, wanasimamia sheria kwa ufanisi mkubwa na dhati kabisa. Kwa upande wa wananchi,

wao wanapaswa kufuata na kuheshimu sheria zilizopo ili Taifa letu liwe la amani, utulivu na maelewano. Hili linafanyika kwa kuhakikisha kuwa wavunjaji wa sheria wanakamatwa na kuadhibiwa kwa wakati. Wananchi wanataka waone wahalifu wakikamatwa na kuadhibiwa ili kuzuia uchukuaji wa sheria mikononi, kwa watu kuwaadhibu wahalifu wenyewe. Majukumu haya makuu yanatekelezwa kupitia taasisi mbalimbali zilizopo chini ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utoaji haki linasimamiwa na Mahakama ya Tanzania ambayo husikiliza na kuyatolea maamuzi mashauri yote ya madai na ya jinai katika ngazi mbalimbali za Mahakama kuanzia za Mwanzo hadi Mahakama ya Rufani. Mahakama pia ndiyo yenye mamlaka ya kutafsiri Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inalo jukumu la kuishauri Serikali na Taasisi zake katika masuala yote ya kisheria kama ambavyo imeainishwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya mwaka 2005 na Sheria nyingine mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Kurekebisha Sheria hufanya tafiti za Sheria mbalimbali ili kuhakikisha zinakwenda na wakati na kutoa mapendekezo kwa lengo la kulinda na kuihifadhi jamii na kuendeleza maslahi ya nchi. Tume hii pia hutoa elimu ya sheria kwa umma ili wananchi wazielewe na kuzitekeleza ipasavyo. Aidha, jukumu la kuhamasisha na kuhifadhi haki za binadamu pamoja na kulinda misingi ya utawala bora husimamiwa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini ndiyo yenye jukumu la kusimamia kwa haki na ufanisi kumbukumbu muhimu za maisha ya binadamu, ufilisi na udhamini ili kuchangia katika maendeleo ya taifa. Katika kutekeleza azma hiyo,huduma zitolewazo na Wakala huo ni kusajili ndoa, vizazi na vifo, watoto wa kuasili, kusimamia mirathi, kuendesha shughuli za ufilisi na upokezi rasmi. Aidha, Wakala pia ni mdhamini wa mali isiyo kuwa na mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa majukumu haya unaongozwa na Dira ya Wizara ambayo ni Haki kwa Wote na kwa Wakati. Dira hii inalenga kuwa na mfumo wa sheria unaozingatia utoaji haki kwa ufanisi katika jamii na vile vile kujenga utamaduni wa utawala wa sheria unaochochea maelewano na kupunguza au kuondoa migogoro na hivyo kutoa huduma bora zaidi kwa watu wote na kwa wakati. Mambo ambayo ndiyo msingi madhubuti wa amani, utulivu, mshikamano na utengamano wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada ya kuboresha muundo wa Mahakama yetu, mnamo tarehe 5 Januari, 2007, Serikali imefanya uamuzi wa kuihamisha Mahakama ya Kazi, kutoka Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana na kuifanya Kitengo cha Mahakama Kuu ya Tanzania. Jukumu kuu la kitengo hicho ni kutatua migogoro ya kiajira na kikazi, kujenga uhusiano mwema kati ya waajiri na wafanyakazi na kudumisha utulivu mahali pa kazi ili kusisimua uzalishaji na kuongeza tija, pato na maisha bora kwa wananchi wote na taifa zima. Aidha, uamuzi huu utaondoa

mkanganyiko uliokuwepo kuhusu nafasi na mamlaka ya Mahakama ya Kazi pamoja na uhusiano wake na Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti 2006/2007, utoaji na uimarishaji haki, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2006/2007, Wizara yangu iliidhinishiwa jumla ya shilingi 66,849,887,000 ili kutekeleza malengo yaliyoainishwa katika Mpango wa Wizara. Malengo hayo yalihusu uimarishaji wa utoaji haki nchini uliotokana na; uendeshaji wa kesi na mashtaka na kupunguza mlundikano wa kesi mahakamani; Kutoa ushauri wa kisheria kwa Serikali na Taasisi zake; Uandishi wa sheria na tafiti za sheria; Haki za Binadamu, Utawala Bora na Mambo ya Katiba; Uimarishaji wa Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu (sasa Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini); Mafunzo na Ajira; Uboreshaji wa Mazingira ya Kazi; Uandaaji wa Sera ya Sekta ya Sheria; Kusimamia Utekelezaji wa Programu ya Kuboresha Sekta ya Sheria; na Utekelezaji wa programu zinazohusiana na janga la ukimwi na vita dhidi ya rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uendeshaji wa kesi na kupunguza mlundikano wa kesi mahakamani, Wizara yangu imeendelea kuchukua hatua kadhaa kwa ajili ya kuharakisha usikilizaji wa kesi, migogoro na mashauri. Hatua hizo ni pamoja na kuongeza idadi ya watendaji katika utoaji haki, ambapo umefanyika uteuzi wa Majaji 23, 2 wakiwa wa Mahakama ya Rufani na 21 wa Mahakama Kuu. Uteuzi huu wa Idadi kubwa ya Majaji, ambao haujawahi kufanywa tangu uhuru, utaongeza uwezo wa Mahakama ya Rufani wa kuendesha vikao vitatu kwa wakati mmoja badala ya viwili. Aidha, vikao vya Mahakama Kuu vinatarajiwa kuongezeka hadi kufikia 102 badala ya 88 kwa mwaka vilivyopangwa kuendeshwa kabla ya uteuzi huo. Hata hivyo, hadi kufikia Juni 2007, vikao vilivyofanyika ni 98 badala ya 88 ambalo ni ongezeko la asilimia 11.4. Ongezeko hili la vikao bila shaka limeongeza kasi ya usikilizaji kesi na hivyo kupunguza mlundikano wa kesi na msongamano wa mahabusu na wafungwa ambayo ni kero iliyolalamikiwa sana na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza ufanisi, Wizara iliajiri Mahakimu Wakazi 77 na Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo 46. Mahakimu hao wamepangwa kufanya kazi katika mikoa yote. Kwa kuwa ilipangwa kuajiri Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo 105, taratibu zinaendelea kujaza nafasi 69 zilizobaki. Hatua hii itapunguza wingi wa kesi zinazopangwa kwa Hakimu mmoja na hivyo kuongeza ufanisi wa kusikiliza kesi na kutoa hukumu mapema zaidi. Aidha, Mawakili wa Serikali 12 na Makatibu Sheria 7 waliajiriwa na kusambazwa kwenye Kanda za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto kinapanuliwa ili kuongeza idadi ya wahitimu toka 200 hadi 500 kwa mwaka. Inategemewa kuwa wengi kati ya hawa wataajiriwa kama Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na Watumishi wengine katika Mahakama zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati za Kusukuma Kesi za Jinai ni njia muhimu ya kupunguza mlundikano wa kesi. Kamati hizi zimeimarishwa kwa kuzipatia fedha za kutosha ili kuziwezesha kukutana mara moja kwa kila robo ya mwaka. Kamati hizi

ambazo zinahusisha Mahakama, Idara ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Polisi na Magereza hupita na kuyajadili mashauri ya jinai yaliyokaa muda mrefu na kuyapatia ufumbuzi. Utaratibu huu umesaidia sana kuharakisha kesi zinazochelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na uanzishaji wa Kamati za kusukuma kesi, Serikali imeshaweka utaratibu chini ya Sheria ya Utumishi wa Mahakama (*The Judicial Service Act*, *2005*), kwamba mara baada ya kesi kumalizika kusikilizwa, Mahakama inawajibika kutoa hukumu mapema iwezekanavyo, lakini isizidi muda wa siku 90. Ina maana, ndani ya muda wa siku 90, hukumu iwe imeshatolewa. Utaratibu huu ni kwa kesi zote za madai na jinai ambao utasaidia kupunguza muda wa watuhumiwa kukaa mahabusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Majaji Wafawidhi, Mahakimu Wafawidhi na Wakuu wa Kanda za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali walitembelea magereza 63 kati ya 122. Huko walipokea malalamiko ya Mahabusu na Wafungwa na kuyashughulikia ili kuhakikisha kuwa msongamano uliopo magerezani unapungua. Mashauri ya muda mrefu ambayo mashahidi wameshindwa kupatikana kabisa kwa sababu mbalimbali yaliondolewa mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hatua zilizochukuliwa na Mahakama kukabiliana na tatizo sugu la mlundikano wa kesi mahakamani, Idara ya Mkurugenzi wa Mashtaka iliendesha mashauri katika vikao 98 vya Mahakama Kuu katika kanda zote 13. Katika vikao hivyo, kesi 1,111 na rufaa 978 zilisikilizwa. Aidha, jumla ya rufaa 268 zilisikilizwa katika vikao 12 vya Mahakama ya Rufaa vilivyofanyika kwenye vituo sita (6) nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kesi za madai, jumla ya mashauri 1,113 yalipokelewa. Kati ya hayo, mashauri 386 yamesikilizwa na kutolewa uamuzi na mashauri 727 yanaendelea kusikilizwa. Aidha, kesi 36 zinazotokana na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005 zimesimamiwa na kuendeshwa na kati ya hizo, 18 zimemalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Biashara ilishughulikia na kuyamaliza mashauri 140 kati ya mashauri 153 yaliyokuwepo mahakamani hapo, ambayo ni asilimia 91.5 ya mashauri yaliyofunguliwa. Mashauri 13 yanaendelea kushughulikiwa. Mahakama hii imejizatiti kujipanua zaidi kwenda katika mikoa mingine ambayo imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa. Mpaka sasa imeweza kukamilisha ukarabati wa jengo la Mahakama huko Mwanza kwa ajili ya Mahakama ya Biashara. Hii itawawezesha wananchi wa kanda ya Ziwa kupata huduma hii kwa karibu pindi Mahakama hii itakapofunguliwa katika mwaka wa fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Ardhi ilipokea mashauri ya migogoro ya ardhi 1,915 kutoka katika Kanda 13 za Mahakama Kuu na kati ya hizo, kesi 612 zilimalizika. Mahakama hii, ambayo bado ni changa, imeweza kukamilisha majukumu yake hayo pamoja na kuwepo matatizo makubwa ya ufinyu wa bajeti na upungufu wa miundombinu ya majengo na Majaji. Sasa hivi Mahakama hii haina Ofisi ya Makao Makuu na inao Majaji watatu tu wanaosikiliza kesi zote hizo zilizofunguliwa. Inakadiriwa kwamba angalau Majaji watano wanaweza, kwa kuanzia, kumudu kazi za

Mahakama ya Ardhi. Aidha, Mahakama mpya ya Kazi ilipokea mashauri 487. Kati ya hayo, mashauri 116 yalitolewa maamuzi, mashauri saba yalikaziwa hukumu na mashauri 364 yanaendelea kusikilizwa. Kanuni mpya za Mahakama ya Kazi zimekwisha kutungwa na tayari zimeanza kutumika kuanzia tarehe 18 Mei, 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli za kuimarisha mfumo wa utoaji haki ziliendelea vizuri. Utaratibu wa kila Jaji kujipangia ratiba ya usikilizaji mashauri uliendelea kutumika. Ukaguzi wa mara kwa mara katika Mahakama za Mikoa, Wilaya na za Mwanzo ulifanyika. Divisheni ya Mahakama ya Biashara, Ardhi na Kazi ziliendesha vikao mbalimbali mikoani ili kusogeza huduma zao jirani na wananchi na hivyo kuwawezesha watu wetu kuzifikia huduma za mahakama kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kuendesha mashtaka, Wizara yangu imeendelea kufanya juhudi za kuboresha utoaji haki na kusogeza huduma kwa wananchi kwa kuendeleza mchakato wa kutenganisha shughuli za upelelezi na zile za uendeshaji mashtaka. Polisi na Asasi nyingine za upelelezi zitaendelea na jukumu la upelelezi tu na Mkurugenzi wa Mashtaka ataendesha mashtaka. Mawakili 156 na wafanyakazi 27 wa kada nyingine wataajiriwa kwa awamu kufanikisha zoezi hili. Aidha, gari moja limenunuliwa kwa ajili ya kushughulikia mchakato huu. Mchakato wa mapendekezo ya kutunga Sheria mpya ya Kusimamia Mfumo wa Kuendesha Mashtaka umekwishaanza na Waraka wa kutunga sheria hiyo upo katika ngazi za juu za majadiliano Serikalini. Sheria hiyo itakapopitishwa na Bunge hili, mwongozo wa uendeshaji wa mashtaka utakaotumika mara mfumo mpya utakapoanza, utatayarishwa. Tayari maandalizi ya mwongozo huu yanaendelea. Katika kutekeleza majukumu yake ya kawaida, Ofisi za Kanda zinafanyiwa ukaguzi wa kazi mara kwa mara ili kuhamasisha utendaji wa kazi unaozingatia maadili ya kazi na uwajibikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa kisheria, uandishi wa sheria na tafiti za sheria, kazi ya ushauri wa kisheria iliendelea kutolewa katika maeneo yote ya kisheria ya Madai na Jinai. Katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilishiriki katika mchakato wa kupitia mikataba mbalimbali kwa ajili ya kuiboresha kwa maslahi ya Taifa. Katika mchakato wa kupitia mikataba hiyo, Serikali hutumia timu za majadiliano (*Government Negotiating Teams*) zenye wataalamu wa taaluma mbalimbali na hivyo kulinda maslahi ya Taifa. Wataalamu hao huwa wa fani mbalimbali hususan zinazohusika na Sheria, Uchumi, Teknolojia, Kodi, Ajira, Uhamiaji na kadhalika utaratibu huu huwezesha timu hizo kupitia mikataba na kuweka msimamo wa pamoja unaokuwa msingi wa majadiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeendelea kutoa ushauri wa kisheria kwa Serikali kupitia Idara ya Madai na Sheria za Kimataifa. Ofisi hiyo imeiwakilisha Serikali katika kesi za madai katika Mahakama za hapa nchini na za kimataifa na kusimamia majadiliano kwa ajili ya kukwamua miradi mbalimbali ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ili sheria zetu ziende na wakati na zikidhi mahitaji ya utoaji haki, kazi ya uandishi na urekebu wa sheria imeendelea kufanyika katika Idara ya

Uandishi wa Sheria. Kazi hii inajumuisha kuandika miswada mbalimbali ya Serikali, kusimamia uandishi wa sheria ndogo ndogo zinazotungwa na mamlaka mbalimbali kwa mujibu wa Sheria husika, kurekebu sheria na kutafsiri sheria kwa lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2006/2007, jumla ya Miswada ya Sheria 21 imeandaliwa na kupitishwa na Bunge. Wizara pia imesimamia uandishi wa Sheria ndogo ndogo 250 na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali. Sheria 10 zimefanyiwa marekebisho na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali na Sheria nyingine 8 ziko katika hatua za mwisho za kuchapishwa. Aidha, Sheria ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira pamoja na Sheria ndogo ndogo tatu (Tangazo la Serikali namba 89, 144 na 145) za mwaka 2003 zimetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili. Aidha, toleo la Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la mwaka 2007 la tafsiri ya lugha ya Kiingereza liko katika hatua za mwisho za uchapishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha kwamba sheria zetu zinakidhi mahitaji ya mabadiliko yanayoendelea kwa haraka katika nyanja za uchumi, kijamii na teknolojia, Tume ya Kurekebisha Sheria imeendelea kufanya shughuli za utafiti wa sheria kwa ufanisi mkubwa ili kukidhi mahitaji ya mabadiliko hayo. Tume ipo katika hatua ya mwisho ya kukamilisha ripoti yake kuhusu sheria na rasimu za utafiti wa sheria ili kuimarisha ushindani katika biashara *(Competition Law Project).*

Pia rasimu ya mwisho ya ripoti ya Uhamishaji wa Teknolojia na Miliki ya Ugunduzi (*Transfer of Technology and Patents Protection*) inakamilishwa, tayari kwa kupitishwa na Tume. Inatarajiwa kwamba taarifa hiyo itakamilika na kuwasilishwa katika mwaka huu wa fedha. Aidha, utafiti wa kina juu ya uanzishaji wa sheria ya kusimamia Teknolojia ya kutambua chembechembe za vinasaba (*DNA*) umekamilika na warsha ya kukusanya maoni ya wadau imefanyika. Maoni yaliyokusanywa katika warsha hizo yatajumuishwa kwenye ripoti ya mwisho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukidhi mahitaji mahsusi ya kijamii nchini, Tume ya Kurekebisha Sheria pia ilifanya utafiti wa awali na kupendekeza marekebisho ya Sheria za mila (*Customary Law*) kwa nia ya kuondoa zile zinazowakandamiza wanawake. Ripoti ya awali imeshaandaliwa ambayo itawasilishwa kwenye warsha ya wadau ili kupata maoni yao. Hali kadhalika, ripoti ya awali juu ya marekebisho ya Sheria ya watu wenye ulemavu imeandaliwa na itajadiliwa na wadau hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamiaji wa kesi za katiba, kesi zinazohusu Katiba na Haki za Binadamu, ambazo zimechukua sura mpya kwa kuhusisha pia mashauri yanayohusu Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ziliendelea kusimamiwa. Jumla ya mashauri 23 yalifunguliwa Mahakamani na kushughulikiwa. Kati ya mashauri haya, 12 yalikuwa ni mapya yaliyofunguliwa mwaka 2006/2007 na mashauri 11 ni yale yanayoendelea kusikilizwa. Mpaka sasa mashauri 3 yameondolewa Mahakamani, mashauri 5 yanasubiri kutolewa uamuzi na mashauri 15 yaliyobaki yanaendelea kusikilizwa.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliweza kusimamia maombi ya kuzuia Uchaguzi wa Jimbo la Tunduru usifanyike, kuzuia kuapishwa kwa Wabunge wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki na lile la kuwianisha mchakato wa kuanzisha kitengo cha Rufaa cha Mahakama ya Afrika Mashariki. Maombi haya yote yalitupiliwa mbali na Mahakama. Aidha, rasimu ya taarifa ya utekelezaji wa mikataba ya haki za binadamu na utawala bora imekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchunguzi wa malalamiko yanayohusu uvunjwaji wa haki za binadamu, uratibu wa masuala ya Haki za Binadamu ulitekelezwa vizuri. Wizara yangu iliendelea kuiwakilisha Serikali katika chunguzi za Kimataifa za madai ya uvunjwaji wa haki za binadamu. Katika kipindi hiki, Wizara yangu imeshughulikia uchunguzi kuhusu kufutwa kwa adhabu ya kifo, kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali (*NGOs*), katika Tume ya Haki za Binadamu na Watu ya Afrika iliyoko Banjul – Gambia. Mashirika hayo yalitaka Tume hiyo itoe tamko dhidi ya adhabu hii. Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kwamba Tume ya Kurekebisha Sheria imefanya utafiti kuhusu hoja hii na wananchi walio wengi walitaka adhabu ya kifo iendelee.

Pia Wizara imewasilisha utetezi, kwa niaba ya Serikali, katika shauri la Mkongo aliyedai kupatiwa uraia wa Tanzania baada ya kumuoa Mtanzania na Serikali kukataa kumpa Mkongo huyo uraia wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu pia ina jukumu la kutekeleza Mikataba na Kanuni zinazohusu Haki za Binadamu na Utawala Bora kama zilivyoainishwa na Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika. Taarifa kuhusu Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu wa mwaka 1981, yaani *African Charter on Human and People's Rights* imeandaliwa. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa itawasilisha taarifa hii Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (*African Commission on Human and People's Rights*) inayoelezea hatua zilizochukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu pia imeendelea kutekeleza majukumu yake chini ya mikataba ya kimataifa na kanuni zinazohusu Haki za Binadamu na Utawala Bora. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa imekamilisha taarifa kuhusu utekelezaji wa haki za kiraia na kisiasa, 1966 (*International Convention on Civil and Political Rights*) na itawasilishwa kwenye Baraza la Haki za Binadamu mwishoni mwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imeendelea kukuza, na kulinda Haki za Binadamu na misingi ya Utawala Bora kwa ajili ya kukuza Demokrasia na Utawala wa Sheria. Tume ilipokea malalamiko 4,523 mapya ya uvunjaji wa haki za binadamu. Kati ya hayo, malalamiko 3,149 yameshughulikiwa na kuisha. Kati ya malalamiko yaliyopokelewa, 195 yalitoka Zanzibar. Katika mkakati wa kusogeza huduma karibu na wananchi, Tume imefungua ofisi mbili za kanda huko Lindi na Mwanza. Tume hii pia ilitembelea Wilaya 36 za Tanzania Bara kwa ajili ya kuwaelimisha wananchi na watendaji juu ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na

umuhimu wa kuzingatia misingi ya Utawala wa Sheria. Tume vile vile imekagua jumla ya magereza 35 na vituo vya polisi 53 katika wilaya 33 za Tanzania Bara ili kuona hali za wafungwa na mahabusu, kuangalia kama haki za binadamu na misingi ya utawala bora zinazingatiwa na kufuatilia malalamiko ya wafungwa na mahabusu kuhusu ukiukwaji wa haki hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara yake hiyo Tume imefanya uchunguzi kuhusu malalamiko ya mahabusu na wafungwa. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha wa 2006/2007 malalamiko kutoka kwa mahabusu yalikuwa 226. Mengi ya malalamiko hayo dhidi ya vyombo vya dola yalihusu mambo matatu, nayo ni kubambikiziwa kesi, mashauri kuchelewa kusikilizwa mahakamani na upelelezi wa kesi kuchelewa.

Walalamikaji 39 walipewa ushauri wa kisheria unaostahili, malalamiko 187 yamefuatiliwa na uchunguzi bado unaendelea. Kushughulikia kero za wafungwa na mahabusu ni namna moja ya kujenga utawala wa sheria nchini. Tayari taarifa za ziara za Tume za ukaguzi wa magereza na vituo vya polisi kwa mwaka 2004/2005 zimewasilishwa Serikalini. Taarifa hizi zenye mapendekezo ni dira nzuri kwa Serikali katika kutafuta ufumbuzi wa matatizo kuhusiana na masuala ya haki za binadamu na utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, semina ya elimu ya haki za binadamu na utawala bora ilitolewa kwa Waheshimiwa Wabunge ambapo wengi wetu tulihudhuria. Tume itawahusisha wadau wengine katika kutoa elimu ya Haki za Binadamu ili kuwafikia watu wengi zaidi. Tayari Asasi 18 zimefanyiwa tathmini ya kujua uwezo wake wa kushirikiana na Tume katika kutoa elimu ya Haki za Binadamu na misingi ya Utawala Bora. Shughuli za utafiti, usikilizaji wa hadhara wa ushuhuda kuhusu vitendo vya ukatili dhidi ya watoto na uandishi wa taarifa kuhusu masuala hayo vilifanyika na kuzinduliwa mwezi Oktoba 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uimarishaji wa usajili wa vizazi, ndoa, talaka, vifo na udhamini, katika mwaka wa fedha wa 2006/2007 jumla ya watoto 23 walipata vyeti vya kuasili, miunganisho 106 ya wadhamini ilipatiwa vyeti; mirathi 6 ilipokelewa na kati ya hiyo mirathi 5 ilipatiwa ufumbuzi. Jumla ya ndoa 46,320, vizazi 829,384 na vifo 118,538 viliandikishwa.

Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini ulipanga kukusanya mapato ya shilingi 642,400,000 na imefanikiwa kukusanya shilingi 667,910,319.50 hadi Aprili 2007, ambazo ni sawa na asilimia 104 ya lengo. Ili kuboresha shughuli za usajili, iliyokuwa Idara ya Kabidhi Wasii Mkuu imegeuzwa rasmi kuwa Wakala wa Serikali, na kuzinduliwa tarehe 23 Juni, 2006. Juhudi zinafanyika kuuimarisha wakala ili kuuwezesha kutoa huduma bora kwa wananchi.

Kwa kuanzia, Wakala itapatiwa jengo jipya la Ofisi litakalo jengwa mahali lilipo jengo lake la zamani. Tayari ujenzi wa jengo hilo upo mbioni kuanza na Wakala umekwishahamia katika jengo jingine ili kupisha ujenzi huo. Wakala umeanzisha tovuti

(*www.rita.go.tz*) ili kutumia fursa ya teknolojia kuwafikia wananchi na kuelimisha umma kuhusu huduma wanazotoa.

Sanjari na kuelimisha umma kwa njia ya tovuti, wakala umeshiriki katika matukio matatu ya, wiki ya mtoto wa Afrika iliyofanyika Dodoma mwezi Juni 2007, wiki ya Utumishi wa Umma Dar es Salaam (17-23 Juni 2007) na Maonyesho ya Biashara ya kimataifa, Sabasaba Dar es Salaam (1-10 Julai 2007).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ushiriki huu Wakala umeweza kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kusajili vizazi, vifo, ndoa na talaka, kuasili watoto, masuala ya mirathi, udhamini na ufilisi. Watu wengi wamejitokeza ili kujionea na kujielimisha kuhusu huduma za Wakala. Ili kusogeza huduma kwa wananchi, wakala uko mbioni kuwashirikisha Maafisa Tarafa katika shughuli za usajili wa vizazi na vifo.

Mafunzo yameanza kutolewa kwa maafisa wa Tarafa wa mkoa wa Dodoma ili kuwajengea uwezo kuhusu masuala ya usajili wa vizazi na vifo. Zoezi hili litaendelea nchi nzima, kwa kushirikisha wadau wa maendeleo ambao wameonyesha nia ya kutusaidia katika azma hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha na kuimarisha utendaji wa kazi na kuleta ufanisi na tija katika utoaji wa haki, Wizara iliwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu watumishi wa kada zote za Wizara. Jumla ya watumishi 117 wa Mahakama wamepata udhamini wa kozi ya stashahada ya sheria na 20 wamepata udhamini wa Cheti cha Sheria kwenye Chuo Cha Uongozi wa Mahakama, Lushoto. Watumishi 72 wa kada mbalimbali katika Mahakama walipata mafunzo kulingana na kazi zao. Mawakili wa Serikali 12 wanahudhuria mafunzo ya shahada za uzamili ikilinganishwa na lengo la kusomesha Mawakili 10. Watumishi 64 wa kada nyingine walipata mafunzo ya muda mfupi. Watumishi wapya 22 waliajiriwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kati yao, kumi na mbili (12) ni mawakili, wachumi wawili (2), Afisa Mawasiliano mmoja (1) na saba (7) wa kada nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inaendelea na jitihada za kuboresha mazingira ya kazi katika Ofisi na Taasisi zake zote. Kwanza kabisa, kazi ya ukarabati wa jengo la muda la Mahakama ya Rufani imekamilika na tayari Mahakama ya Rufani sasa inafanya kazi katika makazi yake ya muda. Hili limeongeza nafasi katika jengo la Mahakama Kuu kukidhi ongezeko la Majaji zaidi na hivyo kuongeza uwezo wa Kanda ya Dar es Salaam na Makao Makuu ya Mahakama Kuu kusikiliza kesi nyingi zaidi kwa wakati mmoja. Pili, Ujenzi wa jengo jipya la Mahakama Kuu huko Bukoba unaendelea vizuri na maandalizi ya ujenzi wa jengo jipya la Mahakama Kuu, Shinyanga yamefikia hatua za mwisho. Hii ni katika kukamilisha jitihada ya kufungua Mahakama katika kila Mkoa Tanzania.

Tatu, ukarabati wa jengo kwa ajili ya Mahakama ya Biashara Kanda ya Mwanza unaendelea vizuri hivyo kupanua shughuli za Mahakama ya Biashara kwenda Mwanza. Vile vile, ujenzi wa jengo jipya la makao makuu ya Mahakama ya Biashara kwa ajili ya upanuzi umefikia hatua nzuri. Ujenzi wa majengo ya Mahakama ya Wilaya ya Hai

umekamilika na kupatiwa samani na ujenzi wa majengo ya Mahakama za Wilaya za Bunda, Iringa Mjini, Mpwapwa, Mtwara Mjini, Kongwa, Mbalali, na Mikindani unaendelea. Aidha, jengo la Mahakama ya Hakimu Mkazi Sumbawanga limejengwa na huko Manyara ujenzi unaendelea. Halikadhalika, jumla ya majengo ya Mahakama za Mwanzo 15 yamejengwa na 54 kukarabatiwa. Mahakama za Mwanzo zilizojengwa au kukarabatiwa kwa kushirikisha nguvu za wananchi ni pamoja na Kishapu (Maganzo), Iramba (Igungumo Mjini), Mbinga (Tingi na Chiwanda), Tarime (Tarime Mjini), Serengeti (Mugumu), Bunda (Ikizu), Ngudu (Ngudu Mjini) na Bunda (Bunda Mjini). Tunawashukuru sana wananchi wa maeneo haya kwa uzalendo wao na tunaomba wale wa maeneo mengine waige mfano huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko Mafia kiwanja kimepatikana kwa madhumuni ya kujenga jengo la Mahakama ya Wilaya na lile la Mahakama ya Mwanzo. Majengo haya yatajengwa mara tupatapo fedha, kwa sasa hivi shughuli za Mahakama ya Wilaya ya Mafia hufanyika katika ofisi mojawapo katika jengo la Mahakama ya Mwanzo Kilindoni. Utaratibu wa kupeleka Hakimu wa Wilaya wa kudumu unaendelea. Ofisi ya Kanda ya Mbeya ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilifanyiwa ukarabati na nyingine kupatiwa vitendea kazi. Majengo ya ofisi mbili za Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora yamejengwa, moja Lindi na jingine Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Wizara yangu iliendelea na mpango wa kuimarisha utendaji kazi wa watumishi wake. Katika kutimiza azma hii, Wizara iliweza kununua vitendea kazi ikiwa ni pamoja na ununuzi wa magari matatu kwa ajili ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, magari 30 kwa ajili ya Majaji na magari 4 kwa ajili ya ukaguzi wa Mahakama za Mwanzo. Aidha, Mahakama zote ishirini na moja za mikoa na Mahakama za wilaya 49 kati ya 88 zimepatiwa magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Wizara yangu iliendelea kutekeleza Programu ya Kisekta ya Kurekebisha na Kuboresha Mfumo wa Sheria Nchini. Katika uratibu wa utekelezaji wa programu hii, Wizara imeimarisha ofisi ya uratibu wa programu kwa kuajiri wataalamu 6 na wasaidizi 4. Aidha, taasisi zinazotekeleza programu hii zimeandaa mpango wa mwaka wa utekelezaji wa programu. Mafunzo yametolewa kwa waratibu toka taasisi za utekelezaji ili kuwawezesha kuandaa mpango na bajeti kulingana na taratibu za kuhusisha sekta mbalimbali **(***Multi Sectoral Implementation Approach***)**. Aidha, mafunzo ya mabadiliko katika uongozi (*Change Management***)** katika kusimamia utekelezaji wa Programu yalitolewa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Ujerumani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfuko wa pamoja (*basket fund*) wa fedha za maendeleo ya programu umeanza kutumika katika mwaka uliokwisha wa fedha. Utekelezaji wa Programu ya Kuboresha Sekta ya Sheria, kwa mara ya kwanza, umeanza kutumia utaratibu wa mfuko wa pamoja (*basket fund*) kwa fedha za maendeleo. Hatua hii imewezesha kutumia fedha za maendeleo baada ya kukubaliana na wadau wa maendeleo **(***Development Partners*) kuhusu taratibu za usimamizi na udhibiti wa matumizi ya fedha za programu na hivyo kuondoa matatizo ya rasilimali na fedha ambayo kwa muda mrefu, yameikabili programu na kuathiri maendeleo ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu iliendeleza jitihada za kuondoa upungufu katika mfumo wa kisheria wa kutatua migogoro ya kibiashara **(***Commercial Dispute Resolution*) chini ya Programu ya Kuboresha Mazingira ya Biashara Tanzania – MKUMBITA – *BEST*). Tayari Wizara imeanza utekelezaji wa maboresho ya mfumo wa sheria za madai ambao, pamoja na mambo mengine, unahusisha kuzifanyia mapitio Sheria ya Mwenendo wa Kesi za Madai (*Civil Procedure Act*), Sheria ya Ushahidi **(***Evidence Act***)**, Sheria ya Mawakili **(***Advocates Act),* Sheria ya Mahakama za Mahakimu (*Magistrates Courts Act***)** na Sheria ya Madalali wa Mahakama *(Court Brokers & Process Servers*). Lengo la maboresho hayo ni kuhakikisha kwamba mfumo wetu wa mashauri ya madai unaendana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wanaelewa nafasi ya pekee ya Wizara yangu katika mapambano dhidi ya rushwa. Idara ya Mkurugenzi wa Mashtaka ambayo ndiyo msimamizi mkuu wa mashtaka yote nchini imeendelea kusimamia kwa karibu mashtaka dhidi ya watuhumiwa wa makosa ya rushwa. Ofisi hiyo kwa kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia Rushwa imeshughulikia majalada 19 ya rushwa. Kati ya hayo, majalada 15 yalionekana yanafaa kufunguliwa kesi Mahakamani na manne yalionekana hayawezi kufunguliwa kesi Mahakamani, hivyo yalifungwa. Majalada yaliyofungwa ni yale ambayo ushahidi uliokusanywa dhidi ya watuhumiwa kuthibitisha tuhuma dhidi zao, ulikuwa hautoshi. Aidha, ili kujenga maadili, viongozi wote Wizarani walishiriki katika warsha kuhusu kazi na majukumu ya Kamati ya Maadili iliyoundwa na Ofisi ya Rais, Kitengo cha Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kwa kutambua kwamba UKIMWI ni janga la kitaifa, imeendelea na mchakato wa kutunga Sheria ya kudhibiti UKIMWI. Baada ya kupokea maoni ya wananchi na wadau kuhusu kutungwa kwa sheria hiyo, Wizara yangu imetayarisha rasimu ya Mswada wa sheria hiyo.

Aidha, Kamati za kudhibiti UKIMWI zimeundwa katika kila Taasisi ya Wizara. Halikadhalika, warsha kuhusu masuala ya Ukimwi zimefanyika kwa viongozi na watumishi mbalimbali wa Wizara katika mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Lindi na Pwani. Aidha, Wizara ilishirikiana kwa karibu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma katika kuadhimisha Siku ya UKIMWI Duniani iliyofanyika Mkoani Mara mwezi Desemba, 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoahidi katika hotuba yangu ya mwaka jana, Wizara yangu imedhamiria kuwa na sera itakayokuwa dira ya kuongoza utekelezaji wa majukumu katika sekta hii. Zoezi la uandaaji wa Sera ya Sekta ya Sheria liliendelea na linatarajiwa kukamilika ifikapo mwishoni mwa mwaka huu wa 2007. Rasimu ya Sera hiyo iko tayari na imeshaanza kujadiliwa katika vikao rasmi vya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Sheria ni msingi muhimu katika kufanikisha utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania. Licha ya kupata mafanikio ya kuridhisha katika kutekeleza shughuli zilizopangwa, Wizara

ilikabiliwa na changamoto nyingi zilizosababisha kutotekelezwa kikamilifu na kwa ufanisi baadhi ya majukumu yake.

Baadhi ya changamoto hizo ni: upungufu wa nyenzo za kufanyia kazi na uduni wa mazingira ya kazi kwa wafanyakazi wa Sekta ya Sheria; upungufu wa majengo na ofisi; upungufu wa wafanyakazi wenye uzoefu katika taaluma ya sheria yaani majaji, mahakimu, mawakili wa Serikali na kada nyingine; kuchelewa kuanzishwa kwa mfumo wa mawasiliano ndani ya Mahakama kwa ajili ya kusimamia kesi na pia kuunganisha Mahakama na Masjala zake zote kwenye vyombo vya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ni pamoja na maslahi na mazingira ya kazi duni yanayosababisha baadhi ya watumishi wenye taaluma na uzoefu kuacha kazi na kutafuta maslahi bora zaidi. Pia kuna uhaba wa mafunzo muhimu ili kuwafanya watumishi wa Wizara kuendana na changamoto za mabadiliko yanayotokana na maendeleo yanayotokea kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka uliopita, napenda nieleze kwa kifupi msisitizo wa vipaumbele vya Wizara yangu kwa mwaka wa 2007/08 katika kuhakikisha kwamba Dira na Malengo yake yanatimizwa kwa kujenga mfumo wa sheria unaozingatia utoaji wa haki. Katika mwaka huu wa fedha Wizara yangu imejizatiti kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

(i) Kuhakikisha kwamba miundombinu katika sekta ya sheria inaimarika ili kuwezesha huduma za kisheria kuwafikia wananchi wengi zaidi kwa ukaribu zaidi;

(ii) Kuhakikisha idadi ya watumishi inaongezeka ili kuongeza uwiano wa Majaji, Mahakimu, Mawakili na Wanasheria kwa kiwango cha kuridhisha ili waweze kumudu majukumu yao ya kutoa haki;

(iii) Kuhakikisha kwamba uwezo wa kitaaluma wa watendaji wa kada zote unaongezeka sambamba na ongezeko na mabadiliko yanayotokea katika nyanja mbalimbali za kiuchumi, kijamii na kiteknolojia;

(iv) Kuiwezesha taaluma na taasisi za sheria kumudu mahitaji mahususi ya kijamii kwa makundi mbalimbali kama vile watu wenye ulemavu, wanawake, watoto na wanaotumia teknolojia mpya ya habari;

(v) Hifadhi ya Katiba na Haki za Binadamu inadumishwa kwa kiwango cha juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka ujao wa fedha 2007/08, Wizara yangu itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kusimamia utawala wa sheria kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 na malengo ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA) ambayo utekelezaji wake unazihusisha taasisi zote zilizo chini ya Wizara yangu na malengo ya maendeleo ya millenia (*Millenium Development Goals).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2007/08, Mahakama ya Tanzania itaendelea na mkakati wake wa kupunguza mlundikano wa kesi Mahakamani. Katika kufanikisha lengo hili, ujenzi wa majengo ya Mahakama Kuu kanda za Bukoba na Shinyanga; Mahakama ya Mkoa wa Manyara; na Mahakama ya Wilaya ya Bunda utaendelea. Vile vile, jengo la Mahakama ya Wilaya ya Mpwapwa linalotarajiwa kukamilika katika mwaka huu wa fedha litapatiwa samani. Mpango Endelevu wa kujenga na kukarabati majengo ya Mahakama za Mwanzo, ikiwemo ya Kalenga, ulioidhinishwa na Bunge hili utaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** sambamba na ujenzi wa majengo ya Mahakama, Mahakama ya Rufani itaongeza idadi ya vikao kutoka 12 hadi 15 na Mahakama Kuu toka 88 hadi 102. Migogoro ya ardhi, ajira na biashara itaendelea kutatuliwa kupitia vitengo vya Mahakama Kuu. Aidha, Mahakama itahakikisha kwamba vikao vyake vya kila siku katika Mahakama Kuu, Mahakama za Mikoa, Mahakama za Wilaya na Mahakama za Mwanzo vitafanyika kwa ufanisi, ili kupunguza mlundikano wa mashauri ya madai na jinai.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** ili kuimarisha mfumo wa utoaji na upokeaji wa habari ndani ya Mahakama zetu, Mahakama katika mwaka ujao wa fedha itaanzisha tovuti ya Mahakama ya Tanzania. Vilevile, viwango vya taaluma vya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo vitaongezwa kwa kuwapatia mafunzo mbalimbali. Jumla ya Mahakimu 177 na Makarani 25 wa Mahakama hizo wanategemea kupata mafunzo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Biashara kwa mwaka ujao wa fedha ina lengo la kuhakikisha kuwa ufanisi uliokwishapatikana unaimarishwa na huduma zake zinawafikia wadau wake kwa urahisi na uhakika zaidi. Katika kutekeleza jukumu hilo, masjala mpya itafunguliwa Mwanza baada ya kukamilika ukarabati wa jengo la Mahakama hiyo. Aidha, baada ya kukamilika kwa ujenzi wa jengo jipya la Mahakama Dar es Salaam, shughuli za Mahakama hiyo makao makuu zitapanuka kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2007/08 Mahakama ya Ardhi itaimarisha huduma zake kwa kuanzisha masjala moja ya kanda, Arusha. Hili litasogeza huduma hii karibu zaidi kwa wananchi wa maeneo ya kaskazini mwa nchi. Aidha, mafunzo kwa viongozi watano (5) wa juu, mhasibu mmoja (1), Afisa ugavi mmoja (1) na watumishi wengine kumi na tatu (13) yatatolewa. Jitihada za kuongeza watumishi wa Mahakama ya Ardhi, ikiwa ni pamoja na Majaji, zinafanyika ikiwa ni hatua za kupunguza msongamano wa mashauri ya ardhi yaliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Mahakama ya Kazi, ambayo sasa imeunganishwa na Mahakama Kuu, itakuwa na mifumo miwili ya kushughulikia mashauri ya kikazi na kiajira. Kwanza, katika kipindi cha mpito cha miaka miwili na nusu ijayo, Mahakama ya Kazi itakamilisha na kukazia tuzo za migogoro yote iliyopo chini ya Wizara ya Kazi. Zoezi hili litakamilika kabla ya kuanzishwa Divisheni ya Mahakama ya Kazi. Pili, itaanza kusikiliza mashauri chini ya sheria mpya za kazi namba 6 na namba 7 za mwaka

2004. Jitihada zitafanyika kuongeza ufanisi wa utendaji kazi kwa kuweka mtambo wa kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano katika shughuli zake. Halikadhalika, ukarabati wa jengo la Makao Makuu la Mahakama ya Kazi lililopo Kinondoni utaanza mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka ujao wa fedha 2007/08 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, itaendelea na majukumu ya kuishauri Serikali kuhusu masuala ya kisheria, Katiba, Mikataba, kuiwakilisha katika mashauri mbalimbali ya madai na jinai pamoja na utoaji wa taarifa za Haki za Binadamu na Utawala Bora. Wizara pia itaendelea na jukumu la kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Programu ya Kuboresha Sekta ya Sheria nchini na kukamilisha utayarishaji wa Sera ya Sekta ya Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itaendelea kutoa huduma ya kuandika sheria kwa kuhakikisha Miswada ya Sheria inaandaliwa kwa wakati na kusimamia uandishi wa Sheria ndogo ndogo zinazotungwa na Mamlaka nyingine pamoja na kutafsiri sheria katika lugha ya Kiswahili**.** Jumla ya Miswada 21 na Sheria ndogo ndogo 300 zitaandikwa na Sheria 5 zenye umuhimu wa juu kwa wananchi, zitatafsiriwa katika lugha ya Kiswahili ili wananchi walio wengi waweze kuzielewa. Aidha, jumla ya Sheria 25 zitafanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria, itaendelea kufanya tafiti, uchambuzi na uhuishaji wa Sheria mbalimbali zilizopitwa na wakati kwa kukamilisha taarifa ya Sheria zinazohusu maeneo yafuatayo: (i) Ushindani wa haki katika biashara (*Competition Law*); (ii) Sheria inayolinda Hakimiliki za Ugunduzi na Uhamishaji wa Teknolojia (*Industrial Property and Transfer of Technology*); (iii) Sheria za Mila (*Customary Law*); (iv) Teknolojia ya utambuzi wa chembechembe za vinasaba (*DNA*); (v) Haki za wenye Ulemavu; (vi) Kulipatia ufumbuzi suala la kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi Tanzania Bara; (vii) Sheria ya Uchaguzi; (viii) Adhabu ya kifo, viboko na vifungo vya muda mrefu; (ix) Sheria ya Makosa ya Kujamiana (*Sexual Offences (Special Provisions) Act*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2007/2008, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kusimamia masuala ya Haki za Binadamu na misingi ya utawala bora kwa kukamilisha uchunguzi wa mashauri ambayo hayakukamilika na kufanya uchunguzi kwa malalamiko mapya. Pia Tume imepanga kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya Haki za Binadamu, wajibu kwa jamii na misingi ya Utawala Bora kwa wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora pia itaimarisha ofisi yake iliyopo Zanzibar na matawi ya ofisi za Mwanza na Lindi. Tume vilevile itapitia sheria zilizopo na zinazotungwa ili kutoa mapendekezo kwenye mamlaka husika iwapo Sheria hizo zitaonekana kukinzana na Haki za Msingi. Watumishi wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora watapatiwa mafunzo ya kuwaendeleza kwa

ajili ya kukuza taaluma zao na kutumia mbinu za kisasa katika utendaji. Aidha, Tume itaendelea kufanya ukaguzi wa magereza, vituo vya polisi na sehemu nyingine wanamoshikiliwa mahabusu na wafungwa ili kuhakikisha kuwa haki zao za msingi zinahifadhiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** mwaka wa 2007/08, Wakala wa usajili, ufilisi na udhamini utaboresha mazingira yake ya kazi katika ngazi zote zinazoshughulikia usajili, ufilisi na udhamini. Wakala umepanga kutoa mafunzo kwa watendaji wa ngazi za wilaya, vijiji na wadau mbalimbali kuhusu huduma zitolewazo na wakala kwa jamii nzima ya Tanzania kwa kutumia warsha, mikutano, semina, tovuti yake na vyombo vingine vya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokwishaeleza, majukumu yanayoikabili Wizara yangu ni mengi na vipaumbele ni vingi vilevile. Mojawapo ya vipaumbele hivyo ni utekelezaji wa Programu ya Kuboresha Sekta ya Sheria. Chini ya programu hii Wizara yangu itaunganisha nguvu ili kuboresha miundombinu ya utoaji haki na utawala wa sheria katika taasisi zinazotoa haki katika wizara husika. Katika mwaka huu wa fedha, Wizara yangu chini ya programu hii itatekeleza ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Wizara, ujenzi wa jengo jipya la Mahakama Kuu Musoma, ujenzi wa Mahakama ya wilaya ya Kiomboi na Ujenzi wa mahabusu tatu katika Kanda za Arusha, Mwanza na Tanga. Ukarabati wa Mahakama za Mwanzo pamoja na ukarabati wa shule ya watoto watukutu iliyopo Mbeya utafanyika. Mahakama zitakazokarabatiwa ni zile za Masoko Wilaya ya Rungwe, Ilalangulu Wilaya ya Tabora, Shelui wilaya Iramba, Bareko Wilaya ya Kondoa, Kirua Vunjo Wilaya ya Moshi na Kilolo Wilaya ya Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chini ya programu hii Wizara yangu pia itaboresha Mafunzo ya Taaluma ya Sheria kwa kuanza kutekeleza mpango wa mafunzo kwa vitendo. Kufuatia Bunge lako Tukufu kupitisha sheria ya kuanzisha Taasisi ya Mafunzo ya Sheria kwa Vitendo Tanzania (*Law School of Tanzania Act* 2007), Wizara yangu ipo katika hatua za mwisho kufungua Taasisi hiyo jijini Dar es Salaam. Tayari yamefanyika makubaliano na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ili Taasisi hiyo ianze kazi zake katika majengo ya Chuo hicho sehemu ya Mlimani, wakati matayarisho ya ujenzi wa majengo ya kudumu ya Taasisi hiyo yakiendelea. Madhumuni ya kuanzisha taasisi hii ni kuhakikisha kuwa wanasheria wanaofanya kazi hapa nchini wanapata elimu bora ya vitendo inayoendana na mazingira ya nchi yetu na utandawazi uliopo duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato wa kutenganisha kazi ya mashtaka na ya upelelezi ni eneo muhimu katika kuboresha utoaji haki kwenye eneo la kuadhibu wahalifu. Kwa muda mrefu Serikali imekuwa katika mchakato wa kuboresha kazi ya upelelezi na uendeshaji mashtaka ili kuongeza uwajibikaji *(accountability*) na taaluma (*professionalism)*. Juhudi hizi ni katika lengo la kuimarisha utoaji wa haki, kusimamia kwa ufanisi haki za watu na kuongeza kiwango cha watu kuheshimu sheria ambavyo pia ni mihimili ya utawala wa sheria. Mchakato wa kutenganisha shughuli za upelelezi na uendeshaji mashtaka kwa polisi na asasi nyingine za upelelezi (*Civilianization of Prosecution*), umeanza. Mpango huu utekelezaji wake utaanza kwa awamu kwa kuanzia

katika mikoa sita anzilishi ya Arusha, Dar es Salaam, Mwanza, Ruvuma, Shinyanga na Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** katika mwaka 2007/2008, Wizara itaboresha mazingira ya kazi katika ofisi zake zote kwa kuzipatia vitendea kazi ukiwemo ununuzi wa kompyuta, samani za ofisi, vyombo vya usafiri; ukarabati wa majengo ya Mahakama za ngazi zote na Ofisi za Kanda za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na nyumba za watumishi**.** Katika kuboresha mazingira ya kazi ya Majaji, Sheria ya Maslahi ya Majaji **(***Judge's Remuneration and Terminal Benefits) Act, 2007* ambayo imeanza kutumika tarehe 25 Aprili, 2007 imeweka wazi maslahi ya Majaji wakiwa kazini, wakiwa wamestaafu na pia haki za warithi wao zimetambuliwa kisheria. Aidha, katika jitihada za kuwapatia waheshimiwa Majaji nyumba za kuishi, Wizara imepata jumla ya nyumba 16 toka Wakala wa Majengo ya Serikali na nyumba 23 za kupanga toka kwa watu binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu katika kuboresha na kuimarisha utendaji wa kazi ili kuleta ufanisi na tija katika utoaji wa haki, itawapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu watumishi wa kada mbalimbali katika Wizara kwa kuzingatia taaluma zao na ujuzi maalumu unaohitajika. Aidha, ajira kwa watumishi 263 wa kada mbalimbali zitafanyika kwa mwaka ujao wa fedha. Kwa upande wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto, Wizara itaendelea na mpango wake wa kuongeza idadi ya wanafunzi toka 200 hadi 500 kwa mwaka ikiwa ni pamoja na kuongeza mitaala na kufanya ukarabati wa majengo ili kumudu ongezeko hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza mkakati wa Kitaifa wa kupambana na rushwa, Wizara yangu katika mwaka ujao wa fedha 2007/08 itaendelea kutoa elimu juu ya kupambana na rushwa kwa njia mbalimbali ukiwemo uandaaji wa vipindi vya radio. Aidha, hatua zingine zitakazochukuliwa ni pamoja na kuimarisha Kamati za maadili ambazo zitatoa elimu ya maadili kuhusiana na kuzuia na kupambana na rushwa na kusimamia ufuataji wa maadili. Eneo mojawapo litahusu kusisitiza umuhimu wa Mawakili wa Serikali kufuata na kuheshimu maadili ya kazi yao. Kwa upande wa Mahakama, utaratibu wa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika ngazi zote za Mahakama utaimarishwa. Aidha, juhudi za kuhamasisha watumishi wa Wizara kupima afya zao kwa hiari ili kujua hali za afya zao na kuchukua tahadhari ya kujikinga na ugonjwa hatari wa UKIMWI, zitaendelezwa. Wizara inadhamiria programu za ukimwi mahali pa kazi zitaandaliwa ili juhudi hizi ziwe endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijahitimisha hotuba yangu, naomba niwapongeze Mheshimiwa Laurean Kalegeya na Mheshimiwa Mshibe Bakari walioteuliwa kuwa Majaji wa Mahakama ya Rufani. Napenda pia kuwapongeza kwa pamoja Waheshimiwa Majaji ishirini na mmoja wa Mahakama Kuu, Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria, Msajili wa Mahakama ya Rufani, Msajili wa Mahakama Kuu ya Tanzania na Wasajili wa Mahakama Kuu, Vitengo vya Kazi na Biashara, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Katibu Mkuu, Mkurugenzi wa Mashtaka kwa kuteuliwa kwao kushika nyadhifa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Barnabas Albert Samatta ambaye tarehe 20 Julai, 2007 amestaafu baada ya kufanya kazi katika utumishi wa umma kwa takriban miaka 41. Utumishi wake uliotukuka utabaki kuwa mfano wa kuigwa siyo tu na Majaji wenzake, bali pia kwa watumishi wote waliowahi kufanya naye kazi. Katika utumishi wake, Mheshimiwa Samatta, ameonyesha juhudi, busara, hekima, uwezo mkubwa wa uongozi na kufundisha na zaidi ameonyesha uwezo mkubwa wa kutenda haki. Tunamwombea kila la heri katika maisha mapya ya kustaafu. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Augustino Stephen Lawrence Ramadhan, kwa kuteuliwa kuwa Jaji Mkuu mpya, bila shaka uwezo wake na busara zake zitakuwa msaada mkubwa wa kuiongoza Mahakama yetu ili iweze kutenda haki kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashukuru Naibu Waziri, Mheshimiwa Mathias Chikawe, Mbunge wa Nachingwea, na Mheshimiwa Johnson Paulo Mathias Mwanyika, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa msaada wao hapa Bungeni. Nawashukuru pia Mheshimiwa Amir Manento, Jaji Kiongozi, Mheshimiwa Jaji Robert Kisanga, Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Profesa Ibrahim Juma, Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria, kwa ushirikiano walionipa katika kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** nawapongeza watendaji mbalimbali katika Wizara, nikianzia na aliyekuwa Katibu Mkuu, Bwana Vincent Kitubio Damian Lyimo, Bwana Sazi Salula, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Katibu Mkuu; Bi. Sophia Wambura, Msajili wa Mahakama ya Rufaa; Bi. Eliamani G. Mbise, Msajili wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Bwana Somi Mayalla, Msajili Mahakama ya Ardhi, Bwana John R. Kayonza, Msajili Mahakama ya Biashara, Bwana Samwel G. Karua, Msajili Mahakama ya Kazi, Bibi Crecencia Makuru, Katibu wa Tume ya Kurekebisha Sheria, Bi Mary Massay, Kaimu Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Dickson Ernest Maimu, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakinipa katika kuiongoza Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia natoa shukrani zangu za dhati kwa wadau wa maendeleo wanaoendelea kutoa misaada mbalimbali ya kuboresha na kuendeleza Sekta ya Sheria nchini ambao ni Sweden, Benki ya Dunia, *Canada, UNDP, Belgium, Denmark, UNICEF* na *GTZ.*

Mheshimiwa Spika, mwisho**,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2007/08, kiasi cha Shilingi 69,860,784,800 zinahitajika kutekeleza shughuli zilizopangwa**.** Kati ya fedha hizo, fedha za Matumizi ya Kawaida ni Shilingi 52,302,890,000 na fedha za Miradi ya Maendeleo ni Shilingi 17,557,894,800**.** Naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe Makadirio hayo ya Fedha za Maendeleo na Matumizi ya Kawaida kwa Mafungu Saba kama ifuatavyo:-

Fungu 40: Mahakama - Matumizi ya Kawaida,Sh. 37,064,243,000, Matumizi ya Maendeleo (Ndani), Sh.3,283,000,000, Matumizi ya Maendeleo (Nje), Sh. 400,000,000, Jumla Sh. 40,747,243,000.
Fungu 41: Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Matumizi ya Kawaida Sh. 9,348,389,00
Fungu 55: Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora: Matumizi ya Kawaida**,** Sh. 2,612,180,000**,** Matumizi ya Maendeleo (Ndani)**,** Sh . 119,115,000, Jumla Sh. 2,731,295,000. Fungu 59: Tume ya Kurekebisha Sheria, Matumizi ya Kawaida Sh. 835,376,000, Matumizi ya Maendeleo -, Jumla Sh. 835,376,000. Fungu 60: Mahakama ya Kazi, Matumizi ya Kawaida Sh. 747,751,000, Matumizi ya Maendeleo Sh. 552,370,000, Jumla Sh. 1,300,121,000. Fungu 64: Mahakama ya Biashara, Matumizi ya Kawaida Sh. 855,005,000**,** Matumizi ya Maendeleo (Ndani)**,** Sh. 188,000,000**,** Matumizi ya Maendeleo (Nje), Sh. 200,000,000**,** Jumla Sh. 1,243,005,000. Fungu 90: Mahakama ya Ardhi, Matumizi ya Kawaida**,** Sh. 839,946,000**,** Matumizi ya Maendeleo **-**, Jumla Sh. 839,946,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2007/08, Wizara yangu inatarajia kukusanya jumla ya Shilingi 2,905,371,200 kama maduhuli ya Serikali kwa mchanganuo ufuatao:

Fungu 40.................................................................. Sh . 762, 806,000
Fungu 41...................................................................Sh. 840,508,200
Fungu 55………........................................................Sh. 752,000,000
Fungu 59................................................................. -
Fungu 64….............................................................Sh. 500,001,000
Fungu 90………........................................................Sh. 50,056,000
Jumla...................................................................... Sh. 2,905, 371,200

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, tunakushukuru kwa hotuba yako. Kabla sijamwita Msemaji wa Kamati niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge, kuhusu utata wa jina. Mheshimiwa Waziri ameliweka vizuri kwamba sasa itaitwa Wizara ya Katiba na Sheria. Kwa hiyo, Msemaji wa Kamati, Msemaji wa Upinzani na watakaochangia baadaye mkumbuke jina hilo kwamba ni Wizara ya Katiba na Sheria. Mheshimiwa Stephen Galinoma atasoma maoni ya Kamati kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala , Mheshimiwa George Lubeleje. Kabla hajaanza kusoma Mheshimiwa Stephen Galinoma, nimkumbushe kushukuru kwa yatakayofanyika Kalenga kwenye Mahakama yake.

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA (K.n.y MHE. GEORGE M. LUBELEJE) - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:-** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijawasilisha Taarifa ya Kamati, naomba nichukue nafasi hii kutoa salamu za rambirambi kwa familia ya Mzee Chifupa kutokana na msiba

mkubwa wa aliyekuwa Mbunge mwenzetu, Marehemu Amina Chifupa Mpakanjia. Pili, nawapa pole ndugu na jamaa wote waliopoteza ndugu zao katika ajali mbalimbali zilizotokea hivi karibuni. Mungu azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi. Amina! Natumia fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Jaji Augustino Ramadhani kwa kuteuliwa hivi karibuni na Mheshimiwa Rais kuwa Jaji Mkuu wa Tanzania kushika nafasi iliyoachwa wazi na aliyekuwa Jaji Mkuu, Mheshimiwa Jaji Barnabas Samatta, aliyestaafu hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu niongeze kwamba pongezi za Uteuzi huu wa Jaji Augustino Ramadhani, ziende pia kwa Jeshi la Wananchi wa Ulinzi waliomlea mpaka kuwa *Brig. General* kabla hajajiunga na Mahakama. Pamoja na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga la Taifa ambayo mimi nilikuwa Katibu Mkuu wake takriban kwa miaka 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa kwa mujibu wa Kanuni 81(1), Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2004, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2007/2008 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuipelekea Kamati yangu kazi ya kuchambua Makadirio ya Wizara hii, Kamati ilikamilisha kazi hii katika Ofisi ya Bunge, Dar es Salaam, tarehe 31 Mei, 2007, kwa kupokea maelezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Dkt. Mary Michael Nagu, (Mb.), Waziri wa Katiba na Sheria, akisaidiwa na Mheshimiwa Mathias Meinrad Chikawe, (Mb.), Naibu Waziri wa Katiba na Sheria na pia Mheshimiwa Johnson Paul Mathias Mwanyika, (Mb.), Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** katika Mwaka wa Fedha 2006/2007, Wizara ya Katiba na Sheria iliidhinishiwa fedha kama ifuatavyo: Fungu 40 – Mahakama, shilingi 36,965,949,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 4,360,001,000.00 kwa ajili ya Maendeleo na kufanya jumla ya fedha zilizoidhinishwa kwa Fungu hilo kuwa shilingi 41,325,950,000.00. Aidha, Fungu 41 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali liliidhinishiwa shilingi 7,667,198,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 11,969,140,000.00 kwa ajili ya Maendeleo na kufanya jumla ya fedha zilizoidhinishwa kuwa shilingi 19,636,338,000.00.

Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora liliidhinishiwa shilingi 2,938,178,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 260,000,000.00 kwa ajili ya Maendeleo na kufanya jumla ya fedha zilizoidhinishwa kuwa shilingi 3,198,178,000.00. Fungu 59 – Tume ya Kurekebisha Sheria liliidhinishiwa jumla ya shilingi 785,972,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Fungu 64 – Mahakama ya Biashara liliidhinishiwa shilingi 857,138,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 233,000,000.00 kwa ajili ya Maendeleo na kufanya jumla ya fedha zilizoidhinishwa kwa Fungu hilo kuwa shilingi 1,090,138,000.00; na Fungu 90 –

Mahakama ya Ardhi liliidhinishiwa jumla ya shilingi 813,311,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** jumla ya fedha zote zilizoidhinishwa kwa Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007 kwa mafungu yote hayo ni shilingi 66,849,887,000.00. Kati ya fedha hizo shilingi 50,027,746,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 16,822,141,000.00 kwa ajili ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Aprili/Mei, 2007, Wizara ya Katiba na Sheria ilikuwa imepokea na kutumia jumla ya shilingi 41,608,843,880.00 kwa Mafungu yote hayo. Kati ya fedha hizo shilingi 38,781,282,217 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 2,827,561,663.00 kwa ajili ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** kutokana na dharura za kitaifa likiwemo janga la njaa na ukarabati wa miundombinu iliyoharibika kwa mvua, Wizara ya Katiba na Sheria ilipunguziwa jumla ya shilingi 5,681,309,399.00 katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2006/2007. Kati ya fedha hizo shilingi 4,021,308,399 zilitokana na Matumizi ya Kawaida na shilingi 1,660,001,000.00 kwa ajili ya Maendeleo. Fedha hizi zilipunguzwa kutoka Fungu 40 – Mahakama (Matumizi ya Kawaida na Fedha za Maendeleo); Fungu 41 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Matumizi ya Kawaida); Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (Matumizi ya Kawaida); Fungu 59 – Tume ya Kurekebisha Sheria (Matumizi ya Kawaida); na Fungu 90 – Mahakama ya Ardhi (Matumizi ya Kawaida).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2006/2007, Wizara ya Katiba na Sheria ilitekeleza majukumu mbalimbali yakiwa ni pamoja na:- utekelezaji wa Programu ya Kisekta ya Kurekebisha na Kuboresha Mfumo wa Sheria nchini; uendeshaji wa kesi na kupunguza mlundikano wa kesi Mahakamani; kutoa ushauri wa kisheria; uendeshaji wa mashtaka; uandishi wa sheria na tafiti za sheria; uimarishaji wa Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu; uimarishaji wa Utoaji Haki; uboreshaji wa mazingira katika Ofisi zilizo chini ya Wizara; kushughulikia masuala mtambuka kama zoezi la uandaaji wa sera ya sekta ya sheria na mkakati wa kitaifa wa kupambana na rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu hayo, Wizara ilikabiliwa na matatizo yaliyosababisha kutotekeleza kikamilifu na kwa ufanisi baadhi ya majukumu yake. Matatizo hayo ni pamoja na:- upungufu wa nyenzo za kufanyia kazi, majengo na ofisi; upungufu wa nafasi za mafunzo; ucheleweshaji wa kutatua migogoro na kutoa haki kwa wakati hali ambayo ilisababisha kuwepo kwa mlundikano wa kesi Mahakamani; ucheleweshwaji wa fedha za utekelezaji au fedha kutotolewa kutoka Hazina kulingana na mpango wa utekelezaji wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa tarehe 18 – 26 Januari, 2007, Kamati yangu ilipata fursa ya kutembelea mikoa ya Iringa na Ruvuma ambapo pamoja na shughuli nyingine, ilipata fursa ya kutembelea Mahakama Kuu -

Kanda ya Iringa, Mahakama ya Hakimu Mkazi ya Iringa, Mahakama ya Mwanzo ya Kalenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nifuate ushauri wako ninashukuru sana Wizara ya Katiba na Sheria kwa kuamua kujenga Mahakama mpya pale Kalenga ambapo ndipo kitovu cha historia yetu ya Ukanda ule na ndiko alikotokea Spika wetu, hayati Adam Sapi Mkwawa. Kuna makumbusho pale na kwa hiyo, ni jambo ambalo litasaidia sana sifa ya nchi hii kama Mahakama hiyo itajengwa upya.

Vilevile Mahakama ya Mwanzo Makambako. Mahakama zingine ni Mahakama Kuu - Kanda ya Ruvuma, Mahakama ya Wilaya ya Songea na Mahakama ya Hakimu Mkazi ya Songea, Mahakama ya Mwanzo ya Mfaranyaki na Mahakama ya Mwanzo ya Namtumbo. Aidha, kabla ya kuanza kwa Mkutano wa Saba wa Bunge, Kamati ilikuwa na ziara fupi, Jijini Dar es Salaam, kutembelea Mahakama ya Rufani, Mahakama Kuu, Mahakama ya Hakimu Mkazi ya Kisutu na Mahakama ya Mwanzo ya Manzese.

Katika ziara hizo Kamati iliona matatizo yanayoikabili Mahakama likiwemo tatizo la usafiri kwa mahakimu, vitendea kazi duni na upungufu wa Mahakimu na Majaji ambalo husababisha mlundikano wa kesi na mahabusu katika magereza na kwenye vyumba vya kuwaweka mahabusu Mahakamani. Aidha, Kamati iliona mafanikio makubwa yaliyopatikana katika ujenzi wa majengo ya Mahakama Kuu, Kanda ya Iringa na Ruvuma na baadhi ya Mahakama za Mwanzo, Wilaya, Mahakama za Hakimu mkazi pamoja na ukarabati wa Mahakama ya Rufani. Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada inazofanya za kujenga na kukarabati Mahakama hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala zima la kuboresha Sekta ya Sheria nchini, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2006/2007, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwa Wizara/Serikali kama ifuatavyo:-

Serikali ijitahidi kuitengea fedha za kutosha Wizara ya Katiba na Sheria na kuipatia fedha kwa wakati ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo; kuweka utaratibu wa kuifanyia ukaguzi wa kina mikataba ambayo Serikali huingia na vyombo vya kimataifa; Kuongeza Bajeti kwenye Tume ya Kurekebisha Sheria; kupeleka Muswada wa Sheria ya Mirathi Bungeni; kuwahamasisha wananchi kushiriki katika ujenzi wa Mahakama; Wizara ya Katiba na Sheria kushirikiana na Wizara ya Usalama wa Raia na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupunguza tatizo la mlundikano wa watuhumiwa wa makosa mbalimbali waliopo katika magereza; kushughulikia tatizo la usafiri kwa Mahakimu; Tanzania kuridhia Makubaliano ya *NEPAD* juu ya Mfumo wa Afrika wa Nchi Kutathminiwa na Kujipima zenyewe katika masuala ya utawala bora na uwajibikaji (*African Peer Review Mechanism*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulithibitishia Bunge lako Tukufu kuwa mengi ya mapendekezo yetu yalitekelezwa. Kamati inatambua kuwa baadhi ya matatizo hayawezi kutatuliwa kwa haraka lakini inaihimiza Serikali kuisaidia Wizara hii kila inapowezekana ili iweze kukidhi mahitaji yake halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti katika mwaka wa Fedha 2007/2008, Wizara ya Katiba na Sheria inatarajia kuendelea kutekeleza jukumu la kusimamia utoaji wa haki kwa wananchi. Aidha, Wizara itatekeleza malengo yafuatayo:Kuimarisha uwezo wa kuendesha na kusukuma kesi ili kupunguza mlundikano wa kesi Mahakamani, malalamiko na mashauri ya haki za binadamu, migogoro ya ardhi na kazi pamoja na mashauri ya biashara;Kushauri Serikali katika masuala ya mikataba, katiba na ya kisheria; Kufanya tafiti na kuhuisha sheria mbaya na zilizopitwa na wakati; Kuandaa miswada ya sheria;Kuhakiki sheria ndogo ndogo, kurekebisha na kutafsiri sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa Fedha 2007/2008, Wizara ya Katiba na Sheria inaomba jumla ya shilingi 69,860,784,800.00, kati ya fedha hizo, shilingi 15,866,755,000.00 kwa ajili ya Mishahara, shilingi 36,436,135,000.00 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi 17,557,894,800.00 kwa ajili ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchanganuo wa maombi hayo ni kama ifuatavyo:

(i) Fungu 40 – Mahakama, shilingi 12,007,870,000.00 kwa ajili ya mishahara, shilingi 25,056,373,000.00 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi 3,683,000,000.00 kwa ajili ya Maendeleo na kufanya jumla ya fedha zinazoombwa kwa Fungu hilo kufikia shilingi 40,747,243,000.00.

(ii) Fungu 41 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, shilingi 2,252,610,000.00 kwa ajili ya Mishahara, shilingi 7,095,779,000.00 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, shilingi 12,815,409,800.00 kwa ajili ya Maendeleo na kufanya jumla ya fedha zinazoombwa kwa Fungu hilo kuwa 22,163,798,800.00.

(iii) Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, shilingi 972,234,000.00 kwa ajili ya Mishahara, shilingi 1,639,946,000.00 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, shilingi 119,115,000.00 kwa ajili ya Maendeleo na kufanya jumla ya fedha zinazoombwa kwa Fungu hilo kufikia shilingi 2,731,295,000.00.

(iv.)Fungu 59 – Tume ya Kurekebisha Sheria, shilingi 203,186,000.00 kwa ajili ya mishahara, shilingi 632,190,000.00 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na kufanya jumla ya fedha zinazoombwa kwa Fungu hilo kuwa shilingi 835,376,000.00.

(v.) Fungu 60 - Mahakama ya Kazi, shilingi 143,958,000.00 kwa ajili ya Mishahara, shilingi 603,793,000.00 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, shilingi 552,370,000.00 kwa ajili ya Maendeleo na kufanya jumla ya Fedha zinazoombwa kwa Fungu hilo kuwa shilingi 1,300,121,000.00.

(vi) Fungu 64 – Mahakama ya Biashara, shilingi 157,355,000.00 kwa ajili ya Mishahara, shilingi 697,650,000.00 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, shilingi

388,000,000.00 kwa ajili ya Maendeleo na kufanya jumla ya Fedha zinazoombwa kwa Fungu hilo kuwa shilingi 1,243,005,000.00.

(vii)Fungu 90 - Mahakama ya Ardhi, shilingi 129,542,000.00 kwa ajili ya Mishahara, shilingi 710,404,000.00 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na kufanya jumla ya fedha zinazoombwa kwa Fungu hilo kuwa shilingi 839,946,000.00.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipokea taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa majukumu yaliyopangwa kwa Mwaka wa fedha 2006/2007 na maombi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008 pamoja na shughuli zilizopangwa kutekelezwa. Baada kupokea taarifa hiyo Kamati ina mapendekezo yafuatayo:-

(i)Kamati inashauri kuwa jitihada zaidi zifanyike kuongeza idadi ya mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, Mahakama za Wilaya, Mahakama za Hakimu mkazi, na majaji. Aidha, Chuo cha Mahakama kilichopo Lushoto kipanuliwe na vyuo vingine vinavyotoa mafunzo ya sheria.

(ii) Kutokana na baadhi ya Mahakimu na Majaji kukosa nyumba na kusababisha baadhi yao kuishi uraiani, Kamati inashauri kuwa Wizara iwe na mpango madhubuti wa kuwajengea nyumba sehemu maalumu.

(iii)Kutokana na matatizo ya usafiri yanayojitokeza kwa Mahakimu na Mahakama kwa jumla, Kamati inashauri kuwa Wizara iendelee na jitihada zake za kuzipatia usafiri Mahakama nchini na kuwatafutia mikopo ya magari na pikipiki mahakimu.

(iv). Pamoja na Serikali kuipatia Mahakama ya Rufani jengo jipya, na kwa kuzingatia kuwa eneo hilo halitoshelezi mahitaji halisi ya Mahakama hiyo; na kwa kuwa Serikali imekwishatoa kiwanja kwa ajili ya kujenga jengo la kudumu la Mahakama ya Rufani, Kamati inashauri kuwa ujenzi huo uanze mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muhtasari haya ndiyo maeneo makuu ambayo Kamati iliyatolea maoni na ushauri wakati ilipojadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii. Kamati iliridhishwa na kazi zilizofanywa na Wizara kwa Mwaka wa Fedha uliopita na Mpango wa Kazi uliowasilishwa na kupendekeza Bunge lako Tukufu liidhinishe Maombi ya Fedha kwa mwaka wa Fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha, kiasi cha shilingi 69,860,784,800.00 kinachoombwa na Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008 kinafanya kuwe na ongezeko la shilingi 3,010,897,800.00 ikilinganishwa na shilingi 66,849,887,000.00 zilizoidhinishwa katika mwaka wa fedha uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia fursa hii kuwasilisha Taarifa ya Kamati. Vilevile napenda kumshukuru Mheshimiwa Dr. Mary Michael Nagu, (Mb), Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mathias Chikawe, (Mb), Naibu Waziri, Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Johnson Mwanyika, (Mb.), Mwanasheria

Mkuu wa Serikali, Bw. Sazi Salula, Katibu Mkuu na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wakuu wa Idara na Vitengo, kwa kutoa maelezo na ufafanuzi wa kina mbele ya Kamati na kuiwezesha kuwasilisha Taarifa hii Bungeni.

Vilevile, nachukua nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa kuonyesha umahiri wa hali ya juu wakati wa kuchambua Makadirio ya Wizara hii na kuboresha maeneo mbalimbali kama ilivyojidhihirisha katika Taarifa ya Kamati.

Naomba niwataje kama ifuatavyo:- Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mheshimiwa Tatu M. Ntimizi, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Athumani S. Janguo, Mheshimiwa Rajab Hamad Juma, Mheshimiwa Shoka Kh. Juma, Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mheshimiwa Salim Yussuf Mohammed, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Fatma M. Maghimbi, Mheshimiwa Dkt. Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa Halima J. Mdee,Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu, na Mheshimiwa Ramadhani A. Maneno.

Mwisho kabisa, namshukuru Katibu wa Bunge, Bw. Damian Foka, watumishi wote wa Ofisi ya Bunge, bila ya kuwasahau, Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Charles Mloka, Ernest Zulu na Emanuel Mpanda, kwa kuratibu na kufanikisha shughuli za Kamati kufikia leo tunapohitimisha Taarifa yetu ya mwisho katika Mwaka huu wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha kiasi cha fedha kinachoombwa kama alivyowasilisha Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha.

**MHE. FATMA M. MAGHIMBI – MSEMAJI WA UPINZANI WIZARA YA SHERIA NA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, napenda kutoa maoni kuhusu bajeti ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba kwa mwaka wa fedha 2007/2008 kwa mujibu wa kanuni za Bunge, Kanuni ya 43(5)(b)(c) na 81(1), Toleo la Mwaka 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema na upendo kwa kunijalia afya njema hata kuweza kusimama hapa leo kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusiana na bajeti hii. Nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawashukuru wapiga kura wa Jimbo la Chake Chake kwa kuniwezesha kuwa mwakilishi wao. Nawaahidi kuendelea kuwatumikia kwa umahiri, uaminifu, uadilifu na kwa umakini mkubwa. Pia napenda kuwashukuru Viongozi wangu wa Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, (Mb.) na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, (Mb.), kwa misaada yote wanayonipa. Pia nawapongeza kwa kazi nzuri wanayofanya.

Vilevile nampongeza sana mume wangu Bwana Mussa Maghimbi kwa kuniruhusu muda mwingi kufanya shughuli za siasa na kuweza kunivumilia.

Namshukuru sana kwa sababu mpaka sasa hivi naamini hajanipatia nyumba ndogo kwa *absence* yangu ya nyumbani. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada na mafanikio kadhaa yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri, Kambi ya Upinzani katika Bunge lako Tukufu inawasilisha uangalizi wa maeneo ya kiutendaji ambayo Wizara hii inatakiwa kuyatafutia ufumbuzi kwa lengo la kufikia vyema dira ya Wizara. Maoni yetu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya sifa kuu za taifa linaloheshimu utawala wa sheria ni kuongozwa na Katiba maana Katiba ndiyo sheria mama ya nchi husika**.** Hata hivyo, si kila nchi inayoongozwa na Katiba ina katiba iliyo bora kukidhi matakwa ya umma wa nchi husika. Kimsingi, Katiba bora ni ile Katiba ya wananchi, inayotokana na wananchi kwa maslahi ya wananchi**.** Kambi ya Upinzani inawatetea Watanzania kupata Katiba yao mpya itayozingatia zaidi mawazo yao na maslahi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kuwa Tanzania inahitaji Katiba Mpya. Maisha bora kwa kila Mtanzania ni ndoto za mchana kama hakutakuwa na Katiba Mpya. Umoja na mshikamano wa Watanzania uko karibu kutoweka kama hakutakuwa na Katiba mpya. Umaskini, Ujinga, na Maradhi vitaendelea kutamalaki kama hakutakuwa na Katiba Mpya. Hoja na haja za kuwa na Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nyingi mno lakini leo napenda niorodheshe zile tu zinazogusa moja kwa moja maslahi ya Watanzania, nazo ni kama ifuatavyo:

(a) Uundaji wa Katiba iliyopo haukuwashirikisha wananchi. Rasimu ya Katiba iliyopo ilipendekezwa na kuasisiwa na Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM). Mchakato wote wa kupata Katiba hii ulifanywa kwa muda wa mwezi mmoja tu. Hivyo, hakukuwa na muda wa kukusanya maoni ya wananchi. Ndiyo maana Katiba hii sasa ina uhalali wa kisheria tu lakini haikubaliki kwa Umma wa Watanzania.

(b) Katiba hii ina utata mkubwa kuhusu suala la Muungano. Kwa vile Katiba hii ni ya Muungano ifafanue wazi mambo yanayohusu Muungano. Hakuna haja ya Katiba ya Zanzibar kuwemo ndani ya Katiba ya Jamhuri, kwa mfano, katika Katiba haijulikani tumeungana nini? Kwani ingawa ibara ya kwanza ya Katiba inatamka kuwa Jamhuri ya Muungano ni nchi moja, ukiangalia orodha ya mambo ya Muungano, ardhi siyo suala la Muungano. Sasa hiyo nchi moja iko vipi kama Zanzibar nao wana ardhi yao?

(c) Katiba yetu haina kabisa suala la umiliki wa ardhi, ingawa ardhi ndiyo msingi wa maisha na uti wa mgongo wa uchumi. Dosari hii imekuwa chanzo cha watu kunyang'anywa ardhi zao bila huruma au kusikilizwa. Mfano wananchi kufukuzwa kwenye maeneo yao ili kupisha migodi au mashamba yao kuuzwa kwa wawekezaji wengine bila kujali maslahi yao.

(d) Katiba inaweka madaraka makubwa sana tena ya mwisho kwa Rais. Ni hatari sana kuweka hatima ya nchi mikononi mwa mtu mmoja na siyo Bunge ambalo ndilo wawakilishi wa wananchi. Cha ajabu, Rais anaweza kuvunja Bunge kama litakataa kupitisha bajeti. Wabunge wamechaguliwa na wananchi, hivyo hawawezi kuondoshwa na mtu mmoja.

(e) Katiba hii haifafanui wala kuzilinda haki nyingi za msingi. Kwa mfano, Haki za Elimu, Vijana, Walemavu, Wazee, Familia, Hifadhi ya Wakimbizi, Vyombo vya Habari, Kuandamana, Kiuchumi, Biashara, Taaluma, Kutendewa haki na watawala, Huduma ya Afya, Chakula Bora, Hifadhi ya Mazingira, Utamaduni, na kadhalika.

(f) Katiba hairuhusu Wagombea binafsi kwenye nafasi mbalimbali za uongozi wa nchi. Hivi sasa mtu akitaka kushiriki uongozi wa nchi lazima awe mwanachama wa Chama cha siasa. Hali hii inawanyima nafasi ya uongozi Watanzania walio wengi ambao si wanachama wa Vyama vya Siasa. Hata Mahakama Kuu imepitisha uamuzi kuwa ni ruhusa mgombea binafsi. (Angalieni Kesi ya Mtikila).

(g) Katiba haifafanui mambo mengi ya msingi kama vile vita dhidi ya rushwa, umiliki wa uchumi na mwelekeo wa sera za nchi. Sehemu ya maelekezo yaliyomo kwenye ibara ya 9 ni pambo tu kwani hayahojiwi mahakamani.

(h) Kuna mkanganyiko mkubwa kwenye Katiba baina ya mamlaka ya Serikali za Mitaa na Serikali Kuu. Kwa mfano, Katiba haifafanui nafasi ya Wakuu wa Mikoa na Wilaya. Aidha, haiko wazi kati ya Viongozi hao na Madiwani na Wabunge, yupi ana nguvu. Imekuwa kawaida Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuwanyanyasa Madiwani ambao ndio waliochaguliwa kwa kura na wananchi. Hata hivyo, Wakurugenzi wa Wilaya wanaingiliwa na Wakuu wa Wilaya ambapo wote wameteuliwa na Rais.

(i) Katiba hii haijaweka Mahakama ya Katiba. Ingawa Mahakama Kuu imepewa mamlaka ya kusikiliza mambo ya kikatiba, kuna utata mwingine ambapo Katiba ni suala la Muungano wakati Mahakama Kuu siyo suala la Muungano, hivyo, maamuzi yake hayana nguvu Zanzibar.

(j) Katiba hii haina kifungu cha mamlaka ya kulinda wananchi wasionewe na Serikali au vitendo vya watawala (*Public Protector).* Hivi sasa wananchi wanapigwa au kukamatwa na Polisi na kubambikiziwa kesi halafu mtu akilalamika polisi walewale ndiyo wanachunguza. Wananchi wengi wamekuwa wananyimwa haki.

(k) Katiba imeweka namna ya Taifa kulipa deni la nchi, lakini haifafanui namna ya kushughulikia madeni ya Serikali ndani ya nchi. Aidha, hakuna kifungu kinachoilazimisha Serikali kuwalipa fidia wananchi inapodhihirika kimahakama kuwa Serikali haikuwatendea haki. Hali hii imesababisha watu wengi kutolipwa na Serikali ingawa Mahakama imeamua walipwe. Serikali imekuwa inalipa fidia kwa watu inaopenda yenyewe kama hisani tu.

(l) Hakuna kifungu cha wazi kuelezea namna ya kubadilisha Katiba. Kifungu kilichopo kinaruhusu Katiba kurekebishwa tu kama sheria nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yenyewe ilishaunda Tume mbalimbali za kutathmini Katiba ya sasa na zote zilishauri wazi kuwa Katiba hii haifai – mfano, Tume ya Jaji Nyalali, Tume ya Jaji Kisanga, na kadhalika. Jasho la Watanzania lilitumika

katika kuunda Tume hizi, kodi za Watanzania zilitumika katika kuunda Tume hizi. Inasikitisha sana kuona kwamba Serikali inachelewa kutekeleza ushauri wa kuwa na Katiba Mpya uliotolewa na Tume hizi. Serikali yenyewe kama ina nia ya dhati na Wananchi wake ni lazima iridhie suala la kuwa na Katiba Mpya itakayotoa zaidi nguvu na Mamlaka ya Umma katika kuendesha mambo yote ya kisiasa na kiuchumi. Tanzania yenye neema haitawezekana kama hakutakuwa na Katiba inayotoa neema kwa wananchi. Nchi hii ni yetu sote na Katiba Mpya tunayoitaka si ya CCM bali ni ya Tanzania kwa maslahi ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba ya Mwaka 1977, Ibara ya 107A inatoa mamlaka yenye kauli ya mwisho ya utoaji haki katika Mahakama. Aidha, Katiba inaagiza kutokucheleweshа haki bila sababu za kimsingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na umuhimu huo wa kikatiba, Mahakama za Tanzania zimekuwa, na bado zinaendelea kuwa na matatizo mengi sana. Baadhi ya matatizo hayo ni uhaba wa majaji, mahakimu na vitendea kazi. Uteuzi wa majaji ishirini wa Mahakama Kuu na wawili wa Mahakama za Rufaa uliofanywa na Mheshimiwa Rais katika kipindi cha Bajeti kilichopita unatia moyo lakini bado changamoto ingali kubwa sana. Sina haja ya kurudia takwimu nilizozitoa mwaka jana juu ya mlundikano wa kesi zilizopo kwenye mahakama zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa utafiti wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, mahakama nyingi hapa nchini hazina Mahakimu wa kutosha. Kwa mfano, Mahakama ya Ilala ilikuwa na Mahakimu wanne (4) tu hadi mwishoni mwa mwaka 2006; Mahakama ya Kisutu ya Dar es Salaam ilikuwa na upungufu wa Mahakimu sita (6) wakati katika wilaya nyingine kama Ruangwa hakukuwa na hata jengo la Mahakama ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchache wa Majaji, Mahakimu na Vitendea kazi vimekuwa baadhi ya sababu ya mlundikano mkubwa wa Mahabusu katika magereza hapa nchini. Kwa sasa hapa nchini kuna wafungwa na mahabusu zaidi ya 43,000 wakati uwezo rasmi wa Magereza yetu ni Wafungwa na Mahabusu 22,699. Kati yao zaidi ya asilimia arobaini na nne (44%) ni mahabusu ambao kesi zao ziko Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inatambua kuwa mkakati wa Serikali katika kukabiliana na tatizo la mlundikano wa mahabusu ulikuwa ni kuanzisha vifungo vya nje (*community services)* chini ya Sheria ya *Community Service Act, 200,* utekelezaji wa Sheria hii umekuwa ni mdogo sana na pengine hauonekani kabisa kufanya kazi. Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa ni vyema sheria hii ianze kutumika ipasavyo nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, utaratibu wa kuharakisha kesi kwa mtindo wa mbinu mbadala za utatuzi wa kesi (*Alternative Disputes Resolution* au *ADR*) haujatumika ipasavyo ama hausaidii kupunguza tatizo la mlundikano na ucheleweshwaji wa kesi mahakamani. Ninasema haya kwa sababu, ni ukweli ulio dhahiri kuwa mbali na kuwepo kwa utaratibu huu kwa miaka 16 sasa, kesi zinazosubiri maamuzi zimekuwa zikiongezeka badala ya kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kumaliza upelelezi ndani ya siku sitini *(60 Days Rule)* kama inavyotajwa katika kifungu cha 225(4) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20 ya Sheria za Tanzania *(Criminal Procedure Act, Cap. 20 of the Revised Edition of the Laws of Tanzania),* umekuwa ukitumiwa na baadhi ya Mahakimu. Isipokuwa tatizo ambalo Wizara hii inatakiwa kulitatua kwa kushirikiana na Wizara ya Usalama wa Raia ni tabia ya baadhi ya askari (tena wengi sana) kuwakamata tena watuhumiwa mara tu wanapoachiwa huru na Mahakama – tena hukamatwa kwenye mlango wa Mahakama na kurudishwa tena rumande kuongeza mlundikano. Bila shaka Waheshimiwa Wabunge wote mnakumbuka mcharuko wa hivi karibuni wa Mahabusu waliokataa kufikishwa Mahakamani kutokana na matatizo yote haya niliyoyaweka bayana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa pia na tatizo la baadhi ya Mahakimu na wasimamizi wengine wa maamuzi katika mahakama na Mabaraza ya Sheria kushindwa kutatua kesi zinazotakiwa kutatuliwa na Mabaraza ya Ardhi kwa mujibu wa Sheria za Ardhi za Mwaka 1999. Aidha, Vyombo vya Maamuzi vilivyoundwa na Sheria mpya za Kazi na Ajira za mwaka 2004 bado hazijawekwa sawasawa wakati tayari sheria hizi zimesharuhusiwa kutumika toka mwezi Desemba 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muda sasa umepita tangu serikali kutoa tamko juu ya suala la mahakama za Kiislamu yaani Mahakama ya Kadhi Mkuu. Kambi ya Upinzani bado hatujaona nia ya dhati ya Serikali kutatua suala hili ambalo linagusa mustakabali wa Taifa hili. Yapo mambo makuu mawili yalitolewa katika tamko la serikali lililowasilishwa na Waziri wa Katiba na Sheria;Mosi, wananchi walitakiwa wafunge mjadala kuhusiana na suala hili; na pili, Serikali iliahidi kuendesha mchakato wa kukusanya maoni kutoka kwa wananchi kuhusiana na suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tamko la Serikali lilikuwa likijipinga lenyewe maana huwezi kufunga mjadala wa wananchi kuhusiana na suala la Mahakama ya Kadhi na wakati huo huo ukaahidi kukusanya maoni kutoka kwao; je, maoni yatapatikana bila mjadala? Lengo la Serikali kuutaka umma wa Watanzania kutojadili suala hili linatia shaka; au nia ya Serikali ni kuzima ili lisisikike?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili karibu kila siku limekuwa likisikia sifa za utekelezwaji wa Ilani ya uchaguzi ya CCM. Ilani ya Uchaguzi ni mkataba kati ya wananchi na Serikali iliyochaguliwa, hivyo ni wajibu wa Serikali kuitekeleza Ilani hiyo. Ilani ya uchaguzi ya CCM iliahidi kulitafutia ufumbuzi suala la Mahakama ya Kadhi lakini hadi leo hakuna jambo la msingi liililofanyika zaidi ya kuitishwa kwa kongamano moja tu la wadau kujadili suala hili. Serikali isifikiri kuwa italimaliza suala hili kwa mkakati wa kuunyamazisha umma wa Watanzania usijadili suala hili. Njia ya kutafuta ufumbuzi wa suala la Mahakama za Kadhi ni kuitisha mijadala ya kitaifa ya wazi na ya haki itakayoshirikisha wananchi wote na hatimaye kuibuka na suluhisho muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sheria nyingi ambazo zimepitwa na wakati, na hizi zinawanyima wananchi haki zao, na pia huwa zinawakwaza wadau wa Utawala Bora

na hapa nitazungumzia Taasisi za Kitaalamu yaani '*Professional Associations'*. Kwa mfano, *Tanganyika Law Society* wameanza kuomba kwa muda mrefu sheria ya Mawakili (*Advocates Act*) ifanyiwe marekebisho lakini hadi leo imewekwa kwenye mashubaka *(shelves).*

Nyingine ni Sheria ya Madaktari, Sheria ya Wahandisi. Nyingi kati ya Sheria za *Association* zilitungwa toka enzi za ukoloni, sijui Wizara ya Katiba na Sheria inaona ugumu gani kukubali maombi ya *Professional Association* hizo. Mwisho, wananchi wanaweza kushangaa kwa nini sheria nyingine zipitishwe haraka, kwa mfano, *PCB*; je, kuna *double standard* katika Wizara ikifika kupitisha sheria?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo jingine la *Professional Association* ya Madaktari ni kuwa kuna sheria nyingine zinazodhibiti *Profession* hiyo. Kwa mfano, kuna Sheria ya Madaktari, kuna Sheria ya Manesi, kuna Sheria ya Madaktari wa Meno, kwa nini Wizara haioni kuwa wote hao ni matabibu wa binadamu na kwa hiyo wanahitaji sheria moja tu.

Wenzetu Zimbabwe kwa mfano, wana sheria moja tu inayoratibu na kudhibiti taaluma ya tiba za binadamu kwa jumla. Nakiri kuwa hao kazi yao sio moja lakini wote kazi yao ni kutibu binadamu. Laiti tungekuwa na sheria moja ufanisi ungekuwa mzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la sheria katika ngazi za Serikali za Mitaa, katika Ibara yake ya 145 na 146 Katiba inaanzisha Serikali za Mitaa lakini Katiba iko kimya haielezi nani ana uwezo wa kuiondoa au kumwondoa Mjumbe wa Serikali za Mitaa anapofanya kosa la uwajibikaji. Kwa ajili ya pengo hilo katika Katiba juu ya kumwajibisha au hatua ya kumchukulia mjumbe wa Serikali za Mitaa anapokosa, tumeshashuhudia viongozi wa Serikali Kuu wanavyovunja Katiba kwa kuvunja Halmashauri.

Kwa mfano, wakati wa Awamu ya Tatu, Waziri Mkuu alishavunja Halmashauri ya Jiji na kuunda kitu kilichoitwa Tume ya Jiji na Wananchi wakaibatiza na kuuita Tume ya Keenja. Huu ni mzaha kwa Serikali inayodai kuheshimu utawala wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri huwa zinachaguliwa na wananchi kwa Mujibu wa Katiba kama nilivyosema, hivyo basi, viongozi wa Serikali hamuwezi kumfukuza Mjumbe wa Halmashauri au kuivunja Halmashauri. Hata hivi sasa huwa tunawasikia viongozi wa juu wanatishia kuvunja Halmashauri au kumfukuza Mtendaji fulani, basi Wakuu wa Wilaya/Mikoa nao wanatishia kwa kuwaiga viongozi wao wa Taifa.

Kwa kuwa chombo kinapoanzishwa na Katiba, kwa mfano Bunge, huwa Katiba hiyo hiyo inasema chombo hicho kitaondoshwaje. Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa Wizara ya Sheria ilete sasa Mswada wa kuonyesha wajumbe wa Serikali za Mitaa wataondoshwaje ili viongozi wa Serikali Kuu waache vitisho kwa wajumbe wa Serikali za Mitaa. Pia itatuondolea masuala na mijadala ndani ya Vyombo vya Habari kuwa Serikali inavunja Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu mwingine uliopo katika sheria zetu ni kuwa hazijatamka bayana kuhusu uwakilishi wa walemavu. Uwakilishi wa Walemavu hivi sasa unapitia kwenye Vyama tu wakati sote tunaelewa kwamba kundi hili ni muhimu kama lile la wanawake.

Mpaka sasa hakuna utaratibu maalumu wa kuwapata wawakilishi ambao ni walemavu zaidi ya kupata nafasi ya uwawakilishi kama zawadi tu kupitia vyama. Masuala ya walemavu yangeshughulikiwa vyema zaidi kama walemavu wenyewe wangekuwemo katika vyombo vya uwakilishi. Ni wakati muafaka sasa kwa serikali kutoa fursa za kisheria zitakazowawezesha walemavu kuwa na nafasi maalumu za uwakilishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ilisaini Mkataba wa Kimataifa unaoitwa, *"The Convention on the Rights of Persons with Disabilities"* tarehe 30/3/2007. Lakini hadi leo hii hakuna dalili ya Mkataba huo kuletwa Bungeni kuridhiwa. Mkataba huu ni muhimu sana maana unatoa ufafanuzi kuhusu haki za Walemavu na unaeleza wajibu wa Serikali wa kuwahudumia walemavu na kuwapa haki zao kama vile Mkataba unavyosema na kama nchi nyingine zinavyofanya. Walemavu sio wanawake tu, na wanaume pia wapo walemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa tamko ni lini Mkataba huu utaletwa Bungeni kuridhiwa ili ndugu zetu na watoto wetu nao waweze kuishi kama Binadamu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza Serikali kwa kukubali pendekezo letu la kuifanya Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu kuwa Wakala. Pamoja na kuwa ofisi hii imekuwa wakala na kupewa jina la *Registration of Insolvency Trustees Agency (RITA)*, changamoto iliyopo sasa ni ukosefu wa teknolojia ya kisasa ya utunzaji wa takwimu za vizazi na vifo. Kwa sasa, bado ni vigumu sana kupata takwimu hizi licha ya ukweli kuwa zina umuhimu mkubwa katika mipango ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uandikishaji wa vizazi na vifo kupitia watumishi walio chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ambao kimsingi una upungufu mkubwa haujabadilishwa na mfumo huu wa *Agency*. Moja ya upungufu uliopo ni kuwa watu hawa hawana taaluma ya sheria. Hivyo basi kuna umuhimu mkubwa wa kuangalia uwezekano wa kurekebisha Sheria ya Usajili wa Vizazi na Vifo, Sura ya 108 *(The Birth and Death Registration Act, Cap. 108)* inayoruhusu watu hawa kufanya kazi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana Kambi hii iliainisha upungufu mkuu wa aina tatu utokanao na Idara hii ya uandishi wa Sheria za Tanzania. Kwa mfano, makosa mengi ya uchapishaji na Sheria karibu zote kubaki katika lugha ya Kiingereza.

Makosa mengi ya uchapishaji, hasa sheria zilizomo katika *Volumes*, kwa mfano Sheria ya Magereza, Sura ya 5, tulizungumzia suala la umuhimu wa kutafsiri sheria zetu kutoka katika lugha ya Kiingereza kuja lugha yetu ya taifa (Kiswahili) kwa kuwa

watanzania wengi hawaijui lugha ya Kiingereza. Hatuna uhakika juu ya namna gani suala hili lilitekelezwa ila kimsingi sheria karibu zote tulizonazo hapa Tanzania bado ziko katika lugha ya Kiingereza.(*Makofi*)

Kuna baadhi ya Wizara ambazo zimeamua kwa juhudi zao wenyewe kutafsiri sheria zinazohusu idara zao. Mfano, Wizara ya Ardhi iko katika mchakato wa kutafsiri kanuni zilizoundwa kwa mujibu wa Sheria za Ardhi Sura ya 113 na 114. Wizara ya Sheria inaweza kuangalia fursa kama hizo katika Wizara nyingine na kutoa miongozo ili sheria hizi zitafsiriwe mapema na pengine kwa bajeti ya Wizara hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili lina umuhimu mkubwa sana kwa kuwa upatikanaji wa haki *(access to justice)* hauishii kuwa na vyombo vya usimamizi wa haki pekee, bali pia hata namna watu wanavyoweza kusoma na kuelewa Sheria zinazowahusu ili kujua haki, wajibu na miongozo ya sheria. Yapo makosa mengi sana ambayo hutendeka kwa sababu tu watu hawajui sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunasisitiza umuhimu wa kuzipanga katika juzuu na sura *(volume and chapters)* sheria ambazo haziko katika juzuu na sura hususan zile zilizotungwa kuanzia tarehe 1/8/2002. Hii itasaidia sana usomaji na utumiaji wa sheria hizi. Tunaomba Wizara ilifahamishe Bunge hili mwenendo wa utekelezaji wa mapendekezo haya yote. Katika utafiti wangu naona tokea 2006 bado swala hili halijafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba yetu katika Ibara ya 9(f) na ile ya 63(3)(e) zinaihusisha serikali yetu katika uwajibikaji wa Mikataba ya Kimataifa hasa ile inayohusu sheria na haki za binadamu. Mfumo wetu wa sheria (*dualistic legal system)* unaelekeza kuwa Mikataba hii haitafanya kazi hapa nchini mpaka ifanywe kuwa ni sehemu ya sheria za Tanzania baada ya kuridhiwa.

Kwa kipindi chote cha Bajeti iliyopita hadi sasa, Serikali imeridhia Mkataba mmoja tu wa Kimataifa wa haki za Binadamu unaoitwa *Protocol to the African Charter on Human and Peoples' Rights on the Establishment of an African Court on Human and Peoples' Rights of* 1998. Pamoja na kuipongeza Wizara kwa kuridhia mkataba huu unaoanzisha Mahakama ya Afrika ya Masuala ya Haki za Binadamu, Kambi ya Upinzani inasisitiza umuhimu wa kuridhia Mikataba mingine ya namna hiyo yenye umuhimu mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikataba ya Kimataifa ya haki za binadamu ambayo ni vyema sana kuiridhia (ambayo tuliitaja tena mwaka jana) ni pamoja na:

(i) Mkataba wa Nyongeza wa Afrika unaohusu Haki za Wanawake wa Afrika *(The Protocol to the African Charter on Human and Peoples' Rights on the Rights of Women in Africa, 2000),* Tanzania iliusaini mwaka 2003 lakini haijauridhua mpaka leo hii.

(ii) Mkataba wa Kimataifa dhidi ya Mateso na Ukatili Mwingine *(The Convention Against Torture and Other Cruel, Inhuman or Degrading Treatment or Punishment, 1984).* Huu pia haujaridhiwa.

(iii) Mkataba wa Nyongeza wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa *(The Optional Protocol to the International Covenant on Civil and Political Rights, 1966)* ambao unaruhusu watu binafsi kupeleka malalamiko ya ukiukwaji wa haki za binadamu moja kwa moja katika Tume/Kamati ya Kimataifa ya Haki za Binadamu *(Human Rights Committee*), huu pia haujaridhiwa.

(iv) Mkataba wa Pili wa Nyongeza wa Haki za Kiraia na Kisiasa *(The Second Optional Protocol to the International Covenant on Civil and Political Rights, 1989)* ambao unaagiza kufutwa kwa adhabu ya kifo, bado haujaridhiwa pia. Kwa sasa nchi nyingi sana duniani zimeshafuta adhabu ya kifo ikiwemo nchi ya Malawi iliyoifuta adhabu hiyo ya kifo tarehe 27/4/2007.

Mkataba muhimu sana ambao pia haujaletwa kuridhiwa ni *Declaration on Gender and Development*. Huu ndio utawasaidia Viongozi wa vyama vyetu vya Siasa kujitayarisha kuweka usawa wa uwakilishi katika sehemu zote za maamuzi, kama vile katika Bunge. Hivi karibuni tumeshaanza kuwasikia wananchi wakijisifu kuwa sera ya 50% 50% katika Bunge ni Sera ya CCM. Kusema hivyo ni kuipotosha jamii ya Watanzania kwa sababu *Declaration* hii imesainiwa na Wakuu wa nchi za *SADC*.

Mheshimiwa Rais Kikwete ni mmoja kati ya Marais waliosaini. Napenda kuwakumbusha Wana-CCM kwamba Rais Kikwete sio Rais wa CCM peke yao hivyo basi Mkataba huo ni wetu sote. Aidha, uwajibikaji wa Serikali katika mikataba ya kimataifa, kama vile, kuandaa taarifa ya utekelezaji wa masharti ya mikataba ambayo Tanzania imeridhia, umekuwa mdogo sana. Kwa mfano, Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa *(International Covenant on Civil and Political Rights)* wa mwaka 1976 unaagiza kutoa taarifa hizo kila baada ya miaka mitano (5), lakini Tanzania imeshapeleka taarifa moja tu toka mwaka huo. Vilevile katika mikataba mingine kama huo uitwao Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni wa Mwaka 1976, Tanzania imepeleka taarifa moja tu na mara ya mwisho kufanya hivyo ilikuwa ni mwaka 1979. Kuingia mikataba mingi ya kimataifa sio sifa, sifa ni kuwajibika kikamilifu kuitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna umuhimu mkubwa sana wa kutekeleza masharti ya Mikataba hii hasa ile ambayo tulikwishasaini. Tunaishauri Wizara kwa mara nyingine, kuwajibika katika masharti ya Mikataba ya Kimataifa ili taifa letu lisiendelee kuwa nyuma katika uwajibikaji huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilianza kufanya kazi takriban miaka sita iliyopita baada ya kutungwa Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Sura ya 391 ya Sheria za Tanzania. Lengo la Tume hii ni kufanya kazi nchi nzima hususan katika maeneo ya vijijini ambako vyombo vya usimamizi wa haki ni vichache sana. Tunaipongeza Serikali kwa mabadiliko ya sheria ya mwaka jana yaliyoiletea ufanyaji kazi wa Tume hii kwa upande wa Zanzibar.

La kusikitisha ni kuwa, Tume hii haijaweza kufungua matawi ama kuwa na Makamishna katika ngazi za wilaya na hata mikoa ambako ndiko hasa kuna ukiukwaji mkubwa sana wa haki za binadamu. Hii ina maana kuwa ni watu wachache tu wanaoweza kuifikia Tume hii kwa njia ya moja kwa moja. Serikali inayoheshimu haki za binadamu haitapimwa kwa kuanzisha tume tu bali kwa ufanisi wa kazi wa tume husika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuone umuhimu wa Tume hii kusambazwa nchi nzima, tarehe 25 Mei, 2007 (Ijumaa) nimesoma gazeti la Nipashe linaloeleza kwamba katika Kisiwa kiitwacho Ghana kilichoko katika Wilaya ya Ukerewe, wananchi wa hapo wamejiwekea sheria za kumwadhibu mwanamke anapofanya kosa katika Kisiwa hicho. Na adhabu iliyowekwa ni wanaume kadhaa huambiwa wafanye ngono na mwanamke huyo.

Huu ni Utumwa wa Ngono (*sexual slavery)* ambao ni aibu kubwa kwa nchi yetu. Lakini muhimu zaidi ni kuwa Tume ya Haki za Binadamu haijasambazwa inavyopaswa na kuwaacha wananchi wengine kuteseka hasa wanawake kunyanyaswa kijinsia na wengine kufanywa watumwa wa wanaume.(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inamwomba Waziri atupe majibu kwa nini Kisiwa cha Ghana Wilayani Ukerewe wanatumia Ngono ya Kundi la Wanaume kumfanyia mwanamke anapokosa katika jamii? Ina maana sehemu hiyo haina Mahakama au Wizara inawaacha wananchi wachukue sheria mikononi mwao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni kuhusu urasimu usio wa lazima wa utekelezaji wa majukumu ya Tume hii kama nilivyoainisha mwaka jana. Mwaka jana niliishauri Wizara hii kuangalia uwezekano wa kurekebisha kifungu cha 28 kinachotoa utaratibu wa kuchunguza suala lililotolewa taarifa kwake, halafu kuiandikia mamlaka inayohusika barua ambayo itatakiwa kujibiwa ndani ya miezi mitatu, halafu baada ya hapo, kama mamlaka hiyo haitatekeleza basi Tume italifikisha suala hilo Mahakamani.

Tatizo hapa ni ucheleweshaji wa haki. Ingekuwa vyema sana endapo muda wa utaratibu huu ungepunguzwa ama kuondolewa kabisa. Wananchi wa Nyamuma, Wilaya ya Serengeti wameathirika sana na kifungu hiki cha Sheria ya Tume. Tunashauri tena, sheria hii iangaliwe upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo mengine niliyotoa mwaka jana ambayo kwa bahati mbaya hayajafanyiwa kazi ni muda wa Makamishna kutumikia Tume hii. Miongo miwili ya miaka mitatu mitatu ni muda mfupi sana. Kanuni ya 6 ya *United Nations Paris Principles of 20th December,* 1993, imesisitiza suala hili la *stable mandate for members of the national institution.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mwaka wa 27 toka Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania iundwe kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria, Sura ya 171 ya mwaka 1980. Moja ya changamoto kuu ambayo imekuwa ikiisumbua Tume hii ni

Serikali (Wizara ya Katiba na Sheria ) kutokutekeleza mapendekezo ya Tume hii mapema kupitia taarifa za mapendekezo zinazotumwa kila mwaka wizarani.

Kwa mfano, mwezi Mei, 2006, Mheshimiwa Jaji Antony Bahati wa Tume hii alisema katika Ripoti yao kuwa mapendekezo ya Sheria za Mirathi *(Succession and Inheritance laws)* yalipelekwa Wizarani mwaka 1994 na hakuna jawabu lolote toka wizarani.

Hivi karibuni Tume ya Kurekebisha Sheria nchini (*Law Reform Commission*), ilitoa taarifa yake ya mapendekezo ya kurekebisha baadhi ya sheria nchini. Katika mapendekezo yao wamependekeza mambo kadhaa:

Kwanza, Kanuni za Mwenendo wa Mashitaka ya Madai *(Civil Procedure Code)* irekebishwe ili kufanya iwe lazima kwa usuluhishi kufanyika kabla ya kwenda kwenye mchakato wa madai na mashitaka mahakamani. Hii ni muhimu kupunguza mlolongo wa mashitaka mahakamani na hivyo kuongeza kasi na kurahisisha utoaji wa haki nchini. Ili hili kufanyika na kufanikiwa kuna haja kubwa ya kuwa na programu ya kuwajengea uwezo mahakimu na majaji watakaohusika na mchakato wa usuluhishi.

Pili, katika vyuo vyote vinavyotoa elimu ya sheria kozi ya usuluhisho na njia mbadala za utatuzi wa migogoro iwe ya lazima ili kutayarisha wataalamu wa kutosha. Kanuni za mwenendo wa mashitaka ya madai *(Civil Procedure Code),* itafsiriwe kwa Kiswahili. Hoja hii ni kama nilivyopendekeza kwenye sehemu ya awali ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ni mfano wa mapendekezo machache tu kati ya zaidi ya mapendekezo ishirini (20) ambayo hayajafanyiwa kazi licha ya kuwa ni ya muda mrefu katika Wizara hii.

Mapendekezo mengine niliyoainisha katika hotuba yangu ya mwaka jana ni ripoti za sheria za ndoa, ucheleweshwaji wa kesi za daawa/madai, sheria ya watoto, sheria 40 za Nyalali, tatizo la mlundikano wa wafungwa na mahabusu, udhibiti wa wizi wa fedha katika idara za umma, sheria ya jinai kwa kutumia komputa *(e-commerce and cyber crimes*), uraia wa nchi mbili *(dual citizenship)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tatizo hili la kutokutekeleza ripoti za Tume hii limekuwa sugu sasa na kuifanya Tume hii kuanza kuonekana haina umuhimu, Kambi ya Upinzani inaiomba Wizara ilieleze Bunge lako Tukufu ni kwa nini na lini masuala haya yatafanyiwa kazi ili kuondokana na malalamiko ya kila mwaka yanayofanana na kutokutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Kurekebisha Mfumo wa Sheria *(Legal Sector Reform Programme)* umekuwa ukitekelezwa kama sehemu ya mpango mkuu wa kurekebisha sekta ya Sheria. Aidha, nia ya mpango huu ni kusaidia kurahisisha upatikanaji wa haki kwa kuondoa vikwazo vilivyopo.

Mwaka 2005/2006 ulikuwa katika *medium term strategy* ambayo itaendelea hadi mwaka 2007/2008. Hata hivyo, haifahamiki ni mambo yepi ambayo yameshafanyiwa kazi kupitia mpango huu kwa kipindi cha miaka miwili iliyopita na hata toka Mpango huu uanze kazi. Kambi ya Upinzani tunataka maelezo.(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa linaloweza kuwa ndiyo sababu ya kutokuwa na ufanisi wa Mpango huu ni namna Wizara inavyouratibu.

Wataalamu katika Mkutano wa *Pan-African Conslutative Forum on Coorporate Governance of the World Bank Group, February 2007* wamesema kuwa sababu mojawapo ya kuchelewa kwa utekelezaji wa mpango huu ni uratibu dhaifu wa mpango huu unaofanywa na Serikali. Kambi ya Upinzani tunashauri kuwa Wizara ihakikishe utekelezaji wa mpango huu kwa kutumia viashiria vilivyoainishwa *(performance indicators).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rushwa ni suala mtambuka (*cross-cutting issue)* katika kila Wizara na idara za Serikali na zisizo za Serikali. Leo hii, ni miaka takriban 11 toka taarifa ya rushwa ya Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba ilipotolewa mwaka 1996. Taarifa hii ilitaja Mahakama kama moja ya vyombo vya dola ambako rushwa imekithiri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilitegemewa kuwa marekebisho ya Sheria ya Kuzuia Rushwa ya zamani (*Prevention of Corruption Act, Cap.* 329) yaliyofanywa mwaka huu yangeleta taswira mpya ya namna suala la rushwa litakavyotatuliwa Tanzania.

Kwa bahati mbaya baadhi ya mambo ambayo yalikuwa ni kikwazo hapo zamani yamejitokeza tena katika sheria mpya ya kuzuia rushwa. Kwa mfano, suala la kuomba ruhusa kwa *DPP* kabla ya kushitaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kwamba Kambi ya Upinzani ilipinga suala la Tume ya Kuzuia Rushwa (TAKURU) kuomba ruhusa ya kushtaki kutoka kwa Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali (*DPP*).

Tulipinga hilo kwa manufaa ya Watanzania ambao siku zote wana kiu ya kuona rushwa ikitokomezwa na haki ikitendeka. Tulipinga hilo tukiamini kuwa *DPP* anaweza, ama kwa ridhaa yake au kwa kushinikizwa, kuondoa kesi halali ya suala la rushwa na hivyo kuwa ameingilia uhuru wa TAKURU.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gazeti la *THIS DAY,* Toleo la 428 liliripoti mgongano kati ya *Director of Criminal Investigation (DCI)* na mwendesha mashtaka mkuu wa Serikali (*DPP*) juu ya kesi ya wizi wa gari ambapo kwa muhtasari *DPP* aliamuru Polisi ifute kesi dhidi ya wizi wa gari, kinyume cha matakwa ya *DCI* na Polisi ambao kwa kuzingatia uchunguzi wao, bado wanaona kuwa washtakiwa wana kesi ya kujibu.

Huu ni mfano mdogo tu unaoonyesha ni jinsi gani *DPP* anaweza kwenda kinyume na idara nyingine. Ni kwa ajili hii basi Kambi ya Upinzani tunaendelea kusisitiza ushauri wetu wa kutaka Tume ya Kuzuia Rushwa kutolazimika kuomba ruhusa ya kushtaki kutoka kwa *DPP* kwani kuna uwezekano mkubwa wa *DPP* kutoshitaki, kufuta au kubadilisha, au kupunguza uzito wa shitaka la rushwa la kupelekwa mahakamani – hofu yetu ni kuwa zisije zikatokea kesi za "kula rushwa bila kukusudia" maana ipo kesi "ya kuua bila kukusudia".

Kurefusha upelelezi na ufunguaji wa kesi kwa sababu ya agizo la kisheria la kuomba ruhusa ya *DPP*, kunapunguza uzito wa nia thabiti ya Serikali na hasa Wizara hii katika kupambana na rushwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa narudia shukrani zangu kwa kupata fursa hii. Pia nawashukuru Waheshimiwa Wabunge na watu wengine wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nachukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza leo na mimi kuwa mchangiaji wa mwanzo katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujalia kuwa wazima na salama katika Mkutano wetu huu wa leo.

Vilevile napenda kuchukua nafasi hii kunipatia nafasi hii mapema inavyowezekana. Pia nichukue fursa hii niwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Micheweni kwa namna wanavyonipa nguvu ya kuendelea na kazi yangu hii ya Ubunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza kuchangia kwenye Hotuba ya leo, kwanza, nataka nizungumzie kuhusu Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Nichukue fursa hii kwanza kuishukuru Serikali kwa kuunda hii Tume. Vilevile nashukuru Tume hii, kwa sasa imefika mpaka katika Visiwa vya Zanzibar na inaweza kufanya kazi. Kama alivyosema Msemaji wetu wa Kambi ya Upinzani, tunaomba kwamba Tume hii iweze kufungua Ofisi zake mpaka Wilayani zikiwemo katika Wilaya za Pemba na Unguja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume hii ina kazi muhimu sana inazozifanya, lakini kuna jambo moja ambalo mimi linanisikitisha. Tume hii haina nguvu za kisheria, inafanya kazi nzuri sana lakini mwisho wa maamuzi yake yanakuwa kama ni mapendekezo tu. Kwa mfano, Tume hii ilifuatilia suala la uvunjwaji wa haki za binadamu wa wananchi wa Serengeti. Wananchi wale walivunjiwa nyumba zao na kuchomwa moto.

Baadaye Tume ikapewe kazi hii ya kufuatilia. Ikafuatilia na mwisho ikaamua kuwa kuwa wananchi wale walipwe fidia. Lakini la kusikitisha ni kuwa Serikali ilikataa

kuwalipa fidia wananchi wale na baadaye haikuwalipa fidia. Kwa hiyo, basi mimi naomba Tume hii kwa umuhimu wake ipewe nguvu za kisheria, iwe sawa sawa na Mahakama, wakati inapotoa maamuzi yake yawe yanakubalika kisheria. Kwa sababu watu waliomo kwenye Tume hii ni watu wazito; kwa mfano, Jaji Kisanga, Mheshimiwa Mohamed Ramia na Makamishna wengine waliomo katika Tume hii, ni watu muhimu. Sifikirii kuwa wanaweza wakatoa maamuzi ambayo hayana maana.

Kwa hiyo basi ili tulinde heshima zao hawa viongozi wetu wakubwa ambao tumewapa jukumu kubwa hili ni bora Tume hii ikaletwa hapa katika Bunge tukaipa nguvu za kisheria. Maamuzi yatakayoamuliwa na Tume yawe ni maamuzi sawasawa na Mahakama. Vinginevyo ikiwa hatutaki kuipa nguvu za Kisheria bora tuivunje! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee na Tume ya Kurekebisha Sheria. Tume ya Kurekebisha Sheria nayo ni Tume muhimu vilevile kama vile Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Tume hii inafanya kazi nzuri sana lakini nao vilevile mwisho ikisharekebisha Sheria, Sheria zake zinapelekwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria na yeye anapeleka nafikiria kwenye Baraza la Mawaziri. Lakini Sheria hizi zinachelewa sana kuletwa hapa Bungeni.

Kwa mfano, mwaka jana sisi tulitembelea kwenye Tume hii tukaambiwa kuna Sheria zaidi ya 13 ambazo zimekwisharekebishwa lakini mpaka hivi sasa ninvyozungumza hakuna Sheria ambayo imeletwa hapa tukaifanyia marekebisho. Kwa hiyo basi naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho hapa atueleze hizi Sheria hasa zinakwama wapi mpaka zisiletwe Bungeni zikafanyiwa marekebisho? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kuna Sheria hii ya mirathi. Tulipokwenda katika Tume hii tukaambiwa toka mwaka 1992 tayari imekwishafanyiwa marekebisho lakini nashangaa mpaka hivi ninavyozungumza Sheria hii bado haijaletwa hapa Bungeni tukaifanyia marekebisho pamoja na Sheria ya Ndoa na Sheria nyingine nyingi ambazo wananchi wanazilalamikia huko nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema kwamba maisha bora kwa kila Mtanzania ni pamoja na Mtanzania huyu huyu kumfanyia Sheria nzuri. Bila sheria nzuri maisha bora hayatakuwa. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri azilete hizi sheria ili tuzifanyie marekebisho kila mara zinapohitajika. Kwa kusema muda uliopo kwenye Bunge ni mdogo basi tuongeze muda ilimradi tufanye kazi za wananchi. Lakini tunakuja hapa wiki mbili tunafanya sheria mbili nyingine tunaziacha wakati kuna Sheria nyingi wananchi wanazisubiri zifanyiwe marakebisho. Kwa hili naishia hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa nizungumzie suala la Katiba lakini kutokana na maelezo ambayo yametolewa na Msemaji wetu wa Kambi ya Upinzani sina haja ya kusema lolote kwa sababu maelezo aliyotoa ni ya kina na yanajitosheleza. Nafikiria nikizungumza chochote nitayaharibu. Kwa hiyo, nayaacha kama yalivyowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia tena suala la uundwaji wa Mahakama ya Kadhi Mkuu kwa Tanzania Bara. Suala hili linasubiriwa kwa muda mrefu na Waislamu. Toka niingie katika Bunge hili nilikuja nikalikuta. Tayari limeshaundiwa Kamati teule mbili za Bunge. Kamati ya kwanza iliongozwa na Mheshimiwa Arcado Ntagazwa na Kamati ya pili iliongozwa na Mheshimiwa Mbunge wa Kisarawe, Athumani Janguo. Hapa ninaposhiriki mimi napafahamu vya kutosha, kwa hiyo, nitazungumza namna ambavyo tulishiriki katika kulifuatilia suala hili la Mahakama ya Kadhi Mkuu wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulijigawa katika makundi matatu. Kundi la kwanza lilikwenda katika nchi za Kenya na Uganda, kundi la pili likaenda katika nchi za Msumbiji na Afrika Kusini ili kuangalia kule wenzetu waislamu wa nchi zile namna wanavyofanya kazi zao juu ya masuala haya ya Waislamu. Wengine tulibaki Dar es Salaam ambalo ndilo lilikuwa kundi kubwa na kwa bahati tulikuwa tunaangalia madhahebu mbalimbali ya kidini ili kuja kutoa maoni yao kuhusiana na suala hili.

Bahati nzuri tulipata maoni kutoka madhehebu ya Kiislamu na vilevile kutoka madhehebu ya Kikristo na madhehebu mengine. Lakini kimsingi hakuna waliokataa suala hili kuanzishwa na wenzetu nchi jirani nchi ya Kenya wao wana waislamu asilimia 10 lakini huduma hii ya Mahakama ya Kadhi wanaipata. Lakini sisi hapa Tanzania ambapo Waislam tunaongoza kwa wingi katika nchi hii hatupati huduma hii. Hili nalisema nikiwa na uhakika kwamba Waislamu ndiyo wengi katika nchi hii, si kwamba nabahatisha, ninalo kwenye takwimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili ambalo Waislamu wanaliomba kwa nchi yao, wao hawataki kuhukumiwa kama vile hukumu za Kiislamu zinavyoendeshwa kama nchi nyingine. Wao wanataka baadhi tu ya hukumu wazipate. Kwa mfano, mambo ya mirathi, mambo ya ndoa, mambo ya talaka na kadhalika.

Lakini yale mambo mengine makubwa makubwa kama ya kukatana mikono kwa wezi na mambo yale ya kupigana mawe mpaka kufa kwa wazinifu yale hatukupendekeza katika mapendekezo yetu, ingawa na hayo yangetusaidia kama tungeyafanya kwani ujambazi ungeondoka. Maana mtu akikatwa mkono kama ni jambazi akitembea na vibutu vya mkono, mtu akimwona mwenzake na yeye atajua hiyo si kazi bora aiache na wazinifu vilevile.

Wanaume na wanawake ambao wameshakua wakizini wanapigwa mawe mpaka wanakufa, wakifaka kama watu 40, wangine waliobaki wote wanarudi nyuma na UKIMWI utakimbia. Lakini sisi hatukutaka kufika huko, tuliomba baadhi ya mambo yale tu niliyoyataja na hayo si lazima kwa watu wote ni kwa wale watu ambao wanataka kutumia nafasi hiyo kwa dini yao wawe na ruhusa kutumia nafasi hiyo; na wale ambao hawataki kwa sababu Mahakama za Serikali zipo wao watakwenda kwenye Serikali.

Lakini na wale wanaotaka na wao wapate. Kwa hiyo, nasema suala hili wakati wake umefika na lisicheleweshwe tena mpaka ikafika mwisho wa mwaka. Kwa sababu huko nyuma siku zote Kamati zilikuwa zikitoa mapendekezo lakini zinatoa mapendekezo

mwisho wa mwaka na zikifika mwisho wa mwaka karibu na uchaguzi inakuwa hazitekelezwi tena. Kwa hiyo, mara hii tunasema mapema suala hili limo kwenye Ilani yenu ya Chama cha Mapinduzi.

Kama mnavyosema Kambi ya Upinzani tunasoma, tayari tumelisoma tumeliona hilo limo. Kwa hiyo, mlifanyie kazi hivi sasa msilicheleweshe mpaka likajafanyiwa kazi mwisho wa mwaka. Huko tutakuja kusema kwamba mnalifanya kwa sababu ya kupata kura.

Kwa hiyo, tunaomba suala hili lifanywe mapema iwezekanavyo vinginevyo itakuwa kila siku tunalisema humu, mkilifanya tutasema. Kama tulivyozungumza juzi hapa kwamba mtasema nyinyi ni sera yenu lakini na sisi itakuwa ni sera yetu maana tunawa-*pump*, hamfanyi mpaka muambiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa suala hili nafikia hapa. Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya majumuisho yake hapa atueleze kinaga ubaga suala hili limefikia wapi ingawa kidogo ameliorodhesha kwenye Hotuba yake kwamba nalo litaanza kuangaliwa na Tume ya Kurekebisha Sheria lakini tunataka ufafanuzi wa kina ili tujue na wenzetu wanaotutuma na kutusikiliza wajue suala hili limefikia wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naona muda unakwenda, naomba nifikie hapa ili niwaachie na wanzangu japo kidogo na mambo mengine naweza nikachangia japo kwa maandishi. Ahsante sana, na nashukuru kwa kunisikiliza.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hotuba hii iliyopo mbele yetu ya Wizara ya Katiba na Sheria. Awali ya yote nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Waziri wa Katiba na Sheria , Naibu Waziri Mheshmiwa Mathias Chikawe, Mwanasheria Mkuu, Mheshimiwa Johnson Mwanyika, Katibu Mkuu wa Wizara hii pamoja na Watendaji wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vilevile kwa niaba ya Wanawake wote wa Mkoa wa Tabora kutoa salama za rambaramba kwa msiba wa Mheshimiwa Amina Chifupa. Nizidi kuwapa pole na niwaombee faraja familia yote ili waweze kuwa na imani kwamba Mwenyezi Mungu ndiyo mwenye maamuzi na niombe Mwenyezi Mungu aweke roho yake mahali pema peponi. *Amin*!

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba niunge mkono Hotuba hii asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni nyeti sana na inagusa mambo mengi sana katika Jamii. Mimi nianze na kuzungumzia Sheria ya Ndoa. Sheria ya Ndoa ina upana wake, si ndoa kama ndoa ya watu wawili kukubaliana, lakini ndani yake kuna mambo mengi sana ambayo yanatakiwa kufanyiwa marekebisho.

Kuna suala zima la mirathi, naomba Serikali iingalie sana. Wajane wanapata taabu sana, hususan anapofariki mwanaume. Anapofariki mwanaume hawa wajane

wananyanyasika sana na familia za wahusika. Mimi natamani hata kulia unavyoniona wanavyohangaika. Kuna akina mama wengi ambao wamefika nyumbani kwangu wanahangaika na makaratasi.

Sasa kama Serikali inaweza kuleta sheria hapa za dharura, kwa nini hii Sheria hawaitilii mkazo na kuiwekea maanani kwamba wanawake ndiyo wenye kukaa na watoto na wanawake ndiyo wenye kupata shida na sasa hivi tuna hili tatizo la ugonjwa wa UKIMWI. Baba anakufa mama anakufa, watoto hawana uwezo wa kuhangaika kutafuta mirathi yao. Hivi kwa nini Serikali isiwe wazi kwamba wale watoto wanaobaki kwa kutumia vifungu vyao wawe ndio warithi wakubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alipokuwa kwenye Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto alifanya kazi nzuri sana kuwasaidia wanawake. Leo kitu gani kimembadilisha asione uchungu wa jinsi wanawake wenzie wanavyopata shida. Lakini pia nimshukuru , kulikuwa na mama mmoja ambaye alikuwa na matatizo sana kutoka Shinyanga, alikuwa na matatizo ya mirathi lakini namshukuru aliweza kumsaidia. Je, atasaidia watu wangapi kwa mmoja mmoja?

Kama Sheria hiyo ingekuwa ipo ndani ya utaratibu sidhani kama hawa watu wanaweza kunyanyasika kama wanavyonyanyasika sasa hivi. Wameunda vikundi vya wajane bila kutarajia kutokana na kufukuzwa kwenye maeneo; lakini nimpongeze pia Mheshimiwa Rais, juzi alipokuwa anahutubia Mkutano wa UWT aliliona hilo, alisisitiza. Kwa hiyo, na mimi niongeze kwamba Mheshimiwa Waziri hebu ipokee hiyo nayo kama ni changamoto kwako wewe kutekeleza hiyo azma ya Rais ya kuhakikisha kwamba katika uongozi wake hili suala lisijirudie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nizungumzie suala la Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, lisiangaliwe kwa namna moja tu. Lakini tuna tatizo pia la uhamisho wa wanawake pale mwanaume anapopata uhamisho kwenda kituo kingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanamke anaambiwa asubiri asimfuate mume wake, tutamthibitisha vipi kama kweli hii sheria ipo kama Serikali haitaweka utaratibu baina ya mtumishi na sheria ili mwanaume au mwanamke anapohamishwa, wafuatane wote pamoja. Serikali iangalie huyu wanayemhamisha ana mume au ana mke? Mimi nina mfano hai, pale kwangu Tabora, kuna mtumishi mmoja amehamishwa ana mwaka wa tano huu, mke wake yuko pale. Kinachozungumziwa ni kwamba, kule anakokwenda hana ajira. Kwa hiyo, hamwoni kwamba, kutakuwa na wimbi kubwa la nyumba ndogo huko anakokwenda baina ya baba na mama. Kwa hiyo, mimi nina imani kwamba, kama itaendelea hivi, kweli suala la UKIMWI litakuwa tatizo katika Nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema Sheria ya Ajira iangalie upya na kujipanga upya ili anapoondoka mwanaume au anapohamishwa aulizwe au katika kumbukumbu za mafaili yao iangaliwe kama ameoa au ameolewa. Kwa hiyo, wanapoanza kumhamisha, wamhamishe na mke wake na watoto wake. Kusiwe na tabaka, mara huyu akae kushoto, mwingine kulia, hivi Serikali hamwoni kwamba ni tatizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Waziri Mwanamke alione hilo na bahati nzuri Wizara ya Utumishi pia yuko Mwanamke, sina wasi wasi nao. Ari Mpya, Nguvu Mpya, wanafanya kazi vizuri Mawaziri wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia hilo suala zima la Sheria hii ya Ndoa kwa uchungu, naomba nizungumzie suala la Mahakama Kuu. Mahakama Kuu ya Kanda, kuna matatizo kwa Mkoa wa Tabora. Mahakama hii imeunganishwa Kigoma, Tabora na Shinyanga. Ningemwomba Waziri, siku moja atembelee Mahakama ambayo wanafanya kazi wale Majaji katika mazingira magumu sana. Ofisi walizonazo hazitoshi, Majaji wako wengi, vitendea kazi hakuna. Hivi unategemea hawa Majaji watafanyeje kazi na kumaliza kesi kwa muda unaopangwa? Kwa hiyo, hilo ni tatizo sana, Jaji anakuwa yuko juu, sekretari anakwenda kumtafuta huko chini, kwa sababu ile nyumba ni ya kupanga, ni jengo la Halmashauri ya Manispaa, kwa hiyo halitoshelezi, haikujengwa kama Mahakama Kuu. Pale, pale pana Mahakama ya Wilaya, sasa inakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba Mheshimiwa Waziri aliangalie kwa sababu, fedha zinazotolewa kwa kujenga Mahakama hii ya Kanda hazitoshi, ni sawa na kukarabati tu, hamna kitu. Lakini kama tungekuwa *serious* kwa jambo kama hili, ile Mahakama ingekuwa tayari ili kuondoa usumbufu. Kwanza, wafanyakazi wenyewe wanavunjika moyo, ila kwa sababu ni kazi ya ajira yao na waliisomea, wanavumilia. Kwa hiyo, mimi naomba Kitengo hiki kiangaliwe sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya Mheshimiwa Waziri, naomba jengo hili liishe, hapo ndipo tutaelewana, naomba liishe, kwa sababu linatia uchungu sana. Ukiwaona watu na visomo vyao, watu na majoho yao, wananyanyasika, hawana hadhi. Mimi naomba hili liangaliwe sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia hata wafanyakazi wa kawaida wa Mahakama hii. Kwa kweli tutawatafuta ubaya, kwa kuzungumza kila siku wimbo wa rushwa. Mheshimiwa Waziri atakapokuja, nitampeleka Mahakama ya Mwanzo, akaone jinsi wafanyakazi au Mahakimu wanavyofanya kazi kwenye Mahakama ya Mwanzo ya Manispaa. Ningeomba Serikali, vitu kama hivi iviangalie sana. Mimi sina wasi wasi na utendaji wa Serikali, nina imani nayo sana. Lakini kwa haya mambo madogo madogo, Waziri hawezi kuyafahamu, ni vyema katika bajeti zao wanazozileta, wawe makini kuangalia mahitaji yao ni nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende haraka haraka, Mahakama ya Kazi, Ardhi, Biashara na kadhalika. Hizi hazitambulikani kwenye Mikoa yetu, kwa sababu ziko Makao Makuu tu peke yake (Dar es Salaam). Sasa huku watu haki zao zitatendekaje? Hakuna haki inayoweza kufuatwa na mtu kutoka Tabora aende mpaka Dar es Salaam ana kesi ya ardhi, ana kesi ya biashara, ana kesi ya ajira, itakuwa siyo rahisi. Tunaomba Wizara ianze kupanua wigo, uwepo muda maalum, watu wapeleke malalamiko yao kwa muda maalum. Hawa Makakimu wa Idara hizi watembee ili angalau wananchi waweze kupeleka malalamiko yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni elimu. Elimu ya sheria itolewe kwa wananchi wote kwa Lugha ya Kiswahili. Mtu anaweza kuwa anajua haki yake, lakini lugha iliyoandikwa, imeandikwa kitaalamu kwa Lugha ya Kiingereza. Unapompelekea mwanakijiji kule atasomaje haki yake? Yeye mwenyewe kama ataijua ile sheria kwa lugha ya kiswahili, atasoma kwanza, atajiridhisha katika nafsi yake kwamba, hapa nimekiuka sheria, hapa sijakiuka sheria, nifanyeje. Siyo wote ambao wana uwezo wa kwenda kwa *Advocate*. Nani anayeweza kwenda kwa wakili huyo wa kujitegemea ili aweze kumsaidia. Mimi naomba pamoja na kwamba wamesema wako kwenye mchakato wa kurekebisha sheria kwa kutumia Lugha ya Kiswahili, nadhani kuna sheria nyingine ziangaliwe haraka sana ili mtu anapodai haki yake, ajue anafanya nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ningemwomba Waziri kwa kupitia kwako, aweze kuangalia sheria hii ya uhalali wa *fifty fifty.* Kwa hiyo, ninaomba aangalie maana nimeangalia hapa, naona kama Majaji kweli tumejitahidi kuwaongeza, lakini naona bado kuna haja kubwa sana ya kuongeza Majaji Wanawake, Mahakimu Wanawake, hiyo *fifty fifty* tuanze kuidai sasa. Ni kwa nia nzuri, naomba Wanaume waelewe. Mnapokuwa na ushauri wa mseto, mnapokuwa na maamuzi ya mseto, ndipo nyumba inaboreka, mnapokuwa wawili ndani ya nyumba. Kwa hiyo, tusione ajabu tunapoomba kuwa wawili ndani ya siasa au kuwa watu wawili wawili ndani ya siasa, ndani ya ajira na kadhalika. Wanaume naomba mtuunge mkono, sisi ndio mama zenu, sisi ndiyo dada zenu. Kwa hiyo, huo uwiano alioweka Mwenyezi Mungu tusiukwepe, lazima tukubaliane sote. Hata sasa hivi kuna suala zima la asilimia 50 kwa 50 ya Ubunge. Naomba Wanaume mtuunge mkono pale sheria itakapokuja kuletwa, sisi chonde chonde tunawaamini sana na ninyi naomba mtuamini katika utendaji wetu wa kazi ili angalau hiyo sheria ikifika, basi mtu wa kwanza kutuunga mkono awe mwanaume. Tunawaomba sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niunge tena mkono hoja hii asilimia mia kwa mia na kumtakia mama yangu, dada yangu, kazi njema na *Inshallah* Mwenyezi Mungu, ataipitisha bila matatizo. Asante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba, tunakushukuru sana kwa mchango wako. Tukukumbushe tu kwamba, *fifty fifty* ni kwa Wanawake na Wanaume si kwa Wanawake tu.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nitoe mchango wangu kidogo. Kwanza kabisa, napenda kumpongeza Mheshimwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Katibu Mkuu na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wakurugenzi, pamoja na Viongozi wa Taasisi zote ambazo zinaungana pamoja kwenye hoja hii iliyoletwa Bungeni hapa ya Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba au Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitakuwa na michango michache tu. Sasa mimi simjibu mtu yeyote, natoa mchango wangu. Lakini kama kuna ambaye atapata majibu, basi ni bahati nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina Katiba, kwa hiyo, suala la kuandika Katiba upya mimi haliniingii, hatuna muda wa kupoteza, haliniingii kabisa. Huenda tunafanya makosa ya viapo. Mimi nilipoingia Bungeni niliambiwa nile kiapo kwa mujibu wa Kanuni ya 25(i) inayosema: "Kiapo cha uaminifu kilichowekwa na Kanuni hii kitaapishwa kwa kila Mbunge" na kiapo hicho kinasema hivi: "Mimi… (kwa kutaja jina), nitakuwa mwaminifu kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuitumikia kwa moyo wangu wote na kwamba nitaihifadhi, nitailinda na nitaitetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, iliyowekwa kwa mujibu wa sheria." Hii hapa, mimi nitaihifadhi, kuitetea na kuilinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunayo Katiba na Katiba hii ya mwaka 1977 imefanyiwa marekebisho kuanzia mwaka 1977 na ndiyo tuliapa sisi tuliomo humu ndani na huwa inarekebishwa kila baada ya miaka mitano tunapoelekea kwenye uchaguzi. Lakini kuna marekebisho makubwa ambayo yalifanyika mwaka 1992, ambayo yalituingiza kwenye Mfumo wa Siasa ya Vyama Vingi. Sasa hii ndio Katiba tunayo, lakini hatuzuiwi kuleta mapendekezo ya kurekebisha Katiba na yana utaratibu wake. Sasa nadhani sisi kama Wabunge tuwasaidie wananchi, tusiwapotoshe. Kama yako mapendekezo yaandaliwe, hoja ziletwe humu ndani, maana inafika mahali kama tunafanya kazi hatuna mwongozo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba ndio Sheria Kuu, ndio Mwongozo Mkuu, halafu ufafanuzi wa ndani uko katika sheria. Sasa kama unataka Katiba iingize kila kitu, basi haitakuwa Katiba. Katiba ni mwongozo wa msingi ambao unafuatwa na utekelezaji wake unatungiwa sheria na ndio kazi tunayotakiwa kufanya hapa Bungeni. Sasa kama kuna hoja yoyote ya kurekebisha Katiba, inaletwa kwa hoja, tusiwapotoshe wananchi wakadhani hapa tumekuja kucheza cheza, hapana, tumekuja kufanya kazi ya maana sana. Kwa hiyo, mimi nitaitetea Katiba hii na ndio tunayoizungumzia na sheria zitakazotungwa zitaelekea kwenye kutekeleza sheria. *(Makofi)*

Nazishukuru sana Mahakama ya Rufaa, Mahakama Kuu na Mahakama zote kwamba, hicho ni chombo cha *checks and balances* kwa Bunge. Kama kuna sheria tumezipitisha zinakwenda kinyume na Katiba, wao wenzetu wanatuelekeza kwamba hii inapingana na Katiba. Sasa mimi hapa ningependa tupate ufafanuzi, utaratibu gani unatumika, maana isije ikawa tunakaa tu, Mahakama imesema hii inakwenda kinyume na Katiba. Sasa tujue utaratibu wa kuanzia hapo ni upi ili sisi Bunge tutekeleze wajibu wetu kwa kusimamia kwamba sheria zinarekebishwa kulingana na matakwa ya Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu utungaji wa sheria. Nadhani Serikali ingetusaidia hasa Wizara hii kwamba, kila wanapokuja kwenye bajeti, baada ya bajeti kupitishwa, watuletee mpango wa kurekebisha na kutunga sheria ili na sisi Wabunge tufanye utafiti, tusome sheria nyingine za wenzetu nchi nyingine wamebadilisha badilisha vipi.

Kwa hiyo, ningesisitiza hapa kwamba, kwa kweli ile programu ya kutunga sheria na kurekebisha sheria, ingekuwa *tabled* kwenye Bunge, tuijue. Hii kwa Kiingereza kwa Mwanasheria Mkuu mnaita *Legislative Programme*, ni kitu muhimu sana kwamba ukiwa

nacho hicho, basi hata mtu mwenye hoja na sheria kwamba inampa tatizo, anajua kwamba hii itafanyiwa marekebisho na vilevile wananchi waingie kwenye mchakato wa kutoa maoni. Ukitoa mapema kwa mwaka, inasaidia wananchi kushiriki katika mchakato wa kurekebisha sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sheria nyingi ambazo zinahitaji kuangaliwa upya, kwa sababu kwanza mazingira yenyewe wakati zinatungwa ni tofauti sana na mazingira ya sasa. Kwa mfano, kwa bahati nzuri mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Bishara, ambayo inatazama Sekta ya Viwanda, Biashara, Nishati na Madini. Katika sekta hiyo kuna sheria kama tisa. Moja ya sheria hizi ina miaka 42 toka imetungwa mwaka 1965 ya *National Development Corporation*. Sasa Shirika kama hili la Maendeleo hali ya utungaji wake mwaka 1965 na sasa hivi ni tofauti kubwa. Kwa hiyo, hizi ni sheria za kuzipa kipaumbele katika marekebisho yake.

Ukiangalia katika sheria hizi tisa za maeneo hayo ni sheria za mashirika ambayo ni muhimu sana katika uchumi wa nchi. Kwa mfano, hii ya *National Development Corporation, Tanzania Petrolium Development Corporation, Tanzania Bureau of Standards, Centre for Agricultural Mechanization and Rural Development (CAMARTEC)* hiyo ya 1981, *Tanzania Industrial Reseach and Development Organization, SIDO* ya mwaka 1979, *TEMDO* ya *Engineering* na kadhalika ya mwaka 1980 na nyingine *BET* ya Biashara ya Nje, ambayo biashara imebadilika sana mfumo wake *(Globalization)* ya mwaka 1978, *College of Business Education* ya mwaka 1974.

Sasa ukiziangalia zote ni kati ya miaka 42 na 27 ni muda mrefu, nchi imebadilika sana. Kwa hiyo, nadhani hiyo *Legislative Programme* au Mpango huu wa Kurekebisha Sheria, kwa kweli ungetusaidia hata kama hatutamaliza zote, lakini tutasema *priority* ni hii kwa wakati huu, hata Bunge liweze kusaidia kujiandaa na kupata maoni ya wananchi wanasema nini kuhusu vyombo hivi vya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ninataka kuchangia ni uandikishaji wa vizazi na vifo. Hili eneo hebu tulitazame tena. Tungeomba lipewe kipaumbele hili. Tulikuwa hatulioni uzito wake, lakini sasa hivi wakati tuna shule za sekondari kwenye kila Kata, sasa vyeti vinahitajika. Watu wengine wamezaliwa kwenye vijiji ambavyo hata zahanati hakuna, yuko shuleni anaulizwa, umezaliwa tarehe gani? Inakuwa tatizo. Sasa hao ambao muda umepita, si kitu tutawashughulikia, lakini ni vuzuri tugange yajayo kuanzia sasa hivi. Labda tungeamua kabisa kwamba, kuanzia mwaka wa fedha 2008/2009, kusiwe na mtoto anayezaliwa ambaye hataandikishwa, kusiwe na kifo ambacho kitatokea ambacho hakitaandikishwa. Sasa tutaifanyaje hiyo? Sasa hivi tunaimarisha Serikali za Vijiji, wasipewe zile kazi za kitaalam zaidi. Lakini hivi daftari la kumwandikisha mtoto aliyezaliwa na Mama Habiba pale Bumbuli kwa tarehe hiyo, Afisa Mtendaji wa Kijiji anashindwa kuandikisha hiyo kweli? Halafu hayo ya sheria sasa yakaja kufanywa vizuri na wale ambao wamesomea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia katika kitabu cha bajeti, kuna utaratibu wa kufanya semina katika ukurasa ule wa 40 kwamba, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini, watafanya mafunzo kwa Watendaji wa ngazi za Wilaya, Vijiji na wadau mbali mbali. Hili kwa kweli lipewe msingi kwa sababu sasa hivi wananchi wanahangaika sana.

Anakwambia sasa kijana wako anakwenda kidato cha kwanza, lakini kuna mahitaji, mojawapo ni hicho cheti cha kuzaliwa. Sasa hao ambao hawakupata nafasi hiyo tutawashughulikia, lakini tugange yajayo, tuweke mahali pa kuanzia kwamba sasa hapo tushughulike na hao ambao wamekosa nafasi hiyo.

Mchango wangu ni huu na nasema naunga mkono hoja hii vizuri sana na Mheshimiwa Waziri, aendelee hivyo hivyo na ushirikiano huu ambao upo sasa hivi. Sisi tuko pamoja naye. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuweza kuchangia wakati huu. Naomba nianzie na Sheria ya Ndoa na Mirathi ya mwaka 1971. Sheria ya Ndoa na Mirathi ya 1971 ni sheria ambayo inapingana na Sheria ile ya Kujamiiana, hasa pale tunapoanza kutazama suala la nani mtoto kiumri. Sheria ya Ndoa na Mirathi ya mwaka 1971, inamtambua mtoto wa kike mwenye umri wa miaka 14 kwamba ni mtu mzima, anaweza akaolewa kwa maridhiano ya muoaji na wazazi wa mtoto anayeolewa. Bado sheria hiyo ina ubaguzi, inamtaja baba akiridhia na siyo mama, inasema labda tu kama baba hayupo, basi ndipo mama anaweza akaridhia sheria hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Kujamiiana inamtambua mtoto ni yule mwenye umri chini ya miaka 18. Kwa hiyo, chini ya hapo sheria hiyo inasema kwamba, huyo mtoto wa kike atakuwa amebakwa. Kwa hiyo, unaona wazi wazi kwamba, sheria hizi mbili zinapingana. Ninaomba Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Katiba, atueleze ni kwa nini sheria hizi bado zinapingana na Serikali hiyo hiyo moja inaziruhusu, wakati huu inaruhusu na wakati huu inageuka kuwa kinyonga kwa mtu yule yule mmoja? Kama Serikali imekusudia kuleta marekebisho; kwa nini haijaleta na kwa nini tusiione Serikali yenyewe kwamba, ndiyo inayovunja sheria kwa kutokuleta mabadiliko haraka iwezekanavyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ambapo Serikali na Bunge imekwisha saini mkataba wa kimataifa kuridhia kwamba umri wa mtoto mdogo ni chini ya miaka 18 lakini bado inakumbatia sheria ya ndoa na mirathi ambayo hata hivyo kwa kiwango kikubwa sana inamnyanyasa mtoto mwenyewe na inamnyanyasa mwanamke. Mheshimiwa Mwenyekiti, Je, Waziri atakuwa na maelezo gani katika hilo ambalo Serikali waziwazi na kwa makusudi inavunja sheria yenyewe na bado inakumbatia? Tuwaeleweje watendaji wetu hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Kurekebisha Sheria ina maelezo gani juu ya hili? Inarekebisha nini; kama kuna sheria mbaya namna hii na wao wapo au wamekwisha rekebisha lakini kikwazo ni Watendaji Wakuu kwa maana ya Baraza la Mawaziri, kwa maana ya kutokuileta haraka Bungeni au ni Mwanasheria Mkuu ndiye anayechelewesha? Sasa ni nani ambaye ni mzembe katika vyombo hivi vinavyohusika kuleta Bungeni sheria hii ibadilike, ili tuweze kumfahamu, siyo hii ya kupakana mafuta kwa mgongo wa chupa na kufichiana madhambi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba leo Mheshimiwa Waziri, atuambie ni nani hasa amekuwa akichelewesha na wakati wote maswali Bungeni yamekuwa yakiulizwa,

wananchi wamekuwa wakiulizwa, watu wamekuwa wakinyanyaswa mahakamani kwa sheria hizo zinazokinzana? Naomba hilo nielezwe kabla sijaondoa shilingi yangu huko tunakoelekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu haki za binadamu, katika haki za binadamu tunapokuwa kwenye usawa mbele ya sheria, naomba ninukuu baadhi ya maneno usawa mbele ya sheria katika kitabu cha Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora - Tambua haki zako na wajibu wako inasema hivi: "(i) watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki bila ubaguzi wowote, kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria. (ii) Ni marufuku kwa sheria yoyote iliyotungwa na mamlaka yoyote katika Jamhuri ya Muungano, kuweka sharti lolote ambalo ni la ubaguzi ama wa dhahiri au kwa taathira yake." Ni moja ya mambo ya usawa mbele ya sheria katika sita yaliyopo. Mawili nimeona niyasome ili kuweza kuendelea na hoja yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usawa mbele ya sheria kwa mtu utekelezaji wake umekuwa ni mgumu mno; ni mahali gani ambapo hutapata malalamiko kutoka kwa Watanzania? Ukienda katika ajira, pensheni, mafao, watu wa *NSSF*, kwa mfano, Bima na kadhalika, kote malalamiko yako mengi. Malalamiko makubwa na mengi ya uonevu katika Serikali ya Utawala Bora.

Mheshimwa Mwenyekiti, ukienda katika vyombo vya sheria tunapotegemea haki itendeke, iwe Polisi, iwe katika Mahakama na katika Vyombo vinavyotetea haki, malalamiko yako makubwa. Mambo ya miradhi, leseni mbalimbali, jinsia, mazingira na ukwepaji wa ulipaji wa kodi mbalimbali, zote hizo ni kukiuka haki za binadamu na kote huko kuna malalamiko chungu mbovu. Kwa mtu mdogo, ndio hana haki kabisa, mara nyingi haki hutendeka kwa walionacho, wasionacho hakuna haki na hata sheria haiwatetei wasiokuwa nacho, inawatetea tu wale walionacho, maana mkono mtupu haulambwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna msemo maarufu tunaufahamu hasa wana-CCM na kwa ujumla niseme Watanzania wote kwamba, "rushwa ni adui wa haki, sitotoa wala kupokea rushwa." Narudia, rushwa ni adui wa haki, sitatoa wala kupokea rushwa. Huu ni wimbo, tena wimbo unaowekewa *rhythm,* wimbo unaowekewa ala za muziki ili uchezwe vizuri. Ingawa tunajua kwamba rushwa hupunguza uwezo wa utendaji bora wa Serikali, pia rushwa kwa yule anayetoa na hasa wadogo wadogo, hukosa uwezo wa kimaisha na kupanga bajeti zao. Kwa wale wanaopokea, hujijenga kimaisha na pia bajeti zao huwa zinakuwa nzuri na maisha yao huwa yanaboreka. Lakini mbaya zaidi, rushwa hupunguza mapato ya uchumi Kitaifa.

Wanasiasa ndiyo tunaowatetea na kuwasemea wananchi, lakini bahati mbaya sana, baadhi ya wanasiasa tena walio wengi, nao wamejiingiza katika rushwa. Ukichaguliwa kwa kutoa rushwa, utatetea haki ya rushwa? Kama mimi nimetoa rushwa nikachaguliwa, mwananchi niliyempatia rushwa akanichagua ana malalamiko juu ya rushwa; je, mimi nitakemea wakati mimi nimechaguliwa kwa rushwa? Watalaam na wasomi wanaojua mambo haya, wanasema hivi; naomba ninukuu kingereza kidogo: *"*Rushwa ya wanasiasa ni satarani." Hii ni kama donda ndugu na yenye madhara

makubwa hasa katika utendaji mkubwa wa Serikali. Mwanasiasa ambaye unategemewa uiongoze Serikali, wewe ukiwa ni mla rushwa na mtoa rushwa, hutaweza kuikemea Serikali. *(Makofi)*

Maana mwanasiasa unaweza ukawa Waziri, ingawa uko katika pande mbili, uko Serikalini na ni mwanasiasa kama wewe unashiriki katika vitendo vya rushwa, umeiua Serikali. Watu wanaokumbatia rushwa na kuharibu zaidi ndugu zangu ni wasomi, wafanyakazi ndiyo hao tunaotaka maisha mazuri. Rushwa kubwa ndizo zinazoua nchi, rushwa ipo popote duniani ingawa Tanzania imejitahidi sana. Katika nchi zote za Afrika, Tanzania ina unafuu, ukianzia kwenye unafuu kabisa pale ambao ni Botswana, inafuatiwa na Mauritius, South Africa, Nambia, Seychelles, zije nchi nyinginezo Tanzania ni ya 17 kwa unafuu. Katika nchi zote za Afrika unazozifahamu sijui hamsini na ngapi, imejitahidi zaidi kwa Ulimwengu mzima ni ya 93. Katika nchi zinazoonekana angalau zina unafuu bora 100 duniani, basi Tanzania ni ya 93. Tunajitahidi sana. Majirani zetu hapa Kenya, wanawataja wabaya zaidi katika haya. Ukitaka kuyapata yote hayo, kasome katika *internet* utayapata.

Sasa ninawaombeni sana ndugu zangu wasomi, popote mlipo, tuwajali zaidi wananchi na hiyo rushwa tunayoichukua kwa wananchi wadogo wadogo, tunawaumiza zaidi maana wao hawana chochote, wewe angalau una uhakika wa kila mwezi kupata chochote. Yeye hana uhakika, lakini wanapokuja kutaka huduma kwako, unataka rushwa kutoka kwao. Naomba tuwasaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia 90. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuongea machache. Kabla ya kuongea, nina usemi aliousema Mkoloni mmoja, Donald Cameroon tarehe 10 Oktoba, 926 wakati akizindua Baraza la Kwanza la Kutunga Sheria katika Shule ya Aghakhan, ambayo sasa hivi ni Tambaza. Alisema: "Nafungua Baraza la Kutunga Sheria siyo kuwa mahali pa Serikali kushinikiza matakwa yake, bali mahali pa wawakilishi wa wananchi kutoa maoni yao na kusema wananchi wao." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisemi hivyo, watu wasinielewe vibaya. Lakini inavyoonekana, haijawa lakini nahofia kwamba, Serikali yetu inaweza ikashinikiza matakwa yake katika Bunge hili kwa kutumia Chama. Sasa kama alivyosema, naomba nitoe maoni pamoja na kusemea watu wa Biharamulo. Watu nitakaowasemea kwanza kwa kuwa ni Wizara ya Sheria ni Mahakama. Mahakama ya Wilaya ya Biharamulo, miaka yote ya uhuru haipo. Hakimu wa Wilaya, anafanyia kazi kwenye gofu la wodi la wanawake katika hospitali ya wakoloni, iliyojengwa miaka zaidi ya 100. Shahidi ni Mheshimiwa Paul P. Kimiti, alipokuwa Mkuu wa Mkoa alikemea, alijitahidi lakini ameacha hivyo hivyo mpaka leo Hakimu wa Wilaya anafanyia kazi kwenye iliyokuwa wodi ya wanawake. Bahati mbaya hata Jaji anapokuja, anakaa pale pale kufanya mambo.

Mimi naona hii kama ni aibu, kwa nini tumejenga Bunge zuri namna hii, tusiende chini ya mti kukaa? Ni shauri ya maudhui. Kama tungekuwa chini ya miti, ndiyo tunge-*discuss* lakini ndipo watu wangetuheshimu kwamba, kweli hapa sheria itatungwa? Hivi kweli Hakimu chini ya mti atatoa haki? Chini ya gofu la wodi ya wanawake! Naomba sana sina matatizo na Mheshimiwa Waziri, lakini naomba uniambie Mahakama ya Wilaya ya Biharamulo, itajengwa lini ili watu watoke kwenye gofu la wodi ya wanawake? *(Makofi)*

Hakimu wa Wilaya hana nyumba anapanga. Kupanga kuna matatizo, anatoa haki hivi akipanga kwenye nyumba ambako wanapika gongo, kesho yule mtu akishikwa na gongo atamhukumu si siku hiyo hiyo atamwambia toka kwenye nyumba yangu? Ni matatizo tunawapa hawa. Miaka yote hiyo hivi kujenga mahakama na nyumba ya hakimu inachukua muda gani; mbona mambo makubwa tumeyafanya?

Sasa ukija kwenye Mahakama za Mwanzo, Biharamulo ina mahakimu wawili na kwa mwaka mzima Mheshimiwa Waziri, amekarabati jengo la Buselesele Wilaya ya Chato. Kweli wananchi tunawatakia wapewe haki; kama watoa haki wenyewe hawakupewa haki, hiyo haki wataitoa kwa namna gani? *(Makofi)*

Yuko hakimu mmoja amehamishwa kutoka Muleba kuja Chato, wao wanahesabiwa shilingi 150 kwa kilomita kwa mzigo, wakati wakatumishi wengine kama wanajeshi wanapewa magari, wanapewa fedha za mizigo lakini huyu anahesabiwa shilingi 150 *per kilometer per* mzigo. Hawa ni watoa haki, ambao tunastahili kuwaheshimu? Mtu anaweza hata akamhukumu Rais unamfanya hivyo? *(Makofi)*

Sasa nimesema machache, naomba niseme kubwa ambalo linanikera. Mwenzangu amelisema lakini nikiongezea si vibaya. Ndugu zangu, rushwa ya siasa, zamani kuku walikuwa hawajisaidii wanapolala, wanachunga sana. Lakini siku moja ikatokea jogoo likajisaidia hapo hapo. Makoo na vifaranga vikasema kumbe tunajisadia na hapa wanajisaidia, vikaanza kujisaidia pale. Sasa wewe jogoo mwanasiasa unapotoa rushwa; unafikiria wengine wafanye nini, wewe si jogoo umeshajisaidia pale pale? Kama Mwenyezi Mungu, angesema Wabunge walioingia kwa kutoa rushwa wafe, naamini ningebaki Kabuye, haki ya Mungu, wote mtakufa. Sidhani kama wapo wengine.

Labda Rais na Waziri Mkuu, lakini nina mashaka ni aibu na mnasema tuna heshima; heshima gani mataifa yanatuona tunatoa rushwa kununua uongozi? Leo hii tunayemuenzi Marehemu Nyerere akifufuka, mtakimbia nawaambieni. Mnamuenzi kwa maneno tu, rushwa imekithiri, mnanunua uongozi mbaya sana. *(Makofi)*

Halafu wewe unanunua uongozi, kuna mtu mmoja nilimwuliza mbona ndugu yangu anatoa rushwa, akasema ninyi wanasiasa mambo yenu yanapopinda mnayanyoosha kwa takrima, sisi tunaponyoosha ni rushwa. Ndugu zangu nchi hii tumeiweka pabaya mno. Chunga rushwa ni kansa, ni mdudu anayekula Tanzania, kesho na kesho kutwa Tanzania itatoweka, kama hatuangalii rushwa ya uchaguzi ni mbaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine haki za binadamu zikoje kama kweli katika nchi inayosifiwa...

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Mwongozo Mheshimiwa Gosbert B. Blandes – Kanuni?

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni ya 50, kifungu cha kwanza kinasema: "Ni marufuku kabisa kusema uongo Bungeni, kwa sababu hiyo, Mbunge yeyote anapokuwa akisema Bungeni atawajibika kuwa na hakika kwamba, maelezo anayotoa ni sahihi na siyo mambo ya kubuni au ya kubahatisha tu. Spika au Mbunge yeyote anaweza kumdai Mbunge huyo atoe uthibitisho wa usemi wake."

Msemaji anayeendelea kuzungumza, Mheshimiwa Phares K. Kabuye, ametoa maneno ambayo ni mazito sana katika Bunge letu hili Tukufu kwamba, kuna watu wanaonunua uongozi isipokuwa yeye peke yake. Sasa nilikuwa namtaka athibitishe usemi wake huo mzito. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Phares K. Kabuye, kabla sijatoa mwongozo wangu.

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo nililitegemea. Mimi ninao ushahidi, ninaweza nikaleta watu wa Biharamulo waliopewa rushwa na wanaohakikisha kwamba mimi sikutoa hata pipi. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, ameeleza vizuri kwa sababu usemi wako ni mzito kwamba, wote humu ndani hata mimi Mwenyekiti, hatujaingia sawa sawa, isipokuwa wewe peke yako. Sasa Waheshimiwa Wabunge, wanahisi hujawatendea haki. Mwongozo wangu ni kwamba, uliweke vizuri jambo hili kwa kulifuta.

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kulazimishwa ninaomba kufuta usemi. *(Kicheko/Makofi)*

Tunakuja kwa mauaji ya holela nayo muwe tayari kutoa hoja zenu. Tunayo sifa yetu kwamba, kweli tunaangalia haki za binadamu lakini ni katika nchi hii ambayo binadamu anauwawa na mwili wake unachomwa hadharani. Binadamu anadhalilishwa kwa tuhuma zinazoweza zikathibitika lakini Serikali inasema ni wananchi wenye hasira.

Hawa wananchi wanakaa mbinguni? Mtu amechomewa hapo viongozi, Mwenyekiti wa Kitongoji yupo hata yule aliyesema ameibiwa hawezi akasaidia Serikali, tunatukanwa na watu wanaopita na matrela, wanakuta moshi, wanakuta mtu anawaka, wanatuambia sisi tunapokuja kwenye Mabunge wanasema nini mmefika pabaya kabisa.

Mwingine alisema kwamba, Wazungu wanatuheshimu hawatusemi vibaya kwa kuwa tumewapa dhahabu wanachimba na kila kitu tumekuwa marafiki. Lakini vinginevyo, hali yetu ni mbaya. Binadamu anauawa na kuchomwa, wako wengi

wameshachomwa na kuuawa, lakini Serikali haisemi. Ni watu wenye hasira, hivi sisi tukisema tuna hasira Rais atoke kwenye Ikulu, atatoka tutakasirika ataondoka, si tutakipata cha mtema kuni? Lakini watu wenye hasira wanaua watu na wanawachoma, hawawezi kupatikana. Lazima pia tuliangalie pamoja na wimbi la ujambazi, vijana wetu wanapofanya kazi lazima waangalie, inaweza ikatokea kabisa kwa kusingizia ujambazi mtu akauawa, tumeua jambazi. Lakini nakumbuka Mkoloni mahali ambapo uhai wa mtu ulitoka, lazima upelelezi upite kuhakikisha kwamba, kweli hili ni jambazi na hili jambazi lilikuwa linapigana?

Nakumbuka Mkoloni kama unapambana na adui ukimpiga mgongoni risasi ni kesi alikuwa anakimbia, mpaka umpige kifuani. Lakini sisi ambao tumejitawala ni watu wetu, leo hii binadamu hana thamani. Unaweza ukakuta unachanja kuni kwenye msitu, ukabambikiziwa huko huko wakatangaza wameua jambazi. Penyewe mkitaka ushahidi naweza nikaleta.

Ndugu zangu, sheria lazima iangalie, sheria inalinda watu, watu wanauawa hivyo na kuchomwa moto. Akina bibi wanaosingiziwa uchawi wanauawa. Mkoa wa Shinyanga karibu kila mwaka mabibi kama 500 wanaondoka, lakini Serikali hii inayojidai inapenda watu ipo hakuna linalofanyika. Je, hao waganga ambao ndiyo wanachonganisha watu...

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo.

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Sawa leo ni kazi yangu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kwa ninayo heshima kubwa kwa mzee wangu Mheshimiwa Kabuye nimevumilia sana lugha yake aliyokuwa akiitumia katika mchango wake toka alipoanza na ninashukuru Mheshimiwa Blandes aliweza ku - *intervene* pale alipoweza kutoa hoja ya kufuta usemi wake. Lakini kila anapozidi kuendelea anazidi kutoa kauli ya kuudhi. Kwa hiyo, namuomba atumie maneno ambayo ni ya busara ambayo yanatakiwa kutumika katika Bunge hili tukufu. Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kabuye ni kanuni ile ile ni mwendelezo pale pale, kutumia lugha ambazo ni za ujumla na zinazoudhi. Sasa mara ya kwanza nilikuvumilia kidogo kwa sababu umri kidogo nikaona labda leo umeamka tofauti kidogo. Uendelee kuchangia lakini kwa lugha inayokubalika lugha ya Kibunge, vinginevyo unilazimisha kukukalisha chini. Malizia dakika zako.

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Katika kutetea watu, siyo kukalishwa tu, watu unaweza hata ukafukuzwa Ubunge.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kabuye, kaa chini. Tatizo unaendeleza mjadala na ubishi dhidi ya kiti kitu ambacho ni kuvunja kanuni zaidi. Ukishapewa mwongozo

unafuata mwongozo unatumia haki yako ya kidemokrasia ndiyo maana Mwenyekiti, yuko hapa. vinginevyo ingekuwa ni nyumba ambayo haina Mwenyekiti hapa kila mtu anajisemea tu. *(Makofi)*

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo. Kanuni ile ile ya 51 ya kutosema uongo Bungeni. Mheshimiwa Kabuye amesema wakongo/wazee karibu 500 wanauwawa Shinyanga kila mwaka, nadhani kwa sisi tunayotoa maeneo hayo ni hali ya wasiwasi sana, naomba afute kauli hiyo. Kweli mauaji yapo lakini siyo kiasi kile. Labda athibitishe kama kuna vikongwe 500 wameshauwawa. *(Makofi)*

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniongezee muda wangu unaopotea. Nilisema kwamba, vikongwe karibu 500 kila mwaka wanakufa na kuna mahali niliposoma. Lakini hata hivyo, kwa heshima ya Mwenyekiti na ndugu yangu, Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, nafuta usemi. *(Kicheko/ Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kwamba leo nimeamka vibaya ni uchungu na kama mzee kuna wakati unakaripia watoto mahali popote. Lakini pengine kwa uchungu ndiyo maana mtu anapofiwa hajui machozi yanatoka wapi. Kwa hiyo, ni uchungu na sijawahi kufanya hivyo. Unapoona mtu anakufa, mimi nimewahi kuona mtu anakatwa kwenye sherehe, mama amekwenda kuchukua kingine anatoka nje na sahani ya vyakula anakatwa shoka na ilikuwa Bwanga. Kama hilo linaendelea na kweli watu inapaswa wote tusikitike, ndiyo maana wakati mwingine unaweza ukasema kwa hasira na pengine ukavuka mipaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba sana tuangalie haki za watu na kama kitu wanakipenda tukiangalie kuna vijana wanahangaika kutafuta riziki kwa kutumia pikipiki, kwa kutumia baiskeli, lakini sheria inasema hivyo vifaa havistahili kufanya biashara. Inawezekana wakati sheria inatungwa, watu walikuwa hawajaingia kwenye ujasiriamali, leo wanatafutia mahali ambapo hata angelikuwa na fedha ya kulipia gari, gari haliendi lazima atumie baiskeli na atumie pikipiki. Vijana wengi wameshapata hasara kwa sababu wamekula mikopo ya pikipiki, leo hii wameambia pikipiki hazibebi, sijui hiyo mikopo watailipaje? Hapa Serikali yetu tukufu ilisema kwamba, italiangalia hilo jambo, lakini naona muda unakwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna vyombo vya Serikali, wakati mwingine vinanyanyasa watu. Nimeshuhudia kabisa mtu anayetuhumiwa uhalifu, anashikwa mkanda ananing’inizwa kwetu tunaita Tanganyika Jeki. Mtanzania aliyepata uhuru karibu miaka 50 ananing’inizwa kwenye Tanzania Jeki, hajabainika kwamba amekosa ni mtuhumiwa tu, licha ya kupigwa. Nalo hilo watu watanikalisha chini, lakini watu wanapigwa. Eti upelelezi, ili akiri makosa, wengine wanakiri baada ya kupigwa ili waweze kujiokoa. Nalo hilo lazima liangaliwe. *(Kicheko/Makofi)*

Lakini naomba kwa kuwa rushwa ilianzia kwetu wanasiasa, nadhani imezagaa, mimi nikipanda nalo basi, muwe tayari kunikalisha, ukifika Kibaha basi limejaa, unavikuta vi-*hiace* wanapunguziwa watu kwenye hivyo vi-*hiace* ili liweze kupita kwenye mzani sawa sawa. Unajiuliza, hawa watu wa mizani hili hawalioni? Nalo mtataka

ushahidi! Pale kuna *DC*, kuna *OCD*, miaka yote wanapunguzia kwenye *hiace* hawa hawaoni? Ukienda Kahama, karibu na mwenzangu yule anasema bibi vizee hawafi, unajiuliza hapa kuna *DC*, hapa kuna kila mtu; vipi? Kwa hiyo, hili mliangalie siyo mambo ya kuchezacheza. Kuna wakati hapa tutafukuzana, kwa kusema kwa uchungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru Mheshimiwa Phares K. Kabuye, amekemea wenye hasira kali, akaishia kuwa na hasara kali Bungeni. Mchana wa leo wazungumzaji wa leo watakuwa Mheshimiwa Diana M. Chilolo, atafuatiwa na Mheshimiwa Gosbert B. Blandes na Mheshimiwa Beatrice M. Shelukindo na baada ya hapo Mwanasheria Mkuu, atapata dakika 15, atafuatiwa na Naibu Waziri dakika 20 na Mheshimiwa Waziri dakika 40 na utaratibu mwingine utaendelea kadri ilivyopangwa. Vinginevyo nawashukuru sana kwa shughuli zilizopangwa kwa asubuhi ya leo, zimekamilika.

Naomba kusitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni.

*(Saa 06.25 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijamwita mchangiaji wetu wa kwanza, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, kutokana na masuala ya muda tumekubaliana naye na ameafiki kwamba, atachangia kwa maandishi. Kwa hiyo, isije ikahesabika kwamba ameenda Mtera. Moja kwa moja namwita Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, atafuatiwa na Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, kama mchangiaji wa mwisho kwa jioni ya leo.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hotuba hii ya Sheria. Kwanza kabisa, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, Mheshimiwa Mary M. Nagu, kwa kuwasilisha hotuba nzuri sana na makini. Vilevile nachukua nafasi hii kuwapongeza watendaji wote wa Wizara ya Sheria na Katiba, kwa kazi nzuri ambazo wanafanya pamoja na mazingira magumu yanayowakabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi nampongeza Mheshimiwa Jaji Augustino Ramadhani, kwa kuteuliwa kuwa Jaji Mkuu. Mimi namfahamu na wanataaluma wote wa sheria wanafahamu jinsi ambavyo Jaji Ramadhani amekuwa ni mchango mkubwa katika kukuza sheria ya nchi hii na tunaamini kabisa kwamba, uteuzi wake utasaidia sana Wizara hii na kuhakikisha kwamba sheria inaboreka nchini kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo nianzie na mlundikano wa wafungwa ndani ya magereza yetu. Wote ni mashahidi kwamba, magereza yetu hapa nchini yamefurika sana

na wafungwa kiasi kwamba hali mle ndani ya gereza inatisha na inatia huruma, pamoja na kwamba, tunajua mtu akishahukumiwa kifungo ni haki yake kwenda jela. Lakini mimi nilikuwa kidogo na mchango hapo hapo wa kuchangia kuhusiana na hali halisi ya wafungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi nilitaka niseme kwamba, ufike wakati Serikali kupitia kwenye Wizara ya Sheria na Katiba, tufanye mabadiliko makubwa kwa makosa ambayo ni madogo, hayastahili mtu kumpeleka jela. Hayo makosa basi yaainishwe na kama ikiwezekana sheria ziletwe hapa tuzibadilishe. Makosa madogo madogo kwa mfano, kama kutukana, mtu ameiba kuku, yale makosa yapewe adhabu ya faini. Yule mtuhumiwa akishatiwa kwenye hatia, basi apewe *option* ya kulipa faini. Mimi naamini kabisa tukifanya hivyo, wale wafungwa wa makosa madogo madogo wataweza kupunguza msongamano katika magereza yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, nigusie uhaba wa Mahakimu katika Mahakama zetu za Mwanzo. Mahakama zetu za Mwanzo ndizo ambazo ziko chini kwa wananchi walio wengi. Ndizo Mahakama ambazo Watanzania walio wengi wanazitegemea. Lakini nadhani kutokana na ufinyu wa bajeti, tunajikuta kwamba, Mahakama zetu za Mwanzo zina upungufu wa Mahakimu. Itakumbukwa kwamba, sasa hivi Wizara ya Sheria na Katiba ilishatoa tamko kwamba, Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo lazima wawe na *diploma.* Mimi hilo kwa kweli sipingani nalo, ninaliafiki kwamba Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ambao wana *diploma,* wana uelewa kuliko Mahakimu wetu ambao wako sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tatizo ambalo linajitokeza ni kwamba, kweli Chuo chetu cha Lushoto kimeendelea kutoa *diploma* kwa vijana wetu ambao tungetegemea waende kule kwenye Mahakama za Mwanzo waweze kusaidia. Lakini niseme kwa bahati nzuri au kwa bahati mbaya, mara nyingi vijana hawa wanapo-*graduate,* wanapotoka Lushoto, wengi wao hawapendi kwenda kule Vijijini, hawapendi kwenda kwenye Mahakama za Mwanzo. Wengi utakuta wanapenda ku-*up grade* kwenda kuchukua digrii Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Mzumbe au Tumaini. Kwa hiyo, kwa maana hiyo utakuta wale ambao tuliwategemea waende kwenye Mahakama za Mwanzo wanapungua. Tunakuwa na upungufu mkubwa.

Lakini vilevile wale ambao hawakuweza kwenda vyuo vingine, hawapendi kwenda Vijijini kwa sababu mazingira ya kule siyo mazuri, hayavutii mtu mwenye *diploma* ya sheria aweze kwenda kule vijijini . Kubwa ambalo linawavunja moyo kwanza kabisa ni mishahara midogo. Huyu mtu mwenye *diploma* anajiuliza kwa nini niende *Primary Court Magistrate* kwa mshahara mdogo namna hii. Kwa hiyo, ana-*opt* kwenda sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine vilevile ni kwamba, *incentives* ni kidogo. Utakuta wanakwenda vijijini; hakuna nyumba, hawana magari, hawana usafiri. Kwa hiyo, kwa maana hiyo, tutabaki kuwa na *shortage* ya watumishi hao. Mimi nilitaka nishauri kwamba, ufike wakati hawa vijana wanapotoka Lushoto, kuwatengea *at least* mshahara ambao unaweza ukawavutia ili waweze kwenda vijijini. Vilevile tuongeze mazingira kwamba, anapokwenda kule kuwa Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo, basi

akute nyumba nzuri na ikiwezekana awe na usafiri hata pikipiki au usafiri mwingine mdogo mdogo. Naamini kwa kufanya hivyo, wale vijana tutawavutia na watakwenda kwenye Mahakama zetu za Mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka kwamba, kwenye Mahakama zetu za Mwanzo, Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo anapokaa kusikiliza ushauri na mwisho kutoa maamuzi, mara zote sheria inamtaka akakae na Wazee wa Baraza, yaani *assessors*. Katika kutoa uamuzi, uamuzi wa Mahakama za Mwanzo unatolewa kwa kupiga kura. Ina maana kwamba, wale *assessors* wawili na Mheshimiwa Hakimu, lazima wote wapige kura ndiyo uamuzi unatoka. Uzoefu unaonesha kwamba, mara nyingi *assessors* wale wawili wakielewana, basi watapiga kura, watamshinda yule Hakimu mmoja na mwisho maamuzi yatakuwa ni kama yametolewa na wale *assessors*. Wananchi wa kawaida wanaamini kwamba, aliyetoa hukumu ile ni Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo.

Sasa utakuta hizi kura zinazopigwa wakati mwingine hawa *assessors* wetu siyo wataalam, watakutana na huyu mtu mwenye *diploma* kutoka Lushoto, Wazee wametoka vijijini, hawajawahi kusoma sheria, hata kidogo, lakini kwenye maamuzi huyu ambaye ni mtaalam anabanwa. Sasa mimi nilikuwa nasema kwamba, hii sheria iangaliwe vizuri, hawa *assessors* sisemi kwamba ni wabaya, lakini katika maamuzi ingekuwa ni vizuri, yule ambaye ni mtaalam wa sheria, mwenye *diploma,* basi aachiwe afanye maamuzi peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Rais, pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Katiba, kwa kuteua Majaji 21 kipindi kilichopita. Hatua hii mimi naipongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka bajeti iliyopita nilisimama hapa nikazungumza nikalalamikia upungufu wa Majaji kwamba, hawatoshi na kazi ni nyingi. Hii nyongeza ya Majaji 21 kwa kweli ni nzuri na itasaidia kupunguza mlundikano wa kesi Mahakamani. Ninampongeza Mheshimiwa Rais, kwa kuteua vilevile Majaji vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku zilizopita, tulikuwa tunaona majaji wanaoteuliwa wenye umri mkubwa sana na wanakaa kwenye benchi muda mfupi wanastaafu, tunarudi tena kwenye tatizo hilo. Lakini safari hii kwa kweli tumeona akina Mheshimiwa Lila, Mheshimiwa Mwanaisha Kwaliko, wamekuwa majaji. Kwa kweli ni vijana na naamini uchapaji kazi wao ni mzuri na wataweza kutumikia Mahakama hii kwa muda mrefu sana. Nilitaka nishauri kwamba, uteuzi mwingine unapofika basi wapo vijana wengi kama hao, waangaliwe na wapewe nafasi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa hapo hapo nilitaka niseme kwamba, kuteua Majaji ni jambo moja na Majaji kuwawezesha wafanye kazi ni jambo lingine. Tunaweza kuwa na Majaji wengi lakini kama hatujawawezesha kufanya kazi, itakuwa ni kazi bure. Kwa nini nasema hivi, nasema hivyo kwa sababu mara nyingi hawa Majaji wa Mahakama Kuu ndiyo ambao wamepewa mamlaka ya kuendesha *trials* au kesi za mauaji.

Kesi hizi mara nyingi hufanyika kwa vikao na kwa kila kanda. Kwa mfano, nitatoa mfano wa Kanda hii ya Dodoma. Kanda hii ya Dodoma inashughulikia kesi za mauaji katika Mkoa wa Dodoma na Singida.

Kwa kipindi hiki tunachozungumza, nadhani ziko kesi za mauaji 170 ambazo ziko *pending*. Sasa hizi kesi 170 kila kikao kimoja zinaendeshwa kati ya kesi nne mpaka nane. Lakini kesi hizi zimeshindwa kuendelea kwa sababu Mahakama ya Dodoma haina fungu haina pesa. Majaji tunao, Mawakili wa Serikali tunao. Makarani tunao lakini fedha hazipo. Nilitaka kusema kwamba ni vizuri tukawatengea mafungu ya kutosha ili waweze kuchapa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nilitaka nizungumzie upungufu wa Mahakimu na Mawakili wa Serikali, hii imekuwa ni kawaida na hasa kwa Mawakili wa Serikali. Tatizo kubwa sana ni kwamba wale wanaoajiriwa Serikalini, kwa sababu ya mishahara midogo, maslahi madogo, wamepaona pale mahali hapakaliki. Basi wamekuwa wakienda kutafuta *green pasture* sehemu nyingine. Matokeo yake tunakuwa tunaajiri vijana wapya na tunakosa watu wenye uzoefu wa kutosha. Ukishakosa mtu mwenye uzoefu maana yake hata ile kazi inayofanyika inaonesha kwamba, yule anayeifanya uzoefu wake siyo mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nizungumzie kitu kimoja ambacho ni muhimu sana. Mara nyingi tumekuwa tukisimama hapa, tunazilaumu Mahakama zetu kwamba wanakula rushwa, lakini ukweli ni kwamba, wakati mwingine hata Serikali inaleteleza hiyo hali. Kwa mfano, utakuta mtu alikuwa ni Karani wa Mahakama, anapandishwa cheo anakwenda gredi fulani, mwingine *Resident Magistrate* anapanda cheo kwenda ngazi fulani. Kupanda cheo maana yake ni kwamba, nyongeza yake ya mshahara imeongezeka, sasa hivi ninapozungumza, wako watu wamepandishwa vyeo muda mrefu sana, tangu wapande vyeo hawajalipwa fedha zao hiyo. Kuna mtu sasa hivi pale Mahakamani anadai karibu shilingi milioni kumi, kila siku anaandika barua anaomba hela yake na ni haki yake kama umempandisha cheo, basi mpeni haki yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kulaumu lakini hawa watu tunawaonea, Idara ya Mahakama inafanya kazi nzuri sana tena katika mazingira magumu. Wasemaji wenzangu waliotangulia, walikuwa wanasema kuna Wizara nyeti. Mimi nilitaka niseme kama kuna Wizara nyeti katika nchi hii, Wizara ya Sheria na Katiba ndiyo Wizara ya kwanza kuwa nyeti. Kwa sababu hii ndiyo inayotafsiri sheria zote tunazotunga hapa Bungeni. Ndiyo Wizara ambayo naweza nikasema kazi zake ni mtambuka, inaingia kila Wizara. Sasa bila kuwawezesha kwa kweli kila siku tutaishia kulaumu kwamba, wenzetu wanakula rushwa, jambo ambalo siyo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, mwaka jana nililalamika hapa kuhusiana na upungufu wa gari Wilayani kwangu Karagwe. Tumepata gari, Mheshimiwa Waziri nakushukuru, lakini bado tuna upungufu wa mahakimu, pale Wilayani Karagwe, yupo Hakimu wa Wilaya mmoja. Sasa inapotokea akipata dharura pengine akisafiri au akiumwa, basi kesi zote zinakuwa zimelundikana. Tunahitaji Mahakimu wa Wilaya pale wa kutosha. Angalau kwa kuanzia

kama wawili kwa safari hii. Vilevile tunahitaji Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, hawatoshi. Mahakama zangu za kule Nyaishozi, Kituntu, Kaisho, Isingiro na sehemu nyingine, kwa kweli hazina Mahakimu. Tunaomba Mahakimu waongezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, ukizunguka katika Mkoa wa Kagera ambako mimi nimezoea kupita sana, yale majengo ya Mahakama kama alivyosema Mheshimiwa Phares K. Kabuye, kwa kweli yanatia kichefuchefu, tunaomba katika bajeti hii zile Mahakama ziweze kufanyiwa ukarabati wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nataka niishauri Serikali, pamoja na kwamba safari hii tumeangalia p*riority* kwamba tunaanza na elimu, afya na nyinginezo na tumenyofoa kidogo kwenye bajeti ya Sheria. Mimi nasema kama inawezekana, *next time* hii Wizara ya Sheria kwa kweli tuipe *priority* ni Wizara ambayo inatakiwa kufanya kazi na bila kupewa fedha hawa ndugu zetu watapata shida na watashindwa kuendesha mambo yao na tutabaki kuwalaumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Asante sana. *(Makofi)*

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Asante Mheshimiwa Mwenyekiti. Moja kwa moja nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kazi nzuri anayoifanya ambayo tunaiona kwa macho. Mimi binafsi nimefanya naye kazi Wizara nyingi nikiwa mtumishi wa Serikali naye akiwa Waziri wangu. Kwa hiyo, umahiri wake ninautambua. Hali kadhalika, nimpongeze Naibu Waziri, huwa namwita yeye ni *quick to act,* unamwambia jambo baada ya dakika tano unapata jibu, kwa hiyo na yeye nampongeza sana. Watendaji wote hasa Mwanasheria tuliyenaye hapa, huwa namtesa sana kwani saa nyingine namdaka njiani nataka ufafanuzi mzito na huwa ananipa bila kusita. *(Makofi)*

Niwapongeze Majaji wote hasa wale Majaji Wanawake. Lakini vilevile nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Jaji Agustino Ramadhani, tumekuwa naye nikiwa Mbunge wa Afrika Mashariki na yeye alikuwa ni Jaji kule. Kwa hiyo, alinipa uzoefu mwingi sana, Sheria nilikuwa naiona ngumu, lakini kwa kupitia kwake na maelekezo yake, nilikuwa naona mambo siyo magumu.

Mwisho ila si kwa umuhimu, nichukue fursa hii sasa kumpongeza *colleague* wangu, tumesoma naye huko nyuma, Mheshimiwa Sofia Wambura, kwa kuwa Msajili wa Mahakama. Huwa tunasema *she is a hard nut to crack* kama Wazungu wanavyosema, lakini ana huruma sana. Yote hii imeonesha kwamba, wanawake tunaweza nafasi zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, nitaenda haraka haraka kwa sababu nina vipengele kama vinne, vitano. Najua mmechoka kuisikia Kilindi, lakini jamani nitaisemea Kilindi mpaka kitakapoeleweka. *(Makofi)*

Nimshukuru sana Mheshimiwa Manento, ambaye ni Jaji Kiongozi, aliweza kutembelea Kilindi, samahani kama nimekosea wadhifa wake, japo kulikuwa na hali mbaya, alikwama, alitaka kupinduka, lakini alipita jimbo zima akikagua shughuli za Mahakama na hakika aliyoyaona yeye mwenyewe hakuamini kama yapo ila namshukuru sana pamoja na *delegation* aliyofuatana nayo. Nimpongeze tu kwa sababu ahadi alizotoa kwamba tutapata Hakimu wa Mwanzo, tuliweza kumpata mapema kwa hiyo, ninamshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri, katika bajeti hii ya mwaka 2008, kwa sababu Kilindi hatuna Mahakama ya Wilaya, tuna Mahakama ya Mwanzo tu, kama Wilaya ambayo inakaribia miaka mitano. Je, tuko kwenye Bajeti mwaka huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu niseme mara nyingi kuchangia mchana huwa nasita sana, kwa sababu unakuta Mawaziri wanakosa muda wa kutafakari na kutoa majibu hasa hizi hoja za siku moja. Lakini leo naamini Mheshimiwa Waziri, atanitendea haki. Kuhusu Mahakama za Mwanzo mpaka sasa hivi tuna hiyo ambayo tunaitumia kama ya Wilaya na nyingine moja. Wananchi wako tayari kuchangia matofali ya kuchoma na kadhalika. Lakini tulikuwa tunaomba, pindi tutakapomaliza hizo Mahakama za Mwanzo, basi tuweze kupata watumishi, maana yake hata sasa hivi hata hizo Mahakama za Mwanzo zilizopo tumshukuru tu Mheshimiwa Manento tumeweza kupata huyo Hakimu mmoja ambaye amefanya wawe Mahakimu wawili wa Mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kulisemea hapa ni kuhusu usafiri. Wilaya ya Kilindi tunatumia Hakimu wa Handeni, ambaye yupo umbali wa kilomita kama tisini na kitu hivi, umbali kutoka hapo ambapo iko Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Kilindi. Sasa analazimika mara nyingi huyo Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo kusafiri na makabrasha muhimu saa nyingine ya siri, inabidi aondoke nayo aende Handeni na penginepo kutoka nayo Handeni kuja Kilindi Songe. Kwa kweli hata kama hatuna Mahakama ya Wilaya, hatuna Hakimu wa Wilaya mahali pale, basi Mheshimiwa Waziri nilikuwa naomba tusaidiwe usafiri hata kama ni pikipiki, ili angalau tuwe na usafiri wa kuaminika ili haya makabrasha ya watu yaweze kufika kwa usalama na wananchi kutendewa haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine Mheshimiwa Waziri nilitaka kuuliza kwa ajili ya shughuli za Mahakama kwenye kila Wilaya, najua zinatolewa fedha za ruzuku na za kwetu baada ya kuuliza tumeambiwa kwamba, zinakwenda Handeni kwa Hakimu wa Wilaya ambaye anatuhudumia sisi. Sasa ukizingatia Handeni yenyewe ni kubwa mno, kwa yule mama, kufika kwetu nayo inakuwa ni shida. Tulikuwa tunaomba kwa sababu fedha nyingi sana zinazotumika kwenye sekta mbalimbali ndani ya Halmashauri, zinapita kwenye Halmashauri yenyewe na sisi kama Kamati ya Fedha, hukaa tukazijadili. Je, hatuwezi kuletewa hizo fedha tukajua zipo lakini zikawa zinasimamiwa na Hakimu huyo wa Wilaya, ambaye hata kama yuko Handeni, tukijua kwamba ziko pale kwetu, tuweze kuzipangia matumizi mengine pengine na kama Kamati ya Fedha ya Halmashauri, kuweza kuzipangia kazi nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mwisho, Mheshimiwa Waziri na kwa hili naomba jibu *serious;* je, ni kigezo gani kinachotakiwa ili tuwe na Mahakimu wa Wilaya, kwa sababu kama ni jengo huyu Hakimu wa Wilaya huwa anakuja kufanya kazi kwenye jengo hilo hilo la Mahakama ya Mwanzo; kama ni nyumba, nyumba za kupanga zipo, ni kigezo gani, kama hakuna ugumu basi mimi nilikuwa naomba sana na sisi tuweze kupatiwa Hakimu wa Wilaya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninalotaka kuliongelea, msemaji aliyekaa amelilisemea. Lakini mimi naomba nisisitize, mishahara ya Mahakimu. Ni kweli kabisa, kwa heshima kabisa na unyenyekevu, nasema kwa nia njema, maslahi na mishahara ya Majaji pale juu, nina hakika hayana matatizo. Huku chini wale Mahakimu nilichunguza wakati fulani nikaenda mpaka kule Wizarani, hakika mshahara wao ni kati ya shilingi laki moja na nusu mpaka laki mbili. Sidhani kama ni zaidi.

Mheshimiwa Waziri hili nitaliombea maelezo kuhusu mishahara yao hawa Mahakimu wa chini huku wa Wilaya na hawa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, pamoja na watumishi wake. Kwa sababu tutaendelea kuzungumzia rushwa, lakini wafanyeje? Hivi laki moja na themanini au laki moja na nusu; unafanyia nini siku ya leo? Huyu anaenda kushughulikia masuala nyeti, ana-*handle documents* na maamuzi mazito. Kwa kweli ni mpaka uwe kule Wilayani, uone wale wananchi wanavyoteseka katika Mahakama hizi ndiyo utaweza kuelewa nasema nini vinginevyo, huwezi kuelewa. Ninaomba Mheshimiwa Waziri, tupate kujua kama mishahara ni kiasi gani ili sisi kama Wabunge basi tuweze kuangalia ni kitu gani tunaweza kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *RITA,* kwanza kabisa nichukue fursa ya kumpongeza Bwana Maimu, ambaye ndiye Mkurugenzi Mkuu wa *RITA,* pamoja na watendaji wake wote. Huyu nimefanya naye kazi, najua uwezo wake wa kazi. Katika kipindi cha mwaka mmoja Mheshimiwa Waziri, nitatoa wasifu wao, wamedhibiti mianya mingi ya rushwa, kwa wale ambao mlikuwa mnakwenda pale mara nyingi kwenye usajili, yaani utasumbuka mpaka utalazimika kufanya mambo yasiyostahili. Lakini katika kipindi cha mwaka mmoja, hakika tumeona sasa hivi rushwa kwa wafanyakazi hakuna. Ukifika unaomba na juzi nilikuwa pale vitu vinakwenda kwa haraka na kwa utaratibu. Aidha, zamani ili kupata cheti itakuchukua miezi mitatu au zaidi. Lakini sasa hivi siku moja mpaka tatu, hakika umekwisha kupata cheti chako. Lakini vilevile kulikuwa na utoaji mbovu wa vyeti, ambapo inabidi urudi kule ambako ulizaliwa uweze kupata cheti chako. Lakini sasa hivi ndugu na wananchi kwa ujumla, wanajua kabisa kwamba, unaweza ukapata cheti chako popote pale ambapo Ofisi ya *RITA* ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile niwapongeze sana kwa elimu ambayo wanaitoa, nadhani wengi mnaona kwenye TV, tovuti, magazeti, redio na vipeperushi wanavyotoa. Aidha, mimi nimekutana nao kwenye maonesho mengi na maadhimisho ya Kitaifa. Kwa mfano, siku ya Utumishi wa Umma na kadhalika. Kwa kweli nawapongeza sana kwa sababu ni eneo ambalo tulikuwa tunasumbuka nalo na ni la muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa nini nimesema yote haya. Nimesema yote haya kwa sababu nia yangu ni kuomba Serikali, angalau iweze kuwawezesha na

kuimarisha mfumo mzima wa usajili wa RITA, ili iweze angalau kukusanya takwimu muhimu zote zinazohusu maisha ya Mtanzania; nina maana gani? Kwa mfano, daftari la kudumu la wapiga kura, kwa sababu hawa wana takwimu ambazo ni za uhakika. Mfumo wa elimu au mfumo wa afya, mfumo wa Taasisi za Fedha., ikibidi hata kusaidia katika Sensa ya Taifa.

Kwa sababu hii sensa tunajua inachukua mabilioni. Lakini hawa watu kwa sababu wanashughulika na takwimu siku hadi siku, nadhani ni wakati muafaka, Mheshimiwa Waziri na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, mtakubaliana tunaweza kutokana na utendaji wao ambao unaendelea kuboreka siku hadi siku, napendekeza tuweze kuwatumia katika nyanja nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume za Haki za Binadamu. Kwa kweli kabisa Tume ya Haki za Binadamu, inafanya kazi nzuri. Waliwahi kupita maofisa kule kwenye Wilaya ya Kilindi. Lakini hakika Waheshimiwa Wabunge, matendo au na matukio ya kukiukwa haki za binadamu huko chini ni makubwa mno. Hawa watu kwa sababu wako mbali, hawafikiki, hawajui hata wafanye nini, hata haki zao zikoje? Kwa hiyo, mara nyingi mimi mwenyewe ninakuwa Hakimu kule kwangu, mara nakuwa askari, vitu vyote tu, kwa sababu watu kama hawa ambao wangeweza kuwashughulikia wanakuwa hawapo. Mimi ninaiomba sana hii Tume ya Haki za Binadamu, ingawa tuliwahi kuulizia hapa Bungeni; je, tunaweza kupata uwakilishi mpaka chini kwenye Wilaya, tukaambiwa kwamba tatizo ni fedha, wao wameshajiweka sawa ila tatizo ni fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri kama ilivyo sekta nyingine tunazozpa kipaumbele, kwa kutafuta fedha kwa njia mbalimbali. Basi mimi naomba angalau tuweze kuwapatia hao pia fedha, hata kama hawatakuwa na mtumishi kila Wilaya basi kila Mkoa angalau kuwe na watu wawili, watatu, ambao tunaweza kuwaita kwenye Mawilaya kwa muda ili waweze kuja kushughulikia matukio mbalimbali. Ninajua ni gharama kubwa kuweka mtu kila Wilaya, lakini basi kwenye Mkoa, kwani hadi sasa nadhani ni Mikoa miwili tu imeweza kupatiwa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimsihi sana Mheshimiwa Waziri, kama ataweza kutusaidia kwenye hilo na sisi Wabunge tuko tayari tutakapotakiwa kuhusika kwenye shughuli mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kama ambavyo amesema msemaji ambaye amekaa, kwa kweli Sekta hii ya Sheria ni muhimu maana yake Wizara zote zinafanya kazi zake, lakini zote zinaongozwa na sheria fulani. Wanaotunga zile sheria ndiyo hawa. Sasa tusipowapa yale ambayo yanakusudiwa ili waweze kutunga zile sheria ipasavyo, tutakuwa tunafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunategemea maamuzi yao na mapendekezo yao ili tuweze kufanya haya ambayo tunakusudia kufanya. Nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii, lakini langu kubwa katika yote niliyosema, mishahara ya Mahakimu na watumishi, narejea kuyasema hayo, kwa sababu kwenye vifungu mara nyingi huwa sipendi

kusimama kwa sababu Serikali ambayo iko madarakani na wanayoyafanya ni ya kwangu. Lakini kwa hili, ninaomba sana nipate jibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Asante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo. Sasa kabla sijamwita Mwanasheria Mkuu, nalitaarifu Bunge kwamba, Mheshimiwa Spika amesharudi na yuko tayari kuchukua nafasi.

*Hapa Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Job Ndugai. Nimetaarifiwa kwamba umekishika Kiti kwa ufanisi mkubwa, kama ambavyo tunakuelewa kazi yako.

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. SALOME J. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kupata fursa hii ili nami niweze kuchangia hoja hii muhimu ambayo iko mezani.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni Wizara mojawapo nyeti sana katika nchi yoyote. Wizara hii ndiyo inayosimamia Mahakama, taasisi ambayo ni moja ya mihimili mitatu ya nchi, nyingine ikiwa ni Bunge na *Executive* (Serikali).

Mheshimiwa Spika, taasisi ya Mahakama inakabiliwa na matatizo mengi sana yakiwemo upungufu wa Mahakimu, miundombinu hafifu, vitendea kazi na tatizo la rushwa. Tatizo la rushwa ni kubwa sana Mahakamani jambo ambalo linawanyima haki walio wengi waliokwenda kupata haki. Anayenyimwa haki kama alistahili atakuwa mnyonge na hatakuwa mwananchi mzuri mwenye ari na furaha. Kadhalika yule aliyenunua haki pasi na kuistahili ataendelea kuharibu *moral fabric* ya jamii na nchi. Kwa ujumla rushwa ni kansa na kitu kibaya katika jamii yoyote. Ningependa kujua Wizara ime-*design* mikakati gani ya ziada ili kupigana na hali hii? Je, kuna utafiti wowote wa kina ambao umefanywa kufuatilia tatizo hili, ukiachilia mbali mambo kama mishahara midogo/maslahi kutotosha na kadhalika?

Mheshimiwa Spika, mara kadhaa kumetokea migongano baina ya Bunge na Mahakama, Bunge likiwa linatunga sheria na Mahakama ikiwa ni msimamiaji wa kutafsiri sheria hizo ili zitoe haki.

Ningeomba kupata maelezo/ufafanuzi ya kwa nini migongano kama hiyo ikitokea, kwa mfano suala la shilingi milioni tano kwa mtu anayetaka kupinga matokeo ya uchaguzi mkuu, hakuna utashi wa dhahiri wa pande zote kama Mahakama na Bunge wa kujadili tofauti hizo bila ya kuathiri nafasi za umihimili wao? Endapo majadiliano

hayo yatakuwa ya afya kama inavyotarajiwa, hatuoni kwamba itajenga zaidi uwepo wa mihimili hiyo?

Mheshimiwa Spika, la mwisho, lakini si kwa umuhimu ni kuchelewa kwa urekebishwaji wa sheria za ndoa, watoto na mirathi. Jamii na hususan wanawake na watoto wanaendelea kuathirika sana na ucheleweshaji wa urekebishwaji wa sheria hizi. Ningeomba kujua ni lini Wizara hii itakamilisha urekebishwaji wa sheria hizi muhimu ili haki itendeke katika makundi haya. Nashauri Wizara iwe na *targeted time* ya kuhamilisha suala hili. Nitafurahi kusikia ahadi hii na naunga mkono hoja.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Waziri Mheshimiwa Dr. Mary Nagu na Naibu Waziri Mheshimiwa Mathias Chikawe, kwa hotuba nzuri na kamilifu ambayo naiunga mkono kwa asilimia mia moja. Pia nawapongeza wataalamu husika kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza kwa aliyekuwa Jaji Mkuu Mheshimiwa Barnabas Samatta ambaye kastaafu, kwa kazi nzuri kwa kipindi chake chote alipokuwa madarakani. Ninamtakia maisha bora hata baada ya kustaafu kwake vile vile ninampongeza kwa nguvu mpya, kasi mpya na ari mpya Mheshimiwa Augustino Ramadhani, kwa kuteuliwa kuwa Jaji Mkuu mpya na Mheshimiwa Rais hivi karibuni. Ninamtakia afya njema aweze kufanya kazi ngumu na vizuri. Pia ninawapongeza Majaji wote, Mahakimu wa ngazi zote na watumishi wengine wa Wizara hiyo kwa kazi ngumu na nyeti.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria ina majukumu makubwa sana. Ndiyo inayomwapisha Rais wa nchi na ni nguzo kubwa kwa chaguzi zetu zote. Majukumu mengi kabla ya kutekelezwa wanaopewa kazi hizo lazima waapishwe na Mahakama. Hivyo Wizara hii isingepaswa iwe na matatizo katika utekelezaji wa shughuli zake kiufanisi kwa mfano kasi ya marekebisho ya maslahi ya Majaji, Mahakimu wa ngazi zote iongezwe ili kuwaondolea ugumu wa maisha. Mahakama ziboreshwe kwani Mahakama nyingi nchini majengo yanayotumika yameazimwa kutoka Wizara nyingine na hivyo hazikujengwa kwa kuzingatia shughuli za kimahakama na siyo hivyo tu baadhi ya Mahakama hizi kama gereji bubu hazina hadhi. Hali hii inapunguza kabisa heshima ya Mahakama nchini.

Mheshimiwa Spika, mimi ni mmojawapo ninayeona Mahakama haitendewi haki kwani siku zote inaonekana kuwa ni sehemu ya rushwa. Kwa nini Mahakama ihusishwe na rushwa wakati wote? Nimefuatilia kwa karibu nimeona jumla ya kiasi cha rushwa kinachoelezwa hadi leo kesi hizo haizidi shilingi milioni moja kwa kesi zote za rushwa ambapo zipo rushwa kubwa ambazo zinadhoofisha uchumi wa nchi hazisikiki na wala hazifuatiliwi kwa karibu. Ninachokusudia kueleza ni kwamba ifutwe sura inayofanya Mahakama ijulikane kwa rushwa zaidi kuliko kutoa haki.

Mheshimiwa Spika, Serikali iongeze kasi ya kuajiri Mahakimu wa ngazi zote pia ipunguze urasimu mrefu unaotumika kuajiri Mahakimu. Pia Serikali iwe na mkakati wa makusudi kutoa muda wa ziada kwa Mahakimu wazuri baada ya kustaafu kwani baadhi

yao wana afya na uwezo na maadili, vinginevyo wote wanaokaribia kustaafu wakitoka kwa mkupuo kazi ya kuziba pengo hilo kwa ajira mpya ni ndoto.

Mheshimiwa Spika, naomba nijikite katika jimbo langu la Liwale ambayo ni Wilaya kamili. Wilaya hiyo yenye eneo mita za mraba 39,000 yenye hifadhi ya wanyamapori wakali ina Mahakama ya Wilaya Liwale Makao Makuu na Mahakama mpya ya Mwanzo Kibutuka kilomeata 60 kutoka Liwale. Mahakama hii haijaanza kutumika kwani inahitaji shilingi milioni 15 kumalizia ujenzi na inatarajiwa kufunguliwa na Mheshimiwa Rais mapema mwezi Septemba, 2007 wakati wa ziara yake Mkoa wa Lindi, maombi yamekwishatumwa kwa wahusika Wizarani na pia Mheshimiwa Mathias Chikawe alifanya ziara ya makusudi kuona maendeleo ya ujenzi wa Mahakama hiyo ya Kibutuka.

Hata hivyo naishukuru na kuipongeza Wizara kwa mchango wake wa awali wa kiasi cha shilingi milioni 31 ambazo zingemaliza ujenzi wa Mahakama. Kwa bahati mbaya mkandarasi husika alihusika na wizi wa kiasi fulani cha fedha hizo na kesi yake ipo Mahakamani na ujenzi ukakwama ambapo umuhimu wa Mahakama upo pale pale. Ahsante na naunga tena mkono hoja kwa asilimia mia noja.

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri na Naibu Waziri wa Wizara Mheshimiwa Dr. Mary Nagu na Mheshimiwa Mathias Chikawe bila ya kumsahau Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Johnson Mwanyika, kwa jinsi wote wanavyofanya kazi kwa kiwango kikubwa na kwa kasi inayostahili. Aidha, nampongeza Katibu Mkuu wa Wizara hii na wasaidizi wake wote wakiwemo Wakuu wa Idara kwa matayarisho mazuri ya hotuba ya Makadirio ya fedha za Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, naomba kuiomba Wizara kupitia kwako na kwa Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii kuandaa mipango ya kuikarabati Mahakama ya Kigamboni ambayo kwa kweli inahitaji kufanyiwa matengenezo ili kuiweka Mahakama hiyo katika hadhi inayostahili pamoja na kufanyiwa upanuzi wa jengo lake kwa kuwa kwa sasa halikidhi huduma. Ni muhimu sana sasa kujengwa uzio katika Mahakama hiyo. Suala la kuongezwa Mahakimu nalo lizingatiwe.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Jimbo la Kigamboni wanapenda kuelewa suala la sheria ya kuanzisha kuwepo kwa Kadhi kwa kusimamia sheria na taratibu za Kiislamu limefikia wapi na naiomba Wizara itoe tamko katika Bunge lako Tukufu wakati Waziri wa Katiba na Sheria atakapokuwa anajibu hoja na michango ya Waheshimiwa Wabunge. Tuige mfano wa wenzetu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ambao wanao utaratibu huu kwa muda mrefu sasa na halijaleta malumbano ya aina yoyote ile.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa matayarisho mazuri ya hotuba ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, maoni, ujenzi wa Mahakama Kuu Tabora, jengo linalotumiwa kwa shughuli za Mahakama Kuu Tabora ni la zamani na hapo awali lilikuwa ni kwa ajili ya shughuli (Ofisi) za Manispaa ya Tabora. Hivyo halikujengwa kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya shughuli za Mahakama. Aidha, utaratibu wa kulipana fidia baina ya mahakama na manispaa kuhusu majengo yao bado haujakamilika. Ipo haja ya msingi ya kumaliza utata huu ili Kanda ya Tabora iweze kutengewa fedha za kujenga jengo la kisasa kwa ajili ya shughuli za Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mahakama Kuu kitengo cha biashara, kitengo hiki cha Mahakama Kuu kinafanya kazi nzuri tena kwa kasi inayoridhisha (nzuri). Lakini kasoro yake kubwa ni ukubwa wa ada zinazotakiwa kulipwa wakati wa kufikisha shauri la madai kwenye mahakama hii. Kutokana na ughali wa ada, kesi nyingi za wadaiwa wa mabenki hapa nchini wanakwepa kutumia fursa nzuri ya mahakama hii na badala yake wanafungua mashitaka dhidi ya mabenki katika mahakama nyingine ambazo kasi za maamuzi yake ni ndogo sana. Hali hii inaathiri sana mapato ya mabenki kutokana na mikopo yenye matatizo.

Aidha, kuanzishwa kwa Mahakama ya Ardhi kumeongeza tatizo lingine kwenye mashauri ya mabenki na wakopaji wanaoshindwa kulipa madeni yao kwani wanapofikishwa katika Mahakama ya Biashara, huko maamuzi hutolewa kwamba mashauri hayo yahamishiwe kwenye Mahakama ya Ardhi eti kwa sababu inahusu *mortgage* ambayo inagusa suala la ardhi. Kuna haja ya haraka kwa *Court of Appeal* kulitolea msimamo tatizo hili ili mabenki yaweze kutumia huduma za Mahakama ya Biashara kwa mashauri yote yanyohusu migogoro ya mikopo iliyoshindikana kulipwa pamoja na kwamba dhamana husika zinahusu majengo (ardhi).

Mheshimiwa Spika, Benki zetu zina fedha nyingi sana ambazo zimefungwa kwenye mikopo isiyolipika ambazo kesi zake katika mahakama zetu zinachukua muda mrefu kumalizika. Wizara ilitazame tatizo hili kwa dhamira ya kulimaliza haraka. Kuhusu upungufu wa wafanyakazi, kuna upungufu mkubwa wa wanasheria katika ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Tatizo hili pia linajitokeza katika upungufu wa Majaji na Mahakimu, upungufu huu unaathiri sana utendaji kazi wa Mahakama zetu.

Kuhusu maslahi duni kwa wafanyakazi, mishahara midogo ya Mahakimu na Wanasheria wa Serikali ni midogo na inaathiri sana utendaji kazi wao. Ili kuongeza ufanisi wao na kupunguza vishawishi vya rushwa, naishauri Serikali iangalie uwezekano wa kuongeza mishahara yao kulingana na unyeti pamoja na uzito wa kazi zao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mahakama ya Kadhi, hotuba ya Waziri haikusema lolote katika hotuba yake kuhusu mustakabali wa Mahakama ya Kadhi hapa nchini kufuatana na tafiti ambazo zimekwishafanywa mpaka hivi sasa kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Wizara hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. MKIWA ADAM KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Waziri wa Katiba na Sheria Mheshimiwa Dr. Mary Nagu na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya na kwa umahiri wao.

Pili napenda kutoa mchango wangu kuanzia kwenye Katiba. Katiba ya sasa haikidhi haja, ni Katiba ya mfumo wa chama kimoja. Hivyo nashauri tupate Katiba ambayo itazingatia mawazo ya Watanzania na kujali maslahi ya nchi pamoja na wananchi wake. Katiba bora nii ile inayotoa haki sawa kwa kila mtu, ni bora basi tuwe na Katiba mpya na siyo kuwekea viraka Katiba hiyo ambapo wataalamu husema marekebisho. Katiba hii haitoi uhuru kwa Tume ya Uchaguzi, itawezekanaje Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiyo anateua Tume ya Uchaguzi? Hivi kweli mteuliwa huyo kazi atayofanya ni kumridhisha aliyemteua na hatoenda kinyume na maelekezo ya aliyemteua, hapo haki iko wapi? Na kama haitohsi kama Tume itatangaza matokeo tofauti hakuna kipengele cha kushitaki na kutengua matokeo ya Urais. Sasa basi ili tufanye kazi za kulingana ni lazima tuwe na Katiba mpya na huru. Suala ni Katiba mpya yenye kutoa haki sawa.

Kuhusu Mahakama ya Biashara, Mahakama hii Watanzania walio wengi hawaielewi vizuri na kazi yake hasa ni nini? Naishauri Wizara itoe matangazo zaidi ili watu waielewe vizuri hasa wadau wa biashara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mahakama ya Kazi, kulingana na wafanyakazi wengi hasa wa viwandani hasa viwanda vya samaki katika Jiji la Mwanza, wafanyakazi hawa hufanya kazi kwa muda mrefu na malipo yao ni madogo sana na hawa wafanyakazi hufikiwa kunyimwa na mabosi wao kuunda vyama vya wafanyakazi. Pia wanapoacha kazi mafao yao ni madogo sana. Tunaiomba Serikali iliangalie hili kwa undani kwani kuna wafanyakazi wengi ambao hata hawajui ni nini wafanye na hata kama kuna Mahakama ya Kazi. Ni wajibu wa Wizara kuwaelimisha wafanyakazi hawa kuwa Mahakama hizo zipo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu rushwa, suala la rushwa mahakamani halitakwisha kama mahakimu hawataongezewa maslahi na kama kesi hazitosikilizwa haraka hasa mahakama ya mwanzo. Huko ni kuchafu hasa kwa wazee wa baraza kulingana na posho zao. Ahsante.

**MHE. FELIX KIJIKO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hotuba ya Wizara hiyo kwa mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, watumishi wa Mahakama katika Mkoa wa Kigoma wanakabiliwa kwa kiasi kikubwa na tatizo la nyumba za kuishi. Watumishi wa Mahakama wanafanyakazi ya hatari kwa usalama wao kama wanavyofanya polisi, hivyo kwa makusudi mazima ni vema Wizara ikatenga fedha za kujenga nyumba za kuishi kuliko kuwaacha na kupanga katika nyumba za kiraia. Mfano hai ni watumishi wa Mahakama ya Kibondo ambao wanaishi kwa kupanga uswahilini.

Mheshimiwa Spika, tatizo la usafiri pia ni kubwa. Ni dhahiri magari yaliyotolewa ni kwa ajili ya wadau. Watumishi wengine wanajikuta wakitembea. Nashauri Wizara katika kununua magari, izingatie ununuzi wa magari makubwa kama vile *land cruiser* ambayo yanaweza kutoa huduma kwa watu wengi.

Mheshimiwa Spika, uchache wa watumishi hao wa mahakama ni tatizo lingine linalokabili watumishi. Nashauri ufanyike utaratibu wa makusudi kupata ama kufundisha na kuweza kupata watumishi wa kutosha ili kila mahakama iweze kufanyakazi. Mfano hai ni Mahakama za Wilaya za Kibondo ambazo zingine hazifanyi kazi kwa kukosa mahakimu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja.

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Spika, naomba awali ya yote nitoe pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hiyo kwa hotuba yao yenye kila aina ya ufasaha na mantiki. Kutokana na hayo naunga mkono hoja moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mbozi Magharibi lenye kata 11 lina upungufu mkubwa wa Mahakama za Mwanzo ziko mbili tu Tunduma na Kamsamba, ambapo hata hivyo Mahakimu wa Mahakama hizo huenda kwa siku chache tu kwa muda wanaoupanga wakitokea makao makuu ya Wilaya. Kata zingine tisa zikiwemo ambazo umbali wake ni zaidi ya kilometa 150 kutoka Makao Makuu ya Wilaya, wakazi wake hulazimika kupeleka kesi zao kusikilizwa kwenye Mahakama ya pale Vwawa, Makao Makuu ya Wilaya ya Mbozi. Hali hii inasababisha usumbufu mkubwa sana kwa wananchi hao na kuwafanya kukata tamaa ya kutendewa haki.

Kwa kuwa hadi miaka ya 1970 kila kata ilikuwa na Mahakama ya Mwanzo na ilikuwa na Mahakama ya Mwanzo na kwa hivi sasa kwenye kata za Msangano, Chiluluma, Kamsamba, Chitete, Ivuma, Myunga, Ndalambo na Kapela. Wananchi ama wamekwishajenga upya au wanaendelea kujenga majengo ya mahakama kwa nguvu zao wenyewe.

Naomba wananchi hao watendewe haki ya kuanzishiwa tena Mahakama za Mwanzo. Kutokana na kutokuwepo Mahakama hizo sasa hivi wahalifu wanatenda makosa na kuendelea kuvinjari kana kwamba nchi hii haina utawala wa sheria.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima wa afya na kuniwezesha kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha vyema hotuba yake. Pia nimpongeze Naibu Waziri na watendaji wote kwa ushirikiano mzuri na Waziri na kwa kufanikisha hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ni mfupi sana na ninaanzia na Mahakama. Mahakama zetu zinachelewesha sana kuendesha kesi na hasa zile zinazokatiwa rufaa. Sote tunaelewa kuwa kutoa hukumu kwa mshitakiwa ni kazi ngumu sana na inahitaji sheria na pia ni haki ya mshitakiwa kukata rufaa kama ataona hakufanyiwa haki, lakini kesi hizi huchukua muda mrefu sana kusikilizwa na kumalizika kwake hali ambayo huleta usumbufu kwa mshitakiwa na ndugu wa mshitakiwa.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kupitia kwa Waziri kutilia mkazo kesi hizi kusikilizwa kwa haraka ili kuepusha malalamiko wanayopewa Majaji na Mahakimu kuwa wanachelewesha kwa makusudi ili mlalamikaji atoe chochote.

Mheshimiwa Spika, tuhuma hizo nzito si mzuri na zinachafua chombo hiki ambacho ni katika mihimili mitatu ya nchi hii na pia Wizara hii ndiyo inayosimamia vitendo vya rushwa.

Mheshimiwa Spika, kama kuna uhaba wa Majaji basi hakuna budi kuongezwa pia jitihada za makusudi zifanywe kuboresha Mahakama na vitendea kazi pamoja na hali za wafanyakazi ili waweze kumudu kazi hii ngumu inayohitaji kutumia akili nyingi wakati wote.

Mheshimiwa Spika, uimarishaji wa usajili wa vizazi, ndoa, talaka, vifo na udhamini. Katika suala hili mimi nitachangia usajili wa vizazi.

Suala la kupatiwa usajili kwa mtoto ni haki ya msingi na kila kizazi kinachozaliwa lazima kipate cheti ambacho kitamwezesha kupata haki zake baadaye kama elimu. Hati ya kusafiria *(Passport)* na kama mtoto hakuandikishwa vitu hivi hatavikosa na itakuwa taabu kuvipata. Pia Serikali itakosa takwimu za vizazi vya watoto wetu wanaozaliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa tabia iliyopo sasa ya kuweka ofisi hizi kuwepo katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ni watoto wengi watakosa haki hii kwa sababu kuna baadhi ya wananchi wanaishi mbali sana na ofisi ya Mkuu wa Wilaya na kuona ni usumbufu kufuatilia suala la watoto wao. Kwa hiyo, nashauri Wizara isongeze huduma hii karibu na wananchi na pia kutoa elimu kwa wananchi faida ya kumuandikisha mtoto na hasara zake.

Mheshimiwa Spika, kwa mchango huo mdogo naunga mkono hoja hii.

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kazi nzuri wanayoifanya. Naomba kupata maelezo ya haya yafuatayo:-

Moja, ni lini Mahakama zitaanza kuendeshwa kisasa kwa maana ya matumizi ya kompyuta, vinasa sauti na kadhalika ili kuwaondolea Mahakimu/Majaji kazi ya kuandika maelezo kwa mkono?

Pili, kwa nini Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo/Wilaya hawapati semina mbalimbali kwa mfano, Haki za Binadamu, rushwa na kadhalika.

Tatu, Serikali iangalie upya sheria ya ubakaji *(rapping)* mbona inamjali mwanamke pekee wakati wapo watoto wa kiume wanaoingiliwa kwa nguvu na kulawitiwa, lakini yule aliyemlawiti mtoto wa kiume tena kwa nguvu anashitakiwa kwa kosa moja tu la kulawiti na sio kubaka na kulawiti. Naunga mkono hoja hii.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Waziri wa Katiba na Sheria, Naibu Waziri Mheshimiwa Mathias Chikawe, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Johnson Mwanyika na watumishi wote wa Wizara hii ya Katiba na Sheria. Wizara hii imesimamia katika moja ya mihimili mitatu muhimu ya nchi ambayo ni Bunge, Utawala na Sheria (Mahakama).

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ni miongoni mwa nchi ambazo zinaendeshwa kwa utawala wa sheria, kwa kufuata Katiba na sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa utawala wa sheria ni muhimu sana kiuendeshaji wa nchi ni muhimu pia wale wanaoongozwa kuwa na ufahamu juu ya masuala mbalimbali ya Katiba na sheria za nchi, kutokujua sheria hakutoi nafasi ya kutenda kosa.

Mheshimiwa Spika, napongeza sana Idara ya Mahakama hasa Mahakama Kuu kwa jinsi inavyosimamia kesi na mashauri mbalimbali yanayohusu raia, Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa zimekuwa ni mfano bora kwa Mahakama zetu za chini katika kusimamia haki.

Mheshimiwa Spika, nilaani vitendo vichafu vinavyofanywa na baadhi ya Mahakama za Mwanzo, Wilaya na Mkoa hasa vile vyote vinavyoashiria rushwa, ukweli vitendo hivi vinaharibu heshima ya muhimili huu muhimu. Nimwombe Mheshimiwa Jaji Mkuu kusimamia kwa uangalifu suala hili, kwa ngazi hizi ikiwa ni pamoja na utendaji haki na kuharakisha usikilizaji wa kesi.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Wizara kwa juhudi zake katika kurejesha ule utaratibu wa kuwa na Mkurugenzi wa Mashtaka *(DPP)* suala ambalo linamfanya *Director of Public Prosecution (DPP)* kushughulikia uendeshaji wa kesi iwapo Mahakamani na hivyo kuuondolea mamlaka polisi ambao mara zote walihusika na kushtaki na kisha kusimamia uendeshaji wa kesi! Kwa kiwango kikubwa kutaonyesha imani kwa wananchi na kujenga imani na Mahakama na watumishi wake.

nitumie fursa hii pia kuipongeza Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Tume hii inafanya kazi vizuri hasa kwa kuzingatia haki na Utawala Bora. Ili huduma ya Tume hii iwafikie wananchi kwa kiwango kikubwa, naomba Tume ipanue wigo kwa kusafiri na kutembelea mikoa ili jamii ambayo mara nyingi haikutendewa haki na baadhi ya vyombo vya sheria au vyenye mamlaka nao wapewe huduma kupitia urahisi wa mikoa yao na sio ilivyo sasa hadi kusafiri kwenda Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, pia nasikitika juu ya kupuuziwa kwa chombo hiki ambacho kipo kwa mujibu wa sheria, hivi kwa nini pale Tume hii inapotoa maamuzi na pengine yakapishana na uamuzi uliotolewa na vyombo nilivyovitaja kwa nini mara nyingi uamuzi wa Tume hupuuzwa?

Mheshimiwa Spika, nashauri maamuzi ya Tume yapewe nguvu na yaheshimiwe kiutekelezaji. Pia nishauri zile sheria zote zilizopitwa na wakati na ushauri umetolewa na Tume ya Kurekebisha Sheria basi ni kama ushauri/maoni yakazingatiwa kiutekelezaji.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kushukuru Wizara kwa hatua nzuri kujenga Mahakama ya Mwanzo mjini Kiomboi jimboni Iramba Magharibi, sasa naomba tujengewe Mahakama ya Wilaya na pia tupewe nyongeza ya Mahakimu wake wa Mahakama ya Mwanzo na Wilaya tunahitaji Mahakimu katika Mahakama za Kaselya, Ndago, Urughu, Shelui, Ntwika, Kinampanda na Kisisiri.

Mheshimiwa Spika, nashukukru Wizara kwa kutupatia gari Mahakama yetu ya Wilaya naomba Mahakimu ya Mwanzo nao wapewe pikipiki. Naunga mkono hoja.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia Wizara hii kama ifuatavyo:-

Kwa vile utaratibu wa ujenzi wa Mahakama kwa mpango wa *Quick Start* ulihusisha wafadhili na mchango wa hali na mali wa wananchi, na kwa vile Wilaya ya Karatu ni moja ya Wilaya zilizokuwa kwenye mpango huo, na kwa kuwa mpango huo tangu uliposimama kumekuwa na ukimya wa kutisha, je, Serikali sasa inatoa tamko gani rasmi kuhusu mpango huo ili wananchi waliotoa fedha zao waelewe kinachoendelea sasa kwani ukimya uliopo unajenga dhana ya kuwa fedha zao zimeliwa kijanja kijanja. Je, ni lini sasa mpango mpya ambao umeelezwa mara kadhaa hapo Bungeni unaoridhia *Quick Start* utaanza rasmi katika maeneo muhimu hasa ya ujenzi wa Mahakama za Mwanzo na Wilaya na upatikanaji wa uhakika wa Mahakimu?

Kwa kuwa Wilaya ya Karatu tangu imeanzishwa sasa ni zaidi ya miaka 10 na haijapata wala Mahakama wala Hakimu wa Wilaya, isitoshe wananchi wa Wilaya ya Karatu wameendelea kuhangaika kufuata huduma za Mahakama hiyo Mbulu na sasa Monduli.

Serikali itakubaliana nami kuwa kwa kuzingatia taratibu za Mahakama zetu ambapo kesi zinapigwa tu tarehe wananchi hao, ambao ni watuhumiwa tu katika hatua hiyo wanapaswa kusafiri kwa gharama kubwa na usafiri usio wa hakika, je, ni lini sasa Wilaya ya Karatu itapata Mahakama ya hadhi ya Mahakama ya Wilaya na Hakimu wa Wilaya kuondoa usumbufu huo mkubwa sana kwa wananchi?

Mheshimiwa Spika, wakati maandalizi hayo yanaendelea na iwapo yatachukua zaidi ya mwaka mmoja, nilikwishawasilisha ombi letu kuwa Mahakama ya Wilaya ya Karatu iwe Mahakama yoyote itakayoteuliwa kwa utaratibu Mjini Arusha ambako kuna usafiri wa moja kwa moja kwenda na kurudi. Lakini pia mji wa Arusha kuna wananchi wengi wa Karatu jambo ambalo ni muhimu sana mtuhumiwa anapohitaji mdhamana. Mji

wa Monduli upo pembeni sana na si rahisi kwa wakazi wa Karatu kupata ndugu, marafiki wa kuwadhamini. Hili ni jambo zito sana kulinda haki za watuhumiwa. Ili kuondoa msongamano wa mahabusu, nadhani kuna tatizo kubwa katika masharti ya utoaji mdhamana iwe wa polisi au mahakamani.

Je, Serikali/Wizara inachukua hatua gani ya dhati kuangalia upya sheria inayohusika na hasa kifungu cha 148 cha *CPA* na ikiwezekana kuweka masharti ya wazi zaidi yasiyoweka mdhamana kuwa mgumu bila sababu za msingi na kuwasiliana/kushirikiana na Wizara ya Usalama wa Raia, angalau kwenye kesi za kawaida, watuhumiwa wakamatwe tu pale ambapo uchunguzi umethibitisha kuwa kuna sababu za kutosha kuamini kuwa mtuhumiwa anahusika. Kwa hali ilivyo sasa, mtu akikuchukia kwa sababu yoyote ile, akazungumza vizuri na askari utakamatwa na kuwekwa rumande na hasa *weekend* kwa lengo la kukomoa tu. Vivyo hivyo, wahalifu wa kweli, kwa kuzungumza na askari huachiwa vivyo hivyo na hivyo, kulinda haki za raia eneo hili linahitaji kuangaliwa sana. Nawasilisha.

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Spika, pamekuwepo na kelele nyingi hasa kutoka katika Kambi Upinzani kuhusu mapungufu yanayojitokeza katika Katiba yetu ya sasa. Ni kweli tumekuwa tukifanya masahihisho ya mara kwa mara ili kwenda na wakati, lakini ukweli ni kuwa viraka katika Katiba vimekuwa vingi na sioni kwa nini Serikali isikubali kuandika upya Katiba ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, wakati Katiba ya sasa ilipoandikwa nchi hii ilikuwa katika mfumo wa chama kimoja kwa hiyo mawazo ya wale wenye uwelekeo wa Upinzani hawakushiriki katika zoezi zima la kuandika Katiba hii. Kwa msingi huo ni vyema kwa sasa Katiba iandikwe upya ili makundi tofauti kama vile Chuo Kikuu, vyama vya Upinzani, wataalamu wote hawa wana michango mizuri ya kuchangia katika Katiba.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Tume ya Haki za Binadamu, hii Tume imekuwa ikifanya kazi bila meno. Maovu ni mengi na watu ni wengi wenye kuitegemea hii Tume, lakini maamuzi mengi ya hii Tume haiwasaidii kwa kuwa Tume haina meno, Tume hii ipewe meno ili iweze kutimiza majukumu yake.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza sana, Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara, Majaji na Mahakimu na ngazi zote kwa kazi nzuri wanazofanya.

Kwa njia ya pekee basi nampongeza Mheshimwa Waziri asubuhi hii kwa kukubali kufanya marekebisho ya jina la Wizara sasa kuwa Wizara ya Katiba na Sheria. Ni dhahiri Katiba ya nchi ndio nguzo na msingi wa sheria za kuilinda na kulinda haki na maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa sasa kutoa ushauri na mapendekezo kama ifuatavyo:-

Kwanza kujenga uwezo wa kuendesha mashtaka nchi nzima. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri haikuweka wazi ratiba ya utekelezaji wa mpango huu ambao unahitaji watendaji wengi kwa nchi nzima kwa wakati mmoja. Mawakili 156 hawatoshi. Je, maandalizi ya kupata Mawakili zaidi na gharama zake uko wapi?

Pili, majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria katika *Government Negotiating Teams*. Serikali Kuu imeingia katika Mikataba duni na dhaifu kimaslahi kwa nchi yetu katika sekta mbalimbali zikiwemo za madini na nishati. Katika migodi ya madini sekta ndogo ya gesi na petroli umeme na utalii na kadhalika. Hata hivyo Wizara hii imekuwa na watendaji wanaoshiriki katika *Government Negotiating Teams* na za wataalamu wa sekta hizo na hivyo kutoa ushauri kwa Serikali (Baraza la Mawaziri).

Kuhusu ubora wa mapendekezo ya Mikataba hiyo, je, Wizara haioni inapaswa kuwajibika kwa jinsi inavyoshiriki kushauri vibaya Serikali? Nini wajibu wa Wizara hii katika *Government Negotiation Teams?* Hivi wajibu wao ni kuona tu kwamba mikataba inaandikwa kwa mfumo mzuri wa kisheria na bila kuchambua maslahi au mitego inayoainishwa katika mikataba hiyo?

Mheshimiwa Spika, ningeshauri kwamba wataalamu wa sheria wa Wizara wapate elimu maalumu za sekta za Kitaifa ili wafanye *specialization* ili kuboresha ufanisi wao ndani ya *Government Negotiating Teams*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapungufu katika sheria ya *Judges Remunerations and Terminal Benefits Act, 2007.* Sheria hii ni nzuri kwa kundi la Majaji nchini. Hata hivyo Sheria ingefaa kuboreshwa ili kukidhi mfumo wote wa watendaji katika Wizara hii. Hivyo ingepaswa pia kuwagusa Mahakimu na hata Mawakili wa Serikali bila kujali ngazi zao, Mkoa, Wilaya Mahakama za Mwanzo na kadhalika hasa ukizingatia mfumo wa utendaji na *risks* za kiutendaji kuwa zinafanana.

Kuhusu ukarabati wa Mahakama hasa Mahakama za Mwanzo, Wizara ya Katiba na Sheria ilikuwa na mpango mzuri wa ujenzi wa majengo ya Mahakama na ukarabati hadi Juni, 2006 kama inavyoonyeshwa katika jedwali namba saba katika Mkoa wa Tanga kumekuwa na ujenzi mmoja tu kwa Wilaya ya Korogwe, *Old Korogwe.*

Je, Wizara ina mpango gani wa ukarabati wa majengo ya Mahakama za Mwanzo katika Wilaya ya Muheza hasa Kata za Nkumbi, Kicheba, Kilulu na Kujenga Mpwa, katika Kata za Bwembwera, Mkuzi, Kisiwani na Zirai. Uchakavu wa majengo ya Mahakama za Mwanzo nilizoainisha zifanyiwe ukarabati unafedhehesha ubora na ufanisi wa Wizara hii mbele ya macho ya wananchi ambapo Mahakama hizo hufanyakazi mara mbili kwa mwezi. Hofu ya kukosa haki imetanda kwa wananchi wetu. Tufanye ukarabati na kusogeza huduma karibu na wananchi. Naunga mkono hoja.

**MHE. SIGFRID S. NG'ITU:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Shida yangu ni ile ile, Hakimu wa Wilaya Ruangwa, nyumba ya Hakimu ya Kwishi na Mahakama ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kwa siku ngapi kutoka Ruangwa kwenda Nachingwea kilomita 47 au Lindi kilomita 148. Naomba utoe ahadi angalau kwa kutapa tu lini tatizo hili litakwisha?

**MHE. MWANTUMU B. MAHIZA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naipongeza Wizara kwa Bajeti nzuri, pia nawapongeza sana watendaji wote kwa kazi nzuri na kwa kujitoa kufanya kazi kwa uaminifu mkubwa wenye uadilifu.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu nauelekeza katika Mahakama za Mwanzo hasa mkoani Tanga, Mahakama za Mwanzo mkoani Tanga karibu zote ni chakavu kiasi cha kuhatarisha maisha ya wanaozitumia, sakafu ni mbovu zimebomoka, kuchimbika chimbika, mabati yameachia na mengine yameng'oka na hali ni mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara iuingize mkoa wa Tanga katika mradi maalumu wa kujenga au kukarabati mahakama zilizopo. Aidha, nashauri Wizara ifanye ukaguzi ili kubaini hali halisi ya majengo yake nchini kote na hususani mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Spika, Mahakama za Mwanzo pamoja na matatizo yaliyopo sasa, pia mahakama zinakabiliwa na uhaba mkubwa wa Mahakimu. Mahakimu waliopo sasa wanalazimika kuhudumia Mahakama zaidi ya moja, hawana vyombo vya usafiri na sina uhakika kama wanalipwa posho ya usafiri.

Mheshimiwa Spika, kinachofanyika sasa ni mteja au wateja wenye haraka na kesi zao humuwezesha hakimu ama kwa kumkodishia gari ama kumpatia fedha ya nauli, nashindwa kuelewa matokeo ya ufadhili huu.

Mheshimiwa Spika, kesi nyingi zinazoahirishwa na nyingine kuchelewa kuanza hata pale upelelezi unapokamilika, hali hii inaumiza sana kwani watuhumiwa hukaa muda mrefu rumande na kusababisha kero zisizo na msingi.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ianze sasa kutoa elimu jamii ili vifungo vya nje vieleweke na dhamana zitolewe kwa wanaostahili badala ya sasa ambapo wenye kesi nzito hupewa dhamana na wezi kama wa mkungu wa ndizi na kuku hunyimwa dhamana.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Mahakimu hutoa hukumu kwa upendeleo na hivyo kupoteza maana ya mahakama, mfano mzuri ni pale mtu aliyesababisha upotevu mamilioni ya fedha za Serikali anafungwa mwaka mmoja na aliyeiba mkungu wa ndizi anahukumiwa miaka minne. Naomba Wizara ilione tatizo hili na kurudisha heshima ya mahakama.

Aidha, ninao mfano wa kutofautisha hukumu kwa mwenye nacho na asiyenacho. Nashauri hekima, busara na haki zitumike mahakamani.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, watumishi na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nyingi wanazofanya za kutetea haki ya Mtanzania. Kazi yao ni nzuri na hotuba ni nzuri ninaiunga mkono.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe maoni yangu katika maeneo kadhaa kama ifuatavyo:-

Katika eneo la uvunjaji haki za binadamu, katika Kanda ya Ziwa na sehemu nyingi hapa nchini kuna makundi ya watu wanaoendesha shughuli za mauaji kwa sababu kadhaa kama vile wizi, migogoro ya ardhi, imani za uchawi na kadhalika. Watu hawa wanajulikana kwa wananchi kwa vile wananchi wanaishi nao, mara kadhaa wameweza kufikishwa mbele ya sheria kwa ushirikiano wa wananchi na kuna wakati wananchi hufikia hatua ya kuvunja sheria kwa kutoa adhabu wenyewe kwa waovu hao.

Mheshimiwa Spika, adhabu zinazofikia hatua ya kuwaua waovu hao kutokana na hasira kubwa. Mtu akimuua mwingine kwa bahati mbaya ni kosa linaloweza kueleweka na hata kusameheka, lakini unapokuta kikundi cha watu tena wenye akili timamu wanaungana tena kwa kupanga na kuamua kuua si kuvunja sheria? Sheria inasemaje kwa kikundi hicho kinachoua kwa kukusudia? Sheria inasemaje juu ya watu hao kama wanakamatwa tena mara kadhaa na kuachiwa huru?

Mheshimiwa Spika, kama kukamatwa huko kunatokana na msaada wa wananchi wema, hawa watu wanashauriwa na sheria waendelee kuwa wema hadi lini wakati wakiona maisha ya raia wema yakiendelea kupotezwa na waovu hao lakini wanaendelea kuachwa huru mbele ya sheria?

Kinachokatisha tamaa ni kutambua ya kuwa waovu hao wanajenga uwezo wa kifedha, uwezo huo huwafanya waweze kuwarubuni Mahakimu na askari wapelelezi na waendesha mashtaka hivyo watuhumiwa hao huachiwa huru siku moja hadi mbili baada ya kufikishwa kituo cha polisi, kwa vile tu taarifa ya mtuhumiwa hufikishwa mahakamani ikiwa imebadilishwa kwa kudhoofishwa, sheria inawashauri nini wananchi wema walio tayari kusaidiana na polisi, mahakama na hawaoni kuwa utayari wao huo unatumiwa kama mradi na askari baada ya polisi kupokea taarifa hizo huwabana waovu hao ili wawape rushwa na kisha kuwaarifu ni nani kawapa taarifa hizo?

Mhesimiwa Spika, natambua kazi nzuri ifanywayo na Jeshi la Polisi na Mahakama kila wanapoamua kufanya kazi ipasavyo, lakini kila wasipoamua ni uchungu mkubwa kwa wanachi, wananchi hujiona kuwa wanatekelezwa kama watoto wa bata, ninafahamu vema kuwa wananchi hawa hujichukulia sheria mkononi kwa kuvunja sheria na utaratibu. Lakini je, kurekebisha sheria zinazokwaza wengi pia ni kuvunja sheria?

Mheshimiwa Spika, naomba nifahamu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kwa nini wananchi katika maeneo yao wasipige kura ili wataje wauaji katika maeneo yao? Kwa nini wananchi nao wasiaminiwe kuwa wanaweza kuwa waadilifu, wao ndiyo wanaojua ukweli, taratibu za kisheria ambazo si lazima kila wakati taratibu hizo ziwe na ukweli?

Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali isikubali Sungusungu kwa taratibu zake isiruhusiwe kuingilia bila kuingiliwa ishughulikie masuala ya mauaji ya mapanga na Sungusungu iwajibishwe inaposhindwa kusaidiana na polisi kwa matukio hayo?

Mheshimiwa Spika, naomba nipewe maelezo kuhusiana na mambo yafuatayo:-

Kulikuwepo na ahadi ya kukarabati Mahakama za Mwanzo za Mwamashimba, ahadi ya zaidi ya miaka minne iliyopita haijatekelezwa, naomba kufahamishwa ni nini kilichotokea hata ahadi hiyo isitekelezwe?

Pia kulikuwa na Mahakama ya Mwanzo Kikubiji ikafungwa, je, kutakuwepo na utaratibu wa kufufua mahakama hiyo? Mahakama ya Wilaya ya Kwimba iko jengo moja na ofisi ya Mkuu wa Wilaya, naomba ofisi mpya zijengwe kutenganisha mihimili hiyo miwili ya dola.

Mheshimiwa Spika, kwa dhati naomba kuwasilisha mawazo hayo na naunga mkono hoja.

**MHE: ANIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kwa maandishi katika Wizara ya Katiba na Sheria.

Kwanza nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalamu kwa ujumla. Pamoja na uboreshaji mkubwa wa vyombo vya mahakama kwa ukarabati na ujenzi wa mahakama na vitendea kazi bado kuwa ni urasimu mkubwa katika uendeshaji kesi na utoaji haki bado rushwa ni kikwazo na ndiyo unaosababisha mrundikano wa kesi.Ni vema sasa Mahakimu na wahudumu wa Mahakama waongezewe mishahara ambayo itasaidia kupunguza adha hiyo.

Kuhusu sheria  mbaya zilizopitwa na wakati pia  Wizara ingeipa kipaumbele sheria hizo kufanyiwa utafiti na kuletwa bungeni ili ziendelee kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, katika haki za binadamu kumekuwa na tatizo kubwa la uvunjwaji  wa haki za binadamu. Katika vyombo vya habari vimetangaza kuwa baadhi ya wafungwa wamekuwa wakipata fedheha kubwa ya udhalilishaji katika magereza kwa kuwalazimisha wafungwa kuvua nguo na kubaki utupu bila nguo, ningependa kupewa ufafanuzi kama kuna sheria ambayo inaruhusu jambo hilo la aibu ambalo linafanyika katika baadhi ya magereza? Jambo hili leo limetoka katika vyombo vya habari ili Watanzania wafahamu ukweli.

Napenda Serikali na Wizara hii kwa uboreshaji wa ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu na sasa mambo ya hati mbalimbali zinazowahusu wananchi kupitia *(RITA)* hili ni jambo zuri na sasa Serikali imesaidia kwa kiasi kikubwa wananchi wanyonge kupata haki zao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu marekebisho ya Katiba tuliyonayo sasa bado haikidhi haja, inahitaji marekebisho ya Katiba na sheria, mambo mbalimbali ikiwemo mfumo wa vyama vya siasa, yako mambo ambayo yanahitaji mabadiliko hayo.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa  Spika, napenda kuchukua fursa hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Mheshimiwa Mathias Chikawe, Katibu Mkuu, Mkurugenzi wa Mahakama za Mwanzo na watumishi wote walioshiriki kuandaa Bajeti mahiri sana yenye sura ya kuboresha Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizi, napenda kuwaombea Mungu awape afya, nguvu, mshikamano na uwezo ili waweze kutekeleza Bajeti kama walivyoandaa.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwani imekuwa tayari kuhakikisha kuwa inaondoa kero mbalimbali za wananchi na watumishi wa Wizara hiyo mara nyingi. Pamoja na juhudi za Serikali bado kuna tatizo la Mahakama za Mwanzo kwani azma ya Serikali ni kuwa na Mahakama ya Mwanzo kwa kila kata yenye wakazi wengi, lakini bado kuna mahakama moja tu kwa kila tarafa na tarafa zingine hakuna.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa dada yangu na mtani wangu kila Bajeti huomba fedha kwa ajili ya kujenga na kukarabati Mahakama za Mwanzo. Hivyo basi napenda kufahamishwa mwaka jana Serikali ilitenga fedha kiasi gani katika eneo hili na kwa Bajeti hii imetenga fedha kiasi gani ili kujenga Mahakama za Mwanzo?

Mheshimiwa Spika, ninayo mifano kadhaa ambayo wananchi wanatembea mwendo mrefu kufuata mahakama pale wanapokuwa na kesi, nayo ni tarafa ya Mungaa kuna Mahakama moja tu inayohudumia kata zote, tarafa ya Shelui nayo vivyo hivyo. Hakimu mmoja anayetegemewa na mahakama mbili hadi tatu hupata mzigo mzito na mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali katika mpango wake wa kujenga Mahakama za Mwanzo, niambiwe mkoa wa Singida tumepewa fedha za kujenga mahakama ngapi? Vile vile nielezwe na mahakama ambazo ni chakavu Singida zitakazoratibiwa ni ngapi?

Mheshimiwa Spika, napenda kuikumbusha tena Serikali kuwa kati ya mikoa yenye watuhumiwa wengi wenye kesi zinazohitaji kusikilizwa na Jaji ni mmojawapo. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri aliwahi kunitia moyo kuwa tutakuwa mmoja wa mikoa itakayopewa kipaumbele kujenga Mahakama Kuu, ningefurahi kusikia endapo azma hiyo imeanza kufanyiwa kazi ili kupunguza kero ya kesi nyingi kuchelewa na kusababisha msongamano wa watuhumiwa na mahabusu gerezani.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwani imekubali kuwakopesha Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ili kuwarahisishia adha ya usafiri wanayoipata. Napenda kuishauri Serikali kwa kuwa hakimu anaishi kwa mshahara tu, mshahara huo una matumizi mengi ikiwa ni pamoja na kujenga nyumba, kusomesha watoto na kadhalika, naiomba Serikali iwape pikipiki mahakimu hawa bure kama zifanyavyo sekta zingine, kama wataalamu wa mifugo, kilimo, afya na kadhalika kwani wote hawa ni watumishi wa Serikali moja. Kuwakopesha pikipiki mahakimu ni kutokuwatendea haki, hii ni kuwavunja moyo wa kutekeleza majukumu yao na kuwachochea kupokea rushwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali kuwa kada hii ya mahakimu ni nyeti sana na inamianya ya rushwa kulingana na majukumu yenyewe. Hivyo basi ili tuwapunguzie vishawishi, ni vyema tuwape mishahara inayoridhisha pamoja na kuhakikisha maslahi yao wanalipwa kwa wakati muafaka kuliko kulimbikiza madai yao.

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Serikali kuwa mahakimu kazi yao ni nzito na ngumu inayohitaji kutenda haki kwa Watanzania wanapofikishana mahakani hata kama anayo hatia na kwa kuwa mahakimu wetu wanakiu ya fedha itakuwa sio rahisi kuacha kupokea rushwa.

Mheshimiwa Spika, dawa pekee ni kuboresha mishahara yao na kuwapa maslahi yao mfano nauli, posho ya safari na kadhalika kila anapopewa kazi inayohitaji malipo ya ziada, tutasaidia sana kupunguza kiu yao na wataachana na rushwa.

Mheshimiwa Spika, naifahamisha Serikali kuwa ni mara chache sana wanawake na watoto hupata haki zao mahakamani kwa sababu nyingi, mfano ni uwezo wa kipesa kuwa duni, umbali wa mahakama, kutofahamu sheria na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imeweza kuanzisha Mahakama ya Ardhi, Mahakama ya Biashara na inaangalia uwezekano wa kuanzisha Mahakama ya Kadhi, naomba sasa ione uwezekano wa kuanzisha Mahakama ya Familia ili kusogeza huduma kwa wananchi na itasaidia wanawake na watoto kutendewa haki.

Mheshimiwa Spika, nayapongeza sana mashirika yasiyo ya Kiserikali ya *TAMWA*, *TAWLA* na *Tanganyika Law Society* jinsi yanavyosaidia wanawake katika kupata haki zao mahakamani hasa wale wasiojua lugha ya Kiswahili ama sheria.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kuyaunga mkono mashirika haya pamoja na kuwahamasisha kupeleka huduma hii vijijini walipo walengwa kwani bado wapo wanawake, watoto hata wanaume wanaopoteza haki zao kwa kutokuwa na uwezo wa pesa ama kutokuwa na uelewa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuijulisha Serikali kuwa ulimwengu wa leo wahalifu ama watuhumiwa wengi wanaelimu ya juu sana hivyo huweza kukwepa makosa kijanja na Mahakimu wetu kwa ajili ya taaluma ndogo au kupitwa na wakati hushindwa kuwatia hatiani hata kama wanahatia, nina hatia mahakimu wengi wako tayari kujiendeleza kama watapatiwa fedha. Naiomba sana Serikali ichukue jukumu la kusomesha watumishi hawa kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika kuwa mahakimu wengi wanakaa kituo kimoja kwa muda mrefu na kuwafanya waolewe na mazingira kisha kuwafanya wasitende haki.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kutowaacha mahakimu kukaa muda mrefu katika kituo kimoja muda mrefu, hii itasaidia sana kutenda haki na kuboresha utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Spika, katika kero zinazowakera Mahakimu ni pamoja na tatizo la nyumba. Kulingana na kazi yao hakimu kukaa uraiani ni kuhatarisha maisha yao.

Naishauri sana Serikali kati ya mambo yanayofaa kupewa kipaumbele ni pamoja na kuwajengea nyumba mahakimu.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wangu ambao nategemea kupata majibu. Napenda kuunga mkono hoja hii mia kwa mia.

**MHE. BEATRICE M. SHELUKINDO:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri kwa kazi nzuri sana anayofanya, pamoja na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Mathias Chikawe, hakika tumeona kwa macho yetu mabadiliko katika sekta hii.

Mheshimiwa Spika, je, Kilindi ipo katika orodha ya ujenzi wa Mahakama ya Wilaya? Hadi sasa ni Mahakama ya Mwanzo, ambapo *District Magistrate* hutoka Handeni kiasi cha kilometa 98 hii husababisha si usumbufu tu kwa hakimu ambaye Wilaya ya Handeni pekee ni kubwa mno, pia hakimu huyu huhudumia Wilaya ya Kilindi lakini vile vile kwa wananchi wa Kilindi kwa Serikali ya ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya, kuna kila sababu ya kujenga Mahakama, mchango wa wananchi upo tunachohitaji ni msukumo wa ziada.

Mheshimiwa Spika, naomba kujua mishahara ya mahakimu na watumishi wa mahakama ni kiasi gani? Nakusudia kushika shilingi kwenye hili.

Mheshimiwa Spika, kwa kiwango ninachojua mimi kama niko sahihi, tutaepukaje rushwa ikiwa hawa wanashikilia haki na maamuzi?

Mheshimiwa Spika, usafiri wa gari au pikipiki upatikane kama Wilaya nyingine, ili mafaili nyeti yanapotolewa Kilindi kwenda Handeni utumike. Kama gari ni mpaka tupate *Disrict Magistrate* kwani kuna shida gani kutuletea Hakimu wa Wilaya?

Mheshimiwa Spika, nashauri tuletewe hakimu kwani hata huyu kutoka Handeni hutoa huduma kwenye mahakama hiyo hiyo anapokuja Kilindi.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, naiunga mkono hoja hii, naitambua kazi kubwa inayofanywa na Wizara ya Katiba na Sheria. Hata hivyo yapo mambo ambayo nitapenda kuyachangia.

Mheshimiwa Spika, kwanza hali ya mahakama zetu nchini hasa za mwanzo ni mbaya sana, napenda nitoe mfano Mahakama ya Mwanzo ya Muhutwe ni mbaya sana.

Namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria ya tarehe 22/11/2006 alijionea hali mbaya ya majengo ya Mahakama hiyo, naamini alijionea kuwa mahakama ina jengo bovu tena la kizamani lililojengwa enzi za ukoloni na kichafu ambalo hakika halikidhi haja ya mahakama ambayo inatumika kutolea haki za wananchi kwa kutwa nzima, haina choo kwa ajili ya wateja wa mahakama hiyo. Hata pale nilipojitolea kuchimba shimo la choo, ngazi zinazofuata hazikuwa tayari kukijenga hali iliyofanya shimo hilo litumike kwa takataka badala ya choo.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Muhutwe haina nyumba ya Hakimu, Hakimu anapaswa kupanga mbali na anatakiwa kuwahi kazini. Pamoja na tatizo la nyumba Mahakama ya Mwanzo Muhutwe haina hakimu wake kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, inakuwa vigumu na kuwanyima haki kwa wakati unaostahili wananchi kwa kuchelewa kusikilizwa na kuamuliwa kesi zao. Ukichukulia ukubwa wa maeneo, Hakimu mmoja kupangiwa zaidi ya Mahakama moja katika tarafa mbili tofauti nayo ni tatizo lingine kwani kesi zinakuwa nyingi kupita uwezo. Hata hivyo nampongeza Hakimu aliyepangiwa Mahakama za Muhutwe na Kamachumu, anaweza kuzitembelea mahakama hizi kwa kila wiki. Hata hivyo nadhani anashindwa kuamua kesi nyingi kwa kuwa muda wake mwingi unaishia kati ya kituo kimoja na kingine. Nashauri hakimu apewe kituo cha ziada kilicho katika eneo la tarafa yake hiyo hiyo na anapopewa tarafa apewe usafiri wa pikipiki ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iendelee kuziangalia mahakama hizi ziwe na majengo ya kisasa yanayozingatia mazingira ya mvua, jua kali na upepo, pia baridi kwa eneo husika ili hakimu aendeshe kesi wakati wote bila kuathiriwa na mazingira.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo la kesi za ardhi kusikilizwa katika mahakama za kawaida, nikitoa mfano wa kesi za mashamba zilizo nyingi katika mfano wa kesi za mashamba zilizo nyingi katika Mkoa wa Kagera zinasikilizwa na Mahakama za kawaida. Napenda kuiomba Serikali ielekeze kesi za mashamba ambazo kimsingi ni za ardhi zisikilizwe na mabaraza ya ardhi ya Wilaya.

Hata hivyo, haya mabaraza ya ardhi ni machache, mfano mkoa mzima wa Kagera kuwa na mahakama moja tu iliyo Bukoba Mjini na hakimu mmoja kwa ajili ya Wilaya nane, ni sawa na hakuna.

Mheshimiwa Spika, mabaraza ya ardhi yangeanzishwa haraka kila Wilaya, lakini pia mabaraza ya kata yaliyopo yaheshimiwe badala ya kuyakiuka.

Mheshimiwa Spika, napenda kuiomba Serikali iongeze kasi ya kujenga Mahakama ya Mwanzo nchini, pia Mahakama za Wilaya ziangaliwe kwani baadhi hazikidhi hoja kama ile ya Muleba.

Mheshimiwa Spika, vitendea kazi hasa usafiri uangaliwe tena maana bado ni wachache waliopo wapatiwe nyenzo za usafiri pia *(lock up)* ya Muhutwe itazamwe.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na kukupongeza sana wewe na Naibu Waziri, Katibu Mkuu, *DPP* na watendaji wengine wote walio chini yake kwa kazi nzuri mnayoifanya katika kuhakikisha sheria zinatafsiriwa vizuri, haki zinatendeka kwenye Mahakama zetu kwa faida ya wananchi wetu. Napongeza sana jinsi mnavyohakikisha Katiba inatunzwa na wananchi wote bila kujali itikadi za vyama nawaomba muendelee hivyo hivyo katika kufanya shughuli zenu kwa faida ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nimeridhishwa na uamuzi wa Serikali kutenganisha kazi za upelelezi na kazi za kuendesha kesi. Huko nyuma wananchi wetu walikuwa hawatendewi haki kwa hatua iliyokuwa inafanya ya mtu mmoja kupeleleza na kuendesha kesi. Naomba waliokabidhiwa dhamana hiyo wasaidiwe kwa hali na mali ili waenee nchi nzima badala ya mikoa michache iliyochaguliwa.

Mheshimiwa Spika, hali za Mahakama zetu za Mwanzo bado zina hali mbaya kutokana na kukosa vitendea kazi, majengo ya mahakama na nyumba wanazoishi mahakama kuchakaa sana.

Mheshimiwa Spika, Mahakama zetu bado zina upungufu mkubwa sana wa mahakimu. Iramba Mashariki, Mahakama za Iambi, Kinyangiri na Kirumu hazina mahakama kwa muda mrefu, naomba sasa zipatiwe mahakimu mapema na kama sasa hivi watapatikana na kupelekwa Iambi, Kinyangiri na Kivumi.

Mheshimiwa Spika, naomba Mahakimu waendelee kupata mikopo ya vyombo vya usafiri kama pikipiki au magari pia naomba sheria zinazopitishwa na Bunge na kupata idhini ya Mheshimiwa Rais ziwe zinapelekwa kwenye mahakama zote zikiwemo za mwanzo, pia naomba Katiba zilizotafsiriwa kwa Kiswahili zipelekwe kwenye Wilaya, Kata na Vijiji ili waweze kununua na kuzitumia.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, napenda nami kuchangia hoja hii. Kwanza kabisa nachukua nafasi hii kuwapongeza viongozi wa Vyama vya Upinzani Mheshimiwa Freemani Mbowe (CHADEMA), Mheshimiwa Profesa Ibrahim Lipumba *(CUF),* Mheshimiwa James Mbatia *(NCCR-Mageuzi),* Mheshimiwa Augustine Mrema *(TLP),* wanaharakati Chama cha Sheria Tanzania, Chama cha Kutetea Haki za Binadamu na Watanzania wote ambao wamejitoa katika kuleta mabadiliko na hasa kuandika Katiba upya.

Mheshimiwa Spika, labda nitoe mfano mdogo tu wa mapungufu niliyoyaona katika Katiba. Katiba inaeleza wazi namna gani ya kumpata Rais, Waziri Mkuu, Spika, Majaji pia namna ya kuwaondoa katika madaraka, Katiba haisemi chochote kuhusu Wabunge na Madiwani namna ya kuwaondoa katika madaraka yao.

Mheshimiwa Spika, jana tu wakati wa semina ya watu wenye ulemavu wameeleza kwamba Katiba yetu inatoa haki kwa wote lakini Katiba haisemi haki za watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, Katiba inatenza nguvu za Wabunge kuwakilisha vyema matakwa ya wananchi hasa pale Katiba inapotamka wazi kwamba Hoja au Muswada wa Serikali unapokataliwa kama ilivyoainishwa na Katiba, Bunge linaweza kuvunjwa?

Mheshimiwa Spika, inakuwaje Wabunge walazimishwe kukubali Miswada ambayo haina manufaa kwa wananchi kwa sababu tu Katiba inatishia maslahi yao? Hiyo

ni mifano michache tu. Nadhani kwa nia njema tu na kwa maslahi ya nchi yetu mjadala wa Katiba uwe wa Kitaifa na haja ya Katiba mpya ipo si vyema kupuuza jambo hili.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, pia napenda kutoa pongezi zangu kwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, pamoja na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Mathias Chikawe na watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, napenda niipongeze Serikali kwa kumteua *DPP* kuendesha shughuli za mashtaka ambazo zote zilikuwa zinashughulikiwa na Wizara ya Usalama wa Raia. Naiomba Serikali kwa utaratibu huu ianze kusikiliza kesi za Sungusungu ambazo zimekaa muda mrefu bila kupata ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu nina kesi mbili za Sungusungu ambazo zinahusiana na mauaji, katika tarafa ya Bugando kata ya Nzera, kijiji cha Igate, Mwenyekiti wa kijiji hicho Ndugu Mahande na mwenzake wamewekwa mahabusu kwa muda mrefu, ufumbuzi wa suala la mauaji ya dereva aliyegonga mtu kijijini hapo baadae wananchi wakampiga dereva hadi kufa. Kitendo cha kuchukuliwa Mwenyekiti wa Kijiji ambaye hakuwepo wakati wa tukio hilo kumeleta chuki kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, pia wananchi watatu wa tarafa ya Kasemwa kata ya Kasemwa kitongoji cha Mwilima, mwizi alipigwa hadi kufa na walichukuliwa viongozi wa Sungusungu wafuatao:- Onesmo Matinde Mtemi - Mtemi, Mathili Malole-Kamanda, Nicolaus Willium Kabadi - Jeshi. Sungusungu hawa wapo mahabusu, ndugu na jamaa zao hawajui hatima yake itakuwaje.

Mheshimiwa Spika, matukio haya mawili yanavunja nguvu ya kuleta amani na utulivi katika maeneo haya. Polisi ni wachache, hivyo shughuli za ulinzi zinaendeshwa na wananchi kupitia Jeshi lao la Sungusungu.

Mheshimiwa Spika, naomba sana suala hili lipatiwe ufumbuzi haraka ili wananchi wa maeneo husika wawe na imani na Serikali yao. Imefika hatua ya ndugu na jamaa kuchanganyikiwa na pia kuwa na imani kuwa haki haiwezi kupatikana.

**MHE. MANJU S. MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kutoa mchango wangu katika mambo mawili muhimu ambayo naomba Serikali kupitia Wizara hii iyazingatie nayo ni kuanzishwa ofisi na wadhifa wa Kadhi Mkuu, ni takribani miaka 12 sasa tangu hoja hii ilipoanzishwa na aliyekuwa Mbunge wa Bagamoyo Marehemu Mohamedi Ramiya. Jambo la kusikitisha ni kwamba suala hili limekuwa linapigwa danadana, zimeundwa Tume mbili tofauti za Bunge na mapendekezo yakawasilishwa na ambaye hata Serikali iliyapata, lakini bado kunakuwa na kigugumizi.

Mheshimiwa Spika, jambo la kushangaza kila unapokaribia Uchaguzi Mkuu zinatolewa kauli tamu za waislamu lakini chaguzi zikipita na suala la Kadhi linatupwa katika kapu la takataka, kwa bahati nzuri Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005

suala la kuanzishwa wadhifa wa Kadhi Mkuu limo, kinachonishangaza ni kuundwa kwa Tume zingine kukusanya maoni. Hivi huku si kufuja mali za umma? Tunamdanganya nani? Kubwa zaidi ni madhehebu ya kikristo yamekuwa yakitia shinikizo la kutoanzishwa kwa ofisi ya Kadhi Mkuu wakidai nao waanzishe mfumo huo. Ieleweke kuwa kwa sehemu kubwa mfumo wote wa sheria uliopo nchini sasa ni sheria za kikristo. Waislamu wanadai ofisi ya Kadhi ili washughulikie yale yanayowahusu, mambo hayo ni ndoa, talaka, mirathi na uamuzi sahihi wa kuandama mwezi, wakfu na mengineyo ya waislamu tu.

Mheshimiwa Spika, wanaosema kwamba ofisi hii itaathiri ndoa mchanganyiko yaani Waislamu na Wakristo hawaoni ukweli. Kwa mujibu wa Uislamu hakuna ndoa mchanganyiko. Wanaoishi hivyo ni mtu na hawala yake. Mahawara watahukumiwa na sheria za huko walikofungia ndoa na sio kwa Kadhi Mkuu. Hoja kwamba kuanzishwa kwa Kadhi Mkuu kutaleta Sharia ni hofu ya kujiunga tu kwani katika Jamhuri hii ya Muungano wa Tanzania upande wa Zanzibar yupo Kadhi Mkuu lakini hakuna Sharia na mambo yanakwenda vizuri tu wakati zaidi ya asilimia 90 ya Wanzanzibari Waislamu. Pia Kenya, Uganda, Msumbiji na Afrika Kusini zina asilimia ndogo ya Waislamu lakini wana ofisi ya Kadhi Mkuu. Uganda kwa mfano katika Afrika Mashariki ni nchi ya Kikatoliki lakini Kadhi yupo. Uingereza ili mtu aweze kuwa Waziri ni lazima awe Muanglikana na kwa nini ofisi hii hapa Tanzania ambapo zaidi ya asilimia 60 ni Waislamu?

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kuona madai ya Waislamu yanapuuzwa na yanaendelea kuwekwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ili kupumbaza Waislamu kwa lengo la kuomba kura zao. Mfano wa kupuuzwa kwa masuala ya Waislamu ni mkutano wa UWT uliofanyika wiki iliyopita ulipangwa na kuendeshwa siku ya Ijumaa ambayo ni siku muhimu na ya ibada kwa Waislamu. Hakuna aliyejali kuwa kwa kufanya hivyo itawanyima wajumbe Waislamu fursa ya kumsabihi Mola wao. Hapa kinachofanyika ni ama washiriki mkutano waache ibada au waabudu wakose haki yao ya msingi ya kumchagua kiongozi wampendaye. Tufike mahala tutambue kuwa nchi hii ni yetu sote na kwamba masuala ya imani yaheshimiwe na kila upande. Swala la Kadhi Mkuu, lisiamuliwe Makanisani kama ambavyo mijadala ilivyokuwa inaendeshwa wakati lilipoibuka mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, napenda kumalizia hoja hii kwa kutamka kuwa sitounga mkono hoja ya Waziri wa Katiba na Sheria hadi nipatiwe ratiba ya haraka ya utekelezaji wa uanzishwaji wa ofisi ya Kadhi Mkuu.

Kuhusu adhabu ya kunyongwa, siwaungi mkono wanaotakaa adhabu hii iondolewe, aliyeua kwa kukusudia naye pia auwawe. Hakuna haja ya kupoteza fedha za Serikali kuunda Tume, haki za binadamu zipi zinazolindwa, yule aliyeuawa kwa kukusudiwa hakuwa binadamu?

Mheshimiwa Spika, suala la rushwa mahakamani yaelekea Serikali hailipi uzito unaotakiwa. Malalamiko ni mengi, mfano ni kesi niliyowasilisha kwa Mheshimiwa Waziri mwaka jana hadi sasa shauri halijaisha, tunakwenda wapi?

**MHE. ZAYNAB M. VULLU:** Mheshimiwa Spika, napenda nichukue fursa hii kumpongeza Waziri na Naibu wake bila ya kusahau watendaji wote.

Mheshimiwa Spika, tatizo la mrundikano wa kesi katika mahakama ifike wakati wa kupatiwa ufumbuzi wa kudumu maana ni kama kutowatendea haki watuhumiwa. Hii inatokana na uhaba wa mahakimu au ucheleweshwaji wa bila kutarajia. Ni vyema Wizara kufanya utaratibu wa kuongeza idadi ya Mahakimu katika Mahakama zote kuanzia ngazi ya Wilaya hadi Mkoa.

Mheshimiwa Spika, kuna haja ya kuangalia aina za kesi na kutoa elimu ya sheria kwa jamii kwani kuna baadhi ya makosa yangeweza kuepukika kwani kuna baadhi ya wananchi hawajui sheria ambayo ni haki yao ya msingi. Hivyo basi ombi langu je, ni lini Wizara itaongeza juhudi zake katika kutoa elimu kwa jamii na hasa shuleni ambapo ndipo tunakotoa na kulea vijana wetu ambao tunataka wawe raia wema.

Naomba nipatiwe jibu kuhusu utaratibu ambao Wizara umeandaa wa kutoa elimu ya sheria shuleni. Ni nini mpango wa Wizara wa kuhakikisha Mahakimu wanapatiwa japo mikopo ya kununua chombo cha usafiri cha kuwawezesha kufanikisha majukumu yao?

Mheshimiwa Spika, ni Wizara inasimamiaje sheria kwa walemavu ili na wao wajione ni sehemu inayolindwa na sheria kama vile kuhakikisha majengo yanakidhi mahitaji ya walemavu kwenye vyombo vya usafiri wa umma na hata vyombo vya mawasiliano nchini?

Mheshimiwa Spika, mwisho ni mategemeo yangu mabadiliko ya sheria ya ndoa ya mwaka 1971 yatawasilishwa Bungeni mwezi Februari kama nilivyojibiwa kwenye swali langu la nyongeza na itapitia kwa wadau wote ili kupata maoni zaidi. Naunga mkono hoja.

**MHE. HEMED MOHAMED HEMED:** Mheshimiwa Spika, ni vema nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani sasa napenda kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika kwa uongozi wako ulio bora, pia natoa pongezi zangu kwa Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, kwa hotuba yake ambayo ina mtazamo wa upatikanaji wa haki nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hayo sasa naomba nitoe mchango katika Wizara husika kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kumbukumbu zangu Serikali iliunda Tume mbalimbali za kutathmini Katiba ya sasa. Mfano Tume ya Jaji Francis Nyalali, Jaji Robert Kisanga, tamko la Tume zote ziliishauri Serikali kuwa Katiba hii haifai, kama kweli Serikali iliunda Tume hizi ikiwa na nia njema ni kipi kichozuia kurekebisha Katiba yetu nchini? Inasikitisha sana Serikali kutumia fedha nyingi za kodi za Watanzania kwa kuunda Tume hizo na hatimaye kudharau maoni ya Tume hizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mahakama ya Kadhi pia nakumbuka kwamba Serikali iliwahi kutoa tamko juu ya kuwepo kwa Mahakama za Kiislamu, lakini mpaka leo hii sura ya kuwepo Mahakama ya Kadhi Mkuu haipo, hii ni kusema Serikali inakigugumizi juu ya suala hili.

Mheshimiwa Spika, kuna makundi ya Watanzania ambao wanautofauti wa kidini na kusema uhuru wa kuabudu upo nchini. Waislamu kuna mambo yao ambayo ni lazima yatendeke kwa misingi ya kiislamu kama vile ndoa, mirathi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kutokuwepo kwa Mahakama ya Kadhi nchini sitegemei kwamba kutapatikana haki kwa Waislamu. Naishauri Serikali kwamba ipatikane Mahakama hiyo ili iwawezeshe Waislamu kupata haki zao.

Mheshimiwa Spika, pia kuna upungufu mkubwa wa mahakimu katika ngazi zote za mahakama nchini, kitendo hiki husababisha kuwa na mrundikano wa mahabusu nchini, naiomba Serikali ihakikishe kuwepo mahakimu wa kutosha nchini ili kuondoa msongamano wa mahabusu magerezani.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri.

**MHE.MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Spika, ningependa kuchukua hatua hii kuchangia suala zima la kuanzishwa Mahakama ya Kadhi Mkuu. Ni muda mrefu sasa wananchi wamekuwa wanatoa maoni mbalimbali kuhusu uanzishwaji wa Mahakama ya Kadhi Mkuu. Kumekuwa na mkanganyiko wa mawazo, Waislamu wakitaka mahakama hiyo ianzishwe na wale wasio waislamu wakipinga mahakama hiyo. Tukipima hoja za wale wanaopinga utaona ni dhahiri hakuna hoja ya msingi. Kinachoonekana ama ni woga au ni njama ya kuupiga vita Uislamu. Kwa kuwa nimechukuwa juhudi kubwa kupima na kuona umuhimu wa kuwepo Mahakama ya Kadhi Mkuu, nachukua nafasi hii kutoa mchango wangu juu ya suala hilo.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote niseme kwamba mimi naunga mkono kwa dhati kabisa kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi Mkuu hapa Tanzania kwa kuzingatia sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, suala la Mahakama ya Kadhi Mkuu ni suala linalowahusu Waislamu pekee na kazi zake muhimu ni kushughulikia ndoa, mirathi na mambo ya wakfu na kwa hiyo sioni sababu kwa wao kuwa Waislamu kupinga suala hilo. Suala la Mahakama hii limetajwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM na kwa kuwa CCM imepata ridhaa ya wananchi kuiongoza nchi hii inawajibika kwa namna yoyote ile kutekeleza ahadi hiyo kwa wananchi ya kuanzishwa Mahakama ya Kadhi Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nchi jirani za Kenya, Uganda na hata Zanzibar wote wameanzisha mahakama hizi na zinafanya kazi kwa ufanisi wa hali ya juu na hatujawahi kusikia migogoro yoyote ya kidini iliyosababishwa na taasisi hiyo, sasa

umefika wakati kwa Serikali kuruhusu kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi hapa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kutunga sheria na Bunge kupitisha sheria inayoruhusu Tume hii kufanya kazi zake Zanzibar, kwa hakika hatua hii imepokelewa kwa moyo mkunjufu na wananchi wanaoishi Zanzibar kwani kwa muda mrefu Tume hii ilikuwa inafanya shughuli zake Tanzania Bara pekee. Lakini pamoja na Tume hii kuwa na mamlaka kamili ya kufanya shughuli zake Zanzibar bado tunaona haijajiimarisha kuweza kufanya kazi zake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, sasa wananchi wa Zanzibar wameanza kujenga hofu iwapo ukiukwaji wa haki za binadamu na upandishwaji wa utawala bora unaofanywa na viongozi na vikosi vya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar hasa wakati wa chaguzi zinapofanyika utashughilikiwa ipasavyo. Wale ambao wamekuwa wakizivunja haki hizi za binadamu, ikiwemo kupiga, kujeruhi, kupora mali, kunajisi, kubaka na kuua wananchi wasio na hatia wanachukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Spika, kama kuna sehemu katika nchi hii ambapo haki za binadamu hazithaminiwi na kuwepo watawala wasiozingatia sheria na utawala bora, basi ni kule Zanzibar. Ni vyema basi Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ifanye juhudi ya makusudi ili kujiimarisha Zanzibar na kuweze kusikiliza vilio vya Wanzanzibari ili hatimaye nao waishi kwa amani bila hofu.

Mheshimiwa Spika, linalowezekana leo lifanyike leo kabla madhara hayajawa makubwa zaidi.

**MHE. KABUZI F. RWILLOMBA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, nampongeza Waziri, Naibu Waziri kwa kazi nzuri mnayoifanya, namshukuru sana Naibu Waziri kwa kila ninachomweleza tatizo linalohusu Wizara yake hunisaidia. Pamoja na shukrani, naiomba Wizara iwe inaharakisha malipo ya wazee wa mahakama katika jimbo langu, wazee wa mahakama hawajalipwa zaidi ya miaka mitatu sasa.

Mheshimiwa Spika, tafadhali naomba majibu kwa vile kitendo cha kutowalipa wazee wa Mahakama kunaongeza wazee hawa kujiingiza katika vishawishi upokeaji wa rushwa.

Mheshimiwa Spika, pia naomba ijengwe Mahakama katika eneo la Katoro na Nyarugusu, maeneo haya hayana jengo na mahali ambapo kesi zinaendeshwa, kweli panatia aibu sana. Hakimu wanatumia kijumba kibovu sana ambacho kinavuja. Naomba sana jengo la mahakama eneo la Mji wa Katoro na Nyarugusu.

Mheshimiwa Spika, naomba mambo yafuatayo yatekelezwe, kwanza ni malipo ya wazee wa mahakama yalipwe haraka na yaongezwe, pili, naomba majengo ya mahakama ya eneo la Nyarugusu, Katoro na Busanda na tatu, kuangalia upya kesi ya wizi wa mgodini Geita ambao wanaendelea kuhangaika ni wale wasiohusika na wizi. Wengi wao wanateseka bila kuwa na ushiriki wowote bali wanaendelea kuteseka mahabusu.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu la Siha, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, kwa hotuba yake nzuri ambayo imetolewa asubuhi hii. Ninatamka bila wasiwasi kuwa ninaunga mkono hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, naomba nikumbushie ombi letu la muda mrefu ambalo halijapatiwa ufumbuzi la kutuongezea Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ambao ni adimu sana katika jimbo la Siha ambalo kwa sasa ni Wilaya ya Siha.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Mwanzo iliyopo Siha Mashariki inaendeshwa mara moja au mbili kwa wiki na wakati mwingine hufungwa mfululizo kutokana na hakimu kulazimika kwenda Mahakama nyingine iliyopo Sanya Juu, naomba Wizara itusaidie kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba nikumbushe kuwa Siha sasa ni Wilaya kwa hiyo tunaiomba Wizara itusaidie katika suala la ujenzi wa Mahakama ya Wilaya, ni ukweli usiopingika kwamba kufuatia kuanzishwa kwa Wilaya ya Siha umuhimu wa kuwa na Mahakama ya Wilaya utakuwa umeongezeka, hii ni kwa sababu ya kupanuka kwa huduma mbalimbali kutaongeza mawasiliano zaidi ya kibiashara na kiuchumi na hata yale ya kihuduma na hivyo vitendo vya uvunjwaji wa sheria haviwezi kuepukika. Naomba sana Wizara ione umuhimu wa kuanzisha huduma hii.

Mheshimiwa Spika, narudia tena kusema naunga mkono hoja hii.

**MHE. MGENI J. KADIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kuchangia Wizara hii. Sasa naanza kuchangia Wizara ya Katiba na Sheria kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mahakama ni chombo na muhimili ndani ya nchi yoyote duniani, kwani chombo hiki hufanya kazi zake kwa mujibu wa sheria na kwa mujibu wa makosa yanayofanyika.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie upya juu ya unyanyasaji wa watoto, wanawake na mirathi.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha wanavyofanyiwa watoto, wanavyonyanyaswa kwa kubakwa na kunajisiwa na kuuliwa pamoja na kutupwa majalalani. Hii sheria iliyopo sasa iangaliwe upya, ni ndogo sana. Kwa hiyo, angalau mtu huyo atakaegundulika kumtendea mtoto basi sheria iwekwe kuhasiwa au kifungo cha maisha au auliwe. Je, Serikali ina mtazamo gani juu ya suala hilo?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mahakama ya Kadhi Mkuu, Serikali tunaiomba suala hili lipatiwe ufumbuzi haraka iwezekanavyo. Ni muda mrefu sasa tokea Serikali ilipozungumzia suala hili, pindi mahakama hii ikifanya kazi zake itawaondolea wanawake matatizo yao juu ya mirathi na juu ya ndoa, kwa sababu dini ya Kiislamu ina Sharia zake ambazo ni tofauti na dini nyingine. Kwa hiyo, kuundwa Mahakama ya Kadhi kutatoa nafasi ya Waislamu kutetea haki yao.

Mheshimiwa Spika, hakimu anatakiwa afanye kazi zake kwa mujibu wa sheria. Awe ni mtu muadilifu asipende kuchukua rushwa wala asipendelee upande mmoja, wala asiwe mbabaishaji na kuchelewesha kesi na kusababisha msongamano wa mahabusu.

Mheshimiwa Spika, kuna mahabusu wengi wanawekwa kizuizini kwa muda mrefu bila ya kesi zao kusikilizwa na kukaa muda mpaka kufikia kufa na bado kesi zao hazijapata ufumbuzi wowote.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Wizara hii pamoja na Naibu Waziri na timu yake kwa Bajeti hii yenye mwelekeo.

**MHE. ZULEIKHA YUNUS HAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naiunga mkono hotuba ya Waziri wa Katiba na Sheria kwa asilimia mia kwa mia. Pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na watendaji wake wote kwa kazi na umahiri. Pia nawapongeza kwa hotuba hii ya Bajeti yenye kueleweka na yenye ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya haya nasisitiza kwamba hiyo mikataba ya Kimataifa ambayo nchi yetu imeiridhia basi iletwe Bungeni haraka ili iridhiwe na kutungiwa sheria kwa ajili ya utekelezaji. Pia zile sheria ambazo zinahitaji kufanyiwa marekebisho ziharakishwe ili kupunguza lawama kwa wananchi wetu pamoja na wanotutuma. Kwa leo uchangiaji wangu ndio huu, nasema tena naunga mkono hoja.

**MHE. MONICA N. MBEGA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Taasisi zilizo chini ya Wizara hii, wataalamu wote wanaofanya kazi katika Wizara hii kwa kazi nzuri inayoendelea kufanyika.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 39, Tume ya kurekebisha sheria itaendelea na marekebisho mbalimbali ya sheria katika kifungu cha ix, sheria ya makosa ya kujamiiana

Mheshimiwa Spika, Tume ione namna ya kurekebisha kwa kuihusisha sheria ya elimu ya mwaka 1978, pia *Marriage Act* ambapo kumekuwa na tatizo katika kuwashughulikia wanaowapa mimba wanafunzi chini ya miaka 18. Mkoa wa Ruvuma umetoa agizo kwa maafisa elimu ili wawafikishe Mahakama ya Wilaya wale wote wanaowatia mimba wanafunzi ili washitakiwe kama kosa la kubaka. Hata hivyo hakuna hata mtu mmoja ambaye ameshitakiwa kwa kuzingatia hilo na hivyo kuifanya vita dhidi ya mimba za wanafunzi kushindwa.

**MHE. KHADIJA SALUM AL-QASSMY:**Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia siku ya leo kufika hapa Bungeni bila kushikwa mkono. Pia napenda kukushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Spika, kwa jitihada zako za kutuongoza.

Mheshimiwa Spika, pia sina budi kumpongeza Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, kwa hotuba yake ambayo imeleta mategemeo kwa Watanzania kuishi kwa misingi ya sheria.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba uniruhusu nitoe mchango wangu katika hotuba husika. Kuhusu Mahakama ya Kiislamu, kwa kuwa nchi yetu ina uhuru wa kuishi na kuabudu, hakuna sababu ya Serikali kuwa na kigugumizi cha kuwaruhusu Waislamu kupewa nafasi ya Mahakama ya Kadhi Mkuu nchini.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo ya ulazima kwa Waislamu, kwa mfano, ndoa, mirathi na kadhalika. Mambo haya ndani ya Waislamu hutokea makosa na kulazimika hukumu. Ni nani atakaetoa hukumu kama si Kadhi? Kwa nini Serikali iwe na kigugumizi juu ya kuwepo kwa Mahakama ya Kadhi nchini?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Katiba, ni muda mrefu sana Serikali iliunda Tume ili kuijadili Katiba yetu. Iliundwa Tume ya Jaji Francis Nyalali na Jaji Robert Kisanga. Matarajio ya Watanzania ni kutumika jasho lao kwa maslahi ya nchi yao kumbe mambo hayakutakiwa hivyo. Dhamira ya Serikali kutumia fedha za watoa jasho wa Kitanzania kwa kusingizia eti Tume ya Kikatiba.

Mheshimiwa Spika, Tume hizo zilipendekeza kuwa Katiba hii haifai, la kusikitisha hadi sasa Serikali inatumia Katiba hii ambayo ina upungufu mkubwa. Ni vyema sasa Serikali iandae Katiba itakayokidhi mahitaji ya nchi yetu hasa ukitilia maanani nchi yetu imeingia katika mfumo wa vyama vingi nchini. Ahsante.

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Waziri wa Katiba na Sheria kwa hotuba nzuri. Aidha, nampongeza Jaji Mkuu Augustino Ramadhani, kwa kuteuliwa kwake hivi karibuni kuwa Jaji Mkuu mpya wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa jimbo langu wanayo matatizo makubwa ya huduma za kisheria, hakuna mahakama na hakuna mahakimu. Mahakama za Bashanet, Dareda, Ufana, Isidas na kadhalika ni za umuhimu mkubwa. Leo hii wananchi wa maeneo hayo wanatembea kilometa hadi 70 kwenda tu kufuatilia Mahakama Babati Mjini. Huu ni uonevu mkubwa na ni kuwanyima haki ya msingi wananchi wa Babati Vijijini.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 hadi sasa mwaka 2007 kumekuwa na ahadi ya Mahakama za Mwanzo za jimbo la Babati Vijijini kupatiwa Mahakimu. Alikuja Babati Waziri wa Katiba na Sheria na kuahidi hivyo. Lakini mpaka leo tunaye hakimu mmoja Mahakama ya Mwanzo Babati Mjini na anazidiwa na idadi kubwa ya kesi zilizopo.

Mheshimiwa Spika, naomba tuletewe Mahakimu, wananchi wapate haki zao za msingi, wapunguze masafa marefu ya kusafiri kutoka Ufana kwenda Babati kilometa 70 na hivyo kuwa kilometa 140 kwenda na kurudi. Tunayo hakika kila mwaka idadi ya mahakimu Lushoto ipo, naomba mwaka huu wa fedha nasi tufikiriwe tupate mahakimu. Ili hayo ninayoomba yatekelezwe naunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa

hotuba hii. Vile vile napenda kumpongeza Msemaji Mkuu wa Upinzani kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ilianza mwaka 1965 na kufanyiwa marekebisho mwaka 1977 kwa mfumo wa chama kimoja. Mfumo wa vyama vingi ulianza 1992 hivyo kuna ulazima wa kubadilisha Katiba ili iendane na mfumo wa sasa.

Mheshimiwa Spika, Katiba yetu ina mapungufu mengi kwa mfano inasema ibara 3(1) ya Jamhuri ya Muungano ni nchi ya Kidemokrasia na ya kijamaa isiyokuwa na dini yenye kufuata mfumo wa vyama vingi vya siasa. Lakini kwa mwenendo wa kiuchumi na biashara huria *(globalization),* ni kweli tunafuata siasa ya ujamaa na kujitegemea?

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, ni lini Tanzania ilifanya elimu ya Katiba kwa wananchi (kushirikisha wananchi) katika kuandaa au kupata maoni yao kuhusu Katiba? Ni kwa nini mtu akihitaji Katiba hazipatikani? Katiba zinatakiwa zipatikane hata kwenye *library* za shule, *bookshop* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapungufu mengine katika Katiba, katika kifungu 55(4) kinasema: "Mawaziri na Naibu Mawaziri wote watateuliwa kutoka miongoni mwa Wabunge." Kwanza kabisa kwa nchi maskini na inayohitaji maendeleo Baraza letu la Mawaziri ni kubwa mno. Kwa mfano Marekani na ukubwa wa nchi ile bado Baraza lao la Mawaziri halifiki hata nusu yetu (wapo 13 tu). Kuwa na Baraza kubwa matumizi ya Serikali yanakuwa makubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, nashauri kuwa ili kusiwe na *conflict of interest,* ili Mawaziri, Naibu Waziri wasipendelee majimbo yao, wote wachaguliwe watu ambao siyo Wabunge. Watakuwa na muda mzuri wa kujibu maswali sababu hawana sababu za kupendelea majimbo yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vitendea kazi/majengo chakavu ya mahakama, hii ni changamoto ambayo bado ipo kwenye Mahakama zetu. Mfano *stationary, computer* zaidi zinahitajika katika ngazi zote. Pamoja na majengo mengine kukarabatiwa bado Mahakama nyingine majengo ni machakavu sana, hayana hata *furniture* za kutosha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uimarishaji wa daftari la kudumu la wapiga kura, kwa kuwa watu wamekuwa wakiongezeka karibu asilimia tatu, ni vizuri kitabu hiki kiwe kinakuwa *up dated* kwa mwaka. Watu wakifikia miaka kumi na nane waandikishwe kwenye daftari hili. Kwa mfano katika uchaguzi mdogo wa Tunduru mwaka 2007 ulikuwa na mapungufu makubwa, vijana wengi waliokuwa wametimiza umri wa kupigakura hawakupata haki yao ya kupiga kura sababu tu walikuwa hawajaandikishwa.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na afya njema.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge, pamoja na viongozi wa Kambi ya Upinzani kwa kutuongoza vizuri.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imeingia katika mabadiliko mbalimbali ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Pia Miswada mbalimbali ya sheria imefanyiwa marekebisho/mabadiliko. Kwa hivyo wakati umefika sasa kuwa na Katiba mpya katika nchi yetu ili kuimarisha umoja na mshikamano kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, kesi huchukua muda mrefu kutokana na uchache wa Mahakimu na Majaji. Kwa hivyo, kuna haja ya kuongezwa kwa idadi ya Mahakimu, Majaji na Mahakama ili kesi zisichukue muda mrefu na hivyo kupunguza usumbufu kwa wananchi wenye kesi Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Mahakama, Mahakimu na Majaji kupatiwa usafiri wa uhakika ili kupunguza usumbufu uliopo hivi sasa kwa ngazi zote za Mahakama pamoja na mahabusu au washitakiwa mbalimbali.

Katika nchi yetu kuna sheria nyingi lakini ukiukwaji wa sheria hizo ni wa hali ya juu. Hii ni kutokana na kuwa, hakujakuwa na umakini wa kutosha katika usimamizi wa utekelezaji wa sheria zilizopo.

Mheshimiwa Spika, mfumo uliopo hivi sasa wa kupata viongozi kupitia vyama vya siasa unawanyima wananchi walio wengi, ambao si wanachama wa chama chochote kupata nafasi ya kuwa viongozi hata kama wananchi hao wana uwezo mkubwa wa kuongoza. Kwa hivyo ni vyema kukawa na mabadiliko katika mfumo wa kupata viongozi ambao hautegemei moja kwa moja vyama vya siasa.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Mahakimu na Majaji kuangaliwa vizuri kimaslahi na kupatiwa nyumba ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, kwa uadilifu na kuepukana na rushwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna baadhi ya mambo yanayowahusu Waislamu ambayo uamuzi wake unapitia kwa Kadhi Mkuu wakati umefika sasa wa kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi Mkuu ili Waislamu wawe na chombo cha kutatua matatizo yao. Ahsante.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa kuisimamia Wizara kwa umakini kwa kushirikiana na viongozi wote walio chini ya Wizara yake, wakiongozwa na aliyekuwa Jaji Mkuu Mheshimiwa Barnabas Samatta. Nampongeza sana Jaji Mkuu mpya kwa wadhifa mpya alioupata, tuna imani naye, ni Jaji anayeheshimika katika jamii ya Watanzania. Tunamtakia kila la kheri katika kazi yake mpya.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana katika Bajeti nilimwomba Mheshimiwa Waziri asaidie kufanya uhamisho kwa makarani wa mahakama za mwanzo katika mahakama za

Nyamikoma, Nyambiti, Ngulla na Malya, hii ni kwa sababu makarani hao wamedumu sehemu hizo kwa zaidi ya miaka 30, wamekuwa kero. Wamekuwa kama miungu watu na hata wanapokuja mahakimu wapya hutumia uzoefu wao kuwachanganya na wao kutokuwa na moyo wa kufanya kazi. Niliomba wahamishwe kama siyo kubadilishwa vituo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mahakama za Nyamikoma, Ngulla na Malya hali za majengo yake hazitamaniki na kulikuwa na ahadi ya kuzijenga au kuzikarabati, ahadi ambayo hadi leo haijatekelezwa. Tunaiomba Wizara kutekeleza ahadi zake hasa ikizingatiwa kuwa Wizara hii inasimamia haki na ikitoa ahadi itekelezwe kama inavyotekeleza katika kutoa haki. Ningependa kujua utekelezaji wa ukarabati /ujenzi utaanza lini?

Mheshimiwa Spika, ningependa kumuomba Mheshimiwa Waziri kwa sababu sisi Wabunge ndio watunga sheria na sisi ndio tunazipitisha ili zikafanye kazi baada ya Mheshimiwa Rais kuzibariki na Mahakama kwenda kuzitekeleza. Kwa sababu hukumu/sheria ya kunyonga tuliitunga na kuipitisha sisi Wabunge na kwa kuwa utekelezaji wa hukumu ya kunyonga ambapo Mheshimiwa Rais humlazimu akubali kwa kuweka saini yake ili mtuhumiwa akanyongwe uamuzi ambao ni mgumu na mzito kwa Rais kuutekeleza kwa kuweka sahihi yake, kwa sababu uamuzi huo ni mgumu na mzito (simsemei Mheshimiwa Rais) lakini tukijiuliza tangu Rais aingie madarakani ni watuhumiwa wangapi walionyongwa chini yake, lakini hata wakati wa Rais wa Awamu ya Tatu?

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema uamuzi huo ni mgumu na mzito, ningeomba Wizara ilete mapendekezo/Muswada wa kurekebisha sheria hiyo ngumu rahisi kiutekelezaji ili tuibadilishe ili iwe katika kuitekeleza. Naunga mkono.

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika Wizara hii ya Katiba na Sheria. Naomba niende katika suala zima la kesi kuwa na muda mrefu bila majibu yoyote hasa kesi za mauaji.

Mheshimiwa Spika, kesi za mauaji zimekuwa zikichukua zaidi ya miaka nane hadi tisa, hii imesababisha mateso makubwa kwa mtuhumiwa kwani anakuwa hapati haki yake ya msingi na anapokuwa amehukumiwa anakuwa tayari anatumikia hicho kifungo kutokana na muda anaokuwa amekaa jela. Serikali ijaribu kuliangalia suala hili upya ili kupunguza mgongano gerezani na kumpa mtuhumiwa haki yake.

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwa wazee wa baraza. Wazee wa Baraza wamekuwa wakilipwa posho ndogo sana, hii ni kuruhusu mwanya wa rushwa, hivyo naomba Serikali iingilie kati suala hili kwani ni tatizo ndani ya Mahakama.

Mheshimiwa Spika, naomba niende moja kwa moja kwenye eneo linalohusu vifaa vya mahakama. Vifaa imekuwa ni tatizo kubwa mno ndani ya Mahakama, kwani wamekuwa wakishindwa kukamilisha kazi zao katika muda unaotakiwa. Naomba Serikali ijitahidi kusaidia katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, naomba niende eneo au kitengo cha walinzi. Walinzi wa Mahakama wamekuwa hawana sifa zinazotakiwa, wengi wao ni walevi na hawafanani na kazi ya ulinzi mahakamani.

Je, ni nani anayehusika na ajira ya walinzi. Kama ni Serikali ni vigezo vipi wanavyotumia na kama ni Wizara husika vile vile ningependa kujua ni vigezo gani wanatumia? Naunga mkono hoja.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali kupitia Bajeti yake ya mwaka 2007/2008 imedhamiria kuboresha mazingira ya kazi katika ofisi zake zote kwa kuzipatia vitendea kazi ikiwemo ununuzi wa kompyuta; kwa kuwa mahakama nyingi za Wilaya bado zina tumia *type writer,* ambao ni mfumo duni na wa kizamani na hivyo kupelekea ufanisi duni ikiwemo ucheleweshaji wa mashauri, je, Serikali itasambaza kompyuta katika mahakama zote za Wilaya ikiwemo Wilaya ya Meatu ili kuziwezesha Mahakama hizo kutekeleza majukumu yake tena kwa ari, nguvu na kasi mpya?

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2006/2007, Serikali ilinunua magari 49 na kuyasambaza kwenye Mahakama za Wilaya na katika Bajeti ya mwaka 2007/2008, Serikali imepanga kununua vyombo vya usafiri, je, Serikali itanunua magari na kuyasambaza katika mahakama za Wilaya zote zilizobaki ikiwemo Wilaya ya Meatu?

Mheshimiwa Spika, kutokana na ucheleweshaji kazi mahakamani kumepelekea mrundikano wa kesi na msongamano wa mahabusu na hivyo kupelekea mahabusu wengi kukaa gerezani kwa miaka 3 hadi mitano bila kesi zao kutajwa wala kusikilizwa, wengi wanakufa kwa kuambukizana magonjwa, nguvu kazi ya Taifa kupungua hata wanaposhinda kesi au kufutiwa hawapewi fidia yoyote, je, ni sababu gani hasa za msingi zinazosababisha ucheleweshaji wa kesi mahakamani?

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ni shukrani kwa Wizara kuiona Mahakama ya Wilaya ya Kilwa kuwa mojawapo ya zile Wilaya 49 zilizopatiwa magari.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Kilwa ina kiwanja chake kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za mahakama, katika hotuba hii sijaona eneo lolote la ukarabati au ujenzi wa mahakama katika Wilaya ya Kilwa. Naomba Bajeti ijayo Mahakama ya Wilaya ya Kilwa ifikiriwe kuitengea fedha kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za mahakama.

Mheshimiwa Spika, ningependa kufahamu sheria ya mirathi. Ili mtu apate haki yake, inachukua muda gani baada ya kila kitu kukamilika katika mahakama? Mahakama inapochelewesha kwa makusudi na hatimaye mali zilizopo zikaisha kwa kuuzwa, nini hatima ya huyu aliyepaswa kurithi? Ni halali kwa yule mjane anayepaswa kurithi kuwanyima mirathi watoto ambao hakuwazaa yeye pamoja na wazazi wa marehemu mume wake, wanaotambuliwa kisheria?

Mheshimiwa Spika, ninao mfano hai na ni wa kuhuzunisha. Naomba majibu Mheshimiwa Waziri.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Hata hivyo ningependa kupata maelezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Wilaya ya Kasulu kidogo imefanyiwa ukarabati, lakini naamini kwa sababu jengo la Mahakama ya Wilaya ni chakavu napendekeza mchakato wa kujenga jengo jipya, tena la kisasa uanze. Jengo lililopo ni kongwe sana na halina hadhi ya Mahakama ya Wilaya. Ni majengo yaliyoachwa na wakoloni miaka 46 iliyopita.

Mheshimiwa Spika, Mahakama nyingi za Mwanzo ni chakavu na mazingira machafu. Napendekeza/kuomba Wizara ya Katiba na Sheria ianze kujenga majengo mapya ya Mahakama katika Wilaya ya Kasulu. Kwa mfano Mahakama za Mwanzo za Makere, Buhoro, Kasangenzi zote ni sawa sawa na mapafu. Tujenge majengo ya kisasa. Sisi Halmashauri ya Wilaya tupo tayari kukusanya nguvu zetu. Tupeni ushirikiano.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa nyumba za mahakimu, ni vizuri utaratibu wa kujenga nyumba za mahakimu ukawekwa kwenye mpango. Wilaya ya Kasulu tangu kuuzwa nyumba ya Hakimu wa Wilaya, Wilaya nzima haina jengo lolote la nyumba ya hakimu. Kwa nini Wizara ya Katiba na Sheria isianze mchakato wa ujenzi wa nyumba hizi hatua kwa hatua? Na ni lini nyumba za Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo zitapewa kipaumbele na Wizara yako? Ujenzi huu unaweza kuwa shirikishi kati ya Halmashauri zetu na Wizara ya Sheria *(joint effort)*. Ahsante.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii kutokana na jinsi Waziri Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Naibu Waziri Mheshimiwa Mathias Chikawe, wakisaidiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Johnson Mwanyika, kwa maandalizi mazuri ya hoja hii ambayo imefafanua vizuri maeneo yote muhimu.

Mheshimiwa Spika, mimi ninayo maeneo machache ambayo ningependa Waziri ayatolee ufafanuzi wa kina, kwa nini sheria ya *Community Service Act* ya mwaka 2002 bado ina suasua kiutekelezaji au kuna kasoro ndani ya sheria inayofanya azma ya Serikali kupunguza mrundikano wa mahabusu wenye kesi ndogo ndogo. Nini kimetokea?

Mheshimiwa Spika, naomba pia nimuombe Waziri kwa ufupi, kulifafanua suala la Kadhi ambalo sisi tunaelewa kuwa maagizo ya Ilani yalikuwa kulitafutia ufumbuzi suala hili. Ufumbuzi unaweza kuwa siyo suala la kuliendeleza haraka haraka kutokana na unyeti wa suala lenyewe kwa jamii ya Kitanzania yenye dini mbalimbali na imani tofauti. Kama litajitokeza basi ni bora kuendelea kusubiri taarifa ya mwisho ya Kamati iliyopewa majukumu hayo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Tume ya kurekebisha sheria kuendelea kuzirekebisha sheria ambazo haziendani na mazingira ya sasa, nashauri sheria ya kifo itazamwe upya na tuchambue upya aina ya kifo ambacho hakidhalilishi utu wa binadamu.

Mheshimiwa Spika, kuna njia nyingi zinazotumika duniani kuuwa wahukumiwa kifo. Mfano, kunyonga kwa kutumia kamba shingoni (sisi Tanzania), kuua kwa umeme (Marekani), kuua kwa sindano ya sumu, kuua kwa kuning'iniza kichwa chini (Misri, Iran, Jordan na kadhalika), kuua kwa kupiga bunduki (China, Vietnam), kuua kwa kupiga mawe (Iran, Afghanistan) na kuua kwa kuchoma visu (Somalia).

Mheshimiwa Spika, njia zote hizi ukizifuata kwa undani, zinadhalilisha sana utu wa mtu. Adhabu za vifungo vikali kwenye magereza maalumu kwa watuhumiwa kama wanavyofanya katika nchi zaidi ya 90 ambazo zimefuta kabisa adhabu ya kifo.

Mheshimiwa Spika, sheria za matunzo ya mtoto nje ya ndoa, sheria ya kubeba mtu kwenye baiskeli na hata ya kuzuia kuweka ngao kwenye gari ndogo za kazi vijijini, ni budi zikapewa uzito unaostahili.

Mheshimiwa Spika, nashukuru Wizara kutujengea Mahakama Kuu Rukwa na tunazidi kuomba suala la zana na samani kwa ajili ya ofisi zote za Mahakama, ikiwa ni pamoja na marupurupu ya watumishi na Mahakimu, Majaji hasa katika mkoa wetu wa Rukwa vipewe kipaumbele kama Mheshimiwa Rais alivyoelekeza kwa mikoa iliyo pembezoni au ile ambayo kwa miaka mingi imeachwa nyuma. Fungu la fedha la kutosheleza nia hiyo ni budi ionyeshwe wazi katika Bajeti zetu tunazoziandaa.

Mheshimiwa Spika, sera zetu nyingi hubaki vitabuni bila kuwa na mtiririko wa mipango ya utekelezaji wa sera hizo. Lakini pamoja na hilo, sheria nyingi hukosekana kuwepo ili kuhalalisha maelekezo ya sera zenyewe kisheria. Hili tusipoliwekea mikakati, sera kama za hifadhi ya mazingira, sera za nishati na madini, sera ya misitu na kadhalika. Naunga mkono hoja hii.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, mahakama bado hazitoshi na haziendani na wakati kwenye majengo na hadhi ya uendeshaji. Bado kesi nyingi za aina mbalimbali za madai na za jinai, za hali, za haki za binadamu na utawala bora na za biashara naomba ziendeshwe vyema.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara hii chini ya Waziri Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, kuisimamia vyema Wizara kupitia Naibu Waziri na watendaji wote kujipanga kwani wananchi mara nyingi huisema Wizara hii hasa kwenye mahakama zote na katika aina zote za kesi kuwa zina usumbufu juu ya haki zao na hutawaliwa na rushwa. Ili kuondosha hayo, Mahakimu na Majaji wawe wengi na kesi zipangwe kwa tarehe na kuendeshwa kwa umakini na kuwajali mahakimu wanaofanya kazi ya Taifa lao.

Elimu na semina itolewe mara kwa mara kwa mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, za Wilaya, Mikoa na hata kwenye vyuo vyote vya sheria vinavyotoa mafunzo ya sheria. Pia kujali maslahi ya Mahakimu na wafanyakazi Mahakamani na sekta za Katiba na Sheria kwa vitendea kazi ili kuepuka usumbuaji, rushwa na mrundikano wa

kesi pamoja na mambo mengine. Sina wasiwasi wakipewa mishahara mizuri, makazi mazuri, usafiri na vitendea kazi vyote, basi patazingatiwa Ilani ya Uchaguzi ya CCM na sera ya Chama Tawala ya ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. Inawezekana kwa Serikali hii ya awamu ya nne na kufuatwa kasi iliyopo.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, kwa kazi nzuri anayofanya tangu ateuliwe kuongoza Wizara hii na tuna matumaini makubwa kuwa akipewa muda na ushirikiano na wadau wote wa Wizara hii atakamilisha majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi wengine ikiwa ni pamoja na Majaji. Nampongeza zaidi Jaji Mkuu mpya Mheshimiwa Augustino Ramadhani, kwa kuteuliwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Mahakama ya Kadhi Mkuu Tanzania Bara, napenda kutoa masikitiko yangu kuwa Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria hakueleza lolote juu ya suala hili, ikimaanisha kuwa kwake yeye Mahakama ya Kadhi sio jambo muhimu na wala sio *priority.*

Mheshimiwa Spika, inawezekana pia ikaonekana kuwa Serikali haiwajali na wala haioni kuwa wanohusika na Mahakama ya Kadhi kuwa ni kundi muhimu nchini. Ndio maana suala hili limechukua takribani miaka 10 bila kupatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, suala hili limekuwa likishughulikiwa wakati wa uchaguzi na hii pia inaweza kutafsiriwa kuwa ni jitihada ya kuombea kura wakati wa Uchaguzi Mkuu.

Mheshimiwa Spika, napenda Serikali ijue kuwa viongozi wa Kiislamu, hasa Mufti na Sheikh Mkuu wa Tanzania, wanafanya kazi kubwa kuwatuliza Waislamu wasifanye vurugu wakati suala hili linashughulikiwa na Serikali kwa kasi ndogo. Ushauri wangu ni kwamba Serikali ikamilishe suala hili kabla ya Uchaguzi Mkuu ujao ili kutekeleza Ilani ya Uchaguzi wa CCM.

Mheshimiwa Spika, mikataba kadhaa iliyofungwa kati ya Serikali na makampuni mbalimbali, hasa ya Kimataifa imekuwa na kasoro. Kwa mfano mikataba ya madini, *ATCL vs SAA, TTCL vs Detecon* na kadhalika, nashauri ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iwe makini sana na kuiepusha Serikali na shutuma za hapa na pale ambazo zinaiaibisha Serikali.

Mheshimiwa Spika, zoezi la kufanya marekebisho ya sheria mbalimbali linachukua muda mrefu. Naomba Tume iongeze kasi zaidi, mfano sheria ya *workmen compensation.*

Mheshimiwa Spika, Mkoani Singida Mahakama za Mwanzo zimechakaa na Mahakimu hawatoshi na kisha hawana vifaa. Naunga mkono hoja.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nawapa shime Wizara hii ambayo ni mtambuka na yenye kubeba mhimili wa Jamhuri (Mahakama).

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara iwe na kampeni ya ondoa kesi katika mahakama zote ili kupunguza mrundikano wa mahabusu na hasa kesi za mauaji.

Mheshimiwa Spika, kesi zinazowahusu sungusungu ambao ni walinzi wa jadi zitazamwe kwa mtizamo wa kusaidia jeshi hili. Katika mpambano dhidi ya majambazi na wezi wa mifugo inapotokea wananchi wenye hasira kali wameua jambazi, polisi huwakamata na kuwafungulia kesi za mauaji ambazo nazo huchukua muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Katiba inawatambua sungusungu na kuwapa hadhi ya *Police Constable* na wanapoumia kulipwa kwa masharti hayo na kwa kuwa makamanda na viongozi wa sungusungu wanajitolea kufanya kazi nzito ya ulinzi wa raia na mali zao sawa na kama walivyo polisi na kwa kuwa askari hawa hawalipwi posho yoyote ile, nashauri yafuatayo:-

Kwanza Serikali ianze kufanya mchakato wa kuona namna nzuri ya kuwapa posho kidogo iwe motisha katika kazi zao na pili, inapotokea kesi dhidi ya sungusungu, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na polisi watambue nafasi kwa kuheshimu mchango wao.

Mheshimiwa Spika, kutokana na wingi wa mashtaka nchini na ukubwa wa mikoa ambazo zimegaiwa katika Kanda za Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Nashauri yafuatayo:-

(i) Serikali ifungue Ofisi ya Mwanasheria Mkuu katika kila Mkoa.

(ii) Ofisi za Kanda za Mwanasheria Mkuu wa Serikali zisaidie Wilaya zilizo mbali na Makao Makuu ya Kanda.

(iii) Maslahi ya watumishi hawa yaboreshwe ili kusaidia wasiondoke kwenda kufanya uwakili *(advocate)* binafsi.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, napenda kupongeza juhudi za Wizara kuanzisha Wakala wa Usajili na Ufilisi na Udhamini *(Insolvency Trusteeship Agency - RITA).* Pia napenda kupongeza uongozi wa *RITA* kwa kazi yake nzuri kwa kipindi kifupi cha mwaka mmoja toka ilipoanzishwa mwaka 2006. Wananchi wengi sana wanafahamu shughuli za wakala hii na huduma za upatikanaji wa vyeti vya vizazi, vifo, ndoa na talaka imeanza kuboreka. Wakala hii umeundwa chini ya sheria Na.30 ya mwaka 1997 ambayo imeupa mamlaka kujiendesha kibiashara kwa lengo la kutoa huduma bora zaidi kwa umma.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sheria ya ufilisi yaani *official receiver under the Bankrupay Ordinance 1920 (Cap.25)* zinaipa mamlaka wakala huu kuwa mfilisi wa umma na binafsi na kwa kuwa Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma

miongoni mwa majukumu yake ni kufilisi masharika ya umma. Hivyo naomba maelezo ya tofauti ya kazi zinazofanywa na *RITA* na zile za Tume ya Rais ya Kurekebisha Masharika ya Umma *(PSRC)* na kama hakuna tofauti kwa nini shughuli hizo zisifanywe na chombo kimoja?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa miongoni mwa kazi za *RITA* ni kusajili na kutoa hati ya usajili kwa wadhamini wa vyama vya siasa kwa nini basi katika mfumo huu wa vyama vingi uhariri wa daftari la wapiga kura usiwe chini ya wakala wa *RITA* badala ya kuwaachia Tume ya Uchaguzi ambao inaonekana kuwa hawawezi kama ilivyotokea kule Tunduru ambapo watu zaidi ya 11,000 hawakupiga kura. Lakini kwa nini katika Bajeti ya mwaka *RITA* haikutengewa fedha ili kuwezeshwa katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, lakini inaelekea kuwa taasisi mbalimbali zinaunda mamlaka zao wakati zinapobinafsishwa. Kwa mfano *NBC Consolidated Holding* kushughulikia madai na madeni ya *NBC*. Kwa nini basi *RITA* isiwe ni chombo pekee kinachoshughulikia madai na madeni kwa taasisi zote badala ya kutumia fedha nyingi kuanzisha wakala wengi kwa jambo hilo hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mahakama ya Kadhi Mkuu, Serikali inaonesha haijatoa uzito wowote juu ya kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi Mkuu la kushangaza ni kuwa suala hili limo katika Ilani ya CCM wakati wa kuomba kura za Rais 2005 lakini hatujaona utekelezaji Tanzania, kama Serikali haina dini lakini Watanzania dini zao. Wanachodai ni haki kwa mujibu wa dini yao, wale waliokuwa hawahusiki na dini hiyo inayodai Mahakama hawapaswi kuwapangia wengine Watanzania wana haki ya kuabudu na wana haki pia ya kudai mambo yatakayosaidia ibada yao kukamilika. Ahsante.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, naomba michango nitakayoainisha kwenye maandishi nipewe majibu ya kuridhisha. Napenda kujua mambo matatu yanayonisikitisha kwenye moyo wangu pamoja na wananchi wangu wa Mkoa wa Kagera. Hivi ni lini Serikali itaona umuhimu wa majengo ya Mahakama kwani majengo ya Mahakama yamechakaa sana yanatia aibu. Kweli pesa zinazoombwa kweli zinaweza kukarabati majengo Tanzania nzima kwa sababu yote ni chakavu.

Mheshimiwa Spika, pili, wazee wa Mahakama kwa mfano wazee wa baraza je, hawa watu watakumbukwa kwa sababu ndio chanzo cha kula rushwa kwa sababu hizo posho ni ndogo kulingana kwenye kesi zinazorundikana kwenye Mahakama, naomba nipatiwe majibu ni kwa sababu gani watu wanasota ndani ya mahabusu wenginge unakuta makosa yao ni madogo wafungwa au mahabusu basi naomba Waziri hii iwe na mkakati kushirikiana na Serikali, hili suala linaumiza wananchi na wengine wanapoteza haki zao.

Napenda nifafanuliwe jambo moja kwa nini Mahakama zinapenda kuzungusha watu wakati wa kuomba dhamana mtu anazungushwa na mwisho wanakata tamaa na hivyo inasababisha rushwa kukidhiri kwenye Mahakama. Naomba tena nijue Kanda ya Ziwa Majaji nafikiri Majaji wana matatizo, kweli Jaji mmoja anahama hama mara Biharamulo, mara Mwanza, mara Mara, mara Musoma, kwa hapo kesi zitaisha lini?

Naomba nipatiwe majibu pamoja na kesi za uchunguzi sioni umuhimu wa kushtaki kwa sababu unapigwa, naona haina haja ya kwenda mahakamani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wizara hii ninayo mengi ila naomba majibu kwanza kwa haya niliyoyaainisha nipatiwe majibu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia tukiwa wazima na salama.

Mheshimiwa Spika, napenda niongelee kuhusu suala la uwakala wa usajili ufilisi na udhamini *(RITA)*.

Mheshimiwa Spika, wakala huu umeanza kufanya kazi vizuri sana mara tu baada ya kuanzishwa. Hivyo basi tunaiomba Serikali isaidie wakala huu kifedha na kiuchumi kwa vile kuna Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma ambayo kazi mojawapo ni kufilisi Mashirika ya Umma, naomba kupata ufafanuzi wa tofauti juu ya shughuli za ufilisi zinazofanywa na wakala *(RITA)* na zile zinazofanywa na Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma yaani *PSRC* kuwa hakuna tofauti kwa nini kazi hizo zisifanywe na chombo kimoja?

Mheshimiwa Spika, kwa nini *PSRC* isifanye zaidi kazi katika kuyaendeleza na kuyawezesha badala ya kazi ya ufilisi ambapo kulingana na sheria ufilisi, inaipa Mamlaka *(RITA)* kushughulikia ufilisi?

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kuomba maelezo kwa nini Serikali kazi kama vile kuandika vitambulisho vya uraia wasipewe wakala humu na badala yake Serikali inatafuta kampuni nyingine ili iweze kufanya vitambulisho vya uraia wa Tanzania?

Mheshimiwa Spika, suala hili nimeona kuandika badala ya kuona nisingepata kulizungumza hivyo naomba maelezo ili tusikutane kwenye vifungu wakati wa kupitisha Bajeti hii. Ahsante sana.

**MHE. BENSON N. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

Pili, naomba niwapongeze Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri mnayofanya katika kuhakikisha utawala wa sheria unafuatwa katika nchi yetu. Mimi binafsi nafarijika sana na utendaji kazi wa Wizara hii kwani mambo mengi niliyofuatilia katika Wizara hii yamepatiwa ufumbuzi. Pongezi sana. Pamoja na hayo yote naomba nipatiwe majibu katika matatizo yafuatayo:-

Kwanza ni kuhusu posho za wazee wa mabaraza. Nimefuatilia sana suala hili la Wizara la kudaiwa na wazee wa baraza hasa katika Jimbo langu la Mbeya Mjini, wapo

wazee wa baraza wa Mahakama za Mwanzo za Mwanjelwa na Iyunga ambao mpaka sasa wanadai Wizara kwa kesi mbalimbali walizosimamia na kuziamua. Ni lini wazee watalipwa fedha yao yote, kama nilivyoahidiwa nilipouliza swali la posho hizo mwaka 2006/2007?

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie upya kiwango cha malipo ya kesi inayosimamiwa na wazee wa mabaraza. Kiasi cha sasa ni kidogo sana na hakikidhi hali halisi ya maisha ya sasa. Naomba *review* ya viwango ifanyike. Pia naomba nipatiwe maelezo ya kina juu ya malipo ya Mahakimu wanaopangiwa kutembelea vituo/Mahakama zilizo mbali na vituo vyao vya kazi. Yapo malalamiko kuwa Mahakimu wengi wanaopangiwa kutembelea vituo vya nje wanacheleweshewa malipo yao na Serikali inalimbikiza madeni kiasi cha Mahakimu kuwa ombaomba na kukopa nauli na malazi, huko wanakokwenda, hali hii itatishia upatikanaji au utoaji haki kwa Mahakimu hawa ni rahisi sana hakimu kushawishika kupokea hongo/rushwa ili kukidhi mahitaji muhimu ambayo yalipaswa kutolewa na mwajiri.

Mheshimiwa Spika, mfano halisi zaidi ya Mahakimu 10 au 11 bado mpaka sasa wanamdai Hakimu Mfawidhi wa Wilaya ya Dodoma. Ni lini Serikali itawalipa Mahakimu hawa? Nitapenda kupewa maelezo thabiti wakati wa vifungu.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kutoa rambirambi zangu za dhati kabisa kwa familia ya Marehemu wote waliopoteza maisha yao kwa sababu mbalimbali zikiwepo ajali za angani, barabarani na kadhalika. Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi, *Amin.*

Lakini pia nitoe rambirambi zangu binafsi kama Mbunge kwa familia ya Marehemu Amina Chifupa Mpakanjia, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Vijana Taifa, Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi, *Amin.*

Naomba sasa nimpongeze Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Naibu Waziri wake kwa hotuba nzuri waliyoileta leo tarehe 30 Julai, 2007. Pia nawapongeza sana wataalamu wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya kwa kutekeleza falsafa ya ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na suala la ubakaji kwa watoto walio chini ya umri wa miaka 10. Naipongeza sana Serikali kwa kuweka sheria ya kwamba anayepatikana na hatia hiyo basi anahukumiwa miaka 30. Lakini sheria hii wala haiwastui wananchi bado wabakaji wanaendelea kwa kuwa kuna hujuma kwenye vyombo husika.

Mheshimiwa Spika, ikiwa kuna baba mzazi aliyembaka binyi yake mwenye miaka tisa darasa la nne katika shule ya msingi Mirerani. Baada ya tendo hilo, mtoto alikwenda mwenyewe kituo cha polisi na kujieleza. Polisi walichukua hatua ya kwenda kumkamata na mtoto kupelekwa hospitali na kukutwa ameharibika vibaya sana nyumba na mbele. Baba wa mtoto yule aliwekwa ndani kwa muda mfupi tu na baadaye alitoka. Je, sheria ipi iliyomwezesha baba huyo aliyebaka mtoto wake mwenyewe kutokufungwa miaka 30? Huo ni uonevu mkubwa. Yule mtoto anatoa harufu mbaya sana pamoja na jitihada zote za matibabu. Je, haki ya huyo mtoto ni ipi?

Naomba kuwepo na Mahakama ya Watoto ili watoto nao wapate mawakili wa kuwatetea kwa kuwa sasa hivi unyanyasaji huo ni mwingi sana hasa Wilaya yetu kwa nini watu wengine huona kuwa mtoto akibakwa ni haki yake, wanasema huyu si mwanamke tu? Pia wengine wakimzomea mtoto aliyebakwa na baba yake kuwa utakula, utavaa nini, utasomaje ikiwa utamfunga baba yako? Hivyo jamii haijali, nashauri kuwepo na mahakama ya watoto. Pia jamii ielimishwe kuhusu hili.

Mheshimiwa Spika, naomba tuonewe huruma, tupate mahakama Mirerani yenye hadhi. Simanjiro kuna shida za Mahakama, mahakama ni chache. Ikiwa mtu atakuwa na kesi inayomtaka apelekwe *RNs Court* – Manyara, Babati, inamgharimu sana. Hivyo wengi wao huacha kabisa kufuatilia kesi zao. Naomba tujengewe mahakama pale Mirerani, eneo tunalo, matofali tunayo. Tunaomba utamke ni lini utafika Mirerani uone jinsi Mahakimu wanavyopata shida mahali wanapoishi. Wanaishi pamoja kwenye nyumba za kupanga tena chumba kimoja. Tupate mahakama yenye hadhi Mirerani, wananchi wapo tayari kusaidiana kutoa fedha na Serikali nayo itusaidie ili tuweze kupata mahakama yenye hadhi. Mirerani tupo tayari kuchangisha.

Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza swali la ufahamu, je, ikiwa hakuan sheria yoyote inayoruhusu madini ya vito kuchimbwa na wageni; na kwa kuwa eneo la Mirerani la *Tanzanite* lilikuwa likimilikiwa na Kampuni ya wazawa ambayo ni *Tanganyika Gemstone Industries* kwa ubia na kampuni ya Uingereza ya *Graphtan,* je, ni sheria ipi ilitumika baada ya kampuni ya *TGI* kujiondoa na kumuachia *Graphtan? Graphtan* akampa *Samax* na *Samax* akampa *Afgem* na *Afgem* akampa Mirerani na Mirerani ikabadiliasha jina na kujiita *Tanzania One,* haya makampuni yote ni ya wageni, hakuna mzawa hata mmoja. Naomba kujua sheria inayowapa uhuru wa namna hiyo na wazawa wanabaki kutizama kwa macho maliasili zao zikimalizika, je, Wizara ya Katiba na Sheria inasemaje?

Mheshimiwa Spika, kuhusu mtiririko huu wa makampuni haya ya madini ya vito hasa kwenye *Tanzanite* najua kabisa suala hili linahusu Wizara ya Nishati na Madini, lakini ninapouliza sijibiwi ipasavyo. Mimi naomba nijue sheria iliyotumika kuleta mtiririko wa makampuni hayo yote kuja kuchezea maliasili yetu. Kwa nini Wizara ya Katiba na Sheria isishitukie mchezo huu unaokiuka sheria za nchi na kuleta mabadiliko kama Wizara ya Maliasili na Utalii?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, kwa kumaliza utata uliokuwa unajitokeza kwa jina la Wizara yake, hivyo kutimiza wajibu wake ipasavyo, kwa hivyo nampongeza.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Jaji Augustino Ramadhani, kwa kuteuliwa na Rais kuwa Jaji Mkuu, kwa kupitia Bunge lako Tukufu nampongeza sana na ninamwombea afya njema, hekima na busara toka kwa Mwenyezi Mungu ili atekeleze vema na kwa haki kazi yake vema. Bila kusahau naunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia zaidi katika maswala ya maisha ya kila siku ya jamii ili kila mtu apate haki yake hasa ya mwanamke na mtoto ili pawepo na maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, sheria ya ndoa ya mwaka 1971 inasema mtu akikaa na mke ama mume kwa muda wa miaka miwili, basi hao tayari wako kwenye ndoa nikiwa na maana kwamba ni wanandoa tayari.

Mheshimiwa Spika, imesaidia sana kwa vijana au watu wazima wanaopendana wenye dini mbalimbali mfano mkristo na muislamu kuoana. Hii imesaidia sana familia nyingi kuheshimiana bila kuwa na vita vya kidini nchini kwani tuko ndugu katika familia zetu.

Mheshimiwa Spika, lakini sheria hii imeongezea kwamba sio lazima mkiishi miaka miwili ndiyo ndoa, lazima mfanye tafrija angalau kidogo mjitambulishe kwa jamii kuwa mke na mume ndiyo jamii iwatambue.

Mheshimiwa Spika, kwa misingi hiyo hiyo, ikiwa wanandoa wametengana miaka miwili au zaidi sheria haitambui kwamba hawakutani kitendo la ndoa, hivyo wahesabike wameachana. Kwa misingi hiyo naomba sheria hii irekebishwe na iletwe mapema Bungeni ili wanandoa kama wanaishi pamoja na kuhudumiwa ipasavyo kwa miaka miwili wanatambulika, sasa kulikoni, mbona wanavyotengana na hawakutani kindoa ama kimatunzo sheria iko kimya?

Naomba kipengele hicho kiwekwe wazi ili watu wawe huru na isiwe siku ya siku mmoja anafariki kisha anakuja kudai haki kama mke na mume na watu wanamsikiliza hali si lolote si chochote kwa miaka nenda rudi, naomba sana ushauri wangu uzingatiwe.

Mheshimiwa Spika, Sheria hiyo hiyo ya mwaka 1971 kuhusu matunzo ya mtoto ni shilingi 100/= kwa mwezi.Shilingi 100/= ni ndogo mno kwa sasa. Wakati ule shilingi 100/= ilikuwa ni zaidi ya 50% au karibu ya 50%, kwani mishahara yao ilikuwa ni shilingi za Kitanzania 219/= *form iv* walioshinda mitihani na 290/= kwa *form iv* walioshinda mitihani. Kwa hiyo, 100/= ilikuwa kubwa lakini sasa si mali kitu. Shilingi 100/= huwezi kununua hata mlo mmoja wa mama ama baba. Hivyo ni wakati muafaka kubadilisha matunzo ya mtoto kulingana na wakati.

Mheshimiwa Spika, watoto hawa sio watoto wa wafanyakazi bali wapo watoto wa wakulima na wanfanya biashara, kwa msingi hiyo sheria hii itazame pia kote ili watoto wote wa wakulima na kadhalika wapate matunzo, kwa wakulima watoe matunzo wakati wanapovuna na kuuza.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kuhusu mirathi kwa mama na mtoto (watoto) yaani yatima, watoto hawa yatima wako aina mbili, hii ndio hali halisi kuwa yatima wa mama aliye kwenye ndoa wakati mume anafariki, lakini kuna yatima wa watoto aidha, mama alipoolewa aliwakuta na pengine ndilo sharti alilopewa kwamba ataolewa kama atawakubali watoto hao ambao wamezaliwa kabla ya yule bwana na anawatambua na kuwatunza.

Msheshimiwa Spika, watoto wamezaliwa na mama mwingine na baadaye wanakombolewa kimila na kuchukuliwa na baba na kuletwa hapo ndani na kuishi humo humo ndani, watoto wa yule mama *current* na wale aidha, aliwakuta ama wameletwa baba akiwa hai, sasa vipi watoto hawa yatima baba anapofariki na hasa baba akiwa tajiri yatima hawapati haki zao?

Mheshimiwa Spika, naomba sheria hii iletwe Bungeni ili tuipitishe ipasavyo, hapa haki inapaswa iwe ni kwa wote yaani mama na watoto. Hawa yatima nawazungumzia wake waliotambulika na kukombolewa, sisemi wale holela ambao hawakukombolewa.

Mheshimiwa Spika, naomba wapatiwe mikopo ya gari ndogo au pikipiki ili kuwasaidia kufika mahakamani kwa wakati

Naomba ielezwe wazi kazi za *RITA* na iwepe meno ili isaidie au ifanye kazi ipasavyo katika kutoa haki za mama na watoto (yatima) hasa kwa akina baba matajiri. Naomba suala hili liangaliwe ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono asilimia mia moja.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA**: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Kwanza napenda kuchangia katika maeneo ya mabaraza ya ardhi. Halmashauri nyingi zilichelewa kuanzisha, mabaraza ya ardhi ya kata na vijiji yameanzishwa bila semina. Hata yaliyofanyiwa hazijawasaidia vya kutosha. Malipo kwa ajili ya shughuli zao hayako wazi, baadhi ya mabaraza yamejiingiza kenye rushwa. Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya ni vyema yasogezwe Wilayani, *Geita Case*, Baraza liko Mwanza Mjini baada ya Geita, ni usumbufu sana.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri aeleze wazi wazi taratibu za kufuata kuvunja mabaraza ya ardhi ya kata, kijijini yanapokuwa kero mbaya kwa wananchi. Kuna tatizo katika kata ya Nyangw'ale, Wilaya ya Geita, kuna malalamiko na tuhuma za rushwa.

Mheshimiwa Spika, pili, Mahakama za Mwanzo na Wilaya ambapo wanaendelea kusikiliza kesi/ migogoro ya ardhi kinyume cha sheria kwa ajili ya manufaa fulani (rushwa). Naomba Serikali itamke kwa sauti kubwa marufuku ya Mahakama hizo kufanya sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, naomba Mahakimu wa Wilaya wafanyiwe ukaguzi wa Mahakama za Mwanzo mara kwa mara. Kitu hiki hakifanyiki kwa kuzingatia ukubwa wa vitendea kazi, kwa sababu hiyo kuna mahakimu wa mwanzo ambao wamekuwa Mungu watu kwa kutumia uhuru wa mahakama na kutokaguliwa.

Mheshimiwa Spika, naomba maeneo yenye watu wengi na shughuli nyingi za kijamii na kiuchumi, mfano, migodi ya madini, uvuvi, mipakani, Wilaya hizo zipewe usafiri na vitendea kazi kwa mfano Wilaya ya Geita.

Mheshimiwa Spika, jambo la nne ni katika kushughulikia mgogoro wa mgomo wa mahabusu wa Keko na Segerea mwaka jana, zipo taarifa kuwa ipo *circular* ambayo imepelekwa ofisi za Jaji Mkuu, Mwanaseheria Mkuu, Jeshi la Polisi inayoelekeza kuwa upelelezi wa kesi ufanyike ndani ya siku 60 na kama hakuna ushahidi basi kesi husika zifutwe. Waraka huu usambazwe hadi ofisi za *RCs, DCs, DEDs, OCDs* na watu walio chini yao na isifanywe siri kama hivi sasa.

**SPIKA:** Asante sana, sasa namwita Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kuchangia kwa kipindi cha dakika 15. Mwanasheria Mkuu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote ni wajibu kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutupatia sisi sote uzima na kuweza kuwa hapa leo. Aidha, nakushukuru kwa kunipatia fursa hii ili niweze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, aliyoitoa Bungeni hapa leo asubuhi na ambayo ninatanguliza kusema kuwa, naiunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea kutoa mchango wangu, napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kutoa pole na rambirambi kwa familia ya Marehemu Amina Chifupa Mpakanjia, aliyekuwa Mbunge mwenzetu kupitia Viti Maalum CCM, ambaye ametutangulia mbele ya haki.

Aidha, natoa pole kwa familia za Watanzania wenzetu waliotutoka kwa majanga na ajali mbalimbali zilizotokea. Mwenyezi Mungu, azilaze mahali pema peponi roho za marehemu wote, *amin.*

Mheshimiwa Spika, pia napenda kutumia fursa hii kumtakia maisha mema ya ustaafu, aliyekuwa Jaji Mkuu, Mheshimiwa Barbanas Albert Samatta, aliyetumikia vyema Taifa kwa kipindi kirefu. *(Makofi)*

Pia nampongeza Mheshimiwa Agustino Ramadhani, aliyeteuliwa hivi karibuni na Mheshimiwa Rais, kuchukua nafasi yake. Namwombea Mwenyezi Mungu, amjalie afya njema, hekima na busara katika kuutumikia wadhifa huo, kwa kuongoza moja ya mihimili mikuu ya dola.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa nichangie kwa kujielekeza katika maeneo mbalimbali, yanayohusu sheria yalizozungumziwa na Waheshimiwa Wabunge, nikianzia na lile la Kambi la Upinzani kuhusu Katiba mpya.

Mheshimiwa Spika, mjadala wa hoja za Katiba mpya, hauna budi kuangaliwa katika misingi na tafsiri ya maana ya neno hili Katiba. Katiba imekuwa ikitafsiriwa na kuelezwa kwa lugha na maelezo mbalimbali tofauti, kutegemea malengo ya tafsiri yenyewe. Watu wengi wa kawaida, wamekuwa wakitafsiri Katiba kuwa ni mkataba kati

ya watawala na watawaliwa, yaani *a social pact.* Tafsiri ambayo napenda niitumie ni ile inayozingatia maudhui na kuipa Katiba, maana pana kabisa kuwa, ramani ya mahusiano mbalimbali baina ya vyombo vya mamlaka kuu ya nchi kwa upande mmoja na uhusiano kati ya mamlaka hiyo na wananchi wake kwa upande mwingine. Tafsiri hii ndiyo huifanya Katiba kuwa sheria mama. Kwa msingi huo, zipo aina kuu mbili za Katiba; ambazo ni Katiba zilizoandikwa na Katiba ambazo hazijaandikwa. Kwa upande wetu wa Tanzania Katiba yetu ni ile ya kuandikwa.

Mheshimiwa Spika, Katiba kama Sheria mama, inaweka msingi wa sheria za nchi. Sheria za nchi zinapata uhalali wake kutokana na Katiba na kupoteza uhalali wake kwa kiwango ambacho kinapingana na Katiba na kukiuka masharti. Katiba pia hutumika kama kioo cha Taifa na kutoa taswira kamili ya sura ya nchi kijiografia na sura ya dola na vyombo vyake, hutoa sura ya kijiografia inayotambulisha maeneo ya nchi na watu wake. Sura hii inapatikana kwa kujumuisha Katiba na mfumo mzima wa sheria, zinazotambulisha maeneo ya nchi. Sura ya dola inapatikana kwa kuangalia vyombo mbalimbali vya dola na mgawanyo wa madaraka yake. Katiba inaainisha sura ya Serikali kama ya Kifalme, ya Kirais au ya Kibunge. Katiba pia huainisha utaratibu wa kuingia katika mahusiano ya kimataifa, kwa njia ya mikataba, miliki ya utajiri na uwezo wa watu mbalimbali kuhodhi mali na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Katiba yetu ni yenye kuzingatia misingi na nguzo zote za kidemokrasia; nguzo hizo ni pamoja na mgawanywo wa madaraka baina ya vyombo vikuu vya dola, baina ya Serikali, Bunge na Mahakama. Utaratibu unaowezesha kukosoana baina ya vyombo hivyo, yaani *effective checks and balances*. Uhuru wa Mahakama na mamlaka ya Bunge kutunga sheria na Serikali inayowajibika kwa Katiba na Bunge na pia kuwa na uchaguzi katika vipindi ambavyo vimepangwa Kikatiba. Katiba yetu pia inazingatia suala la hifadhi ya haki za binadamu na kuzingatia utawala wa Kikatiba na inatoa sura ya nchi yenye ustaarabu wa Kikatiba. Mwaka 1998, Serikali iliandaa Waraka wa kupata maoni ya wananchi kuhusu Katiba. Waraka uliainisha maeneo ya msingi katika nyanja hizo nilizozielezea. Kutokana na kazi ya Tume iliyoundwa kukusanya maoni, naweza kusema kuwa, Katiba inakubalika na wananchi kutokana na utaratibu, mahitaji na mazingira mahususi ya jamii yetu.

Mheshimiwa Spika, nchi zenye Katiba zilizoandikwa, zinazo utaratibu wa kuzingatia mazingira mapya katika jamii; iwe kutunga au kufanya mabadiliko na mazingira yaliyoisababisha. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imewekewa utaratibu maalum ndani yake wa jinsi ya kufanya mabadiliko ya Kikatiba ili kukidhi mahitaji ya Wananchi wa Tanzania pindi umuhimu unapotokea. *(Makofi)*

Aidha, Katiba ya nchi hii imekuwa ikitungwa kulingana na umuhimu wa matukio mbalimbali, ambayo yameonekana na umuhimu wa kipekee katika taifa letu. La msingi ni kwamba, Katiba mpya huandikwa pale panapokuwa na mabadiliko yanayoathiri *sovereignty* katika jamii. Historia ya Katiba ya nchi yetu imezingatia ukweli huo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 1961, Katiba ya Uhuru ilitungwa ili kuhamisha sehemu ya madaraka ya Serikali kutoka mamlaka ya ukoloni kwenda kwa wananchi.

Mwaka 1962 Katiba ilitungwa na Bunge la Tanganyika, kwa ajili ya kukamilisha uhamishaji wa madaraka kutoka mamlaka ya kikoloni uliongozwa na Malkia wa Uingereza kwenda kwa Serikali ya Wananchi wa Tanganyika, ikiongozwa na Rais ambaye ni kiongozi wa Serikali, Mkuu wa nchi na Amiri Jeshi Mkuu wa Nchi.

Mwaka 1977 Katiba mpya ilitungwa kwa ajili ya kukamilisha utaratibu wa mapatano ya Muungano wa mwaka 1964. Katiba hii ilitungwa kwa madhumuni ya kuunganisha maeneo mawili ya mamlaka, yaani *merger of sovereignty* kati ya Serikali ya Jamhuri ya Tanganyika na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ni wazi kwamba, Katiba mpya imeandikwa pale tu ambapo mpangilio wa madaraka ya *sovereignty* ilipobadilika. Hali hii ilitokea wakati Tanganyika ilipopata Uhuru, Tanganyika ilipopata Jamhuri na Jamhuri ya Tanganyika ilipoungana na Jamhuri ya watu wa Zanzibar.

Kwa sasa hakuna tukio lolote kubwa la kufanana na matukio hayo, ambalo litahitaji Katiba kutungwa. Narudia tena, kwa sasa hakuna tukio lolote kubwa la kufafana na matukio hayo ambalo litahitaji Katiba kutungwa. *(Makofi)*

Serikali inatambua kuwa Katiba ni hai kama zilivyo Katiba za nchi nyingine na hufanyiwa mabadiliko ikihitajika ili kukidhi mazingira ya wakati unaohusika.

Mheshimiwa Spika, ipo hoja iliyotolewa kuhusu Mahakama Maalum ya Katiba. Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kupitia ibara ya 125, imeunda Mahakama Maalum ya Katiba. Kazi pekee ya Mahakama hii ni kusikiliza shauri lililoletwa mbele yake, kutoa uamuzi wa usuluhishi juu ya suala lolote linalohusika na tafsiri ya Katiba iwapo tafsiri hiyo au utekelezaji wake unabishaniwa kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja kwamba mambo mengi ya msingi kama vile vita dhidi ya rushwa, umiliki uchumi na mwelekeo wa sera za nchi, hayakufafanuliwa ndani ya Katiba hii sio kweli, kwa hili, napenda kutoa ufafanuzi ufuatao:-

- Katiba ni sheria mama ambayo huweka misingi ya kufuatwa. Misingi inayowekwa na Katiba hutekelezwa kwa kutungiwa sera au sheria.

- Katika kutekeleza misingi ya Katiba, Bunge lako Tukufu hupitisha sheria mbalimbali. Hivi karibuni, Bunge lako limepitisha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, ikiwa ni utekelezaji wa masharti ya Ibara ya 9 ya Katiba. Sanjari na hilo, Sheria ya Ardhi ya 1999, inaainisha utaratibu wa kumiliki ardhi, haki ya mmiliki na taratibu za upitikanaji wa ardhi kwa wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja kwamba, Katiba haina kifungu cha mamlaka ya kulinda wananchi wasionewe na Serikali, hili pia siyo kweli. Katiba kupitia Ibara ya 13(3), inaeleza kuwa, haki za raia, wajibu na maslahi ya kila mtu na jumuiya ya watu yatalindwa na kuamuliwa na Mahakama na vyombo vinginevyo vya mamlaka ya nchi, vilivyoweka na sheria au kwa mujibu wa sheria. Kwa mantiki hiyo, Katiba inalinda haki za wananchi dhidi ya uonevu unaoweza kufanywa ama na mtu au chombo chochote ama cha binafsi au cha Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja kwamba, Katiba yetu haina suala la umiliki wa ardhi, napenda kusema yafuatayo:-

- Ibara 24 ya Katiba inatoa haki ya kumiliki mali na haki ya hifadhi ya mali yake iliyonayo kwa mujibu wa sheria. Ardhi ni mali hivyo, ulinzi wake unatolewa kupitia Ibara hiyo ya 24.

- Kwa kuwa ardhi ni mali na Katiba inatoa haki ya kumiliki, Bunge lako Tukufu limetunga sheria mbalimbali, ambazo zinaweka utaratibu wa kupata ardhi, kuuza au kutwaa ardhi. Baadhi ya sheria hizo ni Sheria ya Ardhi ya Mwaka 1999 na Sheria ya utoaji wa Ardhi.

- Kwa mujibu wa sheria kila mwananchi anayemiliki ardhi kihalali, anastahili kulipwa fidia pale ardhi inapotwaliwa na mamlaka nyingine. Lipo jambo moja ambalo Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi amezungumzia, juu ya Kamati zile za Nyalali na ile ya Kisanga, zilisema kwamba tuwe na Katiba na Mpya.

Mheshimiwa Spika, tutakumbuka kwamba, kitu ambacho kiliwafanya Kamati ile ipendekeze kwamba, kuwe na Katibua Mpya ni kwamba walitoa hoja ya kuwa na muundo mpya wa Serikali, yaani shirikisho. Sasa ni kutokana na pendekezo hilo ndiyo sababu wakasema kwamba, kuwe na Katiba lakini jambo hilo lilikataliwa, kwa hiyo, palikuwa hakuna haja ya kuwa na Katiba mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa haraka nitapitia hoja ambazo zilitolewa na Waheshimiwa Wabunge, walipokuwa wanachangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria. Tabia ya Askari kuwakamata tena watuhumiwa mara wanapoachiwa huru na mahakama, hii imetolewa na Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa mshtakiwa kuachiwa na mahakama chini ya kifungu cha 225 cha sheria ya mwendeleo wa makosa ya jinai, sura ya 20 ni wakisheria. Kuna mshtakiwa aliachiwa na mahakama kutokana na kutokamilika kwa ushahidi au upande wa mashtaka kushindwa kuendesha mashtaka yake. Mshtakiwa anaweza kukamatwa tena kama ushahidi utapatikana wa kuweza kuunganisha na makosa ambayo ameshtakiwa nayo.

Vikwazo vinavyofanywa taasisi za kitaalamu kuzorota kwa mfano, sheria za mawakili kutofanyiwa marekebisho na badala yake kuwekwa kwenye mashelfu.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kufuta sheria ya mawakili iliyopo, umefanyiwa kazi na sasa Muswada wa Sheria mpya unaandaliwa ili uletwe Bungeni. Ibara ya 145 na 146 zinazoanzisha Serikali za Mitaa, hazielezi uwezo wa kuziondoa au kumwondoa Mjumbe wa Serikali za Mitaa anapokosa, hivyo kusababisha Viongozi wa Serikali kuvunja Katiba. Ushauri huu tunaupokea lakini Katiba ya Jamhuri ya Muungano, imeweka msingi ya uwepo wa Serikali za Mitaa kwa mujibu wa Katiba. Suala la utaratibu wa namna ya kuwaondoa Wajumbe kutoka katika Serikali za Mitaa pale wanapokosea, umeelezwa katika Sheria za Serikali za Mitaa, pamoja na Kanuni zake.

Kuwepo makosa mengi ya uchapishaji katika Sheria za Nchi za mwaka 2002, kwa mfano, Sheria za Magereza Sura ya 58. Kupatikana kwa Toleo la Sheria zilizojadidiwa hadi mwaka 2002, kwa kweli ni mafanikio makubwa sana, imetuwezesha sasa tuwe na sheria zote za nchi hadi mwaka 2002, zinazopatikana kwa urahisi. Hata hivyo, ni kweli kuwa yapo matatizo madogo ya kiuchapishaji, ambayo yatawasilishwa katika siku za usoni. Kusudio letu ni kutoa toleo jingine kabla ya miaka kumi, yeyote aliyetugundua au atakayegundua makosa ya uchapishaji, ayawasilishe kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Ni kweli kumekuwepo makosa mengine ya uchapishaji katika Sheria za Toleo la mwaka 2002. Kwa kawaida huwa tunatoa matoleo ya sheria zote zilizopitiwa upya kila baada ya miaka kumi. Lakini kutokana na matatizo hayo ya uchapishaji yaliyoonekana, Wizara imeanza mchakato wa kuzipitia upya sheria zote ili tutoe toleo jipya katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Umuhimu wa kuzipanga katika juzu sura ya sheria ambazo hazipo kwenye juzu, hususan sura zilizotungwa kuanzia tarehe 1 Agosti, 2002. Kuhusu umuhimu wa kuzipanga katika juzu za sura (*volume* na *chapters*), sheria ambazo haziko kwenye juzu na sura hususan zile ambazo zimetungwa kuanzia tarehe 1 Agosti, 2002. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara tayari imeshazipitia sheria ambazo zimetungwa baada ya tarehe 1 Agosti, 2002, isipokuwa zile zilizotungwa na Bunge mwezi Aprili na zimetangazwa rasmi katika Gazeti la Serikali, Toleo la mwezi - tangazo Na. 121 la mwaka 2007, chini ya sheria ya uratibu wa sheria sura ya nne, inayompa uwezo Mwandishi Mkuu wa Serikali kufanya hivyo chini ya kifungu cha nane, kifungu kidogo cha nne.

Serikali kutokutekelza mapendekezo ya Tume kuhusiana na Sheria za mirathi na kanuni za mwenendo wa mashauri ya madai.

Mheshimiwa Spika, Tume inapokamilika ripoti zake huwasilishwa kwa Waziri wa Katiba na Sheria…

**SPIKA:** Endelea Mwanasheria Mkuu, nitapunguza dakika kama tatu kwa Mheshimiwa Waziri, ili umalize vizuri.

**MWANASHERIA MKUU:** Mheshimiwa Spika, asante. Baada ya kutoa mchango huo, naomba kuendelea kuiunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri, mia kwa mia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Asante sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Waheshimiwa Wabunge, sasa ni zamu ya Mheshimiwa Naibu Waziri na wamekubaliana na Mheshimiwa Waziri kwamba, yeye ni dakika 20 ili Waziri amalize kujibu hoja kwa dakika 40. Kwa hiyo Mheshimiwa Naibu Waziri, una dakika zako 20.

**NAIBU WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwanza niruhusu nikushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wetu, kwa kazi nzuri ya kuongoza Bunge letu.

Kutokana na uhaba wa muda, naomba niseme kuwa, naungana na Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, kwa pongezi na rambirambi zote alizozitoa leo asubuhi. Nachukua fursa hii, kumshukuru Waziri, Mheshimiwa Dr. Mary M. Nagu, kwa uongozi wake madhubuti na ushirikiano mkubwa anaonipa. Namshukuru mke wangu mpenzi, Profesa Amandina Lihamba, ambaye kutokana na majukumu yake mengi na mazito, hakuweza kufika hapa leo hii kunipa nguvu. Najua ananiunga mkono pale alipo. Namshukuru kwa uvumilivu wake mkubwa. Kwa hakika tangu nianze kazi hii ya siasa, Amandina ameiongoza nyumba yangu vizuri sana wakati sipo. Namshukuru sana. *(Makofi)*

Mwisho, katika shukrani, nawashukuru sana wapiga kura na Wananchi wa Nachingwea, Wananchi na Viongozi wote wa Mkoa wa Lindi, kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM. Nawaomba waendelee kunipa ushirikiano huo mzuri na wazidi kunivumilia pale ambapo hawanioni mara nyingi Jimboni na Mkoani kama vile ambavyo wote tungependa iwe. Nawaahidi kuwa kwa pamoja tutaitekeleza Ilani ya Uchaguzi na kujiletea maendeleo yetu wenyewe.

Naomba na mimi nichangie hoja iliyopo mbele yetu. Lakini nianze kwa kutamka kuwa, naiunga mkono hoja hii kama ilivyoletwa. Katika mchango wangu, nitatumia muda mwingi, kujibu hoja nyingi ambazo zimeletwa kwetu na Waheshimiwa Wabunge.

Nitaanza na hoja iliyoletwa kwetu na Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini, yeye alizungumzia kuhusu Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na alisema Tume hii haina meno ipo tu na anataka maamuzi yake sasa yapewe mkazo kama vile maamuzi ya Mahakama.

Tume ya Haki ya Binadamu za Utawala Bora imeanzishwa kama Tume nyingine Duniani, kwa kutumia Kanuni za Paris, yaani *Paris Principles* na zina majukumu ya kueneza kulinda, kutetea na kuhifadhi haki za binadamu na misingi ya Utawala Bora. Kwa hiyo basi, Tume si Mahakama Tume hii imeundwa kwa minajili ya kuisaidia Serikali na Sekta Binafsi kuweza kutambua na kurekebisha kasoro kwa madhumuni ya kulinda Haki za Binadamu na misingi ya Utawala Bora. Kimsingi Sheria ya Tume imetoa mamlaka kamili kwa Tume kuweza kufanya kazi na kutoa maamuzi yake kwa uhuru. Katika kipindi cha miaka sita iliyopita, Tume iliweza kufanya uchunguzi na kutoa mapendekezo yake kwa mamlaka zinazolalamikiwa. Idadi kubwa ya mapendekezo yake yalitelekezwa, kwa mapendekezo ambayo hayakutekelezwa, sheria inatoa nafasi kwa Tume kwenda Mahakamani.

Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mbunge wa Micheweni, naye alizungumzia kuhusu Tume, akasema kwamba Tume haina nguvu hilo nimelijibu alisema ipewe nguvu kisheria, nalo nimelijibu, lakini pia alitoa pongezi kwamba sasa tumefungua Ofisi Zanzibar na hilo amelipendelea, namshukuru kwa pongezi zake. Tumefungua tena ofisi huko Lindi na Mtwara na tunaendelea kufungua ofisi kwa kadri uwezo wa pesa utakavyoturuhusu.

Mheshimiwa Ania Saidi Chaurembo, alizungumzia kuhusu udhalilishaji wa wafungwa kwa kupewa adhabu ya kuwa uchi. Suala la kupewa adhabu wafungwa kukaa uchi kama ilivyoripotiwa katika Gereza la Nipashe la tarehe 30 Mwezi wa Saba mwaka huu, katika Gereza la Isanga. Tume italifuatilia na kulifanyia uchunguzi, kwani adhabu za aina hiyo ni uvunjifu wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora.

Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, naye alizungumzia kuhusu Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na akaipa pongezi kwa kufungua ofisi Zanzibar.

Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, aliendelea katika michango yake alizungumzia akitaka Serikali igeuze Tume hii iwe kama Mahakama. Tunasema hiyo haitawezekana kwa kweli Tume ni Tume na ushauri wake unatekelezwa na Serikali kama ambavyo tumekuwa tukifanya siku zote. Mheshimiwa Mbunge, pia alizungumzia mengi kuhusu Tume hii, anasema sheria pia zinakwama. Alizungumzia kuhusu Tume ya Kurekebisha Sheria, akasema Tume inatoa taarifa, Sheria zinakwama haziletwi Bungeni, sasa tunasema ni kweli zile taarifa za Tume ya Kurekebisha Sheria zinaletwa katika Wizara yangu na zinashughulikiwa na kwa utaratibu tofauti haziletwi kama zilivyo Bungeni, lakini nataka kumhakikishia kwamba, Serikali imekuwa ikirekebisha sheria na kuchukua hatua mbalimbali katika kutekeleza mapendekezo ya Tume na mifano ni mingi tu, ila Sheria za Ndoa, Sheria ya Mirathi na Sheria ya Watoto hizi kama nilivyokwishajibu hapa Bungeni katika swali moja nililoulizwa zinaletwa katika Bunge lako Tukufu katika kipindi cha Bunge la mwezi wa Novemba.

Mheshimiwa Phares K. Kabuye, leo alikuwa na mengi ya kusema, moja alilolisema ni kwamba, Mahakama ya Wilaya ya Biharamulo ipo chini ya gofu la Hospitali ya Wilaya iliyojengwa na wakoloni miaka mia iliyopitwa na kwamba, hakuna mahakimu. Tatizo hilo tunalifahamu na Serikali itajitahidi kwa kila hali, kujenga mahakama katika Wilaya ya Biharamulo na kuwapatia Mahakimu kadri watakavyokuwa wanahitaji. Lakini suala lingine alilozungumzia kwamba, Serikali yetu inawaachia tu watu wanachoma moto, watu wanauwana, halafu tunasema ni wananchi wenye hasira kali, alilisema hilo alilifuta baadaye, lakini napenda kumpa malezo tu kwamba, hakuna sheria katika nchi yetu ambayo inatoa mwanya kwa wananchi kuwachoma moto wenzao, Serikali yetu hairuhusu jambo kama hilo na tunakemea vitendo hivyo pale vinapotokea.

Alizungumzia suala la rushwa ya wanasiasa baadaye pia akalitoa hilo baada ya kushindwa kulithitibisha lakini niseme tu kwa ujumla, suala la rushwa katika Sekta ya Sheria limezungumzwa sana na kwa kweli si kubwa kama linavyosemwa, maana hata ile ukubwa wa hizo rushwa unavyosemwa si kubwa kama hivyo, kama sehemu nyingine lakini sitetei kitu cha rushwa. Tunakemea rushwa katika Sekta ya Sheria na vyombo

vyetu vyote tunaviambia rushwa ni adui wa haki na hatutaki wafanyakazi wetu katika Sekta ya Sheria, wajishirikishe katika masuala ya rushwa na ndiyo maana basi tunajitahidi sana kujaribu kuboresha mazingira ya kazi za watumishi hawa, tunajaribu kuboresha hata zile posho ambazo tunawapa. Nia ni kupambana na rushwa na tunajitahidi katika ile tunasema *cross cutting issues,* moja ambalo linazungumzwa katika kila Idara ya Mahakama, Idara ya Sheria ni suala la rushwa tunalikazia sana hilo. Kwa hiyo, tusionekane kama vile hatukemei rushwa tunaikemea sana. Serikali tumetunga sheria za kupambana na rushwa, hizo zote ni katika juhudi hizi hizi.

Mheshimiwa Juma Said Omar, Mbunge wa Mtambwe na Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi, pia walizungumzia hili suala la mgombea binafsi katika ngazi mbalimbali na uchaguzi kwamba, haina Serikali kuanzisha mjadala huu, kwa kweli kama nilivyojibu swali kama hili tena juzi tu kwamba, jamani swali liliamuliwa na Mahakama Kuu, Serikali imekata rufaa, kupeleka Mahakama ya Rufaa na sababu kubwa ya kukata rufaa ni moja tu, jambo zito kama hili, lazima litolewe uamuzi na mahakama ya juu kabisa ya nchi yetu, hatuwezi tukaliacha liishie kwenye Mahakama kuu peke yake.

Kwa hiyo, si kama tuna nia mbaya hapana, tunataka lifikie mahali liwe limekwisha. Kwa hiyo, likifika kule Mahakama ya Rufaa, likishatolewa uamuzi, basi huo ndiyo utakuwa uamuzi, kwa sasa tuliache tusilizungumze.

Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, alizungumzia kuhusu daftari la wapiga kura na akatoa pendekezo kwamba, daftari hili liwe linakuwa *updated* mara kwa mara na huu ni ushauri mzuri, sisi tunaupokea na wazo tunalo, katika kuboresha *RITA* hii ni moja ya kazi ambazo zitakuwa zinafanyika na *agency* hiyo.

Suala lililozungumziwa na watu wengi sana, suala la Mahakama ya Kadhi, limezungumzwa na Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mbunge wa Chonga, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mbunge wa Micheweni, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mbunge wa Tabora Mjini, Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mbunge wa Singida Kusini, Mheshimiwa Manju S. O. Msambya, Mbunge wa Kigoma Kusini, Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassym, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mbunge wa Wete, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi na Mheshimiwa Juma Saidi Omar, hawa wote wamelizungumzia suala hili.

Suala hili kwa uzito wake naweza nikasema tulichofanya Wizara ni kuipatia Tume ya Kurekebisha Sheria, ifanyiwe utafiti ambao tunafahamu, utafiti wao unajumuisha wananchi wengi sana wakishakamilisha utafiti huo na wataukamilisha mwishoni mwa Septemba, 2007, wataleta taarifa yao Serikalini na sisi tutaifanyia kazi taarifa hiyo. Kwa hiyo, ni suala ambalo huwezi ukalichukua tu, kuna masuala mengi ya kujiuliza ni sheria gani taitumia; huyo Kadhi mipaka yake; ni mtu wa namna gani anafaa kuwa Kadhi; na tatizo gani hasa analokwenda kuli-*solve* huyu Kadhi. Kwa hiyo, huwezi ukasema tu kesho tunaazisha fulani achukue, ina mambo ambayo ni lazima yafanyiwe kazi, huku kuna *customary law*, huku kwetu kuna Katiba ni vitu ambavyo lazima

tuviweke sawa ili hapo atakapoanzishwa kama ataanzishwa basi afanye kazi yake bila matatizo.

Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, alikuwa anaulizia kuhusu Mikataba, alisema Serikali iliridhia Mikataba ifuatayo; *The Protocol to the African Charter on Human and Peoples Rights in Africa 2000*, baada ya kusaini mwaka 2003 kama alisema haujaridhiwa mpaka leo. Napenda kumtaarifu kwamba, Mkataba huu umeridhiwa Machi, 2007. Mkataba mwingine aliosema uridhiwe ni *The Convention Against Torture and Other Cruel in Human and Degrading Treatment or Punishment* wa mwaka 1984. Mchakato umeanzishwa ili kupata maoni ya wadau wa Zanzibar, kwa maana hili ni suala la Muungano. Alitaka pia *Protocol to the International Convention of Civil and Political Rights* ya mwaka 1966, alisema turidhie Mkataba huu, tumesharidhia. Mkataba mwingine *Second Protocol to the International Covenant on Civil and Political Rights* ya mwaka 1989, inayoagiza kuhusu kufutwa kwa adhabu ya kifo. Suala la adhabu ya kifo, tumelichukua kwa uzito wake na kwa utaratibu wa Serikali, kwa sababu tumeunda chombo cha kushughulikia masuala haya, tulikabidhi pia Tume ya Kurekebisha sheria ipite nchini, itafute maoni ya wananchi kuhusu kubaki na adhabu hii ama tuiondoe.

Tumegundua humu ndani ya Bunge pia ukiongea na watu kuna wanaosema lazima ibaki, kuna wengine wanasema lazima iondoke. Kwa hiyo, si suala la kulipapalikia kisha baadaye tukatoa uamuzi ambao haukubaliki na wengi. Kwa hiyo, iko sasa hivi Tume. Suala hili pamoja na lile la Kadhi, yanafanyiwa kazi pamoja. Kwa hiyo, tutakapopata mapendekezo ya Tume yetu ya Kurekebisha Sheria, ambayo kama mnavyofahamu sasa, ina wataalamu wengi tu Mwenyekiti wetu ni Profesa wa Sheria wa Chuo Kikuu. Kwa hiyo, tunategemea mapendekezo mazito, ambayo Serikali inaweza ikafanyia uamuzi.

Mkataba mwingine ambao alikuwa ameomba tuuridhie ni *Declaration on Gender and Development, SADC Declaration,* tulisaini na kukubali mwaka 1997 na *addendum* yake 1998, utekelezaji wake umeshafanyika na katika eneo la Kusini mwa Afrika, Tanzania imefanikiwa kuwa na zaidi ya asilimia 30 ya wanawake katika nafasi za uongozi. Hivi sasa tunajiandaa kuwa na asilimia 50 katika nafasi za uongozi, ni masuala ambayo tunayajadili. Kwa kweli ukiangalia katika *SADC,* sisi ndiyo tumepiga hatua kubwa zaidi kuliko wenzetu wengine wote. *(Makofi)*

Suala jingine lililozungumzwa na Mheshimiwa Phares K. Kabuye, pia na Mheshimiwa Lucy F. Owenya ni kuhusu vifungu vya Katiba vinavyozungumzia ujamaa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano, viondoke maana wanavyodai ni kwamba, hatuna ujamaa.

Katika Kitabu cha Marehemu Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, kiitwacho *Freedom and Socialism* au kwa Kiswahili - Uhuru na Ujamaa, kilichopigwa chapa na *Oxford University Press* katika mojawapo ya hotuba zake, Mwalimu anauelezea ujamaa kuwa ni kitendo cha kujenga msingi wa maendeleo ya kijamii, kwa kuzingatia yaliyopita na kuandaa mikakati bora kwa maisha ya baadaye.

Mheshimiwa Spika, anasisitiza kuwa ujamaa lazima uwe na misingi ya kimila na pia uhakikishe kuwa kamwe hauachwi nyuma na sayansi na teknolojia ili jamii iweze kukabiliana na changamoto za maisha zilizoko katika karne ya 20 kwa wakati huo akizungumza, maneno hayo ya Mwalimu aliyazungumza miaka 40 iliyopita lakini bado yana umuhimu ule ule na ni mkubwa zaidi katika falsafa ya Taifa letu. Tunaamini kuwa Ibara ya 3(1) pamoja na mambo mengine inaonesha mwelekeo wa tunakoenda na msimamo wetu kisiasa na mtazamo tulionao katika masuala ya kidini, kwa mantiki hiyo hakuna sababu zozote zile za kimsingi zinazoshawishi kuondoa vifungu vinavyozungumzia ujamaa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la Katiba mpya limezungumziwa na Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassmy, Mheshimiwa Mkiwa Kiwanga, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa William Shellukindo na Mheshimiwa Ania Said Chaurembo. *(Makofi)*

Sasa hili nafikiri nitamwachia Mheshimiwa Waziri aje alizungumzie kwa kirefu ingawa Mheshimiwa *Attorney General* ameshalizungumzia kwa kirefu, nafikiri hoja zitakuwa zimeeleweka. Mheshimiwa Zaynab Vullu na Mheshimiwa ASaid Amour Arfi, hawa walizungumzia walemavu kuwa na sheria ya kusimamia haki za walemavu, Serikali ilisaini mkataba wa Kimataifa wa Haki za Walemavu tarehe 30 Machi, 2007, mchakato wa kuleta mkataba huo Bungeni ili uridhiwe na Bunge unafanywa na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, kwa hiyo, mkataba huu utaletwa na Waheshimiwa Wabunge mkiuridhia basi tutautekeleza kama inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja alilozungumzia Mheshimiwa Mwanne Mchemba, kuhusu uhamisho kwa wanandoa, alilalamika akisema kwamba wanandoa wanahamishwa halafu mmoja anabaki na mwingine anaende kule na akatuonya kuhusu athari au hatari ya kuota kwa nyumba ndogo na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kusema Serikali inatambua umuhimu wa wanandoa kufanya kazi katika eneo moja, Mkoa au Wilaya, hakuna sheria inayowakataza wanandoa kuhama pamoja, tatizo ni kwamba baadhi ya wanandoa wanafanya kazi katika mamlaka za ajira tofauti na kutumia majina pengine tofauti, hivyo siyo rahisi uhamisho ukatoka pamoja lakini mwanandoa mmoja anapopata uhamisho anashauriwa kutoa taarifa ya mwenza wake ili nae aweze kuhamishwa na ili kuwarahisishia uhamisho kwa upande wa TAMISEMI. Ofisi ya Rais, Utumishi imekasimu madaraka kwa TAMISEMI kushughulikia uhamisho wa watumishi toka Halmashauri moja kwenda nyingine. Lakini kama wapo watumishi ambao wamekaa zaidi ya miaka mitano kama alivyoeleza Mheshimiwa Mwanne Mchemba bila ya kupata uhamisho wa kufuata wenzi wao mimi namshauri Mheshimiwa Mbunge awasiliane na Waziri wa Nchi, Ofisi ya rais, Utumishi ili aweze kumsaidia katika kulitatua hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo na Mheshimiwa Kabwe Zitto walizungumzia kuhusu *RITA* na umuhimu wa Idara hii katika nchi yetu. Nataka kuwaeleza kwamba Serikali inautambua sana umuhimu wa Idara ya *RITA* katika mipango

ya uchumi ya nchi yetu, katika ku-*update* daftari la wapiga kura, katika sensa ya Taifa haya yote tunayafahamu na ndio maana basi Serikali sasa tumeupa uzito mkubwa sana *agency* hii ili iweze kutusaidia katika kuweka sawa mipango yetu na taratibu zetu nyingine pamoja na ku-*update* daftari la wapiga kura lakini mawazo yao mazuri tumeyachukua na tutayafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa George Lubeleje, Mweyekiti wa Kamati ya Sheria alitoa mawazo yake kuhusu kuwajengea majaji nyumba ili kupunguza Majaji kukaa hotelini.

Wizara yangu imekuwa ikiwasiliana na Wizara ya Miundombinu ili kupatiwa nyumba za kuishi Majaji na Mahakimu, mwaka 2006/2007 Wizara ya Miundombinu imetoa nyumba 16 Dar es Salaam na nyumba nne hapa Dodoma, juhudi zinafanyika kupata nyumba zaidi, tunamshukuru kuwa aliunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ponsiano Nyami alizungumza kuhusu …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema naunga mkono hoja hii.

**SPIKA:** Pole sana kuhusu muda lakini ndio hivyo, Waheshimiwa Wabunge sasa nafurahi nimwite mtoa hoja Mheshimiwa Waziri mwenyewe yeye anazo dakika 40. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, nimefurahi na ninaomba nikushukuru sana kwa kuamua kurudi Bungeni ili uwe sehemu ya bajeti yetu ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu na pia nakushukuru wewe kwa kunipatia fursa hii ili niweze kuhitimisha hoja yangu niliyoitoa asubuhi ya leo kwa kutoa maelezo kuhusu masuala mbalimbali yaliyojitokeza na yaliyozungumziwa na Waheshimiwa Wabunge, ambayo wameyasema kwa niaba ya wananchi wanaowawakilisha. Naitambua nafasi hii kuwa ni sawa na nafasi ya kutoa majibu kwa hoja za wananchi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu asubuhi kulikuwa na utata kidogo na muda wangu ulichukuliwa kwa ajili ya kutoa tangazo, naomba nichukue muda kidogo kutoa shukrani na pongezi kwa mambo ambayo ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali ya kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge naomba niwapongeze Mheshimiwa Laurian Kalegea na Mheshimiwa Mshibe Bakari, walioteuliwa kuwa Majaji wa Mahakama ya Rufani, napenda pia kuwapongeza kwa pamoja Waheshimiwa Majaji 21 wa Mahakama Kuu, Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria, Msajili wa Mahakama ya Rufani, Msajili wa Mahakama Kuu ya Tanzania na wasajili wa Mahakama Kuu vitengo vya Kazi na Biashara, Naibu

Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye ni Katibu Mkuu wetu wa sasa na Mkurugenzi wa mashtaka kwa kuteuliwa kwao kushika nyadhifa hizo muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Barnabas Albert Samatta ambaye tarehe 20 Julai mwaka huu amestaafu baada ya kufanya kazi katika utumishi wa umma kwa takriban miaka 41. Utumishi wake uliotukuka utabaki kuwa mfano wa kuigwa siyo tu na Majaji wenzake, bali pia kwa watumishi wote waliowahi kufanya naye kazi, tunamwombea kila la heri katika maisha mapya ya kustaafu.

Napenda kumpongeza Mheshimiwa Augustino Stephen Lawrence Ramadhan kwa kuteuliwa kuwa Jaji Mkuu mpya, bila shaka uwezo wake na busara zake zitakuwa msaada mkubwa wa kuiongoza Mahakama yetu ili iweze kutenda haki kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru Naibu Waziri, Mheshimiwa Mathias Chikawe, Mbunge wa Nachingwea na Mheshimiwa Johnson Mwanyika, Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa msaada wao katika kuongoza Wizara na hapa Bungeni kama mlivyoshuhudia leo, wamenisaidia sana kujibu hoja za Wabunge hasa ukizingatia kwamba mimi si mwanasheria. *(Makofi)*

Pia ninawashukuru Mheshimiwa Amir Manento, Jaji kiongozi, Majaji na Mahakimu wote, Mheshimiwa Jaji Robert Kisanga, Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Profesa Ibrahim Juma, Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria na Bibi Joackina Dimelo, Rais wa Chama cha Wanasheria nchini kwa ushirikiano walionipa katika kutekeleza majukumu yangu mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza watendaji mbalimbali katika Wizara nikianza na aliyekuwa Naibu Mwanasheria Mkuu na Katibu Mkuu Bwana Vicent Lyimo ambaye ameshateuliwa kuwa Jaji, Bwana Sazi Salula, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Katibu Mkuu, Bibi Sophia Wambura, Msajili ya Mahakama ya Rufaa, Bibi Eliamani Mbise, Msajili wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Bwana Somi Mayala, Msajili wa Mahakama ya Ardhi, Bwana John Kayonza, Msajili wa Mahakama ya Biashara, Bwana Samuel Karuwa, Msajili wa Mahakama ya Kazi, Bibi Cresensia Makuru, Katibu wa Tume ya Kurekebisha Sheria, Bibi Mary Massay, Kaimu Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Bwana Dickson Maimu, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakinipa katika kuiongoza Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwa wadau wa maendeleo wanaoendelea kutoa misaada mbalimbali hasa katika *basket fund* (mfuko wa pamoja) kuboresha na kuendeleza sekta ya sheria nchini ambao ni Sweden, Benki ya Dunia, Canada, Belgium, Denmark, *UNICEF* na *GTZ*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwatambua wote waliochangia ambao wapo katika makundi makubwa matatu. Wapo wale ambao walitoa michango inayohusu masuala ya Katiba na Sheria wakati wakichangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, pili ni

waliochangia kwa kuzungumza humu Bungeni leo asubuhi wakichangia hoja hii. Mwisho, ingawa siyo kwa umuhimu, wapo wale waliochangia kwa maandishi. *(Makofi)*

Namshukuru sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yao ya ufasaha ya hoja moja hadi nyingine hasa walipomtaja kila Mbunge kwa jina lake na nafikiri mimi mtaniruhusu niende kwenye hoja na kama ikiwezekana nisitaje majina lakini naomba niwashukuru kwa madhumuni ya rekodi. *(Makofi)*

Waliochangia kwa kuzungumza humu Bungeni ni Mheshimiwa Stephen Galinoma, ambaye alizungumza kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na vile vile Mbunge wa Kalenga, Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi Msemaji Mkuu wa Upinzani kwa Wizara ya Katiba na Sheria na Mbunge wa Chake Chake, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Ponsian Nyami, Mheshimiwa Phares Kabuye, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Johnson Mwanyika, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mheshimiwa Mathias Chikawe, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waliochangia wakati wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni wafuatao Mheshimiwa Ali Said Salum, Mheshimiwa Juma Said Omari, Mheshimiwa Phares Kabuye, Mheshimiwa Mercye Emmanuel na Mheshimiwa Shoka Khamis Juma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimwa Dr. Lukas Siyame, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Salome Mbatia, Mheshimiwa Manju Msambya, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa James Musalika, Mheshimiwa Mwamtuma Mahiza, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Ruth Msafiri na Mheshimiwa Lucas Selelii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Sigfrid Ng'itu, Mheshimiwa Ania Chaurembo, Mheshimiwa Maulidah Anna Komu, Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Zaynab Vulu, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Monica Mbega, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Juma Saidi Omar, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Zulekha Yunus Haji, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Mkiwa Kiwanga, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, Mheshimiwa Khadija

Salum Al-qassmy, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Idd Azzan, Mheshimiwa Dorah Mushi, Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Steven Galinoma, Mheshimiwa Mustapha Mkulo, Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mheshimiwa Diana Chilolo na Mheshimiwa Kabwe Zitto, wote hao wamefika sitini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia, wametoa michango mizuri sana yenye lengo la kuimarisha utendaji kazi katika Wizara yetu. Kwa wale waliochangia wakati wa kujadili hoja ya Waziri Mkuu tumejitahidi sana kuzijibu hoja walizozitoa katika hotuba yangu ya Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, michango ambayo Waheshimiwa Wabunge wameitoa ni mingi. Kuna ugumu kuweza kutoa maelezo ya kujibu kila moja ya hoja zilizotolewa. Nitamke tu kuwa michango yote iliyotolewa tunaithamini sana na kwamba tutaifanyia kazi kikamilifu. Kama ilivyo kawaida yetu tutaandaa majibu ya hoja zote kwa kina na tutawasambazia Waheshimiwa Wabunge kabrasha lenye majibu hayo pamoja na wale ambao majibu yao yametolewa hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niwashukuru kwa namna ya pekee Mheshimiwa Johnson Mwanyika, Mwanasheria Mkuu wa Serikali walivyojibu kwa kina hoja za Waheshimiwa Wabunge. Mimi nitajitahidi kwa ujumla kujibu hoja muhimu zilizojitokeza, katika kufanya hivyo sitarejea kutolea maelezo hoja ambazo Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu na Naibu Waziri wamezitolea maelezo labda kwa njia ya msisitizo tu, nitaanza na hoja za jumla na ambazo ndizo msingi na chimbuko la malalamiko mengi ya wananchi yaliyoelezewa humu Bungeni na Wabunge waliochangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la utawala wa sheria, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatamka wazi kuwa nchi yetu ni yenye kuzingatia misingi ya uhuru, haki, udugu na amani. Aidha, inaieleza nchi yetu kuwa ni yenye kuongozwa na Serikali yenye kufuata misingi ya demokrasia. Ili hayo yaweze kufikiwa, Serikali imekuwa ikizingatia utawala wa Sheria. Huu ni utawala unaohimiza kila mtu na kila mtawala au kiongozi kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa katika utendaji na utekelezaji wa majukumu yetu. Hili ni moja ya mambo ambayo Wizara yangu muda wote tumekuwa tukifanya kila liwezekanalo ili Serikali katika ujumla wake iimarishe utawala wa sheria. Tunatambua kuwa utawala wa sheria ndiyo msingi wa uhuru, haki na amani ya kudumu katika jamii. Utawala wa sheria ni muhimu katika shughuli zote za kiuchumi na za kijamii ndani ya nchi. Ili kutimiza lengo la kudumisha utawala wa sheria, yafuatayo yalikuwepo na yanaendelea kutekelezwa:-

(a) Tumekuwa tukizipitia upya sheria za nchi ili kutoa mapendekezo ya kuzirekebisha zile zilizopitwa na wakati au kwa nia ya kuzingatia mahitaji mapya ya jamii. Kama nilivyoeleza katika hotuba yangu, hili ndilo jukumu ambalo tumekuwa tukilitekeleza kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria na pia Idara ya Mwandishi Mkuu wa Sheria. Utawala wa sheria unahitaji kuwepo sheria zinazokwenda na wakati. Ndiyo maana nakubaliana na maoni yaliyotolewa na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kutaka Tume hiyo iongezewe uwezo wa kifedha na Serikali imekuwa ikifanya hivyo kila

uwezo unavyoruhusu. Natoa wito kuwa Waheshimiwa Wabunge mnapoona kuna sheria fulani imepitwa na wakati, msisite kutupatia taarifa ili zifanyiwe kazi. *(Makofi)*

(b) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeendelea kuzipatia ushauri Wizara na Idara za Serikali kuhusu masuala mbalimbali ya kisheria ili utendaji wake uendane na sheria, taratibu na kanuni zilizowekwa. Waheshimiwa Wabunge wengi wametoa mchango wao katika eneo hili. Katika kuimarisha hali hii, sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilipitishwa, ambayo pamoja na mambo mengine, inazitaka Wizara na Idara za Serikali kupata ushauri wa kisheria kuhusu utekelezaji wa shughuli zao. Katika mazingira ambayo kwa makusudi ofisa wa Serikali anaacha kupata ushauri na kusababisha Serikali kupata hasara, anaweza kuwajibishwa binafsi. Kwa nia ya kufanikisha shughuli za Serikali zizingatie utawala wa sheria, ushirikiano wa kila Wizara na Idara za Serikali na Mwanasheria Mkuu ni muhimu. *(Makofi)*

(c) Nguzo kuu ya utawala wa sheria ni uhuru wa Mahakama. Sheria, Taratibu na Kanuni mbalimbali inabidi kutafsiriwa na Mahakama iliyo huru. Mahakama ni lazima isimamie sheria pasipo hofu wala uoga. Uhuru wa Mahakama unazo sifa mbili, ya kwanza ni uhuru wa kiutendaji *(functional independence)* na pili ni uhuru wa kimaslahi. Suala la uhuru wa kiutendaji ni rahisi zaidi kueleweka. Haitakiwi kuingilia Mahakama katika utendaji wa shughuli zake kuhusu nani mwenye haki baina ya pande zinazofika mbele yake. Uhuru kimaslahi ndiyo unahitaji maelezo kidogo na suala hili limechangiwa sana na Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Msemaji wa Upinzani na Waheshimiwa Wabunge wengine wamelizungumzia suala la maslahi ya kimshahara na marupurupu mengine. Ni suala muhimu na Serikali inalitambua na imekuwa ikilifanyia kazi kwa kuzingatia uwezo wake muda wote. Kadri uwezo wa Serikali unavyoongezeka, Serikali haitasita kuongeza maslahi hayo ambayo inatambua ni madogo. Serikali inalizingatia sana hili na ndiyo maana siyo muda mrefu uliopita tuliwasilisha Muswada na Bunge likaupitisha kuwa Sheria ya Majaji ambao pamoja ma mambo mengine, ulizungumzia suala la maslahi na marupurupu ya Majaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria hiyo ilitungwa kwa kuzingatia nafasi muhimu ambayo Majaji na Mahakimu wanaishi katika jamii yetu. Tunapozungumzia suala la maslahi binafsi katika utoaji wa haki ni pamoja na kupiga vita vitendo vya rushwa na ndiyo maana Serikali na Mahakama tumekuwa tukipiga vita vitendo hivyo. Tunaelewa hii siyo vita ndogo au rahisi na ndiyo maana naelewa sababu ya Waheshimiwa Wabunge kadhaa kulizungumzia suala hili. Mapambano yanaendelea ila napenda kusema kwamba pamoja na kwamba maslahi ya Majaji kidogo yameboreka lakini watumishi wakiwemo Mahakama za ngazi za chini kwa kweli inabidi tuziangalie ili vile vile kuboresha maslahi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, katika kudumisha suala la uhuru wa Mahakama, Wizara imekuwa ikihimiza suala la kuzingatia maadili kwa watumishi wa Mahakama. Napenda kusisitiza kwamba uhuru wa Mahakama hauna maana ya watumishi kujifanyia mambo wapendavyo, bali ni nyenzo ya kufanya watumishi hao wasiingiliwe katika

utendaji wao kwa lengo moja kubwa, nalo ni kuhakikisha kuwa chombo chao cha Mahakama kama vilivyo vyombo vingine, inawatumikia na kinawajibika kwa wananchi. Uhuru wa Mahakama hautokei hewani bali unatokana na haja ya kuwatumikia wananchi vizuri na kwa haki zaidi.

Mheshimiwa Spika, lengo la uhuru wa Mahakama ni kufanya kile ambacho Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alikisema tarehe 7 Desemba, 1965 alipokuwa akifungua mkutano wa Majaji na Mahakimu aliposema, kwa kiingereza na ninanukuu: *"The work of the judiciary is nothing less than the maintenance of respect for law in this Country. Judges are, and must be, nothing less than buttress wall supporting the individual justice for which our people struggled when they fought for national independence. You do not control legislation but your actions, together with those of the police, can make that legislation effective or meaningless. Unless your work is done properly none of the objectives of our democratic society can be implemented,"* mwisho wa kunukuu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndio maana tumesema kwamba majukumu ya Wizara hii kwa kweli ni nyeti hasa ukizingatia muhimili wa tatu wa dola ambao ni mahakama uko chini ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshmiwa Spika, tunapozungumzia suala la utawala wa sheria na uhuru wa Mahakama, tunachotaka mwishowe iwe ni mwananchi kupata haki. Hali tunayoihitaji ni ile aliyoieleza Mwalimu Nyerere kuwa, ninanukuu tena: *"Justice demands many things. It demands that the innocent be assured of personal security; and also that the guilt should be punished. It demands impartiality between individual citizens that the law should be the same for all. And it demands an understanding by the judiciary of the people, and by the people of the judiciary; for without this mutual understanding the people's basic sense of justice in their relations with each other may be outraged by the very instrument which they have created to implement justice.*"*(Makofi)*

Kwa hiyo, Mahakama ina nafasi nyeti sana. Unaposikia mtu amepeleka kidhibiti mahakamani na baada ya kesi kuisha akienda anakuta kidhibiti chake kimechukuliwa ni jambo ambalo halivumiliki kwa wananchi. Ni jambo ambalo halivumiliki kabisa kusikia kwamba mirathi ya watoto ambao walikuwa na maisha mazuri baada ya wazazi kufa inapotelea mahakamani, yanapotea kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina hakika Mahakama ya Tanzania inafanya kila njia kuona hali hii haitokei na kama inatokea ni bahati mbaya.

Mheshimiwa Spika, haki isipokuwepo, ndiyo husababisha ukosefu wa amani katika jamii na amani ikipotea, husababisha watu kushindwa kufanya kazi za kawaida za kiuchumi na kijamii katika nchi, mifano ya hali hii si migumu kuiona. Zipo nchi ambazo kutokana na ukosefu wa amani, zimedumaa kiuchumi. Hivyo, naungana na Waheshimiwa Wabunge ambao wamesema kuwa umuhimu wa shughuli za Wizara hii uonwe katika msingi huo. Hata hoja iliyotolewa na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu pendekezo la kuiongezea Wizara ya Katiba na Sheria fungu la fedha naizingatia katika msingi huo. Hatua kwa hatua Serikali itaendelea kuiongezea fedha Mahakama na

kama mkikumbuka katika Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha tumekuwa na vipaumbele katika sekta nne, ni matumaini yangu kwamba siku za usoni basi na sekta hii itapewa umuhimu wa pekee.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia masuala haya ya jumla, napenda sasa nijielekeze katika baadhi ya masuala mengine mbalimbali yafuatayo na nitaanza na yale yaliyoelezwa na Kamati pamoja na Msemaji wa Upinzani, ningependa kwa moyo wa dhati kumshukuru dada yangu mama Fatma Maghimbi, pamoja na kwamba mambo mengine aliyoyasema pengine nikiyapinga siyo kwamba urafiki wetu utaisha bali ndio ukweli wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, namshukuru sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kulisemea hili kwa nguvu zote na kwa utaalamu wake wote kwa sababu yeye ndiyo mtaalamu mkuu wa mambo ya sheria. Hata hivyo, naomba nami nilisemee kwa madhumuni ya kuweka msisitizo zaidi.

Mheshimiwa Spika, tunayo Katiba iliyopitishwa na vyombo vyenye madaraka ya kufanya hivyo hasa hili Bunge ambalo ni Tukufu na linawakilisha wananchi. Katiba tuliyonayo ilipitishwa na Bunge lililokuwa na mamlaka kufanya hivyo. Kumekuwa na hoja kwamba Tume za Jaji Francis Nyalali na Jaji Robert Kisanga zilipendekeza kwamba Katiba iandikwe upya, kama alivyoeleza Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwamba huku ni kukosa kuelewa kwa sababu kilichosemwa kwenye zile ripoti siyo kuandika Katiba upya bali itaandikwa upya kama mapenekezo ya shirikisho yangepita na kwa hivyo hili lieleweke vizuri. Jamani wananchi wana shida nyingi, kuna umaskini tunabidi kufanyia kazi ili tuondokane na umaskini wa Watanzania, hatuwezi kuanza kwenda kukaa upya kuandika Katiba mpya wakati hii tuliyonayo inakidhi haja na kwa miaka mingi inayokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukisoma ripoti hizi suala la kutunga au kubadilisha Katiba lilikuwa linajitokeza iwapo tu kungekuwa na mabadiliko ya msingi katika mfumo wa utawala wa nchi. Mabadiliko haya ni kama vile kuwa na mfumo wa shirikisho kama nilivyoeleza, hili halijatokea bado Tanzania, hivyo hakuna haja ya Katiba mpya kama alivyosema Mwanasheria Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo napenda kusisitiza kuwa Serikali yenu sikivu, wakati wote kunapokuwepo sababu ya kufanya mabadiliko na si kutunga Katiba mpya, ya eneo lolote katika Katiba, Serikali itapokea na kufanya marekebisho ambayo jamii inayahitaji na kwa utaratibu uliwekwa ndani ya Katiba yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imewekewa utaratibu kama alivyoeleza Mwanasheria Mkuu wa Serikali na sina sababu ya kurudia. Aidha, Katiba ya nchi hii imekuwa ikitungwa kulingana na umuhimu wa matukio mbalimbali ambayo yameonekana kuwa na umuhimu wa kipekee katika Taifa letu na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Seikali ameyaelezea vizuri sana. Kwa sasa kama alivyosema Mwanasheria Mkuu wa Serikali hakuna tukio lolote kubwa la kufanana na

matukio haya yaliyoelezwa ambayo litahitaji Katiba kutungwa upya. Serikali inatambua kuwa Katiba ni hai kama zilivyo Katiba za nchi nyingine na hufanyiwa mabadiliko ikihitaji ili kukidhi mazingira ya wakati unaohusika na kama kuna mabadiliko ambayo Kambi ya Upinzani inahitaji ilete kwa utaratibu unaojulikani kwani nimesema Serikali ni sikivu, Wapinzani nchi hii ni yao vile vile, kwa hivyo, tutawasikiliza lakini suala la Katiba mpya kwa kweli si suala la kipaumbele wala si matakwa ya wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo mwaka 1998 Serikali iliunda Tume ya Jaji Robert Kisanga ili kukusanya maoni ya wananchi kuhusu pamoja na mambo mengine muundo wa Muungano. Mapendekezo ya Tume ya Jaji Robert Kisanga yaliendelea kufanyiwa kazi kwa kuingizwa kwenye Katiba kwa awamu kadri mazingira yanavyoruhusu kwa maslahi ya Taifa letu. Sisi Wabunge wakiwemo Wabunge wa Kambi ya Upinzani tuienzi, tuilinde na tuitetee Katiba tuliyonayo kama tulivyoapa wakati tukikubali Ubunge huu tuliopewa na wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kulielezea suala la Katiba na ninategemea kwamba Waheshimiwa Wabunge wa Upinzani watakuwa wamelielewa hili suala ni muhimu kwa maslahi ya Taifa, mmeona nchi nyingine zinavyotikiswa wakati wakitaka Katiba mpya, hii amani yetu ni nyeti, tunaihitaji kwa maendeleo yetu, ni vema tuilinde na kudumisha kupitia Katiba hii ambayo ndio muhimili mkuu wa amani na utulivu wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshmiwa Spika, sasa naomba niongelee suala nyeti lingine. Lenyewe ni suala la kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi, napenda kukiri na kutambua kwamba kupata majibu muafaka kuhusu hoja ya Kadhi Mkuu ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba na majibu yangu ya Bajeti 2006/2007 nilitambua uzito wa hoja hii na umuhimu wa nafasi ya Kadhi Mkuu. Niliomba subira ya Bunge na Wabunge ili kuipatia nafasi Serikali iendeleze ufanisi wa kujenga dhamira timilifu ya kuwa na Kadhi Mkuu kwa taratibu zilizojaa suluhu za Kiserikali na za kijamii na za utawala bora kwa maslahi ya walengwa na kwa maslahi ya Watanzania wote kwa sababu tunategemeana kijamii na kimaisha katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii tena kulipongeza Bunge na kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliotoa hoja ya kuikumbusha Serikali kuwa ina deni la kutekelezwa kwa waumini wetu ambao wanaomba kupata uongozi wa dhamana ya Kadhi Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bunge la Tanzania daima wanaithibitishia dunia kuwa tunatanguliza sifa ya maslahi ya Taifa letu na tunatekeleza sifa ya uongozi na kuonyesha njia. Sifa hii ni kielelezo cha ari ya kuvumiliana kwa msingi wa rai ya kuelimishana kati ya viongozi na jamii hadi tunapata suluhu kwa maslahi ya Watanzania wote hasa kwa masuala nyeti. Sifa hii tuiendeleze na kuilinda kwani katika dunia yetu, wapo wanaohoji amani na utulivu wa watanzania siri yake hasa ni nini.

Mheshimiwa Spika, Mwenyezi Mungu anahimiza wenye subira wapo na Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa kuhimiza fursa ya dhamana ya Kadhi Mkuu. Vivyo hivyo, naomba viongozi wenzangu Waheshimiwa Wabunge muitikie rai ya kuwa na subira. Kupatia ufumbuzi suala la Mahakama ya Kadhi lipo ndani ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM. Lipo kwa dhati na siyo kwa madhumuni ya kuipatia ushindani CCM. Bali ni kwa kutambua kilio cha wenzetu wa Waislam. Serikali ina jukumu la kuona kwamba hili linapatia muafaka. Lakini ina jukumu vile vile kutambua kwamba kuna Watanzania wengine walio na hofu na ndiyo maana Wizara imeiagiza Tume ya Kurekebisha Sheria kufanya utafiti wa kina kuhusu uwezekano wa kupatia ufumbuzi suala la Mahakama hiyo hapa Tanzania Bara. Tume imepewa miezi kumi na mbili, kuanzia Oktoba, 2006 mpaka Oktoba, 2007 kukamilisha kazi hiyo. Tuna miezi miwili tu toka sasa. Tume inalifanyia kazi agizo hilo na inatarajia kuwasilisha taarifa yake ifikapo mwisho wa mwezi Septemba, 2007. Matokeo ya utafiti huo yatawekwa bayana na Serikali itayafanyia kazi kwa kuzingatia mapendekezo ya Tume na maslahi ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Mwanne Mchemba na vilevile Mheshimiwa Ponsiano Nyami kwa sababu wameongelea suala ambalo nalo lipo katika mioyo ya Watanzania walio wengi na vile vile mimi mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha mchakato wa kuifanyia marekebisho Sheria ya Ndoa, Kutunga Sheria ya Watoto na Sheria ya Mirathi na Urithi. Ni matarajio yangu kwamba Serikali kupitia Wizara yangu itawasilisha hapa Bungeni Miswada ya Sheria ili kuomba idhini ya Bunge kutunga sheria hizo. Ni matarajio yangu kuwa Sheria hizo zitatungwa katika kipindi cha mwaka wa fedha tulionao. Kutungwa kwa Sheria hizo kutaondoa matatizo mengi kama yalivyoelezwa na Mheshimiwa Ponsiano Nyami na Mheshimiwa Mwanne Mchemba. Mambo muhimu yanayotarajiwa kuwepo ni kutoa tafsiri ya mtoto. *(Makofi)*

Vile vile kuainisha haki na ulinzi wa mtoto kwa kuzingatia matakwa ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto. Kutokana na Sheria ya Ndoa mapendekezo ni kuainisha haki ya mwanawake aliye katika ndoa na mchango wake katika familia. Haki ya Mwanandoa pindi ndoa inapovunjika na kuanzisha Mahakama ya Familia. Mapendekezo hayo pia yataainisha vizuri zaidi haki ya mtu ambaye ni mtoto anayehitaji kuolewa. Sasa hivi Sheria inaleta utata kwa sababu wakati umri wa mtoto umeamriwa kwamba ni miaka 18, lakini kuna maeneo ambayo Sheria ya Ndoa inaruhusu watoto wa miaka 14, 15 kuolewa. Vile vile Sheria itaainisha wosia na wasia. Taratibu za kugawa mali kwa warithi hasa wale ambao wameumia kwa muda mrefu hususan akinamama na watoto, kuondoa sheria zinazokandamiza haki ya wanawake na nyie mnajua kwamba kwa mila na desturi za kwetu kwa kweli haki za wanawake zinawekwa kando. Kwa jumla kuondoa baadhi ya sheria za kimila zenye ubaguzi wa wanawake na zinazoleta mateso kwa akinamama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais aliongelea kwa kirefu wakati akifungua Mkutano wa Akinamama juzi na aliliongelea kwa uchungu kuona akinamama na watoto wakiteseka kwa sababu sheria zenyewe hazisaidii kuondoa huo mkanganyiko. Kwa hiyo, na mimi nitajitahidi sana kupitia Wizara yangu na kupitia Bunge hili kuona mwaka huu wa fedha pengine sheria hizo zikapita na zikajenga heshima ya Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba nikiri kupokea nakala ya barua ya Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini aliyoandika kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika barua yake aliongelea suala la mfumo wa uchaguzi ambao yeye anaamini unafaa zaidi kwa Tanzania yaani *Proportional Representation*. Kama tulivyoahidi wakati tunajibu swali hapa Bungeni, naahidi kushughulikia suala lake na vile vile tutalijibu wakati ambapo tutakuwa tumelikamilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuongelea hayo mambo ambayo nilifikiri ni nyeti kwa njia ya msisitizo, sasa naomba vile vile niende kwenye maeneo mengine kadri muda utakavyoniruhusu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la uhaba wa Majaji, Mahakimu na vitendea kazi, ni kweli tunalo. Majaji wa Mahakama ya Rufani tunaohitaji ni 15, kwa sasa hivi tunao 12 hivyo tuna upungufu wa Majaji wa Rufani watatu. Majaji wa Mahakama Kuu tunahitaji 70, kwa sasa hivi tunao 52 hivyo tuna upungufu wa Majaji 18. Mahakimu Wakazi tunahitaji 350, tulionao 284, hivyo tuna upungufu wa Mahakimu 66. Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo tunaohitaji 1105, tunao 776 tu, hivyo tuna upungufu wa Mahakimu 329. Kutokana na takwimu hizo, tatizo la upungufu wa Majaji na Mahakimu Wakazi limepungua lakini bado hatujakidhi mahitaji hasa ikizingatiwa kuwa ni nia ya Serikali kuwa na Kanda za Mahakama Kuu kwa kila Mkoa.

Mheshimiwa Spika, hatua za kukabiliana na upungufu huo ni pamoja na zifuatazo:-

Kwanza, kuhusu upungufu wa Majaji, Mheshimiwa Rais hufanya uteuzi wa Majaji kila hali ya fedha inaporuhusu na nyie ni mashahidi. Haijawahi kutokea toka enzi za Uhuru Majaji 21 wa Mahakama Kuu kuteuliwa kwa mara moja. Nampongeza na ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais. Ni mategemeo yangu kwamba Majaji walioteuliwa watakuwa chachu kubwa na kwamba mrundikano wa kesi kwenye Mahakama zetu itakuwa ni historia pamoja na kufanyia marekebisho maeneo mengine ambayo yatachochea ufanisi wa Mahakimu na Majaji. *(Makofi)*

Pili ni kuhusu upungufu wa Mahakimu Wakazi. Mahakimu Wakazi 20 wataajiriwa katika kwa mwaka 2007/2008 na tatu ni kuhusu upungufu wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, hatua zifuatazo zimechukuliwa, kwanza upanuzi wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto ili kuongeza idadi ya wahitimu wa Stashahada ya Sheria ambao wanatarajiwa kuajiriwa kama Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo kutoka 117 hadi 500, pili, kuajiri wahitimu wa stashahada ya sheria kutoka vyuo vingine vinavyotambuliwa na Serikali na tatu kuajiri Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo

wastaafu kwa mkataba, hususan wenye kumbukumbu nzuri za utendaji na maadili. Taratibu za kuajiri kwa mkataba za Mahakimu 28 wa Mahakama za Mwanzo zipo kwenye hatua za mwisho. Namshukuru sana Mheshimiwa Hawa Ghasia kwa ushirikiano wake wa karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kujielekeza sasa katika suala la mrundikano wa kesi zilizopo kwenye Mahakama zetu ili kukabiliana na tatizo hilo, hatua zifuatazo zimechukuliwa:-

(i) Mheshimiwa Rais kama nilivyoeleza ameteua Waheshimiwa Majaji wawili wa Mahakama ya Rufani na Waheshimiwa Majaji 21 wa Mahakama Kuu.

(ii) Mahakimu Wakazi 77 na Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo 46 wameajiriwa.

(iii) Vile vile matumizi ya kalenda za kila Jaji zitatumika na zitafuatwa na Mahakama ya Tanzania.

(iv) Vile vile kufanyika kwa vikao vya Kamati za kusukuma mashauri kwenye ngazi za Wilaya, Mkoa na Kanda zitasisitizwa sana.

Mheshimiwa Spika, hapa madai yalikuwa kwamba hakuna fedha. Lakini Jaji Mkuu na Msajili wa Mahakama ya Rufani imeelekeza Mahakama zote ili kuhakikisha kwamba hizo Kamati za kusukuma kesi au mashauri zinafanya kazi yake ipasavyo na fedha kupelekwa kila mara ili wakutane kama ilivyopangwa kila robo mwaka.

Mheshimiwa Spika, njia nyingine ni kujengwa na kukarabati majengo ya Mahakama mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kupitia Mradi wa Maboresho ya Sekta ya Sheria, jambo ambalo linatiliwa umuhimu wa kwanza kabisa ni kukarabati Mahakama zile ambazo ni mbovu sana. Kwa muda mrefu Mahakama ni mahali ambapo kwa kweli nafikiri palikuwa hapafikiriwi. Lakini kwa miaka mitatu iliyopita na tutaendelea kufanya hivyo kuhakikisha kwamba Mahakama zinakarabatiwa na pale ambapo Mahakama hazipo na zinapaswa kuwepo basi zinajengwa ili kupeleka huduma hiyo karibu na wananchi na ili wananchi wapate haki yao kama wanavyostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile kuhusu matumizi ya njia mbadala ya kusuluhisha migogoro kama alivyoeleza Msemaji wa Upinzani nina maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Msemaji wa Upinzani alieleza kuhusu utaratibu wa kuharakisha kesi kwa mtindo mbadala wa utatuzi wa kesi *(Alternative Disputes Resolution - ADR),* kutotumika ipasavyo ama kutosaidia kupunguza tatizo la mrundikano na ucheleweshaji wa kesi Mahakamani. Napenda kueleza kuwa *ADR* haitumiki kila Mkoa kwa sababu sio Majaji na Mahakimu wote wamepatiwa mafunzo ya utaratibu huo. Ili kupanua wigo wa matumizi ya *ADR,* Wizara imeendelea kuwapatia mafunzo Majaji na

Mahakimu ambao hawajapata mafunzo hayo pamoja na kuwahamasisha wananchi kutumia *ADR* kutatua migogoro yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu tatizo la baadhi ya Mahakimu na wasimamizi wengine wa maamuzi katika Mahakama na Mabaraza ya Ardhi kushindwa kutatua kesi kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999, Mabaraza ya Ardhi yapo chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, hata hivyo Serikali ni moja na tutashirikiana. Kwanza, Mabaraza hayo mengine hayajaanza kufanya kazi. Yale yaliyoanza kufanya kazi hayafanyi kazi vizuri. Nitashirikiana na Wizara wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa jumla kuona kwamba Mabaraza yanafanya kazi. Kwa sababu Mabaraza yasipofanya kazi, kazi kubwa itaenda kwenye ngazi ya Mahakama Kuu na ndiyo maana kuna mrundikano wa kesi. Hata Mahakimu ambao ni wenyeviti wa Mabaraza hayo pamoja na kwamba ni Wanasheria lakini wapo chini ya Wizara hiyo. Tutawasiliana na Wizara husika ili iweze kushughulikia suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la wananchi kuhamasishwa kushiriki katika ujenzi wa majengo ya Mahakama, hapa napenda kuwashukuru na kuwapongeza wananchi kwa dhati kabisa kwa sababu wameona umuhimu wa kuwa na Mahakama na wakajitolea wao kushirikiana na Serikali yao katika ujenzi wa Mahakama katika ngazi mbalimbali. Serikali itajitahidi kuona kwamba inaunga mkono jitihada za wananchi pale ambapo wameanza wenyewe kushiriki ujenzi wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja kuwa Serikali kutoa fursa za kisheria zitakazowawezesha walemavu kuwa na nafasi maalumu za uwakilishi, Serikali kwa upande wake ina sera ya walemavu ya mwaka 2004 ambayo ndio inatoa mwongozo kuhusiana na masuala ya walemavu. Aidha, Tanzania ilisaini Mkataba wa Kimataifa unaoitwa *The Convention on the Rights of Persons with Disabilities* tarehe 30 Machi, 2007. Sera hiyo na Mkataba huu utawezesha kuyashughulikia masuala haya vizuri ya walemavu. Nawapongeza sana wale ambao walileta semina, sijawahi kuona semina iliyokuwa na umuhimu kama ile ya jana (semina ya walemavu). Nina hakika kupitia semina hiyo na sera yenyewe tuhakikisha kwamba walemavu wanapata haki yao zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, imetolewa hoja kuhusu ukosefu wa teknolojia ya kisasa ya utunzaji wa takwimu za vizazi na vifo kwa *RITA* sina sababu ya kulirudia hili kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri alilielezea vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Sheria ya Usajili wa Vizazi na Vifo Sura 108 kufanyiwa marekebisho ili watumishi wasio na taaluma ya sheria waliopo TAMISEMI wasiweze kufanya kazi hiyo. Napenda kutoa maelezo kuwa katika shughuli za usajili, sio lazima watumishi wanaosajili wawe na taaluma ya sheria. Tayari Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini *(RITA),* kwa kushirikiana na TAMISEMI wamekubaliana kwamba kuanzia hivi sasa moja ya majukumu makuu ya maafisa tarafa itakuwa ni kushughulikia usajili. Hii ni kwa sababu tunataka kupeleka huduma hiyo karibu na wananchi ili watoto walio wengi na huduma hii iweze kuwafikisha wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu umuhimu wa kutafsiri sheria za nchi kutoka lugha ya Kiingereza na kuwa katika lugha ya Kiswahili, Wizara inatambua umuhimu huo na kila wakati tutakuwa tunahakikisha kwamba tunafanya kazi hiyo na Waheshimiwa Wabunge wametoa ushauri mzuri kwamba tushirikiane na Wizara husika katika kuharakisha au kuongeza kasi ya kutafsiri. Ni mategemeo yangu kwamba Serikali ni moja na kwa hivyo tutashirikiana na Wizara hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Tume ya Haki za Binadamu kutoweza kufungua matawi ama kuwa na Makamishna katika ngazi za Wilaya na hata Mikoa. Tume imefungua ofisi mbili za Kanda katika Mikoa ya Lindi na Mwanza katika mwaka wa fedha 2006/2007 na ina mpango wa kufungua ofisi nyingine nne za Kanda fedha zitakapopatikana. Ofisi ya Tume Zanzibar imeongezewa hadhi na sasa inaongozwa na Kamishna. Katika ofisi za matawi ya Lindi na Mtwara, ofisi hizo zinapaswa kuongozwa na Kamishna Msaidizi. Mchakato wa kuwaajiri Makamishna wasaidizi umekwishaanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, imetolewa hoja kuhusu suala la Kisiwa cha Ghana, Wilayani Ukerewe kutumia ngono ya kundi la wanaume kumfanyia mwanamke anapokosa katika jamii. Hii ni kuchukua sheria mkononi. Katika nchi ambayo inaheshimu utawala wa sheria hili halikubaliki na kwa sababu limeishaanza kutatuliwa, basi tutalifuatilia ili iwe funzo na wengine wasifanye hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu madai ya Serikali kutokutekeleza mapendekezo ya Tume ya Kurekebisha Sheria hususan sheria za mirathi na kanuni za mwenendo wa mashauri ya madai, kwa kawaida Tume inapokamilisha ripoti zake inazileta na inapozileta si zote zinashughulikiwa na Wizara ya Katiba na Sheria, kuna zingine zinahusu Wizara zingine. Nitajaribu kuwasiliana na Mawaziri wote ili kuona kwamba kila marekebisho yanapofanywa, basi tuchukue hatua za kuendeleza mchakato ili Sheria zije Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la elimu ya sheria, hili ni muhimu sana hasa katika mashauri ya madai. Kwa wale ambao kwa kweli kipato chao ni cha chini hawaelewi sheria na hawawezi kuwaweka mawakili. Kwa vyovyote vile hii inaathiri haki ya wananchi. Kwa hiyo, tutajitahidi sana kutoa elimu hiyo ili wananchi waweze kupata haki wanazozistahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Usalama wa Raia na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kushirikiana, tumekuwa tukifanya hivyo. Tutazingatia ushauri huo na tutaendelea kushirikiana kwa maslahi ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kuendeleza jitihada za kuzipatia usafiri Mahakama.Tumekuwa tukifanya hivyo, tutatumia mikakati mbalimbali kuona hilo linawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika**,** kuhusu kuanza ujenzi wa jengo la mahakama katika kiwanja kilichotolewa kujenga jengo la kudumu la Mahakama ya Rufani, **u**jenzi wa jengo hilo utafanyika chini ya Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria. Mahakama ya Tanzania lazima ipewe hadhi yake inayostahili. Mimi nina hakika jengo hilo likijengwa, basi na wao watajisikia kwamba ni mhimili wa tatu. Ujenzi huo umepangwa kuanza kutekelezwa kwa awamu kuanzia mwaka wa fedha 2007/2008. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimejitahidi, nakushukuru sana. Nimejaribu kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge na ninawashukuru sana wenzangu waliojibu. Nawaombeni sana mnipitishie mafungu hayo na wale ambao sijawataja nitawaingiza kwenye *Hansard.* Ahsanteni.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa naomba kuwakumbusha kwamba Wizara hii ina mafungu saba na kila fungu lina mafungu madogo kadhaa. Kwa mfano, fungu la 40 Mahakama lina *sub-vote* 16. Kwa hiyo, tuna kazi ndefu. Nitaomba mjitahidi kwenda kwenye lengo la kile unachohoji ili tuweze kwenda kwa wakati. Ahsante.

**Fungu 40 - Mahakama**

Kifungu 1001 – *Administration and General* … Sh. 12,956,883,500/=

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge**,** fungu hili linahusu Mahakama. Kwa wale wanaotaka mshahara wa Waziri hapa siyo mahali pake haupo hapa.

Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi na Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba. Basi tutaanza na Mheshimiwa Mohamed Missanga.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kupata ufafanuzi. Mheshimiwa Waziri alipokuwa anatoa majibu yake hapa, ameeleza vizuri namna ya kuboresha Mahakama.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge taja kifungu.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 1001. Mheshimiwa Waziri ameeleza vizuri namna ya kuboresha Mahakama.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge kifungu 1001 kwa vipi sasa?

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 1001.

**MWENYEKITI:** Ndiyo lakini sehemu gani? Maana yake baada ya hapo ndipo zipo zile kasma ndogo.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia sera.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge ukienda hapo utakuta 250100, 250300 ndiyo ninataka ulenge hapo. Naona huna.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalo swali mimi ukinisikiliza labda utanielekeza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, kama linahusu sera basi subiri tukifika kwenye *Vote* 41. Mheshimiwa Siraju Kaboyonga.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu linahusu sera ya Mahakama ya Biashara sijui kama ndiyo mahali pake hapa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge siyo hapa bado. Kwa kukusaidia tu Mahakama ya Biashara ngoja Katibu atusaidie hapo. Biashara ni fungu 64 utalikuta huko.

**MHE. KABUZI R. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *Vote* 40 progamu ya 10, *sub-vote 1001,* kifungu kidogo cha 250300, *employment allowances*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge endelea.

**MHE. KABUZI R. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia kwangu nilichangia mambo mawili kuhusu *allowances* wanazopewa wazee wa Mahakama, wanapewa shilingi 1,500 mpaka kesi iishe. Sasa ile fedha haitoshi na wakati mwingine wanaingia kwenye vishawishi vya kula rushwa. *(Makofi)*

La pili, wazee hao hao katika Jimbo langu labda sehemu zingine hawapewi posho zao kwa muda muafaka kwa sababu, sasa hivi wana miaka mitatu hawajalipwa hizo posho. Nilimwomba Waziri anisaidie kueleza hiyo kama hao wazee wanawa-*treat* vipi. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, umepenya tu kwenye *employment allowances* ambayo haihusiki, lakini sasa kwa sababu ni swali umeliuza, naomba Mheshimiwa Waziri aweze kutoa ufafanuzi.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wazee wa Mahakama kwa kweli ni malalamiko ya muda mrefu na kwa kweli Mahakama lazima tulifanyie kazi. Kwanza, posho yenyewe ni ndogo na mpaka wanapomaliza kesi.

Kwa hiyo, kama kesi inamalizika miaka miwili maana yake ni mpaka wangojee hiyo kesi iishe. Ni suala ambalo linahitaji mabadiliko. Tutaangalia ni njia gani ambayo tutafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu ucheleweshaji tutahakikisha kwamba hatutaendelea kuchelewesha pale ambapo kwa kweli si lazima kwa sababu ni kweli kabisa inawashawishi. Lakini naomba niwaeleze wazee wote wanaohusika wa Mahakama kwamba wanapoteuliwa kuwa wazee wa Mahakama kwa kweli wanapewa heshima kutokana na busara waliyonayo ndani ya jamii na siyo kila mmoja anayepewa kazi hiyo. Kwa hiyo, nawaomba watangulize dhamana pamoja na kwamba Serikali inasikia kilio chao. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2001- *High Court* … … … … … … … … … Sh.674,178,600/=
Kifungu 2002 - *Court of Appeal Dar es Salaam* … … … Sh.604,869,800/=
Kifungu 2003 - *Arusha Zone* … … … … … … … … Sh. 842,958,500/=
Kifungu 2004 - *Dar es Slaam Zone*… … … … Sh. 2,014,565,700/=
Kifungu 2005 - *Dodoma Zone* … … … … … … … … Sh. 817,107,200/=
Kifungu 2006 - *Mbeya Zone* … … … … … … … … Sh. 1,166,795,200/=
Kifungu 2007 - *Mtwara Zone* … … … … … … … … Sh.697,685,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2008 – *Mwanza Zone* … … … … … … Sh. 1,336,843,600/=
Kifungu 2009 - *Tabora Zone* … … … … … … … Sh.1,667,342,600/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2010 - *Tanga Zone* … … … … … … … … … Sh. 562,712,200/=

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote* 40, *Sub-vote* 2010 nazungumzia kipengele 250300 *employment allowances.* Ukiangalia pale mtiririko utaona kwa mwaka huu zimepungua yaani zaidi ya nusu ikilinganishwa na mwaka jana na hata huko nyuma. Lakini safari hii imekuwa ni ndogo mno. Sasa ukizingatia shughuli zilizopo kwa kweli nilikuwa naomba kupata ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile kipengele 260900 hapo kwenye *Travel and Subsistence* ukizingatia sisi Mahakimu wetu wapo kwenye Wilaya tofauti. Sasa hizo shilingi 3,400,000/= kwa mwaka mzima kwa *travel* inanipa wasiwasi. Naomba kupata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Ahsante.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, maswali yake aliyouliza kuhusu *employment allowances*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *employment allowance* ni *allowance* kwa hiyo inatokea pale ambapo hiyo *allowance* inatakiwa kulipwa. Katika kuangalia vipaumbele kwa sababu mwaka huu ni Bajeti ambayo tumetoa vipaumbele sana, tumeona kwamba eneo hilo na kutokana na uzoefu huko nyuma ni eneo ambalo pengine ingebidi tupunguze kutokana na ufinyu wa Bajeti.

Kuhusu Mahakimu wetu wanakwenda kutoka kituo hadi kituo na kwa hivyo wanahitaji hii *allowance*. Ni kweli lakini hatukuwa na la kufanya kutokana na ufinyu wa Bajeti lakini Mahakama itaangalia namna ambavyo itaweza kupunguza hiyo adha ya Mahakimu wetu ambao inabidi waende kwenye vituo vingine kutokana na kuwa wachache.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2011 – *Primary Courts*… … … … … … Sh. 6,418,761,400/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*
Kifungu 2012 *District Courts*… … … ... ... ... ... ...Sh.4,739,140,000/=

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kifungu cha 2012, *Item* 270100 *Maintenance - Physical Infrastructure*.

Katika mchango wangu nimeongelea kwamba Mahakama ya Wilaya Biharamulo ipo katika gofu ya iliyokuwa wodi ya wazazi enzi za mkoloni. Sikuambiwa kuna mpango gani? Pia nikasema Hakimu wa Wilaya anapanga nyumba mbovu mbovu tu na nikasema ni hatari anaweza akapanga nyumba ya wapika gongo akapata shida. Sasa sikujua na hakuniambia Mheshimiwa Waziri haya maswali yangu anayajibuje? Nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ufafanuzi kama hela za Biharamulo nazo majengo kurekebishwa muhimu.

**WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Phares Kabuye kunikumbusha umuhimu wa Mahakama ya Biharamulo kukarabatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia sehemu ya Wilaya ya Biharamulo kuna Mahakama moja ambayo inakarabatiwa, sasa tunajaribu kuona kila mahali kwamba tunafanya linalowezekana.

Kwa hivyo, kama mwaka huu wa fedha hatukuweza kuweka hayo, Mahakama ambayo ameitaja basi mwaka ujao wa fedha tutafanya hivyo lakini akubaliane na mimi kwamba Biharamulo hatujaisahau kwa sababu kuna Mahakama moja ambayo inakarabatiwa.

**MWENYEKITI:** Dawa moja Mheshimiwa Waziri ni kuwatembelea. Bado Mheshimiwa Phares Kabuye?

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu, lakini Waziri afahamu kwamba sasa hivi Biharamulo imetoa Wilaya mbili. Zahanati inayokarabatiwa ni kituo cha Buselesele. Mahakama ya Wilaya bado, kwenye Wilaya ya Biharamulo hakuna jengo lolote linalokarabatiwa na kabla sijaja hapa nilizunguka kila sehemu sikuona mahali ambapo Mahakama ya Biharamulo inakarabatiwa, naomba ufafanuzi zaidi.

**MWENYEKITI:** Lakini Waziri amekwisha fafanua na ameahidi ama yeye ama Naibu Waziri kuja kuona hali halisi, nadhani Mheshimiwa Phares Kabuye uvute subira kidogo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2013 – *Kagera Zone* … … … … ... ... Sh. 672,658,300/=
Kifungu 2014 – *Ruvuma Zone*… … … … ... ... ... ... ..Sh.712,588,000/=
Kifungu 2015 – *Moshi Zone* … … … … … ... ... ... ... Sh. 684,153,400/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 41 – Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba**

Kifungu 1001 – *Administration and General* … … Sh.3,322,294,200/=

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *Vote 41,* programu ya 10, *sub vote* 1001, kifungu kidogo 250100, Mshahara wa Waziri, hili ni suala la sera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya matatizo yetu yaliopo katika Magereza yetu ni msongamano wa mahabusu na wafungwa. Lakini baadhi ya hao watu walio katika Magereza ni watuhumiwa ambao wamekaa kwa muda mrefu. Lakini ukiangalia vile vile matatizo waliyonayo ni kwamba labda wana mashtaka madogo ambayo hata kama wangekutwa na hatia kifungo chao ni kidogo kuliko muda ambao wameshakaa katika Magereza, je, Serikali iko tayari kuwaachia watu hawa?

**WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Charles Kajege kwa kutaka ufafanuzi kuhusu mahabusu na msongamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msongamano wa Mahabusu katika Magereza yetu ni jambo ambalo Mahakama kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wamejitahidi sana kulifanyia kazi na katika kufanya hivyo tumepunguza mahabusu wengi. Lakini ni kweli kama anavyosema kuna wengine ambao wana makosa madogo ambao wanabaki kule kwa muda mrefu na ambao pengine wakitoka au kesi zao zikienda haraka basi msongamano utapungua. Majaji na wale wote wanaohusika na kesi wamekuwa wakitembelea Magereza yetu na wanapokuwa pamoja na kweli kwa maagizo ya Mheshimiwa Jaji Mkuu aliyestaafu wamejitahidi sana kutembelea Magereza na kuona wale ambao wana kesi ndogo ndogo kuachiwa, ni imani kwamba Mahakama ya Tanzania itajitahidi kufanya mchakato huu wa kutembelea Magereza ili kuwaondoa wale ambao si lazima wabaki Magerezani. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, *vote 41,* programu ya 10, kifungu 250100, Mshahara wa Waziri, mambo mawili ya sera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri anajibu hoja alielezea suala la Mahakama ya Katiba kwamba hakuna jambo ambalo lilishababishwa kuwekwa na Mahakama hiyo hivi sasa. Nchi yetu inazo Katiba mbili inayo Katibu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na inayo Katiba ya Zanzibar. Kwa masuala ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Watanzania wamepewa haki ya kwenda mpaka *Court of Appeal.* Kwa masuala ya Katiba ya Zanzibar, Wazanzibari hawaruhusiwi kwenda kwenye *Court of Appeal* iliyopo hivi sasa, ndiyo Katiba inavyosema. Kwa hivyo Katiba yaani Mahakama ya Rufaa hairuhusiwi kutoa tafsiri yoyote ya Katiba ya Zanzibar. *(Makofi)*

Sasa mimi naomba ufafanuzi juu ya suala la sera, je, haionekani kwamba wakati muafaka kuwa na Mahakama ya Katiba ya Nchi ambazo Katiba zote mbili zingepata nafasi ya kuweza kutolewa tafsiri katika Mahakama hiyo wakati Watanzania Zanzibar sasa hawapati hiyo haki. Ukisoma Katiba ya Zanzibar yapo mambo kabisa yanasema hayawezi kwenda kwenye Mahakama ya Rufaa. Hilo lilikuwa la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, Waziri wakati anajibu hoja juu ya suala la Mahakama ya Kadhi Mkuu, alisema kwamba linafanyiwa kazi na mimi namshukuru sana kwa maelezo hayo. Nilitaka tu kupata ufafanuzi kwamba Zanzibar toka mwaka 1800 Mahakama ya Kadhi Mkuu imekuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Zanzibar baba yangu amekuwa Kadhi katika Mahakama na Jaji Mkuu aliyeteuliwa hivi sasa amefanya naye kazi sana pamoja na kina Jaji Mapigano wote walifanya kazi. Kwa hivyo, kuna *experience* kubwa sana imekuwa *gained* katika kipindi chote hicho na hakuna matatizo. Lakini kubwa zaidi Zanzibar ambapo kwa asilimia 99 ni Waislam, Jaji Mkuu amekuwa Mkristo, Mwanasheria Mkuu amekuwa Mkristo wala hakujatokea tatizo lolote. Kenya wenzetu vile vile wana Mahakama ya Kadhi hakujatokea tatizo, huu wasiwasi ambao upo wa upande wa pili ambao Waziri ameuelezea ni wasiwasi gani atufafanulie zaidi. Ahsante sana.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimjibu Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed swali lake la kwanza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed amezungumzia juu ya Wazanzibari kupata ruhusa ya kuweza kupeleka mambo yanayohusiana na Katiba ya Zanzibar kwenye Mahakama ya Rufaa ya Tanzania. Ningemshauri kwamba kama ikiwezekana aliwasilishe suala hilo kule panapohusika yaani Zanzibar ili waweze kulifanyia kazi. Sisi tupo tayari kusaidia maoni namna ya kukamilisha huo mchakato wa kuweza kuwawezesha wenzetu wa Zanzibar kuweza kuomba rufaa ya mambo yao kuja kwenye Mahakama ya Rufaa ya Tanzania. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Lakini yeye hoja yake anavyodai yeye ni kwamba Katiba ya Zanzibar haimruhusu Mzanzibar kwenda Mahakama ya Rufani Tanzania, ndiyo anavyosema.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiit, ndiyo nasema kwamba haya mambo yanahusu wao kule wenzetu wa Zanzibar wayafanyie kazi yaani kwenye Katiba yao wayafanyie kazi kule ili Katiba yao iweze kubadilishwa. Mtu aweze kuomba rufaa kuhusiana na jambo la Katiba Zanzibar kuja kwenye Mahakama ya Rufaa ya Tanzania.

**MWENYEKITI:** Aaah, lakini hapa tuko kama Bunge la Jamhuri ya Muungano hatuwezi? Tunaomba kweli tu yaani mwananchi akitoka hapa aelewe anafanya nini isiwe hivyo tu akienda kule ataambiwa Katiba hairuhusu.

**WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza na kama alivyojibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni kwamba Bunge hili kwa mujibu wa Katiba hii haina uwezo na Katiba ya Zanzibar. Lakini kwa madhumuni haya kwamba kama na sisi tunaweza kulifanyia kazi hakuna matatizo hii ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**MWENYEKITI:** Hiyo nadhani ni vizuri. La Kadhi nataka kusema hivi Waziri wala usisumbuke, umekwishatupa taarifa kwamba mwezi Oktoba taarifa kamili ya Tume ya Kurekebisha Sheria itatolewa. Mimi namwelewa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed ni mtu wa subira kweli, ni vizuri tusubiri yatoke hayo. Ni kweli kama jambo linasubiri miezi miwili kweli tutumie muda wa Bunge kujaribu kulitanguliza hivi sasa. Mimi nadhani limekaa vizuri tu hilo.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na hili la pili la Kadhi kuvuta subira. Ila naomba tu Serikali nafikiri ingeweka bayana. Hapa tunazungumzia raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ndiyo maana mimi nikasema kwamba …

**MWENYEKITI:** Kwa lile la kwanza

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mmoja anapata haki mwingine hapati haki kwa sababu ya matatizo ya Katiba. Ndiyo katika Katiba hiyo ya Jamhuri ita-*provide section* ya kusema kutakuwa na Mahakama ya Katiba ili kuzifanya zote ambazo ziko Tanzania hii ziweze kushughulikiwa. Sasa mimi nikaona hilo waliangalie na namna gani tutaweza kulitatua. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Nadhani ushauri huo umefika.

**MHE. FATMA M. MAGHIMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana *vote 41,* program 10, *sub-vote 1001,* kifungu kidogo 25011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mjadala wangu leo nilipendekeza kuwa Muswada wa Sheria ya Serikali za Mitaa uletwe sasa kwa sababu hapo kuna *vacuum*. Serikali za Mitaa zinaanzishwa kwa mujibu wa Katiba lakini Katiba haikusema kitu juu ya watu hawa wataondolewaje kama wakileta matatizo. Tulishuhudia katika awamu ya tatu Mheshimiwa Waziri Mkuu aliivunja Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam akaunda Tume ya Jiji. Hapo ni ukiukwaji wa Katiba halafu vile vile hivi karibuni Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa mmoja jina lake namjua lakini sijui inaruhusiwa kumtaja alishafukuza wanavijiji wetu 11, kwa sababu hakuna kitu katika Katiba kinachosema kwamba hawa wamewekwa hivi na Katiba lakini haikusema Katiba kama itaondolewaje kwa hivyo ikabidi wafukuzwe na wakawa hawana cha kufanya.

**MWENYEKITI:** Hebu fafanua hilo, kufukuzwa maana yake nini?

**MHE. FATMA M. MAGHIMBI:** Viongozi wa vijiji na hawa…

**MWENYEKITI:** Aliwavua madaraka viongozi wa vijiji?

**MHE. FATMA M. MAGHIMBI:** Eheee !!!!

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu la pili linalohusu Kisiwa cha Ghana, nimesikia jibu nimefurahi sana. Lakini katika shughuli zake atakazokwenda kuzifanya Mheshimiwa Waziri nina ombi na mimi tufuatane nione hao wanaume wa Kisiwa cha Ghana wana sura gani? Wanawaadhibu wanawake anapokosa mwanamke katika jamii anaadhibiwa kwa ngono, hasa huyu Jaji anayetoa hukumu hii ningependa na mimi niende nifanye utafiti wa kisheria.

**MWENYEKITI:** Wewe huogopi wewe? Kwa ziara ya aina hiyo nitamwomba Naibu Waziri ndio ufuatane maana yake. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Fatma Maghimbi, kwa kunikumbusha hayo ambayo kwa kweli kutokana na muda sikuweza kuyafikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni suala la Muswada kuletwa ili kuweza kutekeleza mafungu ya Katiba yetu, basi nitawasiliana na Waziri wa TAMISEMI yupo hapa amesikia tutaangalia ni vipi basi hii sheria ikidhi haja ya sasa hivi.

Kuhusu kwenda Ghana kama Mheshimiwa Mwenyekiti alivyosema tutakwenda wote watatu pamoja na Mheshimiwa Mathias Chikawe. *(Makofi)*

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, langu sio kubwa ni *vote 41,* programu 10, *sub vote 1001* na kifungu kidogo zaidi 250100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kitabu cha hotuba cha Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 58 jedwali namba 7 wameonesha pale orodha ya majengo ya Mahakama za Mwanzo ambayo yamejengwa na mengine kukarabatiwa. Sasa langu ni maelezo tu kwamba nilitaka tu ufafanuzi kwamba katika *column* inaonyesha kwamba Mahakama zilizojengwa yako majengo 15 tu na katika majengo hayo lipo jengo ambalo katika mchango wangu nilimwandikia na limeonyeshwa pale Babati - Bonga. Jengo hili ni muda mrefu limejengwa, limekaa sasa kwa kweli ni miaka ya kutosha hakuna Hakimu wala nini. Sasa *priority* ya Wizara ni nini kwa majengo ambayo tayari yamejengwa na hakuna Hakimu na yako 15 tu ninavyoyaona pale ambayo tayari yamejengwa. Sasa majengo hayo baadaye yanaweza yakaharibika au watu wakayatumia kwa namna nyingine. Kwa hiyo, nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi ni lini basi watahakikisha kwamba pale pana Hakimu. Ahsante.

**WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa hii fursa. Kila ninapokwenda Wilayani kwangu Hanang napitia Bonga na Bonga ni eneo ambalo vile vile mimi nina maslahi nayo. Kwa hivyo, ni kweli na wananchi wenyewe kila nikipita wananikumbusha hilo kwa sababu tumeajiri na tunaendelea kuajiri Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo tutatilia maanani kwamba Bonga wanapata Hakimu.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nipo hapo hapo kwenye *vote 41, sub vote 1001*, kifungu cha 250100. Lakini kwa sababu ulikwishatoa maelezo kwamba tuvute subira suala la Ofisi ya Kadhi. Mimi nakubaliana na kauli hiyo kwamba tuvute subira lakini nina ushauri. Wakati Serikali ikifanyia kazi suala hili naomba iangalie sana Katiba. Katiba kama nilivyosema kwamba Tanzania haina dini lakini Watanzania wana dini, hilo la kwanza.

Lakini la pili naiomba Serikali, ni ushauri wangu isiingie gharama ya kuunda Tume ya Kurekebisha Sheria katika suala la dini na hilo walifikiri tena. Lakini la tatu, naiomba tena na naishauri Serikali isielekee katika kutaka kujenga Makanisa au Misikiti katika suala la Kadhi. Hili ni suala liko kwenye *Quran* na *Quran* haitiwi mikono. Ushauri wangu ulikuwa ni huo.

**MWENYEKITI:** Nadhani na Tume pia imesikia, wataendelea kuangalia lakini ni wajibu wa Serikali kutafuta ushauri jambo hili linazungumzwa na wananchi wote na wana maslahi nalo kwa namna mbalimbali. Ni sahihi kabisa kwa Serikali kutafuta ushauri kutoka kwa Tume. Niseme tu hawafungwi na ushauri huo. Kwa hiyo

watakaoleta nina hakika litakuwa linajibu matarajio ya wananchi wote lakini pia linakwenda na msingi wa Katiba.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *vote 41,* programu 10, *sub vote 1001,* mshahara wa Waziri, sera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilimwomba Mheshimiwa Waziri anipe ufafanuzi wa mambo mbalimbali hasa kuhusu mambo haya ya *RITA*. Pamoja na maelezo ambayo Waziri ameyatoa ningependa nipate ufafanuzi mambo machache kwa bahati mbaya hapa hakuweza kuyatolea ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kwamba *RITA* ni wakala wa Serikali ambayo ipo chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Lakini miongoni mwa kazi zake nyingi ni kufilisi taasisi za kibinafsi na za umma. Wakati huo huo kuna Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma ambayo ni pia ni *PSRC* nayo vile vile inafilisi Mashirika ya Umma. Sasa naona hizi kazi mbili ambazo zimefanana katika Taasisi mbili tofauti ningependa Mheshimiwa Waziri anieleweshe kuna tofauti gani baina ya ufilisi huu wa *PSRC* na *RITA*.

Lakini lingine katika kueleza kazi za *RITA,* Mheshimiwa Waziri alisema kwamba linashughulikia vile vile daftari la wapiga kura jambo ambalo nafikiri ni muhimu katika Mfumo wa Vyama Vingi kwamba inaonyesha kuwa Tume ya Uchaguzi haifanyi vizuri tumesoma kwenye vyombo vya habari kule Tunduru karibu watu 11,000 kupiga kura kwa hivyo hili ni jambo muhimu na ni zuri sana. Lakini swali langu ni kwamba sikuona katika kitabu hiki wapi hawa *RITA* wamewezeshwa katika Bajeti hii. Sasa kama ipo Mheshimiwa Waziri nitaomba anifahamishe. Ahsante.

**WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa Mheshismiwa Salim Hemed Khamis kupata ufafanuzi kuhusu *RITA*. *RITA* ni wakala mpya na kwa hivyo watu watataka kujua zaidi juu ya *RITA*. Sasa *RITA* ina jukumu la ufilisi. *PSRC* ambapo na mimi niliwahi kufanyia kazi, kazi yao ni kubinafsisha Mashirika yaliyokuwa ya umma kuwa Mashirika binafsi. Kwa hivyo, kuna tofauti ya wazi kabisa kati ya *RITA* na *PSRC Bankruptcy*. Wale wengine wana-*privatised.*

Kuhusu Tume ya Uchaguzi, *RITA* ni wakala wa Serikali. Serikali inaiwezesha kufanya kazi na kadri inavyosimama kwa miguu yake siku moja itakuja itajiendesha yenyewe lakini si kwa faida ila kwa kufanya yale ambayo Serikali haiwezi kuifanya katika *bureaucracy* yake.

Kuhusu Tume ya Uchaguzi kutofanya kazi vizuri kule Tunduru kutokana na usajili nafikiri wa wapiga kura. Ni kweli *RITA* ina uhusiano wa karibu sana na usajili. Kwa sababu inakuwa rahisi yule ambaye anajulikana ni Mtanzania kwa sababu ya kuwa ameandikishwa wakati wa kuzaliwa au wakati mwingine wowote inakuwa rahisi kusajiliwa kuwa kama mpiga kura umri unapofika. Kwa hivyo kadri *RITA* inavyofanya kazi yake kwa uzuri zaidi basi na Tume hiyo itakuwa imerahisishiwa kazi yake vizuri zaidi tutashirikiana na Tume ya Uchaguzi.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwamba Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba alishauliza sehemu ya kwanza ya swali langu kuhusu posho za wazee wa Mahakama za Mwanzo.

Sasa swali la pili langu ni kwamba baada ya kujibiwa kwamba suala la kucheleweshа zile posho huko nyuma, wazee hawa walikuwa wanalipwa posho na baadaye ikaelezwa kwamba wazee hao watalipwa posho baada ya kumaliza kazi. Lakini baadhi ya wazee ambao wamenijia wanasema hata pale ambapo wanamaliza kazi inawachukua muda mrefu kupata hizo posho zao, sasa utaratibu ni upi ni kuwalipa posho baada ya kila mwezi au ni kuwalipa posho kwa kipande cha kazi ambacho wamekimaliza. Ahsante.

**WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama inavyojitokeza kwamba suala la posho ya wazee wa Mahakama inaleta utata. Nitaifuatilia na Mahakama ya Tanzania kuona tunafanya nini ili kurahisisha kazi ya hao wazee wa Mahakama. Lakini narudia tena kwa kweli tutajitahidi sana kama Serikali na wazee hao wachukue hiyo kazi kama dhamana wakati sisi tunatambua matatizo yao.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fungu namba 41 programu 10, *sub-vote* 1001, kifungu kidogo 250100 suala la sera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuanzishwa kwa *Commercial Court* ilikuwa kwamba kasi ya kuendesha kesi hasa za kibiashara iongezeke sana, naipongeza Serikali kwa kufanya hivyo. Lakini tuna tatizo hapa kwamba kesi za mabenki na wale wanaowadai zinapopelekwa kwenye *Commercial Court* kwa kuwa *aspect* ya *mortagage* ambayo inahusiana na masuala ya *land* zinahamishwa *Land Court.* Kule *Land Court* hakuna *speed* inayofanana na *Commercial Court.* Kwa hiyo, kesi za mabenki zinaendelea kuchelewa na kwa kufanya hivyo zinaathiri utendaji wa Mabenki kwa maana ya faida zao na fedha nyingi zinafungwa katika mikopo ambayo tunaita *non performing assets*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili kwa kiasi kikubwa linakwenda mpaka kwenye Mahakama ya kawaida, mabenki yetu kesi kwenye Mahakama za kawaida haziendi na kwa maana hiyo zinaathiri *performance* ya mabenki kwa maana ya *non performing assets*. Nilikuwa naomba ufafanuzi wa kisera juu ya hili.

**WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli madhumuni mazima ya kuanzisha *Commercial Court* ni kuongeza kasi ya usikilizaji na kutoa maamuzi juu ya mashauri ya biashara. Mimi naipongeza Mahakama ya Biashara kwa sababu ina ufanisi wake ni takriban asilimia zaidi ya 90. Sasa inapotokea masuala kama haya ya Mahakama ya Ardhi kuchelewesha tena itabidi kwa kweli kufuatilia ili kuona ni namna gani tutafanya basi huku ambako kunaleta matatizo tutatatua namna gani pamoja na kesi ambazo ziko kwenye Mahakama ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeambiwa kwamba kwa wafanyabiashara wa kawaida kupeleka kesi zao Mahakama ya Biashara napo pia ni taabu kwa sababu gharama yao ni ya juu na kwa hiyo mara nyingi wanaenda kwenye Mahakama za kawaida. Suluhisho la kudumu ni kuhakikisha Mahakama zetu zote zinafanya kazi kwa ufanisi, lakini kwa hili nitafuatilia.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nimebakiza dakika tano kabla ya kufikia wakati wa kutumia Kanuni ya 81(vi) na bado nina wasemaji wawili ili kuwatendea haki, natumia mamlaka yangu chini ya Kanuni ya 126 kuwa wote wawili waseme kwa kifupi na wapate majibu. Kwa hiyo, nitaanza na Mheshimiwa Benson Mpesya halafu Mheshimiwa James Musalika halafu Mheshimiwa Waziri aweze kutoa ufafanuzi.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote 41,* Programu ya 10, *sub vote 1001,* kifungu kidogo cha 250100. Naomba ufafanuzi tu. Katika ufafanuzi wake Mheshimiwa Waziri juu ya posho za wazee wa mabaraza ameeleza kwamba wanaandaa utaratibu pamoja na Mahakama kuhakikisha kwamba linakuwa si tatizo. Ningependa kuuliza kwamba je, wasingetumia nafasi hii sasa kulipa kwanza malimbikizo yote ambayo wanadai wazee hawa ili waangalie utaratibu mwingine ambao utakuwa mzuri? Hilo la kwanza.

La pili, kumekuwa na utaratibu wa baadhi ya Mahakimu kutembelea Mahakama mbalimbali na katika kuzitembelea hizi Mahakama wamekuwa wakitumia fedha zao za mikononi kwa ajili ya usafiri, malazi na kadhalika. Lakini Mahakimu hawa wamekuwa hawalipwi hizo fedha kiasi kwamba wengine wanadai mpaka mamilioni sasa hivi. Je, isingekuwa vyema basi Mahakimu hawa wakawa wanapewa fedha ya usafiri na kila kitu na nili Serikali itamaliza tatizo hili la kulipa malimbikizo kuliko kuwakopa Mahakimu hawa wanyonge?

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, ni *vote 41 programme 10,...*

**MWENYEKITI:** Endelea na hoja, hiyo tunaielewa wote.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia kwa maandishi nilitaka ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri juu ya matatizo ya kushughulika Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na Kata; na katika majibu yake amesema kwamba Mabaraza ya Ardhi na Kata na yote yale yapo chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na kwamba watashauriana na Waziri wa Ardhi kuhusu matatizo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina mfano kwenye Jimbo langu lipo Baraza moja la kata moja ambalo limekuwa kero sana na mamlaka za huko chini zimeshafanya kila namna ya kuwakataa lakini Afisa Ardhi pale wa Wilaya limemshinda, Mwanasheria wa Halmashauri limemshinda na alipata *consultation* kutoka Mkoani hatukupata jibu. Wananchi wamekata tamaa, kwa majibu ya Waziri linaweza kuchukua miezi sita au mwaka mmoja. Ningependa kupata ufafanuzi je, wananchi au mamlaka husika zifanye

nini kuhusu Baraza hili linalolalamikiwa kutuhumiwa kwa rushwa na hivyo wananchi hawalitaki? Baraza la Kata ya Nyang'hwale.

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Benson Mpesya na Mheshimiwa James Musalika.

Kuhusu malimbikizo ya posho ya Wazee wa Mabaraza na malimbikizo ya fedha zilizotumika kwa ajili ya Mahakimu kwenda kusikiliza kesi kwenye vituo tofauti na vile vya kwao, ni kwamba ikithibitishwa taratibu zitawekwa za kuwarudishia kwa sababu ni haki yao na pale ambapo Mahakama itapata hela na tutajitahidi kuona kwamba wanalipwa.

Sasa kuhusu utaratibu mpya kama nilivyoeleza tutajaribu kuona ni namna gani kwa sababu hatuwezi kuona tatizo linaendelea kuwepo halafu kuna viongozi tusilitatue. Tutafanya kila linalowezekana kuona ni namna gani hili la Wazee linapatiwa utatuzi.

Sasa kuhusu matatizo ya Mabaraza ya Ardhi, yako chini ya TAMISEMI na ni kweli kwa sababu mimi ni Mbunge wa Jimbo, kuna matatizo makubwa katika vijiji na ngazi ya Kata na hata Wilaya.

Lakini kwa hili linalohusu rushwa, namna ya kushughulikia ni kwamba yupo Bwana *DC*, yupo *DED* na yupo Halmashauri. Lakini kwa wale ambao wanamashauri yao wakiona katika ngazi moja hayawezekani wakate rufaa basi ngazi ya juu na hadi kufikia kwenye Mahakama Kuu pamoja na kwamba nilisema kwamba kesi nyingi sasa zinakimbilia Mahakama Kuu na kusababisha msongamano kwa sababu hizi ngazi za chini hazifanyi kazi vizuri. Tutashirikiana na TAMISEMI na Wizara ya Ardhi kuona kwamba tunajaribu kutatua matatizo haya ambayo yapo kwenye ngazi za chini.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Baraza hilo la Nyang'hwale kama maelezo ya Mheshimiwa Mbunge aliyoyatoa hapa ni sahihi tunachukua hatua mara moja. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaingia katika utaratibu wa Kanuni ya 81 kanuni ndogo ya (6) ambayo tutapitia mjadala bila mjadala wowote.
Kif. 1002 *Finance and Accounts* … … … … ... ... sh. ... 309,486,800/-
Kif. 1003 *Policy and Information Service*.. ... ... ... ... ...sh.470,728,700/-
Kif. 2001 *Administrator General* … … … … ... ... ... ..sh. 680,569,700/-
Kif. 2002 *Public Prosecution* ... ... ... ... ... ... ... ... ... sh. 3,438,228,800/-
Kif. 2003 *Legislative Drafting* … … … … … ... ... ...sh. 534,597,300/- Kif. 3001 *Civil and International Affairs* … … ... ... ... sh. 702,008,700/-
Kif. 4001*Constitution Affairs* … … … …. ... ... ... ... sh. 571,044,500/-

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

**Fuungu 55 - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

Kif. 1001 *Administration and General*... ... ... ... ... ... sh.1,183,321,900/-
\Kif. 1002 *Finance and Accounts* … … … … ... ... ... ...sh.72,354,700/-
Kif. 1004 *Legal Services*… … … … .. ... ... ... .. ... ... ..sh. 174,227,800/-
Kif. 2001 *Administrative Justice* … … … ... ... ... ... sh. 330,404,000/-
Kif. 2002 *Human Rights* … … … … ... ... ... ... ... ... ...sh. 266,540,900/-
Kif. 2003 *Research and Documentation* … … ... ... ... sh. 117,950,600/-
Kif. 2004 *Public Education and Training*… … ... ... ... sh. 214,039,700/-
Kif. 3001 *Zanzibar Office* … … … … ... ... ... ... ... ... sh. 253,340,400/-

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 59 - Tume ya Kurekebisha Sheria**

Kif. 1001 *Administration and General*... ... ... ... ... ... sh. 835,376,000/-

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 60 - Mahakama ya Kazi**

Kif. 1001 *Administration and General*... ... ... ... ... ... ..sh. 634,655,900/-
Kif. 2001 *Arusha Zone*… … … … … … … .... ... ... ... sh. 47,131,900/-
Kif. 2002 *Dar es Salaam Zone* … … … … … ... ... ...sh. 65, 963,200/-

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 64 - Mahakama ya Biashara**

Kif. 1001 *Administration and General*... ... ... ... ... ... sh. 855,005,000/-

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 90 - Mahakama ya Ardhi**

Kif. 1001 *Administration and General*. ... ... ..sh.839,947,000/-

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati bili Mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 40 -Mahakama**

Kif. 1001*Administration and General*... ... ..sh.1,225,000,000/-
Kif. 2001 *High Court*… … … … .... ... ... ... ...sh. 858,000,000/-
Kif. 2002 *Court of Appeal Dar es Salaam*… …sh.300,000,000/-
Kif. 2011 *Primary Courts* … … … … … sh. 1,000,000,000/-
Kif. 2012 *District Courts* … … … … … ... sh. 300,000,000/-

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 41 - Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba**

Kif. 1001 *Administration and General*... ... ... ... ... ... ... ...sh. 0/-
Kif. 1003 *Policy and Information Service*… … ... ... ... ... ... ... ...sh. 12,565,409,800/-
Kif. 4001 *Constitutional Affairs* … … … …sh. 250,000,000/-

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 55. TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA.**

Kif. 1001 *Administration and General* ... ... ... .. shs 119,115,000/-

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati bili Mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 60. MAHAKAMA YA KAZI**

Kif. 1001 *Administration and General* ... ... ... .. shs 552,370,000/-

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati bili Mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 64. MAHAKAMA YA BIASHARA**

Kif. 1001 *Administration and General* ... ... ... .. shs 388,000,000/-

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati bili Mabadiliko yoyote)*

*(Bunge Lilirudia)*

**Taarifa ya Kazi ya Kamati.**

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2007/2008 , Kifungu kwa Kifungu au kwa pamoja na Kuyapitisha bila Mabadiliko. Hivyo naomba kutoa Hoja kwamba Makadirio hayo sasa yakubaliwe na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja, Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba kwa Mwaka 2007/2008 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo machache. Kwanza asubuhi ilitolewa taarifa kuhusu Mkutano wa Mheshimiwa Rais atazungumza na wananchi wa Dodoma kwa ule utaratibu wa kila mwezi. Sasa kuna Mabadiliko *Press Secretary* wa Rais ameandika ifuatavyo; nanukuu.

Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete atalihutubia Taifa kwa kuzungumza na wananchi wa Mkoa wa Dodoma siku ya Jumatano Agosti Mosi badala ya kesho Julai 31. Mabadiliko hayo yanatokana na kuendelea kwa vikao vingine vinavyomhusu. Mazungumzo kati ya Rais na wananchi yatafanyika katika Ukumbi wa Kilimani hapa Dodoma Saa Kumi Jioni na kurushwa moja kwa moja na Televisheni ya Taifa na Redio Tanzania Dar es Salaam. Rais Anatarajiwa kuelezea na kutoa ufafanuzi wa mambo muhimu ambayo hivi sasa yanagusa mwananchi katika maisha yake ya kila siku. Mwisho wa kunukuu.

Kwa hiyo mtaona hili ni jambo sisi Wabunge ndiyo linatuhusu na mnaalikwa kuwepo nafasi zenu zitakuwepo kuweza kumsikiliza Mheshimiwa Rais. Kiswahili cha sasa wanasema Live.

Tarehe 4 Agosti, 2007, Jumamosi ijayo, kutakuwa na Mechi baina ya Timu ya Waheshimiwa Wabunge, subirini msikilize mpinzani mwenyewe, timu ya Shirika la *NSSF* kugombea Kombe la *NSSF*. Natoa tangazo hili mapema ili mazoezi yashike kasi. Kwa sababu hakuna faida ya kusubiri tukawatangazia Ijumaa halafu mkawa mnaanguka anguka hovyo siku ya Jumamosi. *(Kicheko)*

Kwa hiyo Mheshimiwa Mohammed Rajab nakuomba sana sasa mazoezi yawe mazuri, mazito ya kitaalam. Mimi kama Mgeni rasmi nitapenda sana nikabidhi kombe kwa Kapteni wa Timu ya Bunge. *(Makofi)*

Naomba Waheshimiwa Wabunge wote tuiunge mkono timu yetu na tuhudhulie mazoezi, tuangalie tuwakosoe na kikubwa zaidi siku ya mechi tuwepo Jamhuri Stadium ili kuweza kuwashangilia na kuwapa moyo. Tunatakiwa pale saa kumi siku ya Jumamosi.

Waheshimiwa Wabunge kesho Jumanne tarehe 31 ni zamu ya Hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na kesho kutwa Jumatano tarehe 1 Agosti ni zamu ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Natoa taarifa mapema ili wale ambao wanakusudia kuchangia wajue hivyo ndivyo itakavyokuwa katika siku hizo mbili halafu tutaendelea tena na utaratibu wa kuwakumbusha kwa hizo siku nyingine zitakazosalia.

Naomba radhi sana kwa Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi alisimama katika Kamati na sikuweza kumwita aweze kuchangia. Nasikitika sana kwa tukio hilo si la makusudi na Mheshimiwa Phares Kabuye alisimama kwa mara ya pili lakini kuna Mwenyekiti pale anatoa tu ufafanuzi ili tusiendelee na mjadala ambao tayari ahadi yake imekwisha ahidiwa. Kwa hiyo kama bado kuna tatizo nitaomba nitaomba umwone Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba kwa hilo ambalo linahusiana ila Mheshimiwa Mwanawetu namwomba radhi sana. Hapa napo ni pagumu sana msione hivi si rahisi.

Basi baada ya hayo muda wa kuahirisha umefika, kwa hiyo, naahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.45 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne,*
*Tarehe 31 Julai,2007 Saa Tatu Asubuhi)*